Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Thelathini na Tisa – Tarehe 3 Agosti, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:** Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA UCHUKUZI:** Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Juu ya Wizara ya Uchukuzi Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 358

### Kuimarisha Huduma Kwenye Hospitali ya Wilaya ya Mufindi

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA** aliuliza:-

Hospitali ya Wilaya ya Mufindi ipo karibu sana na Barabara Kuu na inahudumia watu wengi sana wakiwemo Wakazi wa Mufindi wanaotumia hiyo Barabara Kuu hasa yanapotokea matatizo ya ajali, hali ha kuwahudumia wanaokumbwa na ajali hizo huwa ngumu sana hospitalini hapo:-

Je, Serikali haioni kuwa ni wakati mwafaka wa kuboresha na kuongeza huduma muhimu katika hospitali hiyo ili iweze kutoa huduma za uhakika kwa wanaokwenda kupata huduma kwenye hospitali hiyo; na je, ahadi hiyo itatekelezeka lini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, Hospitali ya Wilaya ya Mufindi ipo karibu na Barabara Kuu na inahudumia wahanga wengi wa ajali kwenye maeneo hayo. Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi imekuwa ikiboresha huduma mbalimbali katika

Hospitali hiyo ili iweze kukidhi changamoto zinazojitokeza kwa kuhakikisha huduma zote muhimu katika hospitali zinakuwepo ikiwemo:-

(i) Huduma katika chumba cha upasuaji kitakachotoa huduma saa 24;
(ii) Huduma ya *X-ray* na *Ultra Sound* na kutoa huduma muda wote;
(iii) Huduma ya maabara;
(iv) Huduma za Wagonjwa wa Nje *(OPD)* muda wowote; na
(v) Huduma kwa Wagonjwa wa Ndani katika Wodi ambazo zinatoa huduma kuwa na uwezo wa kulaza wagonjwa 150.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutimiza azma hiyo, Halmashauri imeanza mchakato wa ujenzi wa wodi ya wazazi na kuongeza chumba cha upasuaji (*Theatre*), ambacho kitapunguza msongamano katika chumba kilichopo. Halmashauri imetenga shilingi milioni 242 kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya akina mama katika kipindi hiki tulichonacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri imeweka mpango wa kusomesha watumishi katika fani mbalimbali za afya ili kuongeza wataalam na kuimarisha huduma zinazotolewa. Mpango uliopo unawahusisha watumishi 11, ambao wapo masomoni wakisomea Shahada mbalimbali wakiwemo saba wa udaktari wa binadamu, watatu wakisomea shahada ya uuguzi na mmoja akisomea shahada ya kwanza ya dawa. Kati ya hao ni watumishi watano wanatarajiwa kuhitimu masomo yao mwaka 2011.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri:-

(i) Serikali ina mpango gani wa kupeleka Madaktari Bingwa katika Wilaya ya Mufindi?

(ii) Kwa kuwa wodi ya akina mama inachukua wagonjwa wengi wa aina mbalimbali; Serikali ina mpango gani wa kuongeza jengo lingine kuwanusuru akina mama ambao wanakwenda na maradhi ya aina moja lakini wanapata maradhi ya maambukizi kwa sababu wodi hiyo inachukua wagonjwa wa aina zote?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, anachozungumza hapa ili tuweze kuelewana vizuri, Mheshimiwa Mgimwa *point* anayotaka kuileta hapa inafanana na *Tumbi Hospital* ile ya Kibaha kwamba, kuna ajali nyingi sana zinatokea pale, kwa sababu ya matumizi ya barabara na watu wetu wanakwenda wakati mwingine wanazungumza na simu, mwingine amelewa pombe na nini, watu wamegongwa na wengine wamekufa. Anachokisema hapa ndicho kinachotokea kule Mufindi na Hospitali hii iko pale Mafinga. Kwa hiyo, tunakubali kabisa kama Serikali kwamba, matukio yameonesha kabisa kwamba, kwa kweli kumekuwa kuna ajali na Viongozi wa Serikali tumepiga simu kusema msaidie amepata ajali pale. Kwa hiyo, anachokisema hapa ni sahihi kabisa na sisi tunapenda kumpongeza kwa mawazo haya ambayo amekuwa nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuhusu Madaktari, nimeeleza hapa kuwa, sasa hivi kuna Madaktari ambao wamekwenda masomoni, labda sana sana aulize kwamba; je, wakati hawa wanaendelea na masomo na huku Wananchi wanaendelea kuishi inakuwakuwaje? Hili ni jambo ambalo nitawasiliana na Wizara ya Afya, tutaangalia jinsi ambavyo tutawasaidia lakini kwa mpango wa muda mrefu ni hilo la Madaktari ambalo nimeelezea.

La pili, hili la akina mama analolizungumza hapa; hivi tunavyozungumza, nimezungumzia habari ya wodi ya akina mama, wodi hii, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi imeweka pembeni shilingi milioni 242 na *tender* zimekwisha kufunguliwa. Ninaelewa anasema kwamba, sasa unajua wanalala mahali pamoja na nini, hilo tunategemea litawaondolea hilo tatizo na nimezungumza na Mkurugenzi Mtendaji asubuhi hii, nikijua kwamba ataniuliza swali hilo. Kwa hiyo, nina hakika na

ninachosema kwamba, akitaka aulize na *tender* zimeshafunguliwa na hela hizi zipo shilingi milioni 242.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa hali ya Hospitali ya Mufindi Kaskazini haina tofauti sana na Hospitali ya Wilaya ya Mafia na ukizingatia Mafia ni Kisiwa hakuna njia yoyote ya haraka ya mgonjwa kukimbizwa kwenye hospitali nyingine. Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Mtaalamu wa Picha za *X- ray* na Madaktari Mabingwa kwa sababu vifaa vya *X-ray* viko pale lakini hakuna anayeweza kuvitumia?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zaynab Vullu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *problem* anayoisema hapa ni *genuine*, ni sahihi, hawa ni sawa sawa na wale wa kule Ukerewe wanakaa Mafia. Mimi nimekwenda Mafia sikuweza kwenda kwa gari, kwa sababu ni lazima uruke kwa ndege uende mpaka kule maana ni *self contained* na *self contained* ni lazima iwe na kila kitu humo ndani, ndicho anachokizungumza hapa. Sasa ndiyo usipowasaidia Watu wa Mafia watakufa pale.

Kwa hiyo, nitakachofanya hapa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kuwasiliana na Waziri wetu wa Afya sasa hivi, kama hawana mtu wa *X-ray* sasa itakuwaje kule si itakuwa ni matatizo makubwa sana. Kwa hiyo, hili siyo jambo la kukaa tunajadili hapa ni jambo la kutekeleza, wala asiwe na wasiwasi.

Na. 359

**Mkataba wa Uundaji wa Boti Mpya**

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA** aliuliza:-

Tarehe 13 Mei, 2010, Halmashauri ya Wilaya ya Muleba ilisaini Mkataba na *M/S Sam Amzai Boat Builders Co. Ltd* wa uundaji wa boti mpya kwa gharama ya shilingi 91, 360,000. Boti hiyo ilipaswa kuwa tayari imekamilika na kukabidhiwa tarehe 24 Agosti, 2010:-

(a) Boti hiyo iko wapi na imekabidhiwa kwa nani?

(b) Je, ni kwa kiasi gani masharti ya mkataba ya uundwaji boti hiyo yamesimamiwa na kukamilishwa ipasavyo?

(c) Kama kuna kasoro zozote katika utekelezaji wa mkataba huo ni hatua gani zichukuliwe kwa wahusika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlza, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

Kama nimekosea namna ya kutamka jina lake, ninamwomba aniwie radhi.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Muleba iliingia Mkataba na Mzabuni, *M/S Sam Amzai Boat Builders Co. Ltd* wa uundaji wa boti mpya kwa gharama za Sh. 91,360,000. Gharama hii inajumuisha uundaji wa boti Sh. 85,360,000 na Sh. 6,000,000 kwa ajili ya usafirishaji wa boti hiyo kutoka Dar es Salaam inapoundwa hadi Muleba. Hadi kufikia leo boti hiyo haijakamilika hivyo haijakabidhiwa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, makubaliano ya Mkataba yalikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Mkataba ulianza tarehe 25 Mei, 2010 na Boti ilipaswa kukamilika tarehe 24 Agosti, 2010;

(ii) Malipo yatalipwa kwa awamu nne; awamu ya kwanza Mzabuni atalipwa 50% ya uundaji wa boti; ya pili 40% baada ya kukamilisha uundaji; ya tatu 10% baada ya kukabidhi boti; na ya nne atalipwa fedha za usafirishaji kutoka Dar es Salaam hadi Muleba baada ya boti kukabidhiwa na kukaguliwa na mwajiri; na

(iii) Iwapo Mzabuni atachelewa kukamilisha kazi, mwajiri atamkata asilimia 0.05 ya fedha za Mkataba kwa siku kwa kila siku ambazo hajakamilisha kuunda boti mpaka atakapokabidhi boti hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mzabuni hakuzingatia masharti ya Mkataba wa kutengeneza boti kwa muda uliopangwa. Halmashauri kwa upande wake, imemweleza kwamba, masharti ya Mkataba huo yazingatiwe ikiwemo kutomlipa malipo ya awamu ya pili, tatu na nne.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Mzabuni kutozingatia masharti ya Mkataba, Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, tarehe 18 Machi, 2011 ilichukua hatua ya kumwandikia barua ikimtaka kuzingatia makubaliano yaliyoainishwa kwenye Mkataba huo na kama ilivyoeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tarehe 6 Mei, 2011 Halmashauri ilimwandikia Mzabuni notisi ya nia ya kuvunja Mkataba wa utengenezaji wa boti hiyo na kumweleza kuwa iwapo Mkataba utavunjwa, Mzabuni atapaswa kurejesha asilimia 50 ya kiasi cha fedha ambazo ameshalipwa pamoja na kulipa fidia kwa kukiuka masharti ya Mkataba.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru kwa majibu yake na ninataka kumwambia kwamba, majibu aliyopewa siyo sahihi. Mimi nina *hard copy* ya uchunguzi kuhusu boti hiyo. Swali langu la nyongeza linasema hivi:-

Kwa kuwa kumekuwepo na utaratibu wa kukiuka Mikataba na kuweka Mikataba mibovu na imekuwa kama utamaduni katika Tanzania ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Muleba ambayo iliingia Mkataba na Kampuni ambayo inaitwa *Azai Boat Builders* lakini ikashindwa kuleta vielelezo vya kisheria na badala yake ikaleta kampuni nyingine ambayo *inaitwa Sam Amzai Ltd.*:-

(i) Je, Waziri ana taarifa kuhusu jambo hili?

(ii) Kwa kuwa kumeundwa Kamati mbalimbali kupitia Kamati ya Fedha na Kamati Maalum na wamefuatilia boti hiyo wakakuta hakuna chochote na Halmashauri imeshalipa asilimia 50 ya pesa hiyo; Waziri anatusaidiaje kuchukua hatua dhidi ya Watendaji lakini kuhakikisha pia boti hiyo inapatikana?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Conchesta, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hapa nina usingizi, hivi ninavyozungumza, usiku kucha sijalala kwa sababu ya jambo hili linalozungumzwa hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niseme hapa mbele yako, mimi ni Mkristo, Mluteli, nilijifunza kwamba, sipaswi kusema uongo na msomi yeyote duniani akisema kwamba unalosema siyo sahihi, anakupa ushahidi wake. Ninataka niwaambie Viongozi wenzangu kwamba, ninataka nijibu kuwa, jambo hhili na sisi tumeliona; boti iliagizwa, ilipoagizwa, walikwenda kwenye hii kampuni ambayo nimeitaja hapa, ametoka Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba wamekwenda Dar es Salaam akiwa na watu watatu amefuatana na Wenyeviti wa Kamati, wamekwenda kuangalia boti wakaona boti imeweka kibao kimeandikwa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, wakaangalia hawakuona kitu kingine.

Yule ambaye alipewa kazi hiyo akasema, mkitaka mimi nimalize kazi hii, nipatieni tena asilimia 40 iliyobakia. Wale wakasema haiwezekani, kazi hii imechukua mwaka mzima hapa, sasa mwaka mzima halafu unatuambia tukuongezee tena asilimia 40 maana yake tukitoa hizi, huyu akipokea itakuwa tabu. Wameketi tarehe 26 Julai, 2011 wametoa katika Baraza, wamesema mambo yafuatayo:-

(i) Ikifika mwezi Oktoba, boti hii iwe imeripoti pale Muleba;

(ii) Kama mpaka wakati huo boti itakuwa haijafika pale, wale ambao wamehusika na mpango wote huu niliouzungumza hapa, warejeshe fedha za Halmshauri asilimia 50; na

(iii) Wale wote ambao wamehusika na jambo hili, haya ni matamshi ya Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, kama watu wamehusika hapa, wachukuliwe hatua, sisi tunasubiri tarehe ifike.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, atatuagiza hapa, *we shall never leave any stone unturned*, kama ipo hela ya Halmashauri imechukuliwa hapa na Mheshimiwa Conchesta angalia macho yangu na midomo yangu, ninataka nikwambie kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, yamesemwa maneno hapa, hela za Halmashauri zinachukuliwa hapa, watu wanaingia Mikataba ya ajabu ajabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uniwie radhi na hii sauti yangu ipo hivyo hivyo, lakini jambo hili ninaliamini. Ninataka nimwambie Mheshimiwa Conchesta, hili jambo tutalifuatilia kwa nguvu zetu zote za Serikali na mtaliona joto la Serikali pale. Ninataka nimthibitishie sisi tunafuatilia jambo hili kwa karibu. Jana nimeiona imetoka katika Gazeti la Mwananchi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge wala asiwe na wasiwasi. Sasa haya mengine yote anayoyasema hapa kwamba, ninasema nini na nini na kwamba nina habari hizo; mimi nina habari hizi zote, mengine yatahusu TAKUKURU na nini; ninaomba mniamini kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Mkuchika, sisi tutashughulikia jambo hilo. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Ninaizungumzia hiyo boti ya Muleba, Mheshimiwa Conchesta anazungumzia Muleba ni sehemu ya Jimbo langu. Swali langu ninalouliza:-

Katika taarifa hii anayozungumza ni kwamba; Mhandisi alisaini Mkataba wa kupewa malipo akapewa asilimia 50 na akawasilisha vielelezo vya kampuni nyingine ambayo sasa Halmashauri haiwezi kwenda Mahakamani ku-*enforce*; kwa umakini huo unaozungumza Mheshimiwa Waziri; unaweza kuchukua hatua sasa kwa sababu vielelezo vipo vinaonesha kuwa taratibu zimekiukwa? (*Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwijage, kama ifuatavyo:-

Tusiongee mambo mengi hapa, tuelewane kitu kimoja tu; kuna mgogoro umejitokeza hapa, sisi tunachotaka kuahidi kwa niaba ya Serikali, ninatamani kikao hiki kingekwisha haraka haraka, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Mkuchika, waniache niende kule, halafu ndiyo tutaelewana vizuri kule. Kwa hiyo, sisi hili jambo tutafuatilia kwa karibu sana. *(Makofi)*

Na. 360

**Hitaji la Gari la Wilaya Kusimamia Maliasili**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Wilaya ya Chunya ni pana sana ingawa inazo maliasili nyingi kama misitu na wanyamapori, Afisa Maliasili wa Wilaya hana gari la kumwezesha kusimamia rasilimali hizo vizuri:-

Je, ni lini Serikali itanunua gari la Wilaya kwa ajili ya kusimamia maliasili hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Mhesihmiwa Mbunge kuwa, Wilaya ya Chunya ina rasilimali nyingi zikiwemo misitu na wanyamapori, zinazohitaji kulindwa. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, kutokana na ufinyu wa bajeti, iliwasilisha maombi ya kupatiwa gari hilo Wizara ya Maliasili na Utalii kwa barua ya tarehe 24 Agosti, 2010.

Wizara kupitia Katibu Mkuu na Mkurugenzi wa Misitu na Nyuki, iliahidi kuipatia Halmashauri hii gari hilo ili kuiwezesha Idara ya Maliasili kukabiliana na changamoto za uharibifu wa misitu na mazingira kwa ujumla. Halmashauri kupitia Mkurugenzi na Mkuu wa Wilaya, imekuwa ikifuatilia utekelezaji wa ahadi hii ili gari lipatikane kwa kazi hizo za maliasili. Aidha, Viongozi wa Wizara husika wameonesha nia ya kusaidia upatikanaji wa gari hilo.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Chunya kama nilivyosema ni Wilaya pana sana; karibu asilimia hamsini ya Mkoa wa Mbeya ni Chunya. Kutoka Chunya Mjini kwenda kwenye Misitu ya Udinde ni zaidi ya kilomita 200 na kutoka Chunya Mjini kwenda kwenye Hifadhi ya Rungwa ni zaidi ya kilomita 200 ; na inavyoonekana kutokana na majibu ya Naibu Waziri ni kwamba, matumaini ya kupata gari sasa hivi ni madogo sana. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atanihakikishia kwamba ataiomba Wizara ya Maliasili na Utalii au Wizara ya TAMISEMI yenyewe ipeleke gari hata lililotumika kwa dharura ili wakazuie uvunaji wa misitu na mikaa?

(ii) Kama hiyo itashindikana; je, Serikali ipo tayari kumwongezea *OC* Mkuu wa Wilaya ambaye wakati fulani gari lake hutumika kulinda maliasili hizi?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninaomba nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri na pia ninamshukuru Mheshimiwa Mwambalaswa, kwa kuonesha *concern* kuhusu usimamizi wa maliasili. Ni kweli mwaka jana Wizara yangu iliahidi kwamba, ingeweza kupeleka gari. Mpango tuliokuwa nao awali ni ule wa kutafuta gari jipya. Kwa bahati mbaya, kutokana na ufinyu wa bajeti, haikuweza kutekelezeka hivyo. Kwa sasa hivi tumekwisha kukamilisha taratibu zote za kupata gari kwa ajili ya kupeleka Wilaya hiyo ya Lupa na nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa uhakika pengine kabla ya mwezi Desemba, tutakuwa tumeshapeleka gari. *(Makofi)*

Na. 361

**Kurejesha Huduma Katika Hospitali ya KKKT – Izimbya**

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Hospitali ya KKKT Izimbya ilishapatiwa hadhi ya kuwa Hospitali Teule ya Wilaya *(DDH),* tangu mwaka 2008 na hivyo kuwanufaisha Wananchi wa Kata za Izimbya, Buturage, Ruhunga, Mugajwale, Katoro, Kyamulaile, Rukoma, Rubale na Buterankunzi, ambao wengi wao wanaishi zaidi ya km. 100 kutoka Bukoba Vijijini ilipo Hospitali ya Serikali. Mwishoni mwa mwaka 2010 huduma hizi zilisitishwa kwa madai kuwa Hospitali hiyo ilikuwa na kasoro ndogo ndogo:-

Kwa kuwa kasoro hizo zilizodaiwa kuwepo sasa zimesharekebishwa; je, ni lini huduma hjii itarejeshwa katika Hospitali ya Izimbya ili Wananchi wa maeneo hayo waache kuteseka?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua na kuthamini mchango wa Sekta Binafsi ikiwa ni pamoja na Mashirika ya Kidini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kushughulikia ombi la Hospitali ya Izimbya kuwa Hospitali Teule ya Halmashauri, Wizara ilituma wataalamu kukagua Hospitali hiyo ili kuainisha kama inakidhi viwango vya kuwa Hospitali Teule ya Halmashauri ya Bukoba Vijijini. Timu ya Wataalamu wakiambatana na Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kagera, ilifanya ukaguzi wa Hospitali hiyo tarehe 11 Novemba, 2010. Baada ya ukaguzi, ilionekana kuwa Hospitali hiyo, kwa hali ilivyokuwa wakati wa ukaguzi, haikuwa imetimiza masharti ya kuwa Hospitali Teule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Wataalamu hao walitoa taarifa ya upungufu ulioonekana ili ufanyiwe kazi. Tarehe 27 Juni, 2011, Timu ya Wizara ilitembelea tena Hospitali hii ili kukagua na kuangalia kama marekebisho husika yamefanyika. Taarifa iliyopo ni kuwa, wamejitahidi kufanya marekebisho ingawa bado hayajakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uongozi wa Hospitali ya Izimbya umefanya mambo yafuatayo ili kurekebisha upungufu uliojitokeza:-

(a) Wameweka umeme wa sola wenye nguvu;

(b) Wameagiza jenereta kwa ajili ya umeme mbadala;

(c) Ukarabati wa wodi bado unaendelea; na

(d) Ukarabati wa *theatre* bado haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kukupa taarifa kuwa, jana tarehe 2 Agosti, 2011, Mganga Mkuu wa Mkoa aliitembelea Hospitali hii ili kukagua tena upungufu uliobainishwa. Taarifa alizotuletea ni kuwa, bado ukarabati wa *theatre* pamoja na wodi za wagonjwa unaendelea na bado haujakamilika; ameahidi kwenda kukagua tena baada ya wiki mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, mara marekebisho husika yatakapokamilika na vikao husika vya Halmashauri ya Wilaya na Mkoa *(RCC)* kupitisha ombi lao na kuwasilisha Wizarani, Wizara itatoa kibali cha Hospitali hiyo kuwa Hospitali Teule ya Wilaya.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri siyo sahihi, kwa sababu mnamo tarehe 12 Agosti, 2008, Hospitali hii ilipewa hadhi ya kuwa Hospitali Teule ya Wilaya na ikapewa namba ya usajili, Hospitali Teule ya Wilaya Namba 186003 na ikaambiwa kwamba, ilipe ada shilingi laki moja kwa ajili ya usajili huo na ikalipa fedha hizo. Pia ikaambiwa italipa ada kila mwaka shilingi 50,000, ikalipa shilingi 50,000 mwaka wa kwanza. Kwa hiyo, ikawa Hospitali Teule, Wananchi wakapata manufaa ya kuwa na Hospitali Teule Wilayani pale. Sasa swali.

(i) Kwa nini wanamdanganya Mheshimiwa Waziri wanampa majibu ambayo siyo sahihi; na kwa nini asitangaze hapa Bungeni kwamba Hospitali ni Teule ili hao wanaomdanganya, wanaokosea, wahangaike nalo huko; yeye atangaze kwamba; hii ni Hospitali Teule, ina sifa zote na inaendesha huduma?

(ii) Kama kuna upungufu ambao wanadai kwamba upo, Waziri aende mwenyewe kukagua hospitali hiyo, anajua viwango na vigezo, aje mwenyewe aikague Hospitali hiyo aone kwamba ina viwango na inakidhi kuwa Hospitali Teule ya Wilaya. Ninashukuru. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Rweikiza, kwa ufuatiliaji wake wa kero za Wananchi wa Bukoba Vijijini, ikiwemo huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili kidogo ninaona watu wanalichanganya; hiyo Hospitali ya Izimbya wao waliomba kibali kwa wakati ule kupitia kwa Msajili wa Hospitali Binafsi kwamba, ilikuwa Kituo cha Afya baadaye ikapata hadhi ya kuwa Hospitali; ndipo hapo hapo walipoomba iwe Hospitali Teule ya Wilaya. Kimakosa, Msajili wa Hospitali Binafsi aliwapa hiyo hali kwamba, watakuwa Hospitali Teule ya Wilaya. Kiutaratibu ni kwamba, hawakufuata. Kwa hiyo, hii tulikuja kugundua Wizarani baadaye na tuliwapa barua Hospitali hiyo kwamba, kama wanataka iwe Hospitali Teule, wanatakiwa wafuate utaratibu wawasiliane na Halmashauri husika. Hiyo hatua ndiyo waliianza na ndiyo hapa jibu langu la msingi nilisema kwamba, ndiyo tulianza kutuma wataalam wamekwenda kuchunguza pale, imeonekana kwamba, bado kuna hitilafu; baadhi ya masharti hawajatimiza na mpaka leo bado hawajayatekeleza.

Ninaomba niwafahamishe Wananchi wa Bukoba Vijijini kuwa, inaelekea pale kuna siasa; kuna wengine wanatumia nafasi hii kama ndiyo mbinu za kampeni pale, lakini ile Hospitali bado haijawa Hospitali Teule ya Wilaya.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kuniona na kunipa nafasi. Kwa kuwa tatizo la Hospitali ya Izimbya linafanana kwa kiwango fulani na Hospitali ya Machame, ambayo Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete alitoa ahadi yake binafsi na ya Serikali yake ya kuipandisha na kuwa *DDH*; na kwa sababu Halmashauri ya Wilaya ya Hai imeshakaa na Uongozi wa Hospitali ya Machame chini ya Uongozi wa *Diocese* ya Kaskazini ya KKKT na kusaini Mkataba wa kuingiza Hospitali ya Machame katika *DDH* tangu mwaka jana na Mikataba hiyo pamoja na taarifa zingine za vikao kupelekwa Wizara ya Afya Dar es Salaam kwa ajili ya utekelezaji na ufuatiliaji wake na hadi leo tunapozungumza bado Wizara ya Afya haijatoa majibu yoyote kuashiria utekelezaji wa ahadi hiyo Rais pamoja na hatua za awali kumalizika.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutueleza ni nini hasa kinakwamisha utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais na kama atakuwa tayari kulifuatilia na kuhakisha kwamba linakamilika katika muda mfupi iwezekanavyo?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ahadi hiyo imetolewa na Mheshimiwa Rais, kuipandisha au kuifanya Hospitali ya Machame kuwa *DDH* na hii ni miongoni mwa hospitali tisa ambazo tunazishughulikia sasa hivi ndani ya Wizara, kuzipandisha au kuzifanya kuwa Hospitali za *DDH* za Halmashauri.

Na. 362

**Ubaguzi Katika Mfuko wa Bima ya Afya**

**MHE. AGNESS E. HOKORORO** aliuliza:-

Mfuko wa Bima ya Afya unalalamikiwa kuwa na ubaguzi kutokana na kutofautisha madaraja ya wateja kulingana na vipato vyao:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa Mfuko huu umekuwa kero na wa kibaguzi kwa kuwapa huduma nzuri wanachama wenye kadi za kijani tofauti na wale wenye kadi za kawaida ambao kipato chao ni kidogo?

(b) Je, udhibiti wa Mfuko huu kwenye malipo ya matibabu ukoje katika kuhakikisha hakuna ubabaishaji kati ya Bima ya Afya na Taasisi zinazotoa huduma kwa kuzidisha malipo?

(c) Kwa kuwa Mfuko huu hausaidii mgonjwa wa ghafla kwa vile lazima awe na kadi mahali popote na hospitali nyingi huwapa kipaumbele wagonjwa wenye fedha taslimu kwanza; je, kwa nini mfumo huu usivunjwe ili kufanya upya tathmini ya gharama za matibabu?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mhesahimiwa Agness Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko ulipoanzishwa mwaka 2001, uliendelea kutumia miongozo ya Serikali kuhusu utoaji wa huduma kwa watumishi. Watumishi waliokuwa wana mishahara wa ngazi ya TGS 14 (kwa wakati huo), walikuwa wanapatiwa huduma za matibabu katika Daraja la I na II. Hawa ndiyo waliopatiwa kadi za kijani na watumishi wenye mishahara ya ngazi ya chini, kadi za njano. Utaratibu wa madaraja ya upatikanaji wa huduma hii, unatumika duniani kote. Hata hivyo, vituo mbalimbali vimekuwa vikiongeza uwezo wa kuwahudumia wagonjwa na hivyo kutoa huduma kwa wanachama wote bila kujali aina au rangi ya kadi. Hivi sasa utaratibu wa utambuzi wa kadi hizi umebaki katika hospitali mbili tu za Agakhan na Regency za Dar es Salaam.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko unadhibiti malipo ya matibabu kati yake na Taasisi zinazotoa huduma kwa kufanya kaguzi za mara kwa mara na za kushtukiza kupitia timu yake ya madaktari na kukagua madai yote yanayowasilishwa kwa malipo kama Sheria (Kifungu Na. 27(2)) inavyoelekeza na kuupa Mfuko uwezo wa kukataa madai yoyote yasiyo sahihi yatakayowasilishwa au yanatyokiuka Kanuni na Miongozo ya Mfuko na ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utaratibu wa matibabu chini ya mfumo wa matibabu wa Bima ya Afya, huduma hupatikana kwa mwanachama mwenye kadi popote pale penye vituo vilivyosajiliwa na Mfuko Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, tumekubaliana na watoa huduma wote waliosajiliwa na Mfuko, kuwapatia huduma za dharura wanachama wake wote kama hawana kitambulisho kwa wakati huo. Ndugu au jamaa wanaomfahamu kama wapo wanatakiwa kumtambulisha kwa mtoa huduma kuwa ni mwanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Hata hivyo, baadaye mtoa huduma anatakiwa kujihakikishia uanachama wa mteja wake ili baadaye aweze kulipwa na Mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii kuwataka Wanachama wote wa Mfuko wa Bima ya Afya kuwa na tabia ya kutembea na vitambulisho vya wakati wote ili inapotokea dharura aweze kutibiwa bila kuwepo na mashaka yoyote.

**MHE. AGNESS E. HOKORORO:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninapenda kuuliza maswali madogo mawili kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa asilimia tatu ya mshahara wanaokatwa wafanyakazi pamoja na ile inayotolewa na waajiri wao ni chanzo kimojawapo katika Mfuko huu wa Bima ya Afya; Serikali haioni kwamba ipo haja ya kuangalia upya marupurupu na mishahara wanayopata Wafanyakazi wa Mfuko kwa kuwa imelalamikiwa kuwa ni mikubwa inatokana na mishahara ya wafanyakazi wetu wa nchi hii? *(Makofi)*

(ii) Kwa kuwa wataalam wameonesha kwamba kitendo cha kutahiri kinapunguza maambukizo ya UKIMWI kwa asilimia 30; je, kwa nini Mfuko huu usiweke *circumcision* kama gonjwa mojawapo ambalo linalipiwa na Mfuko kuliko ilivyo sasa kwa kuwataka wanaofanyiwa kitendo cha utahiri kutokulipiwa na Mfuko huu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, ninakubaliana naye kwamba, kuna haja ya kuangalia upya marupurupu ya Wafanyakazi wa Mfuko huu, lakini vilevile tukilenga kuboresha huduma zaidi ambazo wanazitoa. Hiyo ninakubaliana na Mheshimiwa Hokororo, tutaifanyia kazi. *(Makofi)*

Swali la pili kuhusu tohara kwa wanaume; ni kweli tafiti za kisayansi zimeonesha kwamba, wale ambao wanapata tohara wanapunguza uwezo mkubwa zaidi wa maambukizi ya Virusi vya UKIMWI, ukifananisha na wale ambao hawakupata tohara.

Ninaomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara ya Afya tuna mpango kwa Mikoa ambayo ina viwango vya chini vya wanaume waliotahiriwa na vilevile wana viwango vya juu vya

maambukizi ya Virusi vya UKIMWI, tunafanya tohara hiyo bure. Vilevile Mfuko huu nao umeliangalia hili suala na ninaomba nimpe taarifa Mheshimiwa Hokororo kwamba, ni mojawapo ya vitita vilivyoongezwa katika huduma ambazo Mfuko wanatoa pamoja na tohara kwa wanaume. *(Makofi)*

**MHE. RITTA E. KABATI:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuniona. Kwa kuwa Serikali imekuwa ikiwasomesha watoto yatima katika vituo mbalimbali hapa nchini; na kwa kuwa katika vituo pamekuwepo na tatizo kubwa sana la upatikanaji wa huduma ya afya; je, Serikali ina mpango gani wa kuweka huduma hiyo katika hivyo vituo vya watoto yatima?

**MWENYEKITI:** Hilo ni swali jipya kabisa, lakini Mheshimiwa Waziri kama lipo kwenye uwezo wa Wizara yako jibu.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikiri kwamba, hiyo ni mojawapo ya shughuli ambazo tunaziangalia namna gani tunaweza tukaboresha huduma za afya kwenye vile vituo vya kulelea hawa watoto. Licha ya hapo, kwa sababu mdau aliyeuliza swali hili ana *interest* na *area* hii; ninamhakikishia kwamba, nitakaa naye, nitaongea naye, namna gani tunaweza tukatanua huduma zetu katika hizi sehemu.

Na. 363

**Mchango wa Mbuga ya Serengeti Kwenye Huduma za Jamii**

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE (K.n.y. MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE)** aliuliza:-

Sehemu kubwa ya eneo la Wilaya ya Serengeti ni Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ambayo inachangia kwa asilimia 27 mapato ya nje na asilimia 47 mapato ya ndani, lakini Wialaya ya Serengeti haifaidiki kwa kiwango cha kuridhisha kutokana na Hifadhi hiyo na huduma za jamii ni duni sana:-

(a) Je, kwa nini Serikali imekaa kimya bila hata kulipa kifuta machozi Wananchi wanaouawa na wanyamapori wakali na mazao yao kuharibiwa na wanyama kutoka kwenye Hifadhi ya Serengeti na kwenye Mapori ya Akiba ya Ikorongo na Grumeti?

(b) Kwa sheria iliyopo sasa ya kulipa kifuta machozi cha shilingi 200,000 na kifuta jasho shilingi 100,000 kiasi ambacho ni kidogo sana. Je, Serikali haioni kwamba sasa umefika wakati mwafaka wa kubadilisha viwango hivyo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dokta Kebwe Stephen Kebwe, Mbunge wa Serengeti, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali haipo kimya katika suala zima la kushughulikia matatizo yanayowapata Wananchi kutokana na madhara ya wanyamapori wakali na waharibifu, hususan kwa kuharibiwa mashamba yao na wakati mwingine kusababisha vifo vya Wananchi. Tatizo lililopo na ambalo kwa kiasi kikubwa, linakwamisha zoezi la kushughulikia matatizo haya kwa haraka ni kucheleweshwa au kukosekana kwa taarifa za uhakiki wa matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu. Taarifa hizo ni zile zinazoanzia kijijini au mahali ambapo tukio limetokea hadi ngazi ya Wilaya kwa kuwahusisha Afisa Mtendaji wa Kijiji, Afisa Wanyamapori wa Wilaya, Afisa Kilimo wa Wilaya, Polisi na Mganga Mkuu wa Wilaya ili kujenga mazingira shirikishi na kutoa fursa ya uwazi katika kutekeleza zoezi la kuandaa malipo ya kifuta jasho au kifuta machozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupatikana kwa taarifa za awali, taarifa hizo za matukio ni muhimu ziwasilishwe Wizarani kwangu kwa ajili ya uchambuzi utakaowezesha kufanya malipo ambayo hupitishwa kwa wasimamizi wa Vituo vya Idara ya Wanyamapori vilivyo karibu na maeneo ya matukio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010, Wizara ilipokea maombi ya malipo ya kifuta machozi kwa ajili ya kifo cha Chausiku Nyakimori Chacha, kilichosababishwa na tembo. Baada ya maombi hayo kuhakikiwa, mrithi wa marehemu alilipwa shilingi 200,000 kwa viwango vilivyokuwepo wakati huo. Aidha, tangu utaratibu wa kulipa kifuta jasho uanze kutumika, Wizara haijapokea orodha ya majina mengine zaidi ya hilo moja nililolitaja kutoka kwa Wananchi wa Wilaya ya Serengeti.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara yangu imepitia upya utaratibu wa kulipa kifuta machozi na kifuta jasho kwa kufanya marekebisho ambapo viwango vinavyolipwa kwa Wananchi ambao wameathiriwa na wanyamapori vimeongezwa. Kwa mujibu wa Kanuni za Uhifadhi wa Wanyamapori za Mwaka 2011, ambazo zilitangazwa kwenye Gazeti la Serikali Namba 146 la tarehe 22 Aprili, 2011, viwango vipya vinavyotumika kwa sasa ni kifuta jasho cha shilingi 100,000 kwa ekari kutokana na uharibifu wa shamba lenye ukubwa kuanzia ekari moja hadi tano. Kifuta machozi cha shilingi 1,000,000 kwa ndugu wa marehemu aliyeuawa na mnyamapori. Mwananchi anayepata ulemavu wa kudumu analipwa shilingi 500,000 na majeruhi analipwa shilingi 200,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongeza pia mifugo, ambayo awali haikuwepo katika utaratibu wa kulipwa. Hivi sasa mifugo kama ng'ombe inalipwa shilingi 50,000, mbuzi na kondoo shilingi 25,000 na mifugo mingine kuku, njiwa na kadhalika inalipwa shilingi 10,000.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Tarehe 20 Julai, 2011 katika Kijiji cha Masanga Wilayani Tarime, nyati alivamia kijiji hicho na kuua mtu mmoja na kujeruhi watu watano. Je, Waziri anasema nini kuhusu tukio hilo?

(ii) Mara kwa mara ndovu huvamia Kijiji cha Gibaso na kuharibu mazao ya chakula na hivyo kusababishia Wananchi wa Gibaso kuishi kwa shida, usalama unakuwa hatarini na vilevile njaa inawakabili kwa muda mrefu kutokana na uvamizi wa hawa ndovu. Serikali inasema nini kuhusu tukio hilo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nyambari Nyangwine, Mbunge wa Serengeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninaomba kutoa pole sana kwa Wananchi wa Tarime na hususan familia ya marehemu na wale waliojeruhiwa kutokana na huyu mnyama, baada ya kuwa ametoka kwenye maeneo ya Hifadhi. Serikali inasema nini; kama nilivyosema kwenye jibu la msingi ni kwamba; Serikali inatoa kifuta jasho kama ni mazao yameharibiwa na inatoa kifuta machozi kama ni binadamu ameuwawa. Kwa utaratibu ambao nimeshausema tulioutangaza na kuanza kutumika tarehe 22 Aprili, 2011, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, atupatie hizo taarifa ili tuweze kulipa kifuta machozi na kifuta jasho na pole kwa majeruhi kama ambavyo nimeshasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uharibifu wa mazao unaofanywa na ndovu Kijiji cha Gibaso na vijiji vingine, ni kwamba, Wizara yangu inaangalia uwezekano wa kuweka Kituo kingine kitakachotumika kudhibiti wanyama wanapotoka Hifadhini kwenye maeneo ya Ukanda huo. Tunategemea katika bajeti ijayo, tutaamua ni wapi tujenge kituo hicho, lakini dhamira yetu ni kuweka kituo upande huo kwa sababu, matukio yamekuwa ni mengi hasa Wilaya ya Serengeti pamoja na Wilaya ya Bunda na Tarime pia yapo.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Kwa kuwa hali ya Serengeti ya uharibifu wa wanyama kwa mazao haitofautiani na Jimbo langu la Nkenge; mpaka sasa hivi wakulima wa Kata ya Ishozi, Ishunju, Gera na Kata zingine, wamekuwa wakilima mazao yao yanaharibiwa na wanyama na wamehangaika sana na tumefikia mahali kuonana na Afisa Wanyama Pori, ambaye ni mmoja tu Wilaya nzima na ana bunduki hana risasi:-

Serikali inasema nini kuhusu hilo maana mpaka sasa wakulima wanashindwa kuendelea kwa sababu ya wanyama hao? Watusaidie namna ya kutekeleza na kusaidia kuondoa tatizo hilo katika Jimbo la Nkenge.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, matatizo ya wanyama waharibifu yameongezeka sana miaka ya karibuni. Sababu zipo nyingi, lakini tunafanya pia utafiti kuweza kujiridhisha ni sababu zipi ambazo ni za msingi sana, sababu za kiujumla ni pamoja na uharibifu wa mazingira, uvamizi wa shoroba, pamoja na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuyatambua haya, tumekuwa tukiziomba Halmashauri na ninaomba nichukue nafasi hii kuiomba Halmashauri ya Wilaya ya Nkenge kwamba, katika maeneo ambayo kunakuwepo na *incident* nyingi za wanyama waharibifu, ni vizuri Halmashauri zikaongeza idadi ya Askari, kwa sababu hawa ni waajiriwa wa Halmashauri. Sisi kama Wizara, tunasaidia kutoa vitendea kazi na kwa maana hiyo, tutasaidia kuongeza silaha pamoja na risasi kwa ajili kusaidia matukio ya namna hii. Vilevile tutakuwa tunatumia askari wetu walioko kwenye mapori ya akiba yaliyoko jirani, kule Kimisi na Burigi, kwa ajili ya kutoa msaada wa haraka pale ambapo matukio ya namna hiyo yanajitokeza.

Na. 364

**Ujenzi wa Barabara ya Mbande – Kongwa – Mpwapwa kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE** aliuliza:-

Katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM *ya* 2010/2015 Chama cha Mapinduzi kiliahidi kuisimamia Serikali yake ili kujenga barabara ya lami toka Mbande – Kongwa hadi Mpwapwa:-

(a) Je, ni lini upembuzi yakinifu utaanza na kumalizika?

(b) Je, ni lini ujenzi huo utaanza na kumalizika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako ninaomba nianze kwa kutoa pole kwa Wananchi 13 wa Wilaya za Kyela na Ludewa, kwa ajali ya boti iliyotokea usiku wa kuamkia leo katika Ziwa Nyasa. Ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwamba, watu wote 13 wameokolewa, lakini boti la Kanisa la Kilutheri Matema limezama. Mimi na Mheshimiwa Mbunge wa Ludewa, Mheshimiwa Deo Haule Filikunjombe, tunashirikiana na Uongozi wa Wilaya zetu, kupata msaada wa kuliopoa boti hilo ambalo ni msaada mkubwa, siyo tu kwa Wananchi na sisi Wabunge, tunapotembelea Wananchi wetu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, sasa ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Jimbo la Kibakwe, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imepanga kuifanyia upembuzi yakinifu Barabara ya Mbande – Kongwa hadi Mpwapwa katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012. Baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu, usanifu wa Barabara hii kwa kiwango cha lami utafanywa katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013. Baada ya kazi hizo kukamilika, inatarajiwa ujenzi kwa kiwango cha lami kuanza, kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninashukuru kabisakwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Dokta Mwakyembe. Wizara hii kwanza, ina Madaktari wawili; ni Wizara muhimu sana na kwa kweli imepata watu muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu hayo, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Katika ukurasa wa 156 wa Kitabu cha Bajeti, fedha zilizotengwa katika usanifu wa barabara hiyo ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami kutoka Mbande - Kongwa mpaka Mpwapwa ni kidogo sana: Je, Serikali, Wizara ipo tayari kuongeza kiwango hiki ili upembuzi huu uweze kufanyika kwa mujibu wa kalenda waliyoitoa hapa ili barabara ikamilike katika kipindi kinachotakiwa kabla ya mwaka 2015?

(ii) Yapo makosa yanajitokeza; unapoizungumzia Mpwapwa ni pamoja na Kibakwe; Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akakubaliana na mimi kwamba usanifu huu unaofanyika, ufanyike pamoja na Kibakwe kwa sababu ni kilometa 30 tu; kwani Kibakwe nako wanatenda dhambi gani wakiwa na barabara ya lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Simbachawene, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nipende kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, ninaomba kwenye Kitabu cha Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, asiishie tu kusoma kiambatanisho cha pili, asome pia na cha nne na cha tano (c).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia kwamba, Wizara imepania kuifanyia hii barabara upembuzi yakinifu. Suala la fedha kutotosha ni la kitaalamu, atuachie; sisi tumedhamiria kutekeleza ujenzi wa hii barabara kufuatana na Ilani na kufuatana na fedha zinazopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu la mwisho kwamba, kutokana na ufuatiliaji wa karibu anaoufanya Mheshimiwa Simbachawene kwenye barabara hii, Wizara inaihudumia vizuri sana hii barabara. Yeye mwenyewe lazima akiri katika mwaka huu unaopita, fedha za matengenezo ya kawaida, Mheshimiwa Simbachawene, tulikutengea shilingi milioni 35 na kitu; matengenezo ya muda maalum shilingi milioni 86 na kitu; matengenezo ya sehemu korofi shilingi milioni 15; na hali ya barabara mpaka sasa ni nzuri, ninachokuhakikishia tu ni kwamba, katika kipindi hiki cha miaka mitano, barabara hii itajengwa katika kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa ajili ya muda...

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili hajajibu!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, mwenyewe.

**WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri sana. Ninataka kumhakikishia tu Mheshimiwa Simbachawene kwamba, tutafanya *addendum* ili ile *feasibility study* tuifanye mpaka Kibakwe ili nayo ihusishwe kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha lami. Hii ni kwa sababu tunaamini tuna fedha za kutosha kwa kutumia Mfuko wa Barabara.

Na. 365

**Ulipaji wa Fidia Kutokana na Upanuzi wa Barabara**

**MHE. SILVESTRY F. KOKA** aliuliza:-

Upanuzi wa Barabara ya Pangani hadi Mapinga kuelekea Bagamoyo kutoka mita 15 – 30 unaendelea na Wananchi walioathirika na upanuzi huo wameambiwa kuwa hawatalipwa fidia:-

(a) Je, taratibu za kisheria za ulipaji fidia wakati wa upanuzi wa barabara zikoje?

(b) Je, ni kwa nini Wananchi hao wenye hali duni za kimaisha wasilipwe fidia kwa ardhi na mazao yao kutokana na upanuzi huo?

(c) Je, upanuzi huo wa kiwango cha lami utakamilika lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, ninaomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Kibaha – Mapinga ina urefu wa Km 32. Barabara hii awali ilikuwa ya Wilaya, yenye hifadhi ya barabara ya upana wa mita 30, ikiwa ni mita 15 kila upande kutoka katikati ya barabara. Mwaka 2008 barabara hii ilipandishwa hadhi kuwa Barabara ya Mkoa, yenye upana wa Hifadhi ya Barabara mita 60, ikiwa ni mita 30 kila upande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo ya utangulizi, sasa ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mwenyekiti, taratibu za Kisheria za ulipaji wa fidia wakati wa upanuzi wa barabara ni kama ifuatavyo:-

(i) Kutokana na kuwa hifadhi ya barabara hapo awali ilikuwa mita 15 kila upande, wale wote watakaokutwa ndani ya hizo mita 15 watahesabiwa kuwa walikuwa ndani ya hifadhi hivyo hawastahili fidia yoyote.

(ii) Wale wote waliokuwa nje ya mita 15 kabla ya mwaka 2007 kila upande, wanastahili fidia ya ardhi, mazao na nyumba.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatana na maelezo niliyoyatoa, Wananchi waliokuwa nje ya mita 15 za awali kila upande watalipwa kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Na. 13 ya Mwaka 2007.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa barabara hii inajengwa kwa kiwango cha changarawe na siyo lami. Ukarabati wa barabara hii kwa kiwango cha changarawe ulianza kufanyika kuanzia mwaka 2009/2010 na utakamilika mwaka 2011/2012.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa maeneo mengi ya Kibaha Mjini na hususan barabara mbalimbali zilikuwa ni za kienyeji kwa maana ya barabara za miguu na za magari; na kwa kuwa kwa Tanzania nzima hakuna *Master Plan* inayoweza kumfanya Mwananchi wa kawaida mwenye eneo lake au shamba lake kujua hapa patakuja kupita barabara baadaye; ni kigezo gani kinachotumika kumfanya Mwananchi huyu kutofidiwa katika zile mita 15 mara barabara hizo zinapogundulika kwambazitakuja kuwa Barabara Kuu kama hii ya *TAMCO* mpaka Mapinga?

(ii) Kwa kuwa sasa Utawala Bora ni pamoja na kuwaelimisha Wananchi kuweza kuelewa taratibu nzuri na mipango mizuri ya Serikali iliyoiweka katika kutengeneza barabara kwa nchi nzima; na kwa kuwa sasa Wananchi wengi hawana ujuzi wala hawajapata maelezo ya kutosha kuhusu Sheria hizi za Barabara; je, Serikali haioni sasa kuwa ni muda mwafaka wa kutoa elimu ya kutosha kwa Wananchi walio wengi Tanzania, kwa kupitia vyombo vya habari na hata kongamano na hata Serikali za Mitaa kupitia *Regional TANROADS*ili Wananchi waweze kupata elimu hii na kuondokana na malalamiko makubwa ya kutopata fidia katika ujenzi wa barabara kwa nchi nzima?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Koka, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninataka nimweleweshe Mheshimiwa Mbunge kwamba, barabara zote anazoziona nchini zimeanzishwa na zipo kisheria na zinaratibiwa kisheria, siyo kwamba, zipo tu bila kumbukumbu zozote za kisheria. Ninaomba nirejee maneno ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, aliyoyatoa jana katika Hotuba yake kwamba, Wizara katika mwaka huu wa fedha, imepania kutoa elimu au kusimamia zoezi la elimu kwa Wananchi pamoja na kwamba, tunaelewa kuwa, kutokujua sheria siyo utetezi!

Tumeona sasa ni wajibu wetu tutoe hiyo elimu kwa Wananchi waweze kujua kuhusu haki zao, waweze kujua mipaka ya barabara. Vilevile kwa kuwaelimisha, inawezekana sana ukalinda barabara zetu, wakaelewa kabisa kwamba, kuna kitu kinaitwa samani za barabara ambazo ni wajibu wetu upande wa Serikali na Wananchi kuzitunza. Pale wanapomwona dereva pengine anagonga samani ya barabara ni muhimu Wananchi waka-*note* gari lake na kuripoti *TANROADS,* pale ambapo mtu anachimba hifadhi ya barabara, ni kosa la jinai, faini siyo zaidi ya shilingi 1,000,000 na kwenda jela miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii ni elimu ambayo tumepania katika mwaka huu wa fedha kuitoa ili Wananchi waweze kuelewa kinaganaga kuhusu haki zao na vilevile wajibu wao katika kutunza barabara.

Na. 366

**Wanafunzi Walioghushi Vyeti**

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA** aliuliza:-

Kuna taarifa kwamba, kuna baadhi ya wanafunzi wamegundulika kughushi vyeti vya elimu na kujipatia mikopo ya elimu ya juu kinyume na sheria:-

(a) Je, ni wanafunzi wangapi wamegundulika kufanya udanganyifu huo; na ni hatua gani za kisheria zimechukuliwa dhidi yao?

(b) Je, miongoni mwao ni wangapi wanaosoma hapa nchini na wangapi wanasoma nje ya nchi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kati ya mwaka 2007/2008 na 2009/2010, jumla ya wanafunzi 16 waligundulika kufanya udanganyifu kwa kughushi vyeti vya elimu na kujipatia mikopo ya elimu ya juu kinyume cha sheria. Miongoni mwa wanafunzi hao walioghushi vyeti, mmoja alikuwa akisoma katika Chuo Kikuu cha Dodoma, wanafunzi 15 walichaguliwa kusoma nje ya nchi, ambapo wanafunzi tisa walichaguliwa kusoma Urusi na sita kusoma Algeria. Aidha, baada ya Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu kugundua tatizo hilo, hatua zifuatazo zimechukuliwa:-

(i) Wanafunzi hao wamefutiwa mikopo yao yote;

(ii) Wanafunzi waliokuwa nje ya nchi, walirudishwa nchini ili sheria ichukue mkondo wake; na

(iii) Taarifa kamili zilitolewa kwa Jeshi la Polisi katika Kituo cha Oysterbay na majalada ya kesi za jinai kufunguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na tatizo hili la vyeti vya kugushi, Wizara yangu inatekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kuunganisha mfumo wa mawasiliano kwa njia ya mtandao, yaani *Network* kati ya Baraza la Mitihani ya Taifa, Tume ya Vyuo Kikuu, yaani *TCU,* pamoja na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Mtandao huu unabaini kwa haraka vyeti vilivyogushiwa na hivyo kutotoa fursa tena kwa wadanganyifu.

(ii) Kuweka picha za wahitimu halali kwenye vyeti vya kuhitimu masomo ya Kidato cha Nne na Sita ambapo muundo huu tayari umeanza kutumika.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Pamoja na kurudishwa kwa wanafunzi hao; je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha pesa walizokopa wanafunzi hao zinarejeshwa ili ziweze kuwasaidia wanafunzi wengine ambao wanahitaji kupata pesa hizo?

(ii) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba wanafunzi hao walipelekwa Kituo cha Polisi Oysterbay na majadala yakafunguliwa; na kwa kuwa Wizara ya Elimu ndiyo shahidi wa kwanza wa kesi hii; je, ni lini upelelezi utakamilika ili vijana hao wafikishwe mahakamani na iwe funzo kwa vijana wengine ambao wana mchezo huo?

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, majibu ili tuweze kumaliza swali lililobakia.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ninaomba kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wanafunzi waliokuwa wamedanganya, kurejesha fedha zao walizokuwa wamekopa Bodi ya Mikopo, kama nilivyosema kwenye jibu la nyongeza kwamba, tayari sisi kama Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, tumewajibika kuwakamata na kufungua majalada pale Polisi Oysterbay.

Kwa hiyo, hatua nyingine zinafuatwa huko polisi na kuendelea mahakamani. Labda tu niseme kwamba, kesi hizi zipo mahakamani, kwa hiyo, mahakama ndiyo watakaotoa hukumu kwamba, fedha zinarudishwa au wale watuhumiwa wanachukua hatua zingine za kisheria.

Kuhusu majalada ya kesi kwamba, Wizara ya Elimu ndiyo shahidi namba moja kwa upelelezi; majibu ni yale yale tu kwamba, ndiyo mashahidi namba moja na tayari tumeshatoa ushahidi polisi na tayari taratibu nyingine zinafanyika katika hatua hizo za kuwapeleka mahakamani.

**MWENYEKITI**: Tunamalizia swali la mwisho Waheshimiwa Wabunge, ninaomba nimwite Mheshimiwa Josephat Kendege, aulize swali la mwisho kwenye orodha ya leo.

Na. 367

**Hitaji la Mahakama za Mwanzo Katika Vijiji vya Matai, Mwimbi na Mwazye**

**MHE. JOSEPHAT S. KENDEGE** aliuliza:-

Katika mfumo unaozingatia Utawala Bora, haki ya Wananchi hupatikana bila ya usumbufu usio wa lazima:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba Mahakama za Mwanzo zilizokuwa zinafanya kazi katika Vijiji vya Matai, Mwimbi na Mwazye zinafanya kazi ili kuwaondolea usumbufu Wananchi wa kwenda hadi mahakama iliyoko Sumbawanga kufuata haki zao?

(b) Je, Serikali imejiandaa vipi kuendana na kasi ya uanzishwaji wa Wilaya mpya ya Kalambo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Joesphat Sinkamba Kendege, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa kwa sasa Mahakama za Mwanzo Mati, Mwimbi na Mwazye Wilayani Sumbawanga, hazitoi huduma za kimahakama na hivyo Wananchi wa maeneo hayo kulazimika kufuata huduma za mahakama katika Mahakama ya Mwanzo Sumbawanga. Kwa upande wa Mahakama ya Mwanzo Matai, Mahakama hii haitoi huduma kutokana na ukosefu wa Hakimu, kufuatia Hakimu wa Mahakama hiyo kusimamishwa kazi. Kuhusu Mahakama ya Mwanzo ya Mwimbi na Mwazye, ambazo zipo umbali wa kilometa 150 kutoka Sumbawanga Mjini, Mahakama hizi hadi kufikia mwezi Machi mwaka huu, zilikuwa zikitembelewa na Hakimu kutoka Mahakama ya Mwanzo Sumbawanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua adha wanayoipata Wananchi wa Mwimbi, Mwazye, Matai na sehemu nyinginezo nchini; na kwa kuzingatia uhaba wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo; Serikali ina mpango wa kuajiri Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo kwa kadiri uwezo utakavyoruhusu. Nichukue fursa hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, pindi tutakapoajiri Mahakimu wengine wapya, tutapelekea walau Hakimu mmoja katika mahakama hizo. Sanjari na hilo, kufuatia kuanzishwa kwa Mfuko wa Mahakama, ni imani yangu kuwa sasa Mahakama itaweza kujipangia vipaumbele vyake ikiwemo ununuzi wa vyombo vya usafiri vitakavyowezesha Mahakimu kutembelea Mahakama ambazo hazina Mahakimu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuchukua fursa hii, kumfahamishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali imejiandaa kikamilifu katika kuanzisha Wilaya mpya ya Kalambo. Serikali ilikwishaamua katika Wilaya zote mpya zinazoanzishwa, ujenzi wa majengo ya Serikali utajengwa sambamba na majengo ya Mahakama.

**MHE. JOSEPHAT S. KENDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Pamoja na majibu ya mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i)Kwa kuwa Waziri amekiri katika jibu lake kuwa adha ambayo Wananchi wanapata kutembea kilometa 150 siyo mchezo; na kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wengi wamekuwa wakiomba mahakama zijengwe katika Makao Makuu ya Kata; je, Serikali haioni kwamba ni wakati mwafaka kuhakikisha kwamba Makao Makuu ya Tarafa kwa maana ya Mwimbi, Kasanga pamoja na Matai, yanapewe kipaumbele katika kujenga Mahakama?

(ii)Kwa kuwa katika uanzishaji wa Wilaya Mpya ya Kalambo, viwanja vilishaanza kupimwa; Mheshimiwa Waziri haoni kwamba ni busara Wizara yake ikawahi kupata kiwanja ambacho kitakuwa sehemu ambayo ni *very strategic?*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Katika swali la kwanza, ni kweli kama nilivyosema kwamba, kwa kweli kufuata haki umbali wa kilometa 150 ni adha; na nimekiri kwamba ni adha kubwa sana na nimemuahidi kwamba, tukiajiri mahakimu, safari hii tutaangalia zile sehemu ambazo zina kero kubwa ikiwepo pamoja na Matai, Mwazye na kadhalika. Kuhusu ujenzi wa Mahakama, Serikali tuna nia nzuri sana kwamba, kila Tarafa tungekuwa na mahakama, lakini kutokana na uwezo wa kifedha unaotukumbuka, tunashindwa kutimiza azma hiyo. Kwa kuwa wametuanzishia Mfuko wa Mahakama na mwaka huu zimetengwa fedha, mwaka ujao na kuendelea tutajitahidi kila njia kuhakikisha kwamba,

tunajenga mahakama na tunakarabati zilizopo. Katika swali lake la pili kuhusu viwanja, wakati mwingine Wilaya mpya zikianzishwa majengo yote ya Serikali au mahitaji yote ya Serikali huwa yanajumuishwa pamoja na Magereza, Mahakama na kadhalika. Kwa hiyo, mimi nitahakikisha kwamba, tunafuatilia ili na sisi tupate kiwanja cha kuweza kujenga mahakama.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa ninaomba mkubaliane na mimi kwamba, muda wa maswali tulikuwa tunafidia zile dakika chache za kuwasilisha Hati Mezani. Unaona hapa hata Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, alikuwa amesimama kutaka kuomba, lakini alipoangalia muda akaniruhusu niendelee. Kama mnavyojua, Kanuni inasema akisimama tu lazima apate nafasi, lakini alipoona muda aliniambia hapana hawezi kufanya hivyo. Kwa hiyo, kwa kweli muda umetutupa mkono tuendelee na hoja iliyoletwa leo mbele yetu.

Sasa kabla hatujaendelea na ajenda inayofuata, ninayo matangazo kadhaa hapa Mezani; kwanza, ninaomba Waheshimiwa Wabunge, mtambue wageni waliopo katika jukwa la Mheshimiwa Mwenyekiti, ambao ni hawa wafuatao, kwanza kabisa ni familia ya Mheshimiwa Omar Rashid Nundu, inaongozwa na Ndugu Fatma Omar Nundu, ambaye ni mke wake, akiwa na Ndugu Felician Mariam Munda, ambaye ni mkwewe, lakini wakiwepo pia watoto wake wawili; ninaomba wote wawili wasimame kwa pamoja. Yupo pia *Engineer* Omar Abdallah Chambo, ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara hiyo na Naibu Katibu Mkuu, ambaye ni Ndugu John Thomas Mngodo. Huyu Mngodo sijui ni ndugu yake Mheshimiwa Rebeca, lakini ni hivyo hivyo tu koo zetu zimekuwa kubwa. Vilevile wapo Wenyeviti wa Bodi zilizoko chini ya Wizara hii; ningeomba Waheshimiwa Wenyeviti wa Bodi zote mngesimama kwa umoja wenu. Ahsanteni sana, karibuni sana.Pia wapo Wakuu wa Taasisi 16 zilizoko chini ya Wizara hii; ninaomba wote wasimame.

Waheshimiwa Wabunge, vilevile wapo wageni wa Mheshimiwa Samuel Sitta, Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ambao wa kwanza ni Mheshimiwa Jaji Harod Lusekela, Jaji Mkuu wa Mahakama ya Afrika Mashariki na Mheshimiwa John Luhangisa, Msajili wa Mahakama ya Afrika Mashariki. Wengine ni wageni wa Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami, Mbunge na Waziri wa Viwanda na Biashara, ambao ni Mheshimiwa Balozi Ali Mchumo, Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Mazao Duniani *(Common Fund For Commodities).* Karibu sana Balozi Mchumo. Vilevile wapo wageni wa Wizara na wageni pia wa Mheshimiwa Omar Nundu, ambao ni Wakurugenzi Wasaidizi na Maafisa 50 kutoka Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii; ningeomba hawa wote nao wasimame kwa umoja wao. Ahsante sana, karibuni sana na ninadhani mtatoa ushirikiano kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa siku hizi mbili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliokuja kujifunza Bungeni ni wanafunzi 40 na walimu watatu kutoka Shule ya Sekondari ya Nala Dodoma; ninaomba wanafunzi wa Nala wasimame. Wanafunzi 47 na walimu wanne kutoka Shule ya Dodoma Mlimani; ninaomba wanafunzi kutoka shule Dodoma Mlimani na walimu wasimame. Karibuni sana. *(Makofi)*

Matangazo ya kazi; nimeagizwa na Mheshimiwa Pindi Chana, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuwa, leo saa saba na robo mchana, kutakuwa na Kikao cha Kamati katika Ukumbi wa Pius Msekwa B. Kwa hiyo, Wajumbe wote mtakuwa na kikao Pius Msekwa B. Nimeagizwa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Juma Nkamia kwamba, niwaarifu Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, uwepo wa kikao leo saa saba na robo mchana, baada ya kusitisha shughuli za Bunge katika Ukumbi wa Msekwa C. Katiba na Sheria watakuwa Msekwa B, Maendeleo ya Jamii watakuwa Msekwa C.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo pia tangazo kutoka Ofisi ya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi na Ofisi ya Wabunge wa Chama cha CHADEMA; hili la Wabunge wa Chama cha Mapinduzi linaniomba niwatangazie Wabunge matokeo ya Uchaguzi wa Wabunge wanawake wa CCM, uliofanyika juzi kama ifuatavyo, aliyeshinda katika Uchaguzi huo; Katibu wa Wabunge Wanawake wa CCM ameshinda Mheshimiwa Mary Chatanda; Katibu Msaidizi wa Kamati hiyo Ndogo ya CCM ameshinda Mheshimiwa Mariam Kisangi; Mtunza Hazina Mheshimiwa Lolensia Bukwimba; Wajumbe wa Baraza Kuu la UWT Taifa, aliyeshinda wa kwanza ni Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid; wa pili ni Mheshimiwa Lucy Mayenga; wa tatu ni Mheshimiwa Pindi Hazara Chana; wa nne ni Mheshimiwa Maida Hamad; na watano ni Mheshimiwa Tauhida Cassian Galos Nyimbo.

Kamati ya Uongozi ya Wabunge hao ina Wajumbe wafuatao; wa kwanza Mheshimiwa Warid Bakar Jabu; na wa pili ni Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe. Kwa hiyo, hayo ndiyo matokeo ya Uchaguzi huu. Pia Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, ameniomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote wa CHADEMA kuwa, leo tarehe 3 Agosti, saa saba na robo; Waheshimiwa Wabunge, tulibadili Kanuni tutamaliza saa saba na robo, Mheshimiwa Mnyika siyo saa saba kamili, kutakuwa na kikao ghorofa ya pili, Jengo la Utawala, Ukumbi Namba 219. Waheshimiwa Wabunge wote wa CHADEMA, mnakumbushwa umuhimu wa kuhudhuria kikao hicho. Hilo ni tangazo kutoka kwa Katibu Mheshimiwa Mnyika.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo ambayo yalikuja hapa Mezani kwangu. Ili tuweze kuendelea na ratiba ya leo, ninaomba nimwite Katibu aweze kunipa mwongozo wa ratiba inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012
### Wizara ya Uchukuzi (Reli, Bandari na Usafiri wa Majini)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa ninamwita Mheshimiwa Omar Nundu, Waziri wa Uchukuzi, ili aweze kusoma mbele yetu Hotuba ya Makadirio ya Matumizi ya Waziri ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012. Mheshimiwa Waziri, tafadhali.

**WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, imechambua Taarifa ya Wizara ya Uchukuzi. Sasa ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema na Rahim, kwa kutujalia uhai na afya njema sisi waja wake na amani na utulivu wa taifa letu na kutuwezesha sote kushiriki Mkutano huu wa Bunge kujadili Bajeti ya Serikali ya msingi ya kuendeshea na kuchochea maendeleo ya nchi yetu na Wananchi wake. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kututunukia sisi Wabunge dhamana hii nyeti na adimu na adhim, tukijua kuwa kwake tutarejea na tutasailiwa kwayo. Ninayasema haya ndani ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kabisa, kwanza, kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Uchaguzi la Tanga lote; Mjini na Vijijini, kwa kuniamini, kunichagua na kuniridhia kuwa Mbunge wao na pia kuwa Kiongozi miongoni mwao, kushirikiana nao kwa dhati kujiendeleza sisi wenyewe katika Jimbo letu na nchi yetu kwa ujumla. Shukrani hizi ninazisambaza mahususi kwa watoto wote wa Tanga, Wana-ZINDABAA, Taifa changa linalojipanga, ambao mapenzi yao kwangu yalinipa nguvu na imani ya ziada na ushindi mkubwa katika kugombea Ubunge. Hapa ninamjumuisha mjukuu wangu Tahmeed Sena, kwa kampeni zake za lugha ya utoto bali nzito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa aina ya pekee, niruhusu nimshukuru ndugu yangu, rafiki yangu, mpenzi wangu na mwenzangu, ambaye pia ni mke wangu Fatma, kwa kuboresha maisha yangu kwa kiasi ambacho hakilipiki kwa miaka mingi sana ikiwemo miaka thelathini na nane ya ndoa. Pia kwa kuwatunza vyema wanetu Rashid, Nia, Omari, Danga na Fatma, katika mila, hulka na desturi za Kitanga na Kitanzania; na wao ninawashukuru kwa uvumilivu wao na kuniamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuniamini, kuniteua na kunipa dhamana ya kuiongoza Wizara ya Uchukuzi. Ninaahidi kuwa, nitajitahidi kwa kadiri ya uwezo wangu na kushirikiana na wenzangu Wizarani na nje ya Wizara, Serikalini kote na kwenye Taasisi zote. Ninaahidi pia kushirikiana na Taasisi za Kimataifa na Sekta Binafsi ndani na nje ya nchi, kutekeleza majukumu niliyopewa ili kusukuma mbele maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya nchi yetu na kutoa mchango wangu kikamilifu katika safari ya kuiweka nchi hii katika orodha ya nchi zilizoendelea duniani. Ahsante sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchukua fursa hii, kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa tena kwa haki zote kuendelea kuwa Rais wetu katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika nchini kote, mwezi Oktoba, 2010. Aidha, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pia, ninatoa pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Pongezi hizi pia ziende kwa Mheshimiwa Seif Sharif Hamad, kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mheshimiwa Balozi Seif Idd, kwa kuteuliwa kuwa makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kumpongeza Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Jimbo la Katavi, kwanza kwa imani kubwa ya wananchi wa Jimbo la Katavi waliomridhia kuwa Mbunge wao bila kupingwa na pili kwa kuendelea kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uteuzi wake unadhihirisha imani kubwa aliyonayo Mheshimiwa Rais kwake na imani ya wananchi kwake kupitia Bunge hili. Mimi binafsi ninafarijika sana kwa uongozi wake thabiti na nami pamoja na Wizara tuanahidi kumpa ushirikiano na usikivu usiotetereka kutekeleza maelekezo yake na kuchangia kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Spika kwa kuwa mwanamke wa kwanza kuwa Spika wa Bunge hili, nampongeza pia Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Jimbo la Kongwa kwa kuchaguliwa kwake kuwa Naibu Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kuchaguliwa kuwawakilisha wananchi katika majimbo yao na wengine kuteuliwa katika nafasi mbalimbali za uwakilishi, hii ni nafasi adimu na adhimu ambao kwayo wananchi wana mategemeo makubwa kwetu na wanatuangalia na kutufuatilia. Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara mbalimbali katika Serikali hii ya awamu ya nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu kuungana na Waheshimiwa Wabunge, kuwapongeza na kuwashukuru Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hotuba zao, hususan Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Jimbo la Katavi, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, Mbunge wa Jimbo la Kilosa na Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Stephen Masato Wassira, Mbunge wa Jimbo la Bunda na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu kwa hotuba zao zilizotoa mwelekeo wa jumla wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano kwa kipindi cha mwaka 2011/2012 – 2015/2016. Aidha, naomba kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba ya Waziri Mkuu na Mawaziri wengine walionitangulia kuwasilisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara zao kwa mwaka 2011/2012 Bungeni hapa. Maoni yao yatasaidia kuboresha mipango ya Serikali katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya Uchukuzi na Hali ya Hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru Kamati ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Peter Serukamba, Mbunge wa Jimbo la Kigoma Mjini kwa kukamilisha kazi ya kupitia, kujadili na kutoa ushauri kuhusu Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka 2011/2012. Wizara yangu itazingatia ushauri uliotolewa na Kamati ya Bunge ya Miundombinu na itaendelea kuyafanyia kazi maelekezo ya Kamati na yale yatakayotolewa na Bunge lako Tukufu wakati wa kujadili Bajeti hii. Ni imani yangu kuwa ushauri na maelekezo yao mazuri yataiwezesha Wizara kusahihisha dosari mbalimbali katika mipango na utendaji, kwa lengo la kuongeza ubora wa huduma zitolewazo na sekta ya Uchukuzi na Hali ya Hewa. *(Makofi)*

Naomba nitumie fursa hii kumpa pole nyingi Mheshimiwa Spika na familia yake kwa kuondokewa na mama yake mzazi. Ni dhahiri kuwa ulimpenda sana na sote tulimpenda na tulipenda kuendelea kuwa naye ila Mwenyezi Mungu amempenda zaidi na ameamua kumpumzisha. Aidha, napenda kutoa pole kwa Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa

Jimbo la Kongwa na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuondokewa na Bibi aliyemlea na kumsomesha na kudhihirisha kwa vitendo kuwa wanawake wanaweza.

Napenda pia nitumie nafasi hii kuwapa pole wafanyakazi na wanachama wote wa Chama cha Wafanyakazi wa Reli *(TRAWU)* kwa kuondokewa na kiongozi wao, Katibu wa Chama Ndugu Silvester Rwegasira. Kifo chake ni pigo kwa Chama cha Wafanyakazi wa sekta ya reli na Taifa kwa ujumla. Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutoa taarifa ya utendaji wa sekta ya Uchukuzi na Hali ya Hewa kwa kipindi cha mwaka 2010/2011, niruhusu kutumia fursa hii kutoa tathmini ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa kipindi cha mwaka 2005 - 2010 na hali ya utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2010 – 2015 katika Sekta za Uchukuzi na Hali ya Hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu muhtasari wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005 – 2010. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 ilielekeza Sekta za Uchukuzi na Hali ya Hewa kutekeleza yafuatayo:-

Ibara ya 45 inahusu usafiri na uchukuzi ambayo inaelekezea:-

(a) Kuendelea kuliimarisha Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* kwa lengo la kulipa uwezo wa kutoa huduma bora kwa bidhaa na abiria wa ndani na wa nchi jirani. Pia Shirika litaendelezwa kama mhimili wa mpango wa maendeleo wa eneo la Ukanda wa Kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Machi, 2010, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliamua kuchukua hisa asilimia 51 za *RITES* ndani ya *TRL.* Baada ya kuchukua hisa hizo, Serikali itamiliki *TRL* kwa asilimia 100 na kuchukua jukumu la kuiendesha Kampuni hiyo wakati akitafutwa mwekezaji mwingine. Maelezo zaidi kuhusu suala hili yametolewa katika hali ya utendaji na mapitio ya utekelezaji wa mpango wa sekta kwa mwaka 2010/2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tuliliarifu Bunge lako Tukufu kuhusu matengenezo na ukarabati wa njia ya reli uliokuwa unaendelea baada ya kuharibiwa na mvua kubwa zilizonyesha Desemba, 2009 na Januari, 2010 katika maeneo kati ya stesheni za Gulwe na Kilosa. Napenda kutoa taarifa kuwa matengenezo hayo yamekamilika. *(Makofi)*

(b) Kuendelea kuimarisha Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia *(TAZARA)* ili iweze kuhimili kwa uwezo mkubwa zaidi majukumu ya kuboresha huduma kwa bidhaa na abiria na kusaidia shughuli za uendelezaji wa mpango wa eneo la Ukanda wa Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa na Serikali za Tanzania na Zambia kwa pamoja zenye lengo la kuimarisha *TAZARA.* Desemba 2009, Mawaziri wenye dhamana ya reli ya *TAZARA* kutoka Tanzania na Zambia walifanya ziara ya kikazi nchini China kwa lengo la kuwasilisha maombi ya msaada wa fedha na ufundi kwa ajili ya kuendesha shughuli za *TAZARA.* Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ilikubali maombi hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kupitia Itifaki ya 14 imetoa mkopo wenye masharti nafuu wa jumla ya dola za Kimarekani millioni 39.9 sawa na shilingi bilioni 59.85 kwa lengo la kuimarisha utendaji wa *TAZARA.* Mkopo huu utasaidia kuongezea idadi ya injini, mabehewa, nyenzo mbalimbali za uendeshaji na mafunzo kwa wafanyakazi. Katika makubaliano hayo Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China pia imefuta nusu ya deni la ujenzi wa reli ya *TAZARA.* *(Makofi)*

Aidha, mwezi Agosti, 2010 Serikali hiyo ilituma timu ya wataalam kuja kutathmini changamoto na mahitaji ya *TAZARA* kwa nia ya kuboresha huduma. Timu hiyo kwa kushirikiana na wataalam wa Serikali za Tanzania na Zambia wameshafanya tathmini na sasa taarifa yao inasubiriwa. *(Makofi)*

(c) Kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa reli mpya za Arusha – Musoma, Isaka – Kigali na eneo la Ukanda wa Mtwara ambayo itaunganisha Bandari ya Mtwara, Songea, *Mbamba Bay,* Mchuchuma na Liganga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka miradi hii katika vipaumbele vya miradi ya maendeleo kutokana na umuhimu wa reli hizi katika kukuza uchumi wa nchi. Reli hizi ni kati ya miradi iliyo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia Mpango Kabambe wa Reli *(East African Railway Master Plan)* wenye lengo la kuboresha huduma za uchukuzi kwa njia ya reli katika nchi za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itajenga bandari mpya katika eneo la Mwambani Tanga; kuboresha reli kutoka Tanga – Arusha (kilomita 438); kujenga reli mpya kutoka Arusha hadi Musoma (kilomita 668) na kupanua bandari ya Musoma. Mradi huu ni wa ushirikiano kati ya Serikali ya Uganda na Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za awali za usanifu wa ujenzi wa reli ya Dar es Salaam - Isaka – Keza - Kigali na Keza – Gitega – Musongati zimeanza. Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)* imekubali kutoa shilingi bilioni 12.56 kugharimia kazi hiyo. Ujenzi wa reli itakayounganisha Bandari ya Mtwara, Songea, *Mbamba Bay,* Mchuchuma na Liganga ni sehemu ya mpango wa uendelezaji wa Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara ambao unatuunganisha na nchi za Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC).* Juhudi za kuwatafuta wawekezaji katika maeneo ya Mchuchuma na Liganga na zile za kuwatafuta wawekezaji wa ujenzi wa reli hii muhimu nazo pia zimeanza. *(Makofi)*

(d) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuimarisha bandari za Kigoma na Kasanga. Kazi ya kuondoa mchanga katika bandari ya Kigoma ili kuongeza kina cha maji na hivyo kuruhusu meli kutia nanga kwa usalama bandarini ilianza mwaka 2009 na inatarajiwa kukamilika Oktoba, 2011. Aidha, kazi ya kujenga chelezo katika bandari ya Kigoma iliyoanza Novemba, 2009 imekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bandari ya Kasanga, kazi za ukarabati wa barabara ya kuingia bandarini na uimarishaji wa gati zimekamilika. Aidha, kazi ya ujenzi wa maghala mawili ya kuhifadhia mizigo itakamilika mwishoni mwa mwezi Agosti, 2011. Kazi ya kujenga gati mpya ili meli mbili kubwa ziweze kufunga nanga kwa wakati mmoja imepangwa kufanyika katika awamu ya pili itakayoanza mwaka 2012/2013 kwa kushirikisha sekta binafsi. Kwa sasa Mamlaka imeajiri mtaalamu mshauri kufanya utafiti na kushauri jinsi ya kushirikisha sekta binafsi katika mradi huu. *(Makofi)*

(e) Kuvutia uwekezaji katika miundombinu ya usafiri na uchukuzi wa reli, barabara, maji na anga katika Kanda za Maendeleo ili kuimarisha biashara kati ya nchi yetu na nchi jirani na kuwafanya wawekezaji kuvutiwa na soko kubwa la bidhaa na huduma zitakazozalishwa. Aidha, uwekezaji katika kanda hizi utaiwezesha Tanzania kutumia nafasi yake ya kijiografia na kuendeleza wajibu wake wa kuzihudumia nchi jirani zisizo na bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea kuzingatia Sera ya Ushirikishwaji Sekta ya Umma na Binafsi pamoja na Sheria yake kuvutia wawekezaji katika sekta ya uchukuzi kupitia Kanda za Maendeleo. Katika kutumia fursa hiyo, mwaka 2010/2011 Wizara ilifanya mazungumzo na wawekezaji mbalimbali walioonesha nia ya kuwekeza katika miundombinu ya reli na bandari ikiwa ni moja ya mpango wa kuimarisha huduma za usafiri katika Kanda za Maendeleo za Tanga, Kati, Dar es Salaam na Mtwara. Kwa ujumla wawekezaji wengi wameonesha nia ya kuwekeza katika bandari zetu hasa ya Dar es Salaam na Tanga pamoja na reli mpya ya kutoka Mtwara hadi Mchuchuma na Liganga kwa lengo la kusafirisha makaa ya mawe na madini ya chuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uchukuzi kwa njia ya maji, Wizara kupitia Mamlaka ya usimamizi wa Bandari *(TPA)* imeanza kutekeleza mpango kabambe wa bandari *(Port Master Plan)* uliotayarishwa mwaka 2009. Miradi mbalimbali ya upanuzi wa huduma za bandari iliyobainishwa katika mpango huo imeanza kufanyiwa upembuzi yakinifu ikijumuisha bandari ya Mbegani, bandari ya Mwambani Tanga, bandari nchi kavu ya Kisarawe na ujenzi wa gati namba 13 na 14 katika bandari ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kusimamia Wakala wa Uwezeshaji wa Biashara na Uchukuzi katika Ukanda wa Kati *(Central Corridor Transit Transport Facilitation Agency - TTFA)* na Ukanda wa Dar es Salaam *(Dar es Salaam corridor)* ili kuleta ufanisi wa shughuli za kibiashara zinazopitishwa nchini mwetu na hivyo kuvutia wafanyabiashara kutumia miundombinu yetu ya uchukuzi. Tayari wakala hizo zimefanya uchunguzi *(baseline survey)* kujua vikwazo vya usafiri vilivyoko katika njia za usafiri kwa lengo la kuvipunguza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafiri wa anga, Wizara imeendelea kushawishi sekta binafsi kuwekeza katika uendelezaji wa miundombinu ya viwanja vya ndege vya Julius Nyerere, Mwanza, Kilimanjaro, Arusha, *Lake Manyara* na Kigoma. Pia kati ya watoa huduma 54 waliopewa leseni za kutoa huduma za usafiri wa anga, ni watoa huduma wawili tu wa Serikali ambao ni Kampuni ya Ndege ya Tanzania *(ATCL)* na Wakala wa Ndege za Serikali *(TGFA)* watoa huduma, waliobaki wote wanamilikiwa na sekta binafsi. Kampuni hizo ni pamoja na *Precision Air, Fly 540* na *Coastal Travel.* Kati ya mwaka 2009/2010 na 2010/2011, kampuni mpya kumi na tisa zilipewa leseni za kutoa huduma za usafiri wa anga. *(Makofi)*

(f) Kuendelea kuutengenezea mazingira mazuri ya kibiashara Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Dar es Salaam yatakayoweza kuuendeleza kuwa kiungo *(hub)* cha usafiri wa anga Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania *(TAA)* imekamilisha matengenezo ya miundombinu na uboreshaji wa mitambo katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere *(JNIA).* Matengenezo haya yaligharamiwa kwa pamoja kati ya Serikali za Uholanzi na Tanzania kwa kutoa shilingi bilioni 52 kila moja. Maeneo yaliyohusika ni ukarabati wa njia ya kurukia ndege, viungio vyake na maegesho ya ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuingia mikataba ya usafiri wa anga *(Bilateral Air Service Agreements - BASAs)* na nchi mbalimbali ili kuwezesha ndege zao kutua katika kiwanja hicho *(JNIA)* na ndege zetu kutoa huduma katika nchi zao. Katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2010, Tanzania imeingia au kupitia upya mikataba na nchi za Uturuki, Jordan, Misri, Zambia, Afrika ya Kusini, Burundi, Rwanda, India, Ujerumani, China, Ubelgiji, Kenya, Comoro, Msumbiji na Bahrain. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imeshaingia jumla ya mikataba 48 na nchi nyingine duniani. Uingiaji wa mikataba hii umewezesha safari za ndege kufanyika kati ya nchi yetu na nyingine, hivyo kuruhusu ushindani katika usafiri wa anga unaoletwa na mashirika mapya. Mashirika hayo mapya ni *Qatar Airways, Emirates* na *Egypt Air.* Aidha, mikataba iliyopitiwa upya imeruhusu safari zaidi *(frequencies)* na pia imeruhusu mashirika mengi kushiriki kutoka kila nchi *(multiple designation).* Faida nyingine ni sekta kutoa mchango zaidi katika Pato la Taifa na kuchangia kwenye akiba yetu ya fedha za kigeni zitokanazo na ongezeko la watalii na malipo ya huduma. *(Makofi)*

(g) Kukamilisha ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe na kuimarisha viwanja vya ndege vya Kigoma, Tabora na Shinyanga. Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Songwe unaendelea vizuri. Hadi sasa awamu mbili za utekelezaji wa mradi huo zimekamilika. Awamu ya kwanza ilianza mwaka 2001 na kukamilika mwaka 2004 na ilihusisha kazi ya uthamini na kulipa fidia ya mali za wananchi, kupima na kusawazisha eneo la kiwanja, usanifu wa miundombinu, ujenzi wa kituo cha umeme na ujenzi wa jengo la abiria awamu ya kwanza. *(Makofi)*

Awamu ya pili ilianza mwaka 2004 na kukamilika mwaka 2008 na ilihusu ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege, ujenzi wa maegesho ya ndege, barabara ya kiungio, barabara ya kuingia kiwanjani kutoka barabara kuu ya Mbeya – Tunduma kwa kiwango cha changarawe, ujenzi wa majengo ya kiwanja kama vile jengo la zimamoto, jengo la hali ya hewa na jengo la kuongozea ndege. *(Makofi)*

Kuhusu viwanja vya ndege vya Kigoma, Tabora na Shinyanga, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa viwanja hivyo zimekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 46 (f) inahusu mawasiliano; "kuimarisha uwezo wa utabiri wa hali ya hewa nchini kwa kutumia vyombo vya kisasa."

Huduma za hali ya hewa nchini ni muhimu kwa usalama na maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla. Serikali inaendelea na mchakato wa kukamilisha Sera ya Taifa ya Hali ya Hewa. Sera hii itatoa mwongozo katika kuimarisha, kuboresha na kutoa huduma za hali ya hewa nchini. Ili kuboresha huduma hizo, Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa imekamilisha ujenzi wa kituo cha hali ya hewa Mpanda na kufanya idadi ya vituo vikuu vya hali ya hewa nchini kufikia 28. Hatua hii inakaribia kukamilisha mpango wa kuwa na vituo vikuu 33 vya uchunguzi wa hali ya hewa nchini ifikapo mwaka 2015. *(Makofi)*

Mamlaka kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika imefanikiwa kufufua vituo 185 vya kupima mvua nchini na kuanzisha vituo vipya 211 pamoja na kuboresha vituo 496. Mafanikio mengine yanajumuisha utekelezaji wa mradi wa mabadiliko ya hali ya hewa unaofadhiliwa na Serikali ya Denmark. Aidha, kazi ya ujenzi wa kituo na ufungaji wa rada ya hali ya hewa katika eneo la Pugu, Dar es Salaam imekamilika. *(Makofi)*

Ibara ya 35 (f) inaelezea utalii; "Kulisaidia Shirika la Ndege la Tanzania ili lichukue nafasi yake ipasavyo ya kuwa Shirika la Ndege la Taifa *(National Flag Carrier)* kwa lengo la kuliwezesha Taifa kufaidika zaidi na mapato yatokanayo na Utalii."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuliwezesha Shirika la Ndege la Tanzania kuendelea kutoa huduma, Serikali ilitoa jumla ya shilingi bilioni 37.25 kati ya mwaka 2008/2009 na Juni 2011. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 3.97 zilitumika kulipia mishahara ya wafanyakazi wa kampuni kwa kipindi cha mwaka 2010/2011. Fedha nyingine zilitumika kulipia madeni ya kampuni, kugharamia zoezi la kupunguza wafanyakazi 155 walioachishwa kazi na shughuli za uendeshaji wa kampuni kama vile matengenezo ya ndege, mafunzo ya marubani, wahandisi na ununuzi wa vipuri. *(Makofi)*

Ibara ya 67; Usafiri na Uchukuzi; (a) Kuendelea kuimarisha Kampuni ya Reli Tanzania *(TRL)* kwa lengo la kuipa uwezo wa kutoa huduma bora kwa kusafirisha abiria na mizigo ya ndani na nchi jirani. Pia reli itaendelezwa kama mhimili wa mpango wa maendeleo wa eneo la Ukanda wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Wizara ilitekeleza kazi mbalimbali za kuboresha utendaji wa Reli ya Kati. Kazi hizo ni pamoja na kuendelea kuboresha miundombinu iliyoharibiwa na mvua katika maeneo ya kati ya Kilosa na Gulwe, kuendelea kubadilisha reli zenye uzito mdogo na kuweka zenye uzito wa ratili 80 kwa yadi kwa lengo la kuiongezea uwezo. *(Makofi)*

(b) Kushirikiana na Serikali za Rwanda na Burundi, kuanza ujenzi wa reli mpya kutoka Dar es salaam kwenda Kigali (Rwanda) na Musongati (Burundi).

Serikali za Tanzania, Rwanda na Burundi zimekubaliana kwa pamoja kutekeleza mradi huu mkubwa. Awamu ya kwanza ya mradi huu ambayo ni upembuzi yakinifu ilikamilika Desemba, 2009. Usanifu wa kina wa uendelezaji wa reli kutoka Dar es Salaam – Isaka – Keza - Kigali (kilomita 1,464) na Keza - Musongati (kilomita 197) unatarajiwa kuanza kufanyika katika mwaka 2011/2012. Serikali zote tatu zinaendelea kutafuta wawekezaji kwa ajili ya ujenzi wa reli hii. *(Makofi)*

(c) Kuimarisha Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia *(TAZARA)* kwa kuboresha miundombinu ya reli na kuendeleza juhudi za kubadilisha mfumo wa uendeshaji wa shirika kwa lengo la kuboresha huduma za abiria na mizigo.

Serikali za Tanzania, Zambia na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China zimeendelea na juhudi za kukarabati na kuboresha miundombinu ya reli ya *TAZARA.* Juhudi zimefanyika katika kukarabati maeneo korofi ya reli hususan kilomita 79 kati ya stesheni za Kitete na Mpanga zilizopo

kati ya Mlimba na Makambako. Aidha, Serikali za Tanzania na Zambia zimeteua timu ya wataalamu kutoka Tanzania, Zambia na nchi nyingine za Afrika ili kushauri kuhusu kutatua matatizo yanayoikabili *TAZARA. (Makofi)*

(d) Kujenga na kuimarisha miundombinu ya Reli na Bandari kwa kukamilisha mtandao wa reli na kuunganisha bandari ya Tanga na reli ya Arusha – Musoma.

Mkataba wa Makubaliano *(MoU)* baina ya Serikali za Tanzania na Uganda kuhusu mradi wa ujenzi wa reli ya Tanga – Arusha – Musoma na bandari za Mwambani, Musoma na Kampala umesainiwa tarehe 29 Juni, 2011 mjini Dodoma. Mazungumzo kati ya Serikali za Tanzania na Uganda kuhusu upatikanaji wa fedha za kutekeleza mradi huu yanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa ujenzi wa bandari ya Mwambani umeanza kutekelezwa ambapo jumla ya hekta 174 za ardhi zimenunuliwa kwa ajili ya ujenzi wa bandari hiyo. Kazi ya kufanya upembuzi yakinifu inaendelea na itakamilika Novemba, 2011. Mradi huu utatekelezwa sambamba na mradi wa ujenzi wa reli ya Tanga - Arusha - Musoma na bandari ya Musoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya upembuzi yakinifu wa kuboresha reli ya Tanga – Arusha inatarajiwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2011/2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kujenga reli mpya kati ya Arusha na Musoma. Upembuzi yakinifu na maandalizi ya michoro kwa ajili ya ujenzi wa reli ya Arusha – Musoma yanatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2011/2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upembuzi yakinifu wa kuboresha bandari ya Musoma unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2011/2012.

(e) Kuanza ujenzi wa reli ukanda wa Mtwara kwa kuchukua hatua za maandalizi ya mradi wa ujenzi wa reli ya Mtwara – Mchuchuma- Liganga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kuunganisha bandari ya Mtwara na machimbo ya Mchuchuma na Liganga imekamilika. Kazi hii iligharamiwa na Shirika la Maendeleo la Japan *(JICA)*. Hatua za kumtafuta mwekezaji kwa ajili ya utekelezaji wa mradi zinaendelea. *(Makofi)*

(f) Kuendeleza huduma za uchukuzi kwenye maziwa kwa kuimarisha bandari za Kigoma, *Mbaba Bay,* Mwanza, Bukoba na Nansio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kuondoa mchanga katika bandari ya Kigoma kwa kutumia mtambo wa kuondoa mchanga inaendelea na itakamilika Desemba, 2011. Kazi ya ujenzi wa sakafu katika eneo la kuhudumia abiria katika Bandari za Mwanza Kaskazini ilikamilika Juni, 2011 na Bukoba inaendelea na inatarajiwa kukamilika Septemba, 2011. Aidha, kazi za ujenzi wa uzio katika Bandari za Mwanza Kaskazini na Kusini na jengo la abiria katika Bandari ya Nansio zilikamilika Oktoba, 2010. Kazi ya kuboresha Bandari ya *Mbamba Bay* itaanza katika mwaka wa fedha 2011/2012. *(Makofi)*

(g) Kuboresha huduma za uchukuzi katika Bandari za Mwambao na kupanua Bandari za Dar es Salaam na Mtwara.

Mikakati ya kupanua Bandari ya Dar es Salaam ni pamoja na ujenzi wa gati namba 13 na 14 na upanuzi wa lango la bandari. Kazi ya usanifu wa kina ilikamilika Oktoba, 2009 na kazi ya kufanya tathmini ya athari za mazingira ilikamilika Juni, 2010. Serikali ipo katika mazungumzo na wawekezaji na taasisi mbalimbali za fedha ili kuona uwezekano wa kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bandari ya Mtwara, mikakati wa kuendeleza bandari ni pamoja na kuimarisha maeneo ya kufanyia kazi, miundombinu kama magati na ununuzi wa vifaa.

Mikakati hii imezingatia mahitaji ya kuhudumia shehena za korosho, ufuta na miradi iliyoainishwa katika Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara pamoja na shughuli za utafutaji mafuta na gesi. Aidha, ardhi yenye ukubwa wa hekta 2,647 katika maeneo ya Ng'wale, Msemo na Msanga Mkuu ilinunuliwa mwaka 2004. Eneo hili ni nje ya eneo la bandari ya sasa lenye ukubwa wa hekta 70. Hivi sasa mtaalamu mshauri anafanya upembuzi yakinifu kubaini mahitaji ya upanuzi wa Bandari ya Mtwara na kushauri matumizi sahihi ya ardhi. Katika kipindi cha mwaka 2011/2012, jumla ya shilingi milioni 6,460 zimetengwa na *TPA* kwa ajili ya kuendeleza bandari ya Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari ya Bagamoyo ulikamilika Julai, 2010. Utafiti umependekeza ujenzi wa bandari kubwa ya kisasa eneo la Mbegani, Bagamoyo kwa ajili ya kuhudumia meli kubwa za kontena, shehena mchanganyiko na magari. Mradi utatekelezwa kwa kushirikisha sekta binafsi na juhudi za kumpata mwekezaji zinaendelea. Tayari hekta 518 zimetengwa kwa ajili ya mradi huu na hekta 2,000 za nyongeza zimeombwa kutoka Mamlaka ya *EPZA. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya ujenzi wa gati la Mafia inaendelea na ujenzi unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2011. Kuhusu bandari ya Lindi, kazi ya uchunguzi wa chanzo cha kujaa mchanga imekamilika na kupendekeza kujenga gati jipya la mita 100 kuingia baharini. Aidha, kazi ya uchunguzi wa vina vya maji imekamilika na ujenzi wa gati hili umepangwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2011/2012. *(Makofi)*

(h) Kutekeleza Programu ya Uwekezaji katika sekta ya uchukuzi kwa kuvutia wawekezaji binafsi katika uendeshaji wa sekta ya uchukuzi kwa kuzingatia Sera ya Sheria ya Ushirikishaji wa Sekta Binafsi *(PPP).*

Wizara imeendelea kutekeleza Awamu ya Kwanza ya Programu ya miaka kumi ya uwekezaji katika sekta ya uchukuzi *(Transport Sector Investment Programme – TSIP).* Kwa ujumla utekelezaji wa miradi iliyopo kwenye programu hii umeendelea kutegemea fedha za Serikali na washirika wa maendeleo. Mchango wa sekta binafsi katika utekelezaji wa programu hii bado ni mdogo. Lengo la Wizara katika mwaka 2011/2012 ni kuongeza juhudi katika kuvutia wawekezaji wengi zaidi kutoka ndani na nje ya nchi ili kutekeleza miradi ya sekta ya uchukuzi. Awamu ya kwanza ya *TSIP* itakamilika Juni, 2012 na maandalizi ya awamu ya pili ya programu hiyo *(TSIP – Phase 2)* yameanza ili utekelezaji wake uanze Julai, 2012. Aidha, ushirikishwaji wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya uchukuzi iliyopo katika programu hiyo utazingatia sera ya ushirikishaji wa sekta ya umma na binafsi pamoja na sheria yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuimarisha usafiri wa anga ili uchangie kwenye Pato la Taifa kwa kuchukua hatua zifuatazo; kuimarisha na kuboresha kiwanja cha *JNIA* kwa kujenga jengo jipya la abiria na majengo mengine ya huduma za abiria. Ujenzi wa jengo jipya la watu mashuhuri *(VIP Building)* katika kiwanja cha ndege cha *JNIA* umekamilika. Aidha, mchakato wa kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la abiria *(Terminal III)* unaendelea. Usanifu kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa jengo la abiria *(Terminal II)* umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kuandaa mpango kabambe wa usafiri wa anga *(Civil Aviation Master Plan - CAMP)* inaendelea. Lengo la mpango huu ni kufanya tathmini kuhusu uwezo wa sasa wa utoaji huduma za usafiri wa anga na mahitaji ya huduma hiyo na kuweka mikakati ya kuhakikisha kwamba huduma zinazotolewa zinakidhi mahitaji na matarajio ya wadau katika sekta ndogo ya usafiri wa anga. Mpango huu wa miaka 25 ijayo utatoa mapendekezo ya namna ya kuboresha utoaji huduma, ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu ya viwanja vya ndege ili vikidhi mahitaji ya sasa na ya siku zijazo. Utafiti wa awali kuhusu mpango huu ulikamilika mwishoni mwa mwaka 2010. Aidha, hadidu za rejea za kuandaa upembuzi yakinifu kwa ajili ya utayarishaji wa *CAMP* zimeandaliwa na kuwasilishwa Benki ya Dunia ili kupata idhini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kukamilisha ujenzi wa kiwanja kipya cha Kimataifa cha Ndege cha Songwe (Mbeya). Ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege cha Songwe (Mbeya) unatarajiwa kukamilika Desemba, 2011. Kwa sasa kazi zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa jengo la abiria,

kituo cha zimamoto, kituo cha kuongozea ndege, uwekaji wa lami kwenye barabara ya kutua na kuruka ndege na majengo mengine ya kiwanja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuanza ujenzi wa kiwanja kipya cha Kimataifa cha ndege cha Msalato (Dodoma). Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa kiwanja cha ndege cha Msalato. Kazi hizo zilikamilika mwaka 2007/2008 kwa msaada wa Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika *(BADEA).* Aidha, zoezi la ulipaji fidia kwa wakazi waliokuwa wanaishi katika eneo litakalojengwa kiwanja kipya cha Msalato limekamilika. Serikali imeanza kufanya majadiliano na wadau wa maendeleo na taasisi mbalimbali za fedha kama vile Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika *(BADEA)* na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)* ili kupata fedha za ujenzi wa kiwanja ambazo zinafikia dola za Kimarekani milioni 105. Kati ya wadau hawa, Benki ya Maendeleo ya Afrika imeonyesha nia ya kutoa mkopo wa muda mrefu kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja hicho na mazungumzo bado yanaendelea. Ujenzi utaanza mara fedha zitakapopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kufanyia upembuzi na usanifu Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Bagamoyo. Wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege tayari imepata eneo la ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege eneo la Zinga, Bagamoyo lenye ukubwa wa hekta 8,000. Kazi zinazoendelea kwa sasa ni upimaji wa mipaka na tathmini ya mali zilizopo katika eneo hilo. Kazi hizi zinafanywa kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo. Kazi za kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Bagamoyo zitaanza katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kiwanja cha ndege cha Mwanza imekamilika. Mchakato wa kumpata mkandarasi umeanza na zabuni za ujenzi zilifunguliwa Julai, 2011. Kazi inayoendelea ni uchambuzi wa zabuni ili kumpata mkandarasi wa ujenzi. Kuhusu kiwanja cha ndege cha Mtwara, kazi ya uimarishaji wa kiwanja imeanza ikiwa ni pamoja na ukarabati wa jengo la abiria na ujenzi wa uzio. Kazi hizi zinatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2011/2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kukamilisha uboreshaji wa viwanja vya ndege vya Mafia, Arusha, Mpanda, Sumbawanga, Bukoba, Kigoma, Tabora na Shinyanga. Kazi ya kuboresha miundombinu ya viwanja vya ndege vilivyotajwa inaendelea. Katika kiwanja cha ndege cha Bukoba, ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege kwa kiwango cha lami utaanza mwaka 2011/2012. Kazi nyingine zitakazofanyika katika kiwanja hicho ni ujenzi wa maegesho ya ndege na viungio vyake kwa kiwango cha lami pamoja na ujenzi wa jengo jipya la abiria. Katika viwanja vya Mpanda, Tabora, Kigoma, Arusha na Mafia kazi zitakazofanyika katika mwaka 2011/2012 ni ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege kwa kiwango cha lami. Kuhusu viwanja vya ndege vya Shinyanga na Sumbawanga, Wizara inaendelea kutafuta fedha ili viweze kujengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuunda upya Shirika la Ndege la Taifa kwa kushirikisha sekta binafsi. Wizara inaendelea na tathmini ya kina kwa lengo la kutafuta mwekezaji binafsi ili kushirikiana na Serikali katika kuunda upya Shirika la Ndege la Taifa. Hadi sasa Wizara imefanya mazungumzo na Kampuni mbalimbali ili ziweze kuwekeza katika Kampuni ya *ATCL.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 68 inazungumzia kuimarisha uwezo wa utabiri wa hali ya hewa nchini, pia kukamilisha na kutekeleza Sera ya Taifa ya Hali ya Hewa. Taratibu za kukamilisha Sera ya Taifa ya Hali ya Hewa zinaendelea na itakamilika Desemba, 2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuiongezea uwezo Mamlaka ya Hali ya Hewa *(TMA)* ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Serikali inaendelea kuboresha Chuo cha Hali ya Hewa cha Kigoma ili kuongeza uwezo wa kitaalamu wa Mamlaka. Aidha, ununuzi wa vifaa na mitambo ya kisasa ya kupima na kutabiri hali ya hewa upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendelea kutanua mtandao wa rada hadi kufikia rada saba nchi nzima. Lengo la Serikali ni kununua rada saba za hali ya hewa na kuzifunga katika maeneo mbalimbali ya nchi ili kuimarisha utabiri wa hali ya hewa hapa nchini. Rada moja tayari imefungwa

mkoani Dar es Salaam na rada ya pili itanunuliwa katika mwaka wa fedha 2011/2012 na itafungwa Mwanza. Rada nyingine zitafungwa katika mikoa ya Kigoma, Dodoma, Mbeya, Mtwara na Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuendeleza miundombinu ya kutoa utabiri na mawasiliano katika Kituo Kikuu cha Utabiri wa Hali ya Hewa. Serikali imekamilisha ununuzi wa mitambo na vifaa kwa ajili ya Kituo cha Hali ya Hewa cha Mpanda na kimeanza kufanya kazi. Aidha, Serikali inatarajia kuanza ujenzi wa Kituo cha Hali ya Hewa cha Babati, Mkoani Manyara na Kituo cha Hali ya Hewa na Kilimo *(Agromet station)* huko Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuboresha mfumo wa kutoa taarifa za hali ya hewa mapema na kuhakikisha kuwa taarifa hizo zinafika kwa watumiaji mapema. Serikali ipo katika mchakato wa kuboresha mfumo wa mawasiliano utakaohakikisha kuwa taarifa za hali ya hewa zinawafikia watumiaji kwa wakati kuanzia mwaka 2011/2012. Uboreshaji huo unahusisha mitambo ya *Transmet, Synergy* na *RETIM,* pamoja na kubadilisha mfumo wa zamani wa kuhifadhi data (kutoka *CLICOM* kwenda *CLIDATA).* Studio ya Mamlaka itaboreshwa kwa kupatiwa vifaa vya kisasa. Vilevile mtandao wa mawasiliano utaimarishwa ili vituo vyote vya hali ya hewa viunganishwe katika mtandao huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenekiti, kuhusu hali ya utendaji na mapitio ya utekelezaji wa mpango wa sekta kwa mwaka 2010/2011 na malengo ya mwaka 2011/2012, ubunifu na utekelezaji wa Sera za Sekta. Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia sera za kisekta. Sera hizo ni pamoja na Sera ya Taifa ya Uchukuzi (2003) ambayo kwa sasa inafanyiwa mapitio kwa lengo la kuiwezesha kuendana na mahitaji ya sasa na ya baadaye ya sekta ya uchukuzi. Mapitio ya sera hii yanatarajiwa kukamilika Juni, 2012. Aidha, Wizara imeendelea kukamilisha Sera ya Taifa ya Hali ya Hewa ili kukidhi haja ya kutoa huduma bora za hali ya hewa. Sera hizi zitaendelea kutumika kama miongozo ya kusimamia maendeleo ya sekta pamoja na kutoa taratibu za uwekezaji katika kufikia malengo ya muda mfupi, kati na muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya sera ya uchukuzi ni pamoja na kuunganisha maeneo yote ya nchi yetu na nchi jirani kwa njia kuu za uchukuzi zenye ufanisi, tija, gharama nafuu na kuhakikisha kuwa bandari zetu kuu zinakuwa lango kuu la biashara kwa nchi yetu na nchi jirani zinazotumia bandari hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafiri wa anga, malengo ya muda wa kati ni pamoja na kuishirikisha sekta binafsi ili iweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi na kuvifanya viwanja vya ndege vya Kimataifa vya Julius Nyerere na Kilimanjaro kuwa viungo vya usafiri wa anga Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. *(Makofi)*

Wizara pia itaendelea kuweka mikakati ya kuyavutia makampuni yenye uwezo ili yaanzishe mashirika ya ndege hapa nchini yatakayoendeshwa kwa misingi ya gharama nafuu ili wananchi wengi waweze kutumia usafiri huu. Aidha, Serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri ili mashirika ya ndege ya nje yaweze kutumia viwanja vya *JNIA* na *KIA. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sekta ya reli, mkakati wa muda mfupi unaotekelezwa ni kuongeza uwezo wa reli kwa kuondoa reli yenye uzito mdogo (ratili 56.12 kwa yadi) na kuweka yenye uzito mkubwa (ratili 80 kwa yadi). Serikali ina mkakati wa muda mrefu wa kuiboresha reli ya kati kwa kuibadili njia yake kutoka kwenye hali ya sasa yenye njia nyembamba na yenye uwezo mdogo na kuifanya iwe pana na yenye uwezo mkubwa. *(Makofi)*

Suala la urekebishaji wa taasisi za Wizara na ushirikishwaji wa sekta binafsi, kufuatia utendaji usioridhisha wa Kampuni ya Reli Tanzania, Serikali iliamua kuhamisha hisa zote za *RITES* kwenda Serikalini. Ili kufikia azma hiyo, Serikali ilitoa ridhaa ya kujadiliana na *RITES* ili kununua hisa hizo. Kwa sasa hati ya makubaliano ya wanahisa *(Deed of Settlement)* kuhusu kuondoka kwa *RITES* na namna *TRL* itakavyolipa madeni yao imekamilika. Makubaliano kati ya Serikali na Shirika la Fedha la Kimataifa *(IFC)* lililokopesha fedha *TRL* kuhusu namna ya kulipa mkopo huo nayo yamefikiwa. Kwa mantiki hiyo, mkataba kati ya Serikali na *RITES* utafutwa na hivyo Serikali itamiliki kampuni ya *TRL* kwa asilimia mia moja. Changamoto inayoikabili Serikali katika utekelezaji wa

hatua hii ni madeni makubwa inayodaiwa Kampuni ya *TRL* na uchakavu wa miundombinu, injini za treni, mabehewa ya abiria na mizigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *TAZARA,* katika hatua ya kuishirikisha sekta binafsi kuendesha shughuli za *TAZARA,* mwezi Agosti, 2010 Serikali ya China ilituma timu ya wataalam kufanya tathmini ya hali halisi ya miundombinu ya reli na menejimenti ili kutoa mapendekezo ya jinsi ya kurekebisha uendeshaji wa reli. Timu hiyo kwa kushirikiana na wataalam kutoka Zambia na Tanzania walifanya kazi na sasa ripoti ya tathmini yao inasubiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utendaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania umekuwa katika hali ya kutoridhisha kwa muda mrefu. Serikali kwa sasa inachukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa huduma za Kampuni zinarejeshwa. Serikali pia itapitia upya muundo wa Kampuni na kufanya marekebisho ili Kampuni iweze kujiendesha kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA), Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuiwezesha UDA kuwa na mtaji wa kujiendesha yenyewe. Wawekezaji mbalimbali wamekuwa wakijitokeza ili kuendesha UDA. Hata hivyo, wawekezaji hao wamekuwa hawakidhi viwango vinavyotakiwa na hivyo kushindwa kukabidhiwa uendeshaji wa Shirika. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali itamwajiri mtaalam mwelekezi wa kuandaa nyaraka muhimu kama vile thamani ya mali na kutafuta thamani ya hisa ili kujitayarisha kwa zoezi la uuzaji wa hisa za Serikali katika Shirika la UDA mwekezaji mahiri atakapopatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imezindua Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano wa utekelezaji wa Dira ya Taifa 2025. Mpango huo unahusisha sekta muhimu katika ukuaji wa uchumi ikiwa ni pamoja na Sekta ya Uchukuzi. Katika mpango huo, sekta ndogo za Reli, Bandari na Viwanja vya Ndege zimepewa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uchukuzi imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali. Ili kuziibua na kuzijadili changamoto hizo, Wizara imekuwa ikiandaa kongamano la sekta ya uchukuzi *(Joint Infrastructure Sector Review – JISR).* Kongamano hili limekuwa likifanyika kila mwaka na kwa mwaka jana lilifanyika mwezi Septemba, 2010 likiwa ni kongamano la nne. Kongamano la tano linatarajiwa kufanyika mwezi Oktoba, 2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kongamano hili ni kuwaleta pamoja wadau wote wa sekta ya uchukuzi ikiwa ni pamoja na Serikali, washirika wa maendeleo, nchi jirani zinazotumia bandari zetu, sekta binafsi, vyama vya kiraia, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, taasisi za kitaaluma na watu binafsi kwa lengo la kujadili na kutafutia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la huduma za uchukuzi kwa njia ya nchi kavu na huduma za usafiri kwa njia ya barabara. Mchango wa sekta binafsi umeendelea kuongezeka katika kutoa huduma ya usafiri wa nchini. Hali ya ushindani imesaidia kuinua kiwango cha ubora wa huduma na kurahisisha upatikanaji wake. *SUMATRA* kwa upande wake imeendelea kuboresha utaratibu wa utoaji leseni kwa kusogeza huduma karibu zaidi na wateja. Hivi sasa fomu za kuomba leseni zinapatikana kwenye tovuti ya Mamlaka *www.sumatra.or.tz. (Makofi)*

Aidha, ofisi za *SUMATRA* zipo katika mikoa ya Dar es Salaam, Iringa, Tanga, Kigoma, Dodoma, Arusha, Tabora, Mwanza, Rukwa, Mbeya, Kilimanjaro, Kagera, Mtwara na Morogoro. Jitihada zinafanyika kufungua ofisi za *SUMATRA* katika mikoa iliyosalia ifikapo mwaka 2013/2014 ili kusogeza huduma karibu zaidi na wateja. Katika kipindi cha mwaka 2010/2011, jumla ya leseni 33,887 na ratiba 3,721 za mabasi ya abiria zilitolewa ikilinganishwa na leseni 28,771 na ratiba 3,214 zilizotolewa katika kipindi cha mwaka 2009/2010. Ongezeko hili limechangiwa na hatua zilizochukuliwa za kusogeza huduma karibu na wasafirishaji pamoja na ongezeko la vyombo vya usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarika kwa usafiri wa umma na hasa kutumia mabasi makubwa mijini kutavutia watu wenye magari madogo ya binafsi kutumia usafiri wa umma na hatimaye kupunguza msongamano. Hatua nyingine za kupunguza msongamano katika Jiji la Dar

es Salaam ni mtambuka, hivyo Wizara inashirikiana na Wizara ya Ujenzi, Halmashauri ya Jiji na wadau wengine kutekeleza mikakati ya pamoja katika kutatua tatizo hili. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na *SUMATRA* iliendelea na juhudi za kupunguza magari madogo ya abiria (vipanya) katika Jiji la Dar es Salaam kwa kusimamisha utoaji wa leseni za kuingia katikati ya Jiji la Dar es Salaam. Hatua hii imesaidia kuingiza mabasi makubwa katika usafiri wa umma Jijini Dar es Salaam ambapo jumla ya mabasi makubwa 4,574 yalisajiliwa hadi Juni, 2011 ikilinganishwa na mabasi 4,182 yaliyosajiliwa kufikia Juni, 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012 *SUMATRA* itaendelea kudhibiti usafiri wa abiria kwa kuboresha utoaji leseni, ratiba na kuhimiza utoaji wa huduma ya usafiri kwa kutumia makampuni badala ya watu binafsi. Mamlaka pia itaendelea kudhibiti gharama za tozo mbalimbali kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafir na uchukuzi wa reli, katika mwaka 2010/2011, Kampuni ilisafirisha jumla ya abiria 290,358 ikilinganishwa na abiria 543,001 waliosafirishwa mwaka 2009/2010 na hivyo kuwa na upungufu wa abiria 252,643 sawa na asilimia 47. Katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Kampuni ilisafirisha tani 256,190 za mizigo ikilinganishwa na tani 453,493 zilizosafirishwa mwaka 2009 na hivyo kuwa na upungufu wa tani 197,303 sawa na asilimia 44.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kurejesha hali ya miundombinu ya reli katika hali yake ya awali baada ya mafuriko yaliyoharibu kabisa njia ya reli katika eneo kati ya stesheni za Kilosa na Gulwe imekamilika. Kazi inayoendelea kwa sasa katika eneo hilo ni kufanya matengenezo ya kudumu yenye lengo la kuzuia madhara ya mafuriko katika miundombinu ya reli. Kazi hii inahusisha kurekebisha mwelekeo wa Mto Mkondoa kwa kujenga matuta, kuimarisha kingo za tuta la reli katika sehemu hatarishi, kujenga madaraja na kuhamisha njia ya reli ya urefu wa kilomita 1.1 ili kukwepa mkondo wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa muda mfupi wa uboreshaji wa huduma za reli ya Kati, mwezi Mei, 2011 Wizara yangu ilifanya mazungumzo na Benki ya Dunia kwa lengo la kupatiwa fedha za dharura za kutekeleza mpango wa kuboresha huduma za Reli ya Kati. Mpango huu utajumuisha ukarabati wa miundombinu ya reli, ununuzi wa vichwa vya treni na mabehewa. Taratibu za makubaliano kati ya Benki ya Dunia na Serikali zinatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Desemba, 2011. Aidha, taratibu za kumpata mtaalam mwelekezi wa kufanya utafiti kuhusu mahitaji ya Reli ya Kati na kuandaa mpango kazi wa uboreshaji wa reli hiyo chini ya mradi wa *Transport Sector Support Project (TSSP)* unaogharamiwa na Benki ya Dunia zimeanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya ujenzi wa kituo cha kuhifadhia makasha *(ICD)* cha Shinyanga imekamilika mwezi Mei, 2011 na kugharimu shilingi bilioni 3.665. Ujenzi wa Kituo cha Mwanza unatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2011/2012 na kiasi cha shilingi bilioni 2.5 kimetengwa. Uboreshaji wa Kituo cha Ilala utaanza baada ya kukamilika kwa Kituo cha Mwanza. Aidha, mitambo mitano ya kupakua na kupakia makasha kwa ajili ya vituo vya Shinyanga, Mwanza na kile cha Ilala ilikwishawasili Aprili 2011 ambapo mtambo mmoja utakuwa kwa ajili ya kituo cha Ilala, mitambo miwili kwa ajili ya kituo cha Shinyanga na mitambo miwili kwa ajili ya kituo cha Mwanza. Mitambo hiyo mitano kwa pamoja ina thamani ya shilingi bilioni 3.92 zilitolewa na Serikali ya Ubelgiji kupitia shirika lake la *Belgian Technical Cooperation (BTC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012 Serikali za Tanzania, Rwanda na Burundi zinatarajia kufanya upembuzi wa kina wa uendelezaji wa reli kutoka Dar es Salaam - Isaka – Kigali na Isaka - Keza - Musongati kwa kiwango cha Kimataifa. Tathmini ya zabuni kwa ajili ya kumpata mshauri mwelekezi atakayefanya upembuzi huo zinaendelea. Aidha, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Uganda inatarajia kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa reli ya kutoka Arusha – Musoma na ukarabati wa reli kutoka Tanga – Arusha ikiwemo uendelezaji wa Bandari za Mwambani (Tanga), Musoma na Kampala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *RAHCO* inatarajia kufanya upembuzi yakinifu wa reli kutoka Tabora – Kigoma, Isaka – Mwanza, Kaliua – Mpanda, Manyoni – Singida, Ruvu – Mruazi

kwa lengo la kuinua kiwango cha reli ya Kati ili kifanane na kile cha reli inayotarajiwa kujengwa kati ya Dar es Salaam – Isaka - Kigali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha hali ya *TAZARA,* kazi zilizofanyika katika mwaka 2010/2011 ni pamoja na kuboresha sehemu korofi za miundombinu ya reli ambazo zina mmomonyoko wa udongo katika eneo la Mlimba – Makambako. Mradi wa kukarabati na kufufua injini za treni ambao ulianza mwaka 2007 katika karakana ya Mbeya, umewezesha kukarabati jumla ya injini za treni 13 na mabehewa 300 ya mizigo. Aidha, *TAZARA* imeendelea kuboresha maeneo yaliyokuwa yamewekewa vizuizi mwendo kwa kubadilisha mataruma mabovu na kufunga mengine mapya katika maeneo hayo. Jumla ya madaraja 163 tayari yameondolewa vizuizi mwendo na mataruma mapya 2,401 ya mbao yamefungwa kwenye madaraja na makutano ya reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia itifaki ya 14 kati ya Serikali za Tanzania, Zambia na China, *TAZARA* imepatiwa mkopo usio kuwa na riba wenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 39.9 sawa na shilingi bilioni 59.85. Mkopo huo utatumika kuendelea kuimarisha *TAZARA* katika maeneo kumi na moja ikiwamo ununuzi wa vichwa vipya vya treni sita, ukarabati wa vichwa vingine tisa vya treni, ununuzi wa mabehewa 90 mapya ya mizigo, ukarabati wa Kreni nne za mizigo na okoa mbili, ununuzi wa malighafi ya utengenezaji wa mataruma ya reli, ununuzi wa vipuri vya mabehewa 1,200 ya mizigo, na kugharamia mafunzo kwa wafanyakazi wa kada mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Mamlaka ilisafirisha shehena jumla ya tani 533,964 ambayo ni wastani wa tani 44,497 kwa mwezi ikilinganishwa na tani 522,966 zilizosafirishwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010 sawa na wastani wa tani 43,580 kwa mwezi. Utendaji huu ni ongezeko la asilimia 2.1 ikilinganishwa na kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, *TAZARA* ilisafirisha jumla ya abiria 787,666 ambayo ni wastani wa abiria 65,639 kwa mwezi ikilinganishwa na jumla ya abiria 767,066 waliosafirishwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010 sawa na wastani wa abiria 63,922 kwa mwezi. Utendaji huo uliongezeka kwa asilimia 2.7. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012, *TAZARA* itaendelea kukarabati na kuboresha maeneo yenye mmomonyoko wa udongo kati ya Mlimba na Makambako, kwa upande wa Tanzania. Aidha, jumla ya mataruma 7,757 mabovu ya mbao yatabadilishwa na kuwekwa mapya kwenye madaraja na makutano ya reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara imepanga kuanza kutumia miundombinu ya reli iliyopo jijini Dar es Salaam kwa ajili ya usafiri wa abiria kwa kushirikisha sekta binafsi. Lengo ni kupunguza tatizo la msongamano wa magari jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu udhibiti wa huduma za usafiri wa reli, usimamizi wa huduma za reli nchini umeendelea kufanywa na Wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini *(SUMATRA).* Ukaguzi ulibaini upungufu ikiwa ni pamoja na utunzaji duni wa miundombinu, mawasiliano hafifu na hali mbaya ya mabehewa. Aidha, Mamlaka ilifanya ukaguzi wa ubora wa huduma zitolewazo na kampuni kwenye treni za abiria na kutoa maelekezo kwa kampuni kurekebisha upungufu uliobainika. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Mamlaka imepanga kuboresha nyenzo zake za udhibiti ikiwa ni pamoja na kukamilisha uandaaji wa viwango vya ujenzi wa maboti ya mbao, viashiria na vigezo vya utendaji vya huduma za reli na uondoshaji shehena bandarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri na uchukuzi majini pamoja na huduma za uchukuzi katika Maziwa. Huduma za usafiri wa abiria na mizigo katika maziwa makuu ya Tanganyika, Victoria na Nyasa zimeendelea kutolewa na Kampuni ya Meli *(MSCL)* ikishirikiana na sekta binafsi. *MSCL* inamiliki meli 14. Kati ya hizo, meli 11 zinafanya kazi kwa sasa. Meli hizo ni Mv. Victoria, Mv. Serengeti, Mv. Clarias, Mv. Umoja, ML. Wimbi, MT. Nyangumi na MT. Ukerewe katika Ziwa Victoria, Mv. Liemba na MT. Sangara katika Ziwa Tanganyika, Mv. Songea na Mv. Iringa katika Ziwa Nyasa. Katika mwaka 2010, jumla ya tani 77,272 zilisafirishwa ikilinganishwa na tani 123,279 zilizosafirishwa mwaka 2009 ikiwa ni pungufu kwa asilimia 39. Aidha, abiria 325,595 walisafirishwa katika mwaka

2010 ikilinganishwa na abiria 474,252 waliosafirishwa mwaka 2009 ikiwa ni pungufu kwa asilimia 31. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zinazoendelea kuikabili kampuni ni pamoja na meli nyingi kuwa chakavu na hivyo kuchukua sehemu kubwa ya mapato yapatikanayo kwa kufanya matengenezo ya mara kwa mara. Kampuni pia inakabiliwa na changamoto ya kupanda kwa bei ya mafuta na ongezeko la matumizi ya mafuta kutokana na uchakavu wa mitambo ya meli. Kusimamishwa mara kwa mara kwa meli ya Mv. Umoja kutokana na kukosa mizigo kunakosababishwa na kupungua kwa mizigo inayosafirishwa kwa reli ya kati kumeathiri kwa kiasi kikubwa mapato ya kampuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Kampuni ya *MSCL* inatarajia kusafirisha jumla ya abiria 408,464 na mizigo tani 111,628. Ili kufikia malengo hayo, Kampuni imeandaa mkakati wa kufanyia matengenezo makubwa na madogo meli zake ili kuziongezea uimara na kuziwezesha kufanya safari zake kwa uhakika na usalama. Kampuni pia itazifanyia meli zake ukaguzi wa mara kwa mara na kwa wakati uliopangwa ili kuboresha usalama wa meli na abiria pamoja na mali zao na kuweka bima za meli, abiria, mizigo na wafanyakazi. Aidha, Kampuni itaendelea kuweka vifaa vya kuokolea maisha melini vinavyotosheleza mahitaji, kuendelea kutoa elimu ya usalama kwa abiria, kuboresha huduma kwa wateja na kupanua soko la huduma zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za uchukuzi baharini, Kampuni ya *SINOTASHIP* inayojishughulisha na usafiri wa masafa marefu baharini inamilikiwa kwa ubia na Serikali ya Tanzania na Serikali ya Watu wa China kwa uwiano wa nusu kwa nusu. Katika mwaka 2010, kampuni ilitumia meli yake inayosafiri masafa marefu baharini yenye uwezo wa kubeba jumla ya tani 57,000 kufanya safari kumi ikilinganishwa na lengo la safari sita zilizokuwa zimepangwa. Katika safari hizo jumla ya tani 519,700 za shehena zilisafirishwa kwa mwaka 2010, ambazo ni ongezeko la asilimia 291 ikilinganishwa na jumla ya tani 132,740 za shehena zilizosafirishwa mwaka 2009. Hadi kufikia Desemba 2011, kampuni ya *SINOTASHIP* inatarajia kusafirisha jumla ya tani 520,000 za shehena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uendeshaji wa shughuli zake kwa kipindi cha mwaka 2010, Kampuni ya *SINOTASHIP* iliendelea kukabiliana na changamoto mbalimbali zikiwemo zile zilizotokana na mtikisiko wa uchumi duniani uliosababisha msukosuko katika vyombo vya fedha duniani pamoja na tishio la utekaji nyara meli unaofanywa na maharamia katika pwani ya Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto hizo, kampuni iliendeleza juhudi zake za makusudi za kubana matumizi na kuepuka gharama zisizokuwa za lazima. Aidha, jitihada kubwa zilielekezwa katika kutafuta aina ya shehena zinazoweza kusafirishwa kwa tozo kubwa na masafa mafupi ili kuongeza mapato kwa kampuni. Hivi sasa kampuni ipo katika mchakato wa kujenga meli mpya. Ujenzi wa meli hiyo yenye uwezo wa kubeba tani 34,000 unatarajiwa kukamilika Desemba, 2011. Kukamilika kwa ujenzi wa meli hii kutaongeza uwezo wa kampuni wa kubeba shehena kwa wakati mmoja kutoka tani 57,000 mwaka 2010 hadi kufikia tani 91,000 mwaka 2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za Bandari, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *(TPA)* imeendelea kusimamia, kuendesha na kuendeleza bandari za mwambao na zile za maziwa kwa ufanisi. Mapato ya Mamlaka yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka kutoka shilingi bilioni 141.41 mwaka 2005/2006 hadi shilingi bilioni 219.776 mwaka 2009/2010. Katika kipindi cha mwaka 2010/2011, *TPA* imehudumia jumla ya tani milioni 12.43 sawa na ongezeko la asilimia 3.15 ikilinganishwa na lengo la kuhudumia tani milioni 12.05 katika kipindi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la mapato ya *TPA* limechangia kuongezeka kwa uwekezaji katika Bandari, huduma za jamii na pia kukuza ajira katika sekta nyingine za uchukuzi kama wakala wa mizigo, usafirishaji majini, barabara na reli. Bandari pia inatoa huduma kwa wateja wa aina mbili yaani wenye meli na wenye mizigo. Wenye meli wanajumuisha makampuni na mawakala wa meli. Wateja wenye mizigo wanatoka ndani na nje ya nchi. Nchi

zinazohudumiwa na bandari zetu ni pamoja na Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi, Rwanda, Uganda na Malawi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shehena iliyohudumiwa na Mamlaka inajumuisha tani za makasha yaliyohudumiwa kupitia kitengo cha makasha kinachoendeshwa na *TICTS.* Katika mwaka 2009/2010, *TICTS* ilihudumia makasha 304,155 ikilinganishwa na mwaka 2010/2011 ambapo jumla ya makasha 352,737 yalihudumiwa. Hili ni ongezeko la asilimia 16. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka kwa kushirikiana na wadau wengine imefanikiwa kuvutia shehena ya nchi jirani inayopita katika bandari zetu. Katika kipindi cha 2009/2010 jumla ya tani milioni 2.441 kwenda na kutoka nchi jirani zilihudumiwa katika Bandari ya Dar es Salaam ambayo ni ongezeko la asilimia 4.7 ikilinganishwa na tani milioni 2.332 zilizohudumiwa mwaka 2008/2009. Katika kipindi cha 2010/2011 jumla ya tani milioni 2.475 kwenda na kutoka nchi jirani zilihudumiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hatua ya Serikali kuondoa kipengele cha ukiritimba katika kuhudumia meli za makasha, msongamano wa meli zinazosubiri kutia nanga katika Bandari ya Dar es Salaam umepungua na hivi sasa meli tano zinaweza kuhudumiwa kwa wakati mmoja ukilinganisha na meli tatu hapo awali. Muda wa makasha yaliyopakuliwa kukaa bandarini *(import container dwell time)* umepungua kutoka siku 15 katika mwezi Julai, 2010 hadi kufikia siku kumi katika kipindi cha mwezi Juni, 2011. Muda wa meli kukaa bandarini ikijumuisha muda wa kusubiri kuingia *(ship turn-round time)* umepungua kutoka wastani wa siku nane uliofikiwa mwezi Juni, 2010 hadi siku 7.3 kwa kipindi kilichoishia mwezi Juni, 2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka inakabiliana na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na uwezo wa kuhudumia meli kubwa zinazohitaji kina cha maji cha zaidi ya mita 12 na gati lenye urefu zaidi ya mita 250. Kwa sasa Bandari ya Dar es Salaam inaruhusu meli zenye kina cha mita 10.5 na urefu wa mita 240. Tatizo la kina kifupi ikilinganishwa na meli zinazotaka kutia nanga pia lipo katika Bandari za Tanga ambayo ina kina cha mita tatu, Mafia mita 0, Lindi mita 0, Kigoma mita mbili na Mwanza mita mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada za makusudi za kuvutia shehena za nchi jirani zinafanywa kwa kutafuta masoko na kusogeza huduma zaidi kwa wateja kwa kufungua wakala katika nchi za Uganda, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Pia kubuni viwango vya ushuru vya kiushindani na kuimarisha ushiriki wetu katika kuvutia matumizi ya bandari zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha 2011/2012 Mamlaka imepanga kutekeleza kwa ufanisi zaidi mikakati mbalimbali inayolenga katika kuongeza shehena, mapato na faida, tija na uwekezaji. Mipango hii itazingatia utekelezaji wa sera za kisekta, Kitaifa na Kimataifa, utekelezaji wa miradi mbalimbali inayoendelea, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 - 2015, ahadi za viongozi wakuu na mpango kabambe wa kuendeleza bandari. Katika kipindi cha 2011/2012, Mamlaka imelenga kuhudumia jumla ya tani milioni 12.854 ikiwa ni ongezeko la asilimia 3.4 ya tani milioni 12.43 zilizohudumiwa mwaka 2010/2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu udhibiti na usalama wa usafiri majini, *SUMATRA* kwa kuzingatia Sheria ya Usafiri Majini *(Merchant Shipping Act, 2003),* imeendelea kutekeleza majukumu ya Usalama na Ulinzi wa vyombo vya usafiri majini. Aidha, Mamlaka imeendelea kusimamia usalama na ulinzi wa vyombo vya majini kwa kuzingatia itifaki na mikataba mbalimbali ya Kimataifa inayosimamiwa na Shirika la Kimataifa linaloratibu Usalama wa Usafiri wa Majini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010 jumla ya vyombo vidogo 185 na vyombo 56 vyenye ukubwa wa zaidi ya tani 50 vilikaguliwa katika mwambao wa Bahari ya Hindi. Aidha, katika kipindi hicho ukaguzi wa aina hii ulifanyika kwa vyombo vidogo 2,740 na vyombo 170 vyenye uzito wa tani 50 katika Maziwa ya Tanganyika, Victoria, Rukwa na Nyasa. Kwa wale ambao vyombo vyao havikidhi viwango vya ubora, wenye vyombo hulazimika kuvifanyia marekebisho kabla ya kupewa vyeti vya ubora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni matukio ya uharamia katika mwambao wa Tanzania yamekuwa yakiongezeka. Katika kipindi cha Julai, 2010 hadi Mei, 2011 kulikuwa na matukio ya uharamia kumi na nne. Katika matukio haya, meli nne zilitekwa na kumi ziliokolewa na vyombo vya usalama au kujiokoa zenyewe. Matukio haya ya uharamia yanasababisha madhara makubwa ya kiuchumi nchini ikiwa ni pamoja na meli za mizigo na za kitalii kutofika Tanzania na kuongezeka kwa gharama za uchukuzi. *SUMATRA* kupitia kituo cha utafutaji na uokoaji imekuwa ikifuatilia kwa karibu mwenendo wa meli na wanapobaini matatizo ya utekaji wa meli hutoa taarifa kwa vyombo vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na tatizo la uharamia, Serikali kupitia *SUMATRA* imeingia mkataba na kampuni ya *Fulcrum Maritime Solutions* ya Uingereza kwa meli zilizosajiliwa Tanzania ziingizwe katika mtandao wao wa kufuatilia mwenendo wa meli zikiwa baharini *(Long Range Identification and Tracking System).* Hadi sasa meli 45 zenye usajili wa Tanzania zinafuatiliwa mahali popote zilipo duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuendelea na uratibu wa usalama wa vyombo vya uchukuzi nchini, *SUMATRA* pia imeendelea kudhibiti huduma za Makampuni yanayohudumia mizigo bandarini pamoja na Wakala wa Meli. Katika mwaka 2009/2010, kampuni 577 zinazoshughulikia huduma za mizigo bandarini zilisajiliwa na leseni 33 kutolewa kwa Makampuni ya Uwakala wa Meli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SUMATRA* imeendelea kuthibitisha sifa za wafanyakazi katika vyombo vya usafiri majini na kutoa vyeti kwa mujibu wa makubaliano ya Kimataifa ya viwango vya mafunzo, utoaji vyeti na uangalizi wa wafanyakazi baharini. Idadi ya vyeti vilivyotolewa na *SUMATRA* baada ya Mabaharia kupata mafunzo kutoka Chuo cha Bahari cha Dar es Salaam katika mwaka 2010 ni 6,409 ikilinganishwa na vyeti 5,581 vilivyotolewa mwaka 2009. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010 ajali zilizotolewa taarifa katika bahari na maziwa ni 13 ikilinganishwa na ajali saba mwaka 2009. Kupatikana kwa taarifa za matukio ya ajali mapema kumesaidia kufanikisha uokoaji wa wahanga katika ajali hizo hasa baada ya kituo cha utafutaji na uokoaji kuanza kazi rasmi mwezi Machi, 2009. Aidha, katika mwaka 2011/2012, *SUMATRA* itaendelea kukabiliana na ajali za majini kwa kuimarisha usimamizi wa usalama wa vyombo vya usafiri majini kwa kuvifanyia ukaguzi, kutoa elimu ya usafiri salama kwa wamiliki wa vyombo, waendeshaji wa vyombo vya usafiri majini, abiria na wadau wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za anga na huduma za viwanja vya ndege, katika mwaka 2010/2011, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania *(TAA)* iliendelea kuhudumia viwanja vya ndege kwa kuzingatia mwongozo unaosisitiza viwanja vya ndege kujiendesha kibiashara, kujitosheleza na kujitegemea kimapato. Aidha, Mamlaka imeendelea kuhudumia ndege, abiria na mizigo ambapo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 idadi ya safari za ndege ziliongezeka kwa asilimia 13 kutoka jumla ya safari za ndege 117,245 mwaka 2009/2010 hadi kufikia safari za ndege 132,584 mwaka 2010/2011. Aidha, idadi ya abiria iliongezeka kwa asilimia 10.3 kutoka jumla ya abiria 2,054,499 mwaka 2009/2010 na kufikia idadi ya abiria 2,265,658 mwaka 2010/2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwelekeo wa biashara unaonyesha kuwa kutokana na kuongezeka kwa mashirika mapya ya ndege na mashirika yaliyokuwepo kuongeza idadi ya miruko, idadi ya safari za ndege zitaongezeka kutoka 132,584 mwaka 2010/2011 na kufikia jumla ya safari 141,865 mwaka 2011/2012 ongezeko ambalo ni sawa na asilimia saba. Aidha, kutokana na ongezeko la viwanda, biashara na utalii na shughuli nyingine za kiuchumi, idadi ya abiria inatarajiwa kuongezeka kutoka 2,265,658 mwaka 2010/2011 na kufikia abiria 2,492,224 mwaka 2011/2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka iliendelea na matengenezo ya kawaida ya viwanja vya ndege ili kuwezesha ndege kuruka na kutua kwa usalama. Aidha, Mamlaka imekamilisha matengenezo ya miundombinu na uboreshaji wa mitambo katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere chini ya ufadhili wa Serikali ya Uholanzi. Matengenezo haya yamejumuisha ukarabati wa njia ya kuruka ndege, viungio vyake na maegesho ya ndege. Aidha,

usimikaji wa mitambo kwa ajili ya uhakiki wa abiria na mizigo unaendelea na upo katika hatua za mwisho ili kwenda sambamba na mifumo ya kisasa iliyopo kwenye viwanja vingine vya Kimataifa duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege cha Songwe, Mbeya unaendelea baada ya kukamilisha kazi za awamu ya kwanza na ya pili. Kazi zinazoendelea katika awamu ya tatu na ya mwisho ni pamoja na ujenzi wa tabaka la lami kwenye barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara ya kiungio, eneo la maegesho ya ndege na barabara ya kuingia kiwanjani. Kazi nyingine zinazoendelea ni ujenzi wa jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la zimamoto, ujenzi wa Kituo cha Hali ya Hewa, ujenzi wa mfumo wa maji safi na maji taka. Aidha, ununuzi wa vifaa vya ukaguzi na vifaa vya hali ya hewa ni sehemu ya awamu ya tatu ya mradi huu. Kazi za ujenzi wa kiwanja hicho zinatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba, 2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania imeendelea kuimarisha miundombinu ya viwanja vyake kwa kufanya matengenezo ya kawaida kwenye viwanja vya ndege vya Arusha, Musoma, Bukoba, Lake Manyara, Shinyanga, Sumbawanga, Tabora, Mtwara na Dodoma hususan kwenye barabara za kuruka na kutua ndege, pamoja na maegesho ya ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kiwanja cha Arusha, Mamlaka imekarabati njia ya kuruka ndege, viungio vyake pamoja na maegesho ya ndege kwa kiwango cha lami. Aidha, Serikali imekamilisha ukarabati mkubwa na urefushaji wa barabara ya kutua na kuruka ndege kwa kiwango cha changarawe katika kiwanja cha ndege cha Bukoba. Eneo jipya la maegesho ya ndege pamoja na viungio vyake pia vimejengwa kwa kiwango cha changarawe. Serikali pia imekamilisha ukarabati wa njia ya kuruka na kutua ndege kwa kiwango cha changarawe katika kiwanja cha ndege cha Mafia. Ukarabati mkubwa kwa kiwango cha lami wa njia ya kutua na kuruka ndege katika kiwanja cha ndege cha Mafia unaofadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia Mfuko wa Changamoto za Milenia *(MCC)* utaanza katika mwaka 2011/2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha usalama wa viwanja vyetu vya ndege, Mamlaka inaendelea na juhudi za kuinua viwango vya usalama hasa katika viwanja vya Julius Nyerere, Arusha, Mtwara, Mwanza, Bukoba, Tabora, Kigoma, Lake Manyara, Lindi na Dodoma. Kwa kuanzia Mamlaka imekamilisha ujenzi wa uzio katika viwanja vya Mwanza, Musoma, Kigoma na Dodoma. Mamlaka pia inaendelea na ujenzi wa uzio katika viwanja vya Mtwara, Moshi, Bukoba na *Lake Manyara. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyingine zilizochukuliwa kuimarisha usalama ni pamoja na ununuzi wa mitambo ya kutambua vitu vinavyoweza kulipuka, ununuzi wa mitambo ya ukaguzi wa mizigo, ununuzi wa milango maalum ya ukaguzi wa abiria na mashine maalum za mkono za kutambua vyuma na vitu vingine vya hatari. Aidha, mtambo maalum wa kuona kwa njia ya televisheni *(CCTV)* umefungwa katika kiwanja cha Kimataifa cha ndege cha Julius Nyerere. Mamlaka pia inaendelea na usimikaji wa mitambo *(Common User Terminal Equipment - CUTE)* kwa ajili ya kuhudumia na kuhakiki mizigo na abiria, ili kwenda sambamba na mifumo ya kisasa iliyopo kwenye viwanja vingine vya kimataifa duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha na kuboresha viwanja vingine vya ndege, Serikali imeweka mipango endelevu itakayoiwezesha kuendelea kuboresha miundombinu ya viwanja vya ndege. Katika mwaka 2011/2012, Serikali itakamilisha ukarabati na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Mpanda ambapo barabara ya kuruka na kutua ndege itajengwa kwa kiwango cha lami ili kuwezesha ndege zenye uwezo wa kubeba abiria 50 kutua na kuruka kwa usalama. Vilevile, maegesho ya ndege pamoja na viungio vyake yatajengwa kwa kiwango cha lami.

Aidha, ukarabati mkubwa wa barabara za kutua na kuruka ndege kwa kiwango cha lami unatarajiwa kufanyika katika viwanja vya ndege vya Kigoma, Bukoba na Tabora pamoja na ujenzi wa jengo jipya la abiria katika kiwanja cha ndege cha Bukoba chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi za kushirikisha sekta binafsi kuboresha miundombinu ya uchukuzi, Mamlaka kupitia sekta binafsi imejenga jengo jipya la kufikia watu mashuhuri *(VIP*

*Building)* pamoja na karakana ya kufanyia matengenezo ya ndege katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere *(JNIA).* Pia wawekezaji mbalimbali wamejenga vituo vya mafuta ya ndege katika viwanja vya Mwanza na Mtwara na huduma zinatarajiwa kuanza. Wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(TAA)* inaendelea kuhamasisha wawekezaji binafsi kujitokeza kuwekeza katika kujenga miundombinu ya viwanja vya ndege na utoaji huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutoa nafasi ya upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere, Wizara kupitia *TAA* imekamilisha ulipaji fidia na utoaji wa viwanja mbadala kwa wakazi wa Kipawa na Kigilagila wapatao 2,085. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Wizara itakamilisha zoezi la kuwahamisha wakazi waliojenga kandokando ya kiwanja hicho ambapo wakazi 1,185 wa Kipunguni watalipwa fidia na kupewa viwanja mbadala kabla ya kuhamishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imenunua hisa zote za Kampuni inayoendesha Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro *(KADCO).* Taratibu za kumtafuta Mshauri Mwelekezi *(Transaction Adviser)* atakayeshauri Serikali kuhusu namna ya kumpata mwekezaji katika kiwanja hicho zimekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za usafiri wa ndege, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Kampuni ya Ndege ya Tanzania *(ATCL)* imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na madeni makubwa, gharama kubwa za uendeshaji na huduma zisizoridhisha. Katika kipindi hicho, Serikali iliendelea kuisaidia *ATCL* kulipa gharama mbalimbali za uendeshaji ikiwa ni pamoja na mishahara ya wafanyakazi, kugharamia matengenezo ya ndege mbili za Kampuni na mafunzo kwa wafanyakazi. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali itaendelea kusimamia kwa karibu utendaji wa Kampuni ili kuongeza ufanisi. Serikali bado inaamini kuwa kuishirikisha sekta binafsi ni muhimu katika kuwekeza na kuendeleza Kampuni hii. Hivyo, Serikali itaendelea kufanya majadiliano na wawekezaji mbalimbali ili kuwekeza kwenye *ATCL.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Wakala wa Ndege za Serikali *(TGFA),* umeendelea kutoa huduma kwa viongozi wakuu wa Kitaifa na Serikali kwa ujumla. Aidha, Wakala umeendelea kuhakikisha kwamba ndege zake zote nne yaani *Fokker* 28, *Gulfstream* 550, *Fokker* 50 na *Piper Navajo* 31 ziko salama kuhudumia viongozi wakuu wa Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Wakala ulikabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na uchakavu wa ndege na mabadiliko ya teknolojia. Ili kukabiliana na changamoto hizo, Wakala uliendelea kufanya matengenezo kwa wakati, kutoa mafunzo kwa marubani na wahandisi pamoja na watumishi wengine ili kukabiliana na mabadiliko ya kiteknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha 2011/2012, Wizara kupitia Wakala itaendelea kuboresha huduma za usafiri wa anga kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa na kuziweka ndege katika hali ya kuwa tayari kwa safari wakati wowote zitakapohitajika. Wakala pia utaendelea kuwapeleka watumishi katika mafunzo ya ndani na nje ya nchi ili kuwaongezea uwezo wa kufanya kazi zao kwa tija na ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa usafiri wa anga, Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania *(TCAA)* imeendelea kutekeleza majukumu yake iliyopewa kisheria katika kuboresha huduma na usalama wa usafiri wa anga. Katika kipindi cha mwaka 2010/2011 safari za ndege zilikuwa 185,278 ikilinganishwa na safari 170,777 mwaka 2009/2010, ikiwa ni ongezeko la asilimia 8.5. Abiria waliotumia usafiri wa anga waliongezeka kufikia abiria 3,358,499 mwaka 2010/2011 ikilinganishwa na abiria 3,082,254 waliotumia usafiri huo mwaka 2009/2010, ikiwa ni ongezeko la asilimia tisa. *(Makofi)*

Aidha, mizigo iliyosafirishwa kwenda nje na kuja nchini iliongezeka na kufikia tani 25,917 mwaka 2010/2011 ikilinganishwa na tani 24,941 zilizosafirishwa mwaka 2009/2010, ikiwa ni ongezeko la asilimia 3.9. Ongezeko hili lilichangiwa na kuwepo kwa mashirika na kampuni za ndege

zilizobeba mizigo kama *KLM (Royal Dutch Airlines), Ethiopian Airlines, Emirates, Astral Aviation, Egypt Air* na *Turkish Airlines.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, sekta hii inatarajiwa kukua, ambapo abiria 3,660,522 wanatarajiwa kutumia usafiri wa anga ikiwa ni ongezeko la asilimia tisa kutoka abiria 3,358,499 waliotumia usafiri huo mwaka 2010/2011. Katika mwaka 2011/2012 inatarajiwa kuwa jumla ya kampuni mpya nne za ndege zitakuwa zinatoa huduma za usafiri wa anga na hivyo kufanya jumla ya kampuni za ndege ambazo zimeidhinishwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga kutoa huduma za usafiri wa anga kuwa 58 kutoka kampuni 54 zilizopo sasa, ikiwa ni ogezeko la asilimia 7.4. Ongezeko hili litachangia kukua kwa safari za ndege, idadi ya abiria na mizigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu za ukaguzi zimeendelea kuimarishwa kwa lengo la kuzuia matukio ya kuhatarisha usalama kwa kushirikisha wadau wote wa usafiri wa anga. Katika kipindi cha mwaka 2010/2011 kufikia mwezi Juni, 2011, yalitokea matukio matano ya ajali. Kati ya hayo, ajali moja iliua watu wawili. Aidha, ndege nne ziliharibika kabisa. Katika kipindi cha 2009/2010 kulitokea ajali moja ya ndege na ndege hiyo iliharibika kabisa. Hakuna mtu aliyepoteza maisha. Lengo la Mamlaka ni kusimamia na kuhakikisha ajali hazitokei katika mwaka 2011/2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Usafiri wa Anga imeendelea kuhakikisha kwamba shughuli zote za usafiri wa anga zinafuata sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Mamlaka inajitayarisha kwa zoezi la ukaguzi litakalofanywa wakati wowote na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga *(ICAO),* ili kubaini kama Mpango wa Marekebisho ambao ulikubaliwa na *ICAO* unatekelezwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikataba ya usafiri wa Anga *(Bilateral Air Services Agreements-BASAs)* kati ya Tanzania na nchi nyingine, Wizara imeendelea kufanya mazungumzo na nchi mbalimbali ili kupitia upya mikataba kwa lengo la kuiboresha ili ikidhi mahitaji ya soko na hali halisi ya maendeleo na mabadiliko katika sekta hii. Katika kipindi cha mwaka 2010/2011, makubaliano ya usafiri wa anga kati ya Tanzania na Kenya yalipitiwa upya ili yakidhi mazingira ya biashara ya sasa. Aidha, makubaliano ya usafiri wa anga kati ya Serikali ya Tanzania na Jordan *(BASA)* yalitiwa saini mwezi Januari, 2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupanua uwanja wa ushindani wa biashara ya usafiri wa anga, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uchukuzi (2003). Lengo ni kuruhusu uwekezaji kutoka nje na ndani ya nchi kwenye sekta ya usafiri wa anga ili kuvutia ukuaji wa sekta na kuboresha huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka ya usafiri wa anga imeendelea kutoa huduma za uongozaji ndege kwenye viwanja kumi na vitatu vya Dar es Salaam, Zanzibar, Mwanza, Arusha, Dodoma, Kigoma, Tabora, Mtwara, Pemba, Songea, Mbeya, Iringa na Tanga. Aidha, Mamlaka imeendelea kutoa huduma hizo kwenye anga lote la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia juu ya Bahari ya Hindi hadi nyuzi 44 Mashariki na kwenye anga la Burundi na Rwanda kwa kukasimiwa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga *(ICAO)* na kuridhiwa na nchi hizo. Mamlaka imejipanga kutoa huduma ya uongozaji ndege katika kiwanja cha ndege cha Songwe mara kitakapofunguliwa. Aidha, *ICAO* imebadili utaratibu wa usimamizi wa usalama *(safety).* Chini ya utaratibu mpya, mdhibiti na mtoa huduma wanafanya kazi kwa pamoja badala ya mdhibiti kuja wakati wa ukaguzi tu na kutoa mwongozo wa kuondoa matatizo pindi anapoyabaini. Utaratibu huu *(Safety Management System-SMS),* unamwezesha mdhibiti kupata dalili za matatizo kila wakati na pia unawawezesha watoa huduma kuhakikisha kuwa wanakidhi viwango vya usalama kwa hiari. Tayari utekelezaji wa SMS umeshaanza na unaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa huduma za uongozaji ndege zinaendelea kutolewa katika Viwanja vya Kimataifa, miundombinu ya kutoa huduma hiyo itaboreshwa. Pamoja na mambo mengine, Mamlaka ya Usafiri wa Anga inatarajia kuanza kutumia teknolojia ya *Automatic Dependency Surveillance – Broadcast (ADS-B)* ambayo licha ya kuwa ya gharama nafuu, itasaidia kusimamia kwa usahihi zaidi uongozaji ndege na pia kutoa fursa ya kukabili

changamoto ya ongezeko la ndege angani *(space congestion),* kupunguza gharama kwa mashirika ya ndege itokanayo na upunguzaji wa matumizi ya mafuta, na kupunguza uharibifu wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka inaendesha Chuo cha Mafunzo *(Civil Aviation Training Centre)* kwa taaluma za uongozaji ndege, mafundi wa mitambo ya uongozaji ndege, wataalamu wa mawasiliano kwa urukaji na usalama. Kwa kiasi kikubwa Chuo hiki kimesaidia kupunguza gharama zitokanazo na kupeleka wanafunzi nje ya nchi. Aidha, Chuo hiki hupokea wanafunzi kutoka nchi mbalimbali za Afrika na hivyo kuitangaza vema nchi yetu na pia kuingiza fedha za kigeni. Katika mwaka 2010/2011 Chuo kilipokea wanafunzi 283 ambapo 196 kati yao ni kutoka ndani ya nchi na wanafunzi 87 kutoka nje ya nchi. Idadi hiyo ni kubwa ikilinganishwa na jumla ya wanafunzi 171 (wanafunzi 156 kutoka ndani ya nchi na 15 kutoka nje ya nchi) waliopokelewa mwaka 2009/2010. Katika mwaka 2010/2011 Chuo kilinunua mtambo mpya na wa kisasa kwa ajili ya mafunzo ya waongoza ndege *(simulator).* Mipango ya kuimarisha Chuo kitaaluma na kukipatia majengo yake yenyewe inaendelea.

Mheshimiwa Mmweyekiti, mwaka jana ilitolewa taarifa kwamba Mamlaka ya Usafiri wa Anga ilikuwa inaendelea kujenga jengo lake la Makao makuu. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba jengo hilo sasa limekamilika na tayari Makao Makuu ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga yamehamia katika jengo hilo tangu mwezi Machi, 2011. Jengo hilo limejengwa katika eneo la Ukonga karibu na Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere. Vilevile Mamlaka ya Usafiri wa Anga imepata usajili wa viwango vya kimataifa *(ISO 9001:2008).* Hati hii imesaidia kuboresha viwango vya utendaji vya Mamlaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za hali ya hewa, sekta ya hali ya hewa ni muhimu kwa usalama wa maisha, mali na mazingira. Zaidi ya asilimia 80 ya majanga ya asili yanatokana na mabadiliko ya hali ya hewa na tabia nchi. Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa *(TMA)* imeendelea kuboresha huduma za hali ya hewa nchini ili kukidhi mahitaji ya sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Katika mwaka wa fedha 2010/2011 Mamlaka ilitunukiwa cheti cha Kimataifa cha ubora wa utoaji huduma za hali ya hewa kwa usafiri wa Anga *(ISO 9001:2008).* Mamlaka itaendelea kutoa huduma zake kwa kuzingatia viwango vya ubora vilivyofikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha miundombinu ya utabiri wa hali ya hewa, mwaka 2010/2011 Mamlaka imekamilisha ujenzi wa kituo cha rada ya hali ya hewa eneo la Bangulo, Pugu (Dar es Salaam) na kitazinduliwa hivi karibuni. Aidha, mchakato wa kununua rada ya pili ya hali ya hewa inayotarajiwa kufungwa mkoani Mwanza umeanza. Mamlaka pia imekamilisha ujenzi wa kituo cha hali ya hewa cha Mpanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TMA* imeendelea kuboresha taaluma ya wafanyakazi wake kwa kuwapeleka katika vyuo mbalimbali kuchukua mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi. Mafunzo ya muda mfupi yamekuwa yakitolewa na Mamlaka kwa wafanyakazi wa kada mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Mamlaka inatarajia kuanza ujenzi wa kituo cha hali ya hewa cha Babati, Mkoani Manyara na kituo cha hali ya hewa na kilimo *(Agromet station)* huko Lindi. Aidha, Mamlaka itaendelea kuboresha vituo vyake kwa kununua vifaa na mitambo ya kisasa ya hali ya hewa pamoja na kuboresha studio zake za kutayarishia taarifa za hali ya hewa. Mafunzo kwa wafanyakazi yataendelea kutolewa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuwaongezea wafanyakazi uwezo wa kutoa huduma bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kanda ya Uchukuzi, Wizara imeendelea kusimamia miradi ya sekta inayotekelezwa katika Kanda nne za Uchukuzi zilizoainishwa. Kanda hizo ni Ukanda wa Uchukuzi wa Dar es Salaam (Dar es Salaam – Mbeya - Zambia), Ukanda wa Uchukuzi wa Tanga, Ukanda wa Uchukuzi wa Kati (Dar es Salaam – Isaka - Rwanda/Burundi/*DRC*/ Uganda) na Ukanda wa Uchukuzi wa Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufuatilia na kuhakikisha Tanzania inahudumia na kufaidika na uchumi wa kijiografia, Wizara yangu ikishirikiana na nchi jirani imeunda wakala za

kusimamia kanda za uchukuzi ili kubainisha matatizo, mahitaji, mipango na hatimaye kutoa mapendekezo kwa lengo la kuboresha uchukuzi na biashara katika kanda hizo. Wakala zilizoundwa ni wa Ukanda wa Kati *(Central Corridor Transit Transport Facilitation Agency - TTFA)* na Ukanda wa Dar es Salaam *(Dar Corridor Committe - DCC).* Wakala hizo zikisaidiana na taasisi zinazotoa huduma za usafirishaji zinawajibika kusimamia na kuleta ufanisi katika utoaji huduma katika kanda hizo. Aidha, taratibu za kuunda wakala kwa ajili ya kusimamia Kanda za Tanga na Mtwara zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Machi, 2011 Serikali iliridhia Wakala za Kanda kuwa na Sekretarieti zake Dar es Salaam hivyo kuziwezesha kuanza kazi rasmi. Aidha, Wakala hizo zimefanya uchunguzi wa kujua vikwazo vilivyoko *(Baseline Survey)* katika njia kuu za kwenda Rwanda, Burundi, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo *(DRC)* kwa upande wa Ukanda wa Kati na kwenda *DRC* (Lubumbashi), Zambia na Malawi kwa Ukanda wa Dar es Salaam. Katika mwaka 2011/2012, Wakala zimepanga kuweka vituo ili kufuatilia mwenendo mzima wa utoaji huduma ya uchukuzi katika kanda hizo. Utafiti utafanyika kuhusu kuweka vituo vya pamoja vya utendaji kwa kukagua magari katika kanda hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki *(EAC),* Wizara imeendelea kushiriki kwenye mikutano mbalimbali ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuzungumzia masuala yanayohusu uboreshaji wa miundombinu ya uchukuzi na masuala ya hali ya hewa. Katika ushirikiano huu, miradi mbalimbali ya miundombinu imeibuliwa na kufanyiwa maamuzi ya pamoja. Mradi mkubwa ni ule wa uwezeshaji wa uchukuzi na Kibiashara Afrika Mashariki *(East Africa Trade and Transport Facilitation Project – EATTFP)* unaolenga katika kuhakikisha kuwa ujenzi wa miundombinu ya uchukuzi unaboreshwa na kuoanishwa na sera na mikakati mbalimbali ya sekta. Aidha, Jumuiya inakamilisha maandalizi ya mkakati wa miaka kumi wa kuendeleza sekta ya uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafiri wa reli, nchi wanachama wameandaa mpango kabambe wa uendelezaji wa reli. Aidha, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zipo katika mchakato wa maandalizi ya mwongozo wa kisheria na kiutendaji kuhusu ushirikishwaji wa sekta binafsi utakaosaidia pia kuendeleza reli za kikanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa usafirishaji majini, Tanzania imeendelea kushirikiana na nchi nyingine wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kupambana na vitendo vya kiharamia katika Bahari ya Hindi. Aidha, ushirikiano huo unahusisha Shirika la Kimataifa linalosimamia Usafiri Majini *(IMO),* Umoja wa Afrika *(AU)* na ushirikiano wa nchi saba za Afrika *(Intergovernmental Authority on Development – IGAD)* yaani Sudan, Eritrea, Djibouti, Ethiopia, Somalia, Uganda na Kenya. Hivi sasa makubaliano ya ushirikiano wa kupambana na kuzuia vitendo vya kiharamia yamefikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya uratibu wa *IMO* na mradi wa *Djibouti Code of Conduct,* kituo cha utafutaji na uokoaji cha Dar es Salaam kimeteuliwa kuwa miongoni mwa vituo vitatu vitakavyoratibu taarifa za matukio ya uharamia katika Bahari ya Hindi. Vituo vingine ni Sanaa (Yemen) na Mombasa (Kenya). Aidha, nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubali kuwa Kituo cha utafutaji na uokoaji katika maziwa kijengwe Mwanza na Serikali imetoa kiwanja kwa ajili ujenzi wa kituo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ziliunda Wakala wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa kusimamia ulinzi na usalama wa anga kwa ajili ya kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu usalama na ulinzi wa usafiri wa anga katika nchi wanachama. Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Wakala huu katika kuoanisha taratibu za usimamizi wa usalama wa usafiri wa anga na pia kuhakikisha kuwa nchi wanachama zinaondoa kasoro zinazotokana na kaguzi za *ICAO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza makubaliano ya itifaki ya uchukuzi, mawasiliano na hali ya hewa ya nchi wanachama wa *SADC* ya mwaka 1998, Wizara imeendelea kushiriki katika vikao mbalimbali vya *SADC* kuhusu uendelezaji wa Kanda za uchukuzi na ulegezaji

wa masharti katika usafiri wa anga. Lengo ni kufungua njia za mawasiliano ya uchukuzi ili kukuza biashara kwa nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na utekelezaji wa masuala muhimu yaliyopo katika Itifaki ya Uchukuzi, Mawasiliano na Hali ya Hewa, Wizara bado ina jukumu la msingi katika uendelezaji wa miundombinu ya uchukuzi ili kuiunganisha nchi yetu na nchi wanachama wa *SADC.* Miongoni mwa miradi inayotekelezwa ni pamoja na uboreshaji wa usafiri wa reli ya *TAZARA* na huduma za usafiri katika Bandari za Mtwara, Kasanga, *Mbamba Bay* na uboreshaji wa huduma za hali ya hewa *(SADC Meteorological Project - SAMPRO). (Makofi)*

Aidha, nchi wanachama wa *SADC* zimeendelea kushirikiana katika mtandao wa mawasiliano wa *VSAT* na hivyo kuboresha huduma za mawasiliano na utoaji taarifa za ndege zinazotumia anga la nchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi wanachama wa *SADC* zimekuwa na utaratibu wa kuwa na wawakilishi wao kwenye Baraza la Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga *(ICAO),* badala ya uwakilishi wa nchi moja moja. Utaratibu huu ulianza mwaka 1993 kwa kuzunguka ambapo kila nchi hupata fursa ya kuteua mtaalamu wake ambaye atawaikilisha *SADC* katika Shirika hilo la Kimataifa kwa kipindi cha miaka mitatu. Kwa kufanya hivyo, nchi wanachama zimeweza kupunguza gharama za kuweka mtaalamu mmoja kwa kila nchi kwenye Shirika hilo na pia kuwa na nguvu ya pamoja kama Jumuiya. Tanzania itapata fursa ya kuwaikilisha *SADC* kwenye Shirika hilo ifikapo mwaka 2013. Kwa sasa mchakato wa kumpata Mtanzania mwenye sifa na uwezo na ambaye atakubalika na nchi wanachama wa *SADC* kuwa mgombea wao umeanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maendeleo na mafunzo ya watumishi, katika mwaka 2010/2011, Wizara imeendelea kuwahudumia watumishi wake katika nyanja za kitaaluma na kijamii. Katika kipindi hiki, Wizara ilipeleka watumishi 74 katika mafunzo ndani na nje ya nchi yanayohusiana na taaluma zao ili kuongeza ujuzi mbalimbali. Kati yao, watumishi 18 walipelekwa mafunzo ya muda mrefu ndani ya nchi na mmoja nje ya nchi. *(Makofi)*

Aidha, watumishi 49 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi na watumishi sita walipelekwa mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi. Wizara iliwapandisha vyeo watumishi 14 wa kada mbalimbali na kuwathibitisha kazini watumishi 12. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, utaratibu wa kupeleka watumishi mafunzoni utaendelea kwa awamu kwa lengo la kuwaongezea ujuzi, ufanisi na tija katika kufanya kazi zao. Watumishi 83 wamepangiwa kupewa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ndani na nje ya nchi. Kati ya hao, watumishi 56 wanatarajiwa kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi na wengine 15 watapelekwa kwenye mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi. Watumishi kumi watapelekwa katika mafunzo ya muda mrefu ndani ya nchi na wengine wawili watapelekwa katika mafunzo ya muda mrefu nje ya nchi. Aidha, Wizara inatarajia kujaza nafasi 55 zilizo wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taasisi za mafunzo, Wizara imeendelea kuvihudumia vyuo vyetu vya mafunzo kwa lengo la kuviwezesha kutoa wataalam wa kada mbalimbali katika sekta za uchukuzi na hali ya hewa. Vyuo vilivyo chini ya Wizara ya Uchukuzi ni Chuo cha Taifa cha Usafirishaji *(NIT),* Chuo cha Bahari Dar es Salaam *(DMI),* Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma, Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam, Chuo cha Bandari na Chuo cha Reli Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji *(NIT)* kimeendelea kutekeleza majukumu yake ya kutoa elimu, ushauri na utafiti kwa umma wa Tanzania.

Katika mwaka 2010 chuo kilidahili jumla ya wanafunzi 288 wa kozi ndefu ikilinganishwa na jumla ya wanafunzi 269 waliodahiliwa katika mwaka 2009 ikiwa ni ongezeko la asilimia saba. Kwa upande wa kozi za muda mfupi, chuo kiliendesha kozi kwa wanafunzi 1,991 mwaka 2010 ikilinganishwa na wanafunzi 1,477 mwaka 2009 sawa na ongezeko la asilimia 35%. Aidha, chuo kimeweza kuboresha mitaala yake na kutoa mafunzo ambayo yanakidhi mahitaji ya soko la ajira na kujiajiri kulingana na taratibu za ithibati kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE)* na

Taasisi ya Kimataifa ya *Chartered Institute of Logistics and Transport – UK.* Mafunzo hayo yanatolewa katika mfumo wa *Competence Based Education and Training (CBET)* katika ngazi ya Stashahada na Shahada ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, chuo kimeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na upungufu wa vifaa vya karakana, magari, vitabu na kompyuta za kufundishia. Pia uhaba na uchakavu wa majengo na miundombinu ya chuo kama madarasa, mabweni, barabara za ndani ya chuo na uzio. Aidha, uhaba wa wahadhiri wa ajira za kudumu ambapo kati ya wahadhiri 75 waliopo 15 ni wahadhiri kutoka nje ya chuo. Serikali itaendelea kufanyia kazi changamoto hizi ili kuboresha hali ya chuo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012, chuo kitaendelea kuboresha elimu na mafunzo ili kikidhi mahitaji ya soko na kuongeza programu za elimu na mafunzo kwa lengo la kufikia kiwango cha ngazi ya Shahada ya Uzamili na hatimaye Shahada ya Uzamivu katika sekta ya uchukuzi. Aidha, chuo kitaendelea kujitangaza ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuongeza idadi ya wanafunzi kufikia 690 ifikapo Oktoba, 2011 sambamba na kuimarisha na kuongeza uwezo wa wahadhiri katika kiwango cha Shahada ya Uzamivu kwa asilimia 25%. *(Makofi)*

Katika kipindi hiki, chuo kitaendelea kufanya tafiti kwa kushirikiana na wataalamu wa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kutoa ushauri wa kitaalamu. Wizara kwa kushirikiana na chuo na wadau mbalimbali itakamilisha taratibu za kuunda Bodi ya Kitaalamu ya Uchukuzi na Usafirishaji kwa lengo la kuishauri sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Bahari Dar es Salaam *(DMI),* kimeendelea kutoa huduma za mafunzo, utafiti, ukarabati wa vifaa vya kuokolea maisha na uwakala wa ajira kwa wafanyakazi melini. Mafunzo yaliyotolewa yalilenga katika kuendeleza rasilimali watu katika sekta ya usafiri majini. Katika mwaka 2010/2011, wanafunzi 480 wa kozi ndefu na 7,644 wa kozi fupi walijiunga na chuo ikijumuisha wanafunzi wa ndani na nje ya nchi. Aidha, udahili wa wanafunzi wa kozi ndefu umekuwa ukiongezeka baada ya wanafunzi wa Stashahada ya Juu kupata udhamini wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chuo kimeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo uhaba wa vifaa vya kufundishia, miundombinu inayokidhi mahitaji ya utoaji elimu na mafunzo yahusuyo bahari na ugumu wa kupata mafunzo melini *(sea time)* kwa wanafunzi wa chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia kusainiwa kwa makubaliano ya ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Serikali kupitia chuo ina mpango wa kutekeleza mradi wa maendeleo kati ya Chuo cha Bahari cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Usafiri majini cha Dalian cha China. Chini ya mpango huo, Chuo Kikuu cha Dalian kitajenga tawi la chuo hicho ndani ya Chuo cha Bahari cha Dar es Salaam. Lengo ni kuwezesha kutoa shahada ya kwanza na ya pili, kushirikiana katika kutoa mafunzo, kusaidia taasisi za Kiserikali na za kiraia katika sekta ya bahari na kuendeleza miundombinu ya chuo ili kiweze kukidhi mahitaji ya soko la elimu na mafunzo yanayohusu bahari. Tayari Chuo Kikuu cha Dalian kimeshaandaa michoro ya majengo ya chuo, Bajeti yao ya ujenzi wa chuo imeishakamilika na mchakato wa vibali vya mradi na ujenzi unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Bahari cha Dar es Salaam kwa kushirikiana na *SUMATRA,* kitaelekeza nguvu zake katika kutafuta ajira kwa wahitimu wake katika meli za Kimataifa ambapo kitasaini mikataba ya ushirikiano na *SUMATRA* ya kutambua vyeti vya wahitimu kutoka Chuo cha Bahari cha Dar es Salaam. Aidha, chuo kitaendelea kujitangaza ili kupata wanafunzi wengi zaidi wa ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Usafiri wa Anga Tanzania *(CATC)* kimeendelea kutoa mafunzo yahusuyo fani za usafiri wa anga na uendeshaji wa viwanja vya ndege kwa wanafunzi wa ndani na kutoka nje ya nchi. Taaluma zilizoendelea kutolewa katika chuo hiki ni pamoja na mafunzo ya uongozaji ndege, mawasiliano na utoaji habari wa safari za ndege, mafunzo ya matengenezo ya mitambo na ya ukaguzi wa abiria na usalama wa viwanja. Chuo tayari kina

usajili wa mpango wa mafunzo unaosimamiwa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga *(ICAO TRAINAIR)* na kwa sasa kinaendelea na taratibu za usajili wa Baraza la Taifa la Mafunzo ya Ufundi *(NACTE).* Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2010 hadi Juni, 2011, chuo kimetoa mafunzo kwa jumla ya wanafunzi 283 ambapo kati ya hao 110 ni wanawake (39%). Aidha, chuo kilishinda na kupewa mkataba wa kuendesha mafunzo ya muda mfupi ya kitaalamu kwa ajili ya Mamlaka ya viwanja vya ndege nchini Namibia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Chuo cha Usafiri wa Anga kitaendelea kutoa mafunzo kwa kuzingatia ubora na kimepanga kuongeza idadi ya kozi zinazotolewa na idadi ya wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Hali ya Hewa imeendelea kuboresha Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma ili kiweze kukidhi matakwa ya kusajiliwa na *NACTE.* Maboresho hayo yanahusisha ujenzi wa maabara na chumba cha kompyuta. Chuo pia kimehamishia mafunzo ya *Meteorological Technician Senior Level (class II)* huko Kigoma kutoka kampasi ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka imeendelea kutoa mafunzo ya awali na ya kati ya hali ya hewa katika Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma. Jumla ya wanafunzi 45 walimaliza mafunzo ya utabiri daraja la tatu mwaka 2010/2011. Wanafunzi 28 wanaendelea na mafunzo ya utabiri daraja la pili na wanafunzi 39 wanaendelea na mafunzo ya utabiri daraja la tatu. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma kinatarajia kuendelea kutoa mafunzo ya taaluma ya awali na kati na kupata usajili wa *NACTE.* Aidha, mamlaka itaendelea kuboresha mazingira ya chuo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Reli Tabora kimeendelea kutoa mafunzo yanayohusu shughuli za usafiri wa reli. Taaluma zinazotolewa na chuo hiki kwa sasa ni *Station Master* na *Train Guard*. Chuo kilidahili jumla ya wanafunzi 43 katika kipindi cha mwaka 2010/2011 ikilinganishwa na wanafunzi 21 katika mwaka 2009/2010 ikiwa ni ongezeko la asilimia 49. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia maamuzi yaliyofikiwa na Serikali ya kurudisha Kampuni ya Reli Tanzania na kuwa mmiliki pekee, pamoja na mambo mengine, Serikali itaendelea kuwekeza katika eneo la mafunzo kwa watumishi wa taaluma mbalimbali za reli. Hivyo chuo kinatarajiwa kuanza mafunzo ya taaluma zote ili kukidhi mahitaji yatokanayo na upungufu wa watumishi ndani ya kampuni yanayotokana na watumishi kustaafu na kuacha kazi kwa sababu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari imeendelea kuhudumia Chuo cha Bandari Dar es Salaam kama idara nyingine za mamlaka. Chuo hiki hutoa mafunzo katika nyanja za shughuli za kibandari. Chuo kimefanikiwa kuwa na ongezeko la wanafunzi kutoka 326 mwaka 2006 hadi 887 mwaka 2011 ikiwa ni ongezeko la asilimia 63. Chuo kinatoa mafunzo ya kuwaendeleza wafanyakazi wa Mamlaka ya Bandari katika fani zote za shughuli za kibandari kwa kuzingatia miongozo inayotolewa na *NACTE* ili kuongeza tija na ufanisi. Aidha, chuo kinatoa huduma za ushauri na kinaendesha kozi fupi za jioni. Chuo hiki pia kinaendesha kozi za Stashahada na kutoa vyeti vya fani mbalimbali za shughuli za meli na uendeshaji wa bandari, uondoshaji mizigo bandarini, usimamizi wa matengenezo na uendeshaji wa mitambo na mashine za kuhudumia mizigo bandarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala mtambuka; utunzaji wa mazingira. Utekelezaji wa miradi yote ya maendeleo ya miundombinu ya uchukuzi unazingatia utunzaji na uhifadhi wa mazingira kwa kutumia Sera, Sheria, Kanuni na Mikataba ya Kimataifa iliyoridhiwa na Serikali. Wizara kwa upande wake imehakikisha kuwa sera na sheria hizo zinazingatiwa ipasavyo. Katika 2010/2011, Wizara iliendelea kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 ikiwa ni pamoja na kupitia taarifa za tathimini ya athari kwa mazingira kutokana na utekelezaji wa miradi ya viwanja vya ndege, reli na bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2011/2012, Wizara itaendelea kuhakikisha kuwa miradi ya miundombinu ya uchukuzi inatekelezwa kwa kuzingatia maendeleo endelevu ya

uhifadhi wa mazingira na kuandaa tathmini ya athari za mazingira kabla ya miradi ya miundombinu ya uchukuzi kuanza kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa imeendelea kuwaelimisha wafanyakazi wote katika semina mbalimbali, kuhusu athari za rushwa katika sekta yetu, makosa ya rushwa yanayoweza kutendeka na kuwahimiza kuepukana na makosa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu udhibiti wa UKIMWI. Katika mwaka 2010/2011 Wizara iliendelea kuwasaidia watumishi waliojitokeza waishio na virusi vya UKIMWI kwa kuwagharamia chakula chenye lishe bora. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kuwasaidia watumishi waishio na virusi vya UKIMWI kwa kuwagharamia chakula chenye lishe bora kwa watakaojitokeza na kuwahamasisha watumishi wengine kupima afya zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la habari, elimu na mawasiliano, mojawapo ya jukumu la Wizara ni pamoja na kuendelea kuelimisha umma kuhusu shughuli za sekta za uchukuzi na hali ya hewa kupitia njia mbalimbali za upashanaji habari. Aidha, tovuti za taasisi zilizo chini ya Wizara ya Uchukuzi zimeunganishwa katika tovuti ya Wizara ili kumwezesha mtumiaji kupata rejea za taarifa mbalimbali kwa urahisi. Wizara pia imeendelea kuratibu na kuandaa vipindi maalum vya kuelimisha umma kwenye vyombo vya habari kwa lengo la kutangaza matukio mbalimbali ya sekta, mafanikio yaliyopatikana na matarajio ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali zinazosimamiwa na Wizara ya Uchukuzi. Kwa mfano kipindi cha Safiri Salama kinachoandaliwa na *SUMATRA* na kurushwa kila Jumamosi na Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa umma juu ya shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Wizara hasa kwa kulenga miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara kwa kupitia vyombo vya habari, mabango, vipeperushi na majukwaa mbalimbali yakiwemo matamasha. Lengo likiwa ni kuelimisha Umma kuhusu tulikotoka, maendeleo yaliyopatikana, changamoto zilizopo na namna tunavyokabiliana nazo katika sekta ya uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wizara ya Uchukuzi, napenda kutoa shukrani za dhati kwa wadau wote wa sekta ya uchukuzi na hali ya hewa ikiwemo sekta binafsi kwa ushirikiano wao katika kutimiza malengo yetu. Shukrani zetu pia ziwaendee washirika wetu wa maendeleo katika kutekeleza programu na mipango yetu ya sekta. Washirika hao ni pamoja na Mashirika ya Kimataifa na Taasisi za Kimataifa zinazochangia katika kuboresha utoaji huduma na miundombinu ya sekta zetu. Nchi na mashirika hayo ni pamoja na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga *(ICAO),* Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Majini *(IMO), Intergovemental Standing Committee on Shipping (ISCOS),* Shirika la Hali ya Hewa Duniani *(WMO),* Benki ya Dunia *(WB),* Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB),* Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika *(BADEA),* Kuwait, Jamhuri ya Korea, *OPEC Fund,* Shirika la kuhudumia Wakimbizi Duniani *(UNHCR),* Umoja wa Nchi za Ulaya, Afrika Kusini, Uingereza, Marekani, Uholanzi, Japan, Korea, India, China, Denmark, Norway, Ubeligiji, Ujerumani na wengine wengi. Tungependa waendelee kushirikiana nasi katika kuimarisha sekta yetu na kufanikisha malengo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru tena Kamati ya Bunge ya Miundombinu na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa michango na ushirikiano waliotupa katika kuboresha sekta za uchukuzi na hali ya hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapofika mwisho wa hotuba hii sina budi kuwashukuru viongozi wenzangu katika Wizara nikianza na Naibu Waziri, Mheshimiwa Mhandisi Athuman Rashid Mfutakamba, Mbunge wa Jimbo la Igalula, Tabora, Katibu Mkuu, Mhandisi Omar Abdallah Chambo, Naibu Katibu Mkuu, Ndugu John Thomas Mngodo, Msaidizi wangu, Ndugu Alphonce Mwingira, Wakuu wa Idara, Wakuu wa Vitengo, Viongozi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara pamoja na watumishi wote wa Wizara na Taasisi. Wote kwa pamoja wananipa ushirikiano mkubwa ambao umenisaidia kutekeleza majukumu niliyopewa ya kusimamia uendelezaji wa Sekta za Uchukuzi na Hali ya Hewa. Michango yao ya mawazo na utendaji wao mzuri imetuwezesha kufanya kazi yetu kuwa rahisi na yenye mafanikio. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusimama kwangu hapa leo ni ushuhuda wa malezi bora na miongozo mema waliyonipatia Baba yangu Rashidi Mwagamoyo Nundu, Shangazi yangu Mzuri Nundu, Bibi yangu Mwansada Danga, Mkuu wangu Mwatime Sena Mnyatibu, Kaka yangu Mohamed Nundu na pia walimu wangu wote. Ninawashukuru sana kwa niaba yangu na kwa niaba ya Mama yangu mpenzi Nia Maulid. Mama sikukuona lakini ninakujua na ninakupenda sana na kutokuwepo kwako kwa matakwa ya Mwenyezi Mungu hakukuwa pengo bali dira ya maisha yangu, uadilifu, uchapa kazi na ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ipasavyo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 237,563,802,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 69,585,672,000 ni kwa Matumizi ya Kawaida na shilingi 167,978,130,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha shilingi 40,021,777,800 za mishahara ya watumishi na shilingi 29,563,894,200 ni fedha za Matumizi Mengineyo *(OC).* Fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha shilingi 95,000,000,000 za ndani na shilingi 72,978,130,000 fedha za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba hii nimeambatanisha jedwali la miradi yote itakayotekelezwa katika mwaka 2011/2012 pamoja na kiasi cha fedha kilichotengwa kutekeleza miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa mara nyingine nitoe shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya *www.mot.go.tz. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante! Hoja imetolewa na imeungwa mkono na ninaomba wenzetu wa *Hansard* wairekodi hotuba hii yote kama ilivyotolewa kwenye hiki kijitabu. *(Makofi)*

Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua Bajeti hii Mheshimiwa Peter Serukamba, ili aweze kutoa maoni ya Kamati kuhusu Wizara husika. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabla sijaanza kusoma maoni ya Kamati yangu kuhusiana na Bajeti hii naomba hotuba iliyo kwenye kitabu ndiyo iingie kwenye *Hansard* kwa sababu ninayosoma hapa ni *summary* ya *speech* yetu yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kigoma Mjini kwa heshima kubwa waliyonipa kwa kuendelea kunichagua kuwa mwakilishi wao. Naweza kuwaambia hakika sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati yangu kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, kuhusu taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2011/2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu naipongeza Wizara ya Uchukuzi kwa maandalizi, ushirikiano na mawasilisho mazuri kuhusu taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati na Mipango ya Bajeti ya mwaka wa 2010/2011 pamoja na kazi zilizopangwa kufanyika kwa mwaka wa fedha 2011/2012 sanjari na maombi ya fedha kwa ajili ya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nilikumbushe Bunge lako Tukufu kuwa Wizara hii imeundwa mwezi Novemba, 2010. Kwa sababu hiyo, haikuwa na Makadario ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Hata hivyo, Kamati ilipata fursa ya kujadili utekelezaji wa shughuli za Wizara hii tangu ilipoanzishwa hadi Mei, 2011 pamoja na kuchambua Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2011/2012 kama yalivyowasilishwa mbele ya Kamati. *(Makofi)*

Napenda kutoa taarifa baada ya kupitia Bajeti ya Wizara hii, Kamati yangu haikuridhishwa na Bajeti finyu ambayo haikidhi mahitaji ya utekelezaji wa shughuli za msingi za Wizara hii. Kutokana na hali hiyo, Kamati iliitaka Serikali kutafuta fedha za kutosha kwa ajili ya kuimarisha usafiri wa reli, usafiri wa majini na kukomboa ndege za Shirika la Ndege la Tanzania zilizoko kwenye matengenezo nje ya nchi. Kutokana na hali hiyo, Kamati iliitaka Serikali kutafuta namna ya kupata fedha za kutosha kwa ajili ya kuimarisha usafiri wa reli, usafiri wa majini na kukomboa ndege za Shirika la Ndege la Tanzania zilizoko kwenye matengenezo nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hiyo ilitokana na kuzingatia majukumu ya msingi ya Wizara hii kama yalivyoainishwa katika Hati ya Serikali ya kuanzisha Wizara *(Government Instruments).* Moja ya majukumu hayo ni kusimamia shughuli za uchukuzi hapa nchini. Hata hivyo, tangu tarehe 11 Februari, 2011, hakuna ndege yoyote ya Shirika la Ndege la Tanzania iliyokuwa ikifanya kazi. *(Makofi)*

Aidha, Kampuni ya Meli Tanzania ilikuwa inakabiliwa na matatizo ya uchakavu wa meli zake na madeni makubwa yaliyofikia kiasi cha shilingi bilioni 1.6. Hali hii iliathiri uendeshaji wa Kampuni hiyo pamoja na kuhatarisha usalama wa abiria wanaotumia meli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuongezea maelezo hayo, usafiri wa treni za mizigo na abiria kwa kipindi hicho nao haukuwa wa uhakika na hasa baada ya kutelekezwa na kampuni ya *RITES* jambo liliosababisha kero kubwa kwa usafiri na usafirishaji wa mizigo na abiria. Wananchi wa Kanda ya Magharibi ambao hawana usafiri wa barabara waliathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na kasoro hizo za usafiri wa reli. Athari za tatizo hili ziliongezeka kwa kukosekana kwa usafiri wa ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hali hii niliyoilezea, Kamati ilitegemea kwamba Serikali, kupitia Bajeti ya Wizara hii, ingekuja na mipango kabambe ya kufufua Shirika la Ndege, kuimarisha usafiri wa reli na meli. Hata hivyo, Bajeti iliyoletwa kwenye Kamati kwa mara ya kwanza haikuonyesha dhamira hiyo. Kamati ilijulishwa kuwa mahitaji halisi ya Bajeti ya Wizara kwa ajili ya shughuli za maendeleo kuwa ni shilingi bilioni 492.02. Hata hivyo, randama zilizowasilishwa awali mbele ya Kamati zilionyesha kuwa fedha iliyokuwa imetengwa kwa madhumuni hayo ni shilingi bilioni 167.97 ambazo ni sawa na 34% ya mahitaji halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara ya Miundombinu kwa mwaka 2010/2011, katika Mkutano wa Ishirini wa Bunge la Tisa, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ilitoa maagizo kuhusu mambo mbalimbali ya sekta ya uchukuzi. Nafurahi kusema kuwa Wizara imejitahidi kutekeleza baadhi ya maagizo ambayo ni sehemu ya majukumu yake. Utekelezaji wa maagizo mengine ulipaswa kuripotiwa na Wizara ya Ujenzi kwa kuwa Wizara hizi mbili zimegawana majukumu yaliyokuwa ya Wizara ya Miundombinu hapo awali. Pamoja na hivyo, yapo maagizo ambayo utekelezaji wake haukukamilika kutokana na ufinyu wa Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2010/2011, ukusanyaji Mapato na Matumizi ya Kawaida kama nilivyoeleza awali, Wizara hii ilikuwa ni sehemu ya Wizara ya Miundombinu na kwa hivyo ukusanyaji Mapato na Matumizi ya Kawaida yalikuwa pamoja. Kwa sababu hiyo, imekuwa ni vigumu kwa ya Uchukuzi kuwa na takwimu za peke yake katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Serikali ilitenga shilingi bilioni 160.477 kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo iliyoihusu Wizara hii. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 95.477 zilikuwa ni fedha za ndani na shilingi bilioni 65.132 zilikuwa ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutathimini utekelezaji wa mpango na majukumu kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Kamati ilielezwa mafanikio na changamoto mbalimbali. Moja ya mambo yaliyojitokeza ni ukweli kuwa kutokana na matatizo ya kutokuwa na fedha za kutosha kukidhi mahitaji katika mwaka 2010/2011 Wizara pamoja na taasisi zake hazijaweza kutekeleza malengo yake kwa kiwango cha kuridhisha. Aidha, katika kipindi hicho zilijitokeza changamoto mbalimbali zikiwemo:-

(a) Wizara kutokuwa na uwezo wa kifedha kulinganisha na mahitaji halisi ya miradi ya maendeleo.

(b) Uwezo duni wa sekta binafsi katika ujenzi na matengenezo ya miundombinu.

(c ) Ubovu wa miundombinu ya uchukuzi hasa reli na bandari.

(d) Mrundikano mkubwa wa mizigo katika bandari ya Dar es salaam.

(e) Kuendelea kupanda kwa gharama za vifaa vya Ujenzi kutokana na mfumuko wa bei.

(f) Kuwepo kwa majanga yanayosababishwa na hali ya hewa ikiwemo mafuriko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuwepo kwa changamoto hizo, Kamati ilielezwa baadhi ya mikakati ya kukabiliana na changamoto zilizotajwa ikiwemo ifuatayo:-

(a) Kuimarisha uwezo wa kiutendaji wa bodi na taasisi zilizo chini ya Wizara ili ziweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

(b) Kufanyia mapitio Sera ya Taifa ya Uchukuzi ya mwaka 2003 na kuandaa mikakati yake ili iweze kuendana na mahitaji ya sasa na ya baadaye katika maeneo yote ya uchukuzi.

(c ) Kufanya mapitio ya utendaji wa sekta ya Uchukuzi na Hali ya Hewa.

(d) Kufanya mapitio ya Sheria na Mikataba ya Uchukuzi ili ziwe katika viwango vinavyokubalika na kuweza kuendana na zile za Kikanda kama vile *EAC* na *SADC.*

(e) Kuendelea kufanya marekebisho ya Sheria za Kisekta ili ziendane na mazingira na mfumo wa utendaji uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwelekeo wa Bajeti na Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2011/2012. Katika kikao cha Kamati cha kupitia na kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, Kamati ilielezwa kuwa katika Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara inalenga kuendelea kusimamia utekelezaji wa miradi yote ya uchukuzi sambamba na kuboresha huduma za Hali ya Hewa na Taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara kupitia Idara mbalimbali na vitengo vyake inatarajia kukusanya jumla ya shilingi 26,000/= kiwango ambacho ni kidogo na pengine ni kwa ajili ya kulinda kasma inayohusu mapato *(token).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 Wizara imetengewa jumla ya shilingi 69,585,671,800 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 40,012,777,800 ni kwa ajili ya kulipia mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi zake na shilingi 29,563,894,000 ni fedha kwa ajili ya Matumizi Mengine *(OC). (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokutana na Wizara hii mwezi Mei, 2011 ilielezwa kuwa kwa mwaka 2011/2012 Wizara imetengewa shilingi 167,978,130,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 95,000,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 72,978,130,000 ni fedha za nje. Hata hivyo, Kamati ilipokutana na Wizara hii tarehe 16 Juni, 2011

ilielezwa kuwa Serikali imeahidi kuiongezea shilingi bilioni 95.6 kwa ajili ya shughuli za maendeleo nje ya Bajeti iliyowasilishwa awali katika mgawanyo ufuatao:-

(a) Ununuzi na ukarabati wa vifaa vya uendeshaji wa reli shilingi bilioni 29.6;

(b) Kulipa madeni ya *TRL* shilingi bilioni 20.2;

(c) Miradi ya sekta ndogo ya reli shilingi bilioni 23;

(d) Kuboresha huduma za Shirika la ndege Tanzania shilingi bilioni 21.27; na

(e) Kulipa madeni na bima za Kampuni za Huduma za Meli *(MSCL)* shilingi bilioni 1.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa reli katika uchumi wa nchi unafahamika duniani kote. *Warren Buffett,* mwekezaji na bilionea maarufu nchini Marekani wakati ananunua Kampuni kubwa ya Reli Duniani (*BNSF),* alisema na nanukuu*; "Railroads represent the future. They're best-positioned to haul the raw material and finished goods for a nation and economy. Unlike trucks, trains don't have to compete on congested highways. Nor do railroads depend on strapped governments to maintain infrastructure."* Mwisho wa kunukuu.

Tafsiri isiyo rasmi ya kauli hiyo ni kwamba; "Njia ya reli inamaanisha mustakabali mzuri. Ni njia bora zaidi kusafirishia malighafi kwa ajili ya Taifa na uchumi wake. Kinyume na malori, usafiri wa garimoshi hauhitaji kushindana katika msongamano kwenye barabara kuu. Aidha, usafiri wa reli hautegemei sana ukarabati unaofanywa na Serikali yenye uwezo mdogo kifedha." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo hayo, ni dhahiri kuwa katika uchumi wa Tanzania, sekta ya usafirishaji na uchukuzi inategemea usafiri wa reli kwa kiasi kikubwa. Ni usafiri unaosaidia kusafirisha mizigo mingi kwa wakati mmoja. Kulithibitishia Bunge lako Tukufu, utafiti umebaini kuwa mizigo inayosafirishwa na treni mara moja, ikisafirishwa kwa njia ya barabara, itahitaji wastani wa malori 62 kuisafirisha. Hali hii ndio hasa iliyomfanya mwekezaji huyu wa Kimarekani niliyemnukuu awali kusema na naomba nimnukuu tena; *"The rail business is actually in tune with the future. Trains move goods using far less fuel than alternatives."*Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana ya maneno hayo ni kuwa biashara ya reli inakubaliana kabisa na dhana ya kuzingatia mustakbali wa baadae. Garimoshi husafirisha mizigo mingi zaidi kwa kutumia mafuta kidogo ikilinganisha na njia nyingine za uchukuzi na usafirishaji. Hali hii huwezesha bidhaa zinazosafirishwa kwa treni kuwa na bei nafuu katika soko na hivyo kuzuia mfumuko wa bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli zetu zote zina matatizo na hivyo kutokidhi matarajio ya wananchi na nchi jirani zinazohudumiwa na reli hizo. Tukiendelea na mwenendo tulionao nchi yetu itaachwa nyuma kimaendeleo, kwani nchi jirani zinajenga na kuimarisha reli zao kwa kasi kubwa.

Kamati imefanya utafiti na kugundua kuwa nchi ya Angola inajenga reli kuanzia Bandari ya Benguela hadi Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ambayo ikikamilika mwaka 2012. Aidha, nchi ya Msumbiji inajenga reli kuanzia Bandari ya Nacala kwa ajili ya kuhudumia nchi za Malawi, Zambia na Zimbabwe. *(Makofi)*

Tafsiri yake ni kwamba reli ya Kati na Reli ya *TAZARA* hazitakuwa na mizigo ya kutoka na kwenda nchi za Zambia, Malawi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo au kutakuwa na ushindani mkubwa kutokana na kujengwa kwa reli hizo. Kutokana na ushindani unaotarajiwa Kamati inashauri Serikali kuharakisha ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge* na pia kuimarisha reli ya *TAZARA* kwa ajili ya kuhimili ushindani na kuinua uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inapaswa kuwa makini zaidi na kuchukua uamuzi wa haraka kushughulikia reli zetu kwani reli ya Nacala – Malawi itakapokamilika itakuwa na unafuu zaidi kwa Malawi kuliko kutumia reli ya *TAZARA* ambayo mizigo yake inashushwa Mbeya na kusafirishwa kwa malori kupitia Tukuyu, Kyela na Kasumulo kupelekwa Malawi wakati reli ya Msumbiji – Malawi itashusha mizigo nchini Malawi na hivyo wenzetu wa Msumbiji kuteka biashara

ya mizigo kutoka Malawi kwani Malawi haitapata usumbufu wanaopata wa kupakia na kupakua mizigo njiani kama inavyotokea hivi sasa kwa kutumia reli ya *TAZARA. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miji mingine reli pia zinatumika kusafirisha abiria katika miji yao. Kamati inashauri usafiri wa reli jijini Dar es Salaam uanzishwe ili kupunguza msongamano wa magari jijini. Usafiri ukianza utasaidia kupunguza msongamano wa magari. Kusudio lililopo ni kuanzisha usafiri wa treni kuanzia stesheni ya Dar es Salaam hadi Ubungo Maziwa. Usafiri huo ukianza inakisiwa kuwa utasafirisha abiria wapatao 9,600 kwa siku. Hii itasaidia pia kuinua uchumi wa jiji la Dar es Salaam na Taifa kwa ujumla kwani wakazi wa jiji watafika maeneo yao ya uzalishaji mali kwa wakati na bila ya uchovu wa kuwa katika foleni kwa muda mrefu kama ilivyo sasa. Baada ya eneo hili kuanza kupata usafiri wa treni mpango wa usafiri wa aina hii kwa reli ya *TAZARA* kutoka stesheni ya Mwakanga hadi stesheni ya *TAZARA* Dar es salaam pia uanze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ina wataalam wa kutosha kujenga na kuendesha usafiri wa reli. Badala ya kupuuza uwezo wa ndani na kuthamini wawekezaji wa nje, ni vema Serikali iboreshe mazingira ya kufanyia kazi na kuwapatia vifaa na maslahi ya kutosha wataalamu wetu. Serikali ikumbuke kuwa ni wataalam wa Kitanzania waliofufua reli iliyong'olewa na mafuriko kati ya Kilosa na Gulwe na kufufua injini za treni ambazo mwekezaji wa *RITES* alizitelekeza kwa maelezo kuwa hazifai tena. Kamati inashauri wataalam na wafanyakazi waliopo wathaminiwe kwa dhati ili waweze kutoa mchango wao kwa dhati katika kuleta ufanisi wa reli yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafiri wa anga na viwanja vya ndege. Ulimwengu wa utandawazi unaendeshwa na usafiri wa anga. Kasi ya maendeleo ya nchi yetu itategemea ni kwa kiasi gani nchi yetu inafikiwa na mashirika makubwa ya ndege duniani, lakini pia ni kwa kiasi gani sehemu mbalimbali za nchi yetu zinaunda mtandao wa usafiri wa anga, umefika wakati sasa nchi yetu kutumia fursa yake ya kijiografia. Katika kufanikisha azma hiyo, ni vema Serikali ikiwezeshe kiwanja cha Ndege cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Dar es salaam, kuwa kitovu (*Hub*) cha safari za ndege katika ukanda huo. Aidha, viwanja vingine vyote nchini viboreshwa ili kutengeneza mtandao wa safari za anga nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Ndege Tanzania *(ATC)* kwa nchi nyingi duniani, Mashirika ya Ndege ya Taifa *(National Flag Carrier)* ni sehemu ya utambulisho wa Taifa na ni fahari ya nchi hizo. Miaka ya nyuma, Shirika la Ndege Tanzania *(ATC)* lilikuwa pia vivyo hivyo kwa nchi yetu. Hata hivyo, leo hii hali ni tofauti. *(Makofi)*

Kwa sasa Kampuni ya Ndege ya Tanzania *(ATCL)* inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo kukabiliwa na madeni makubwa. Hadi kufikia Desemba, 2010 ilikuwa na madeni ya jumla ya shilingi bilioni 75.99. Kutokana na madeni hayo miongoni mwa wadai *(Celtic Capital Corporation* na Kampuni ya Ndege ya Afrika Kusini) wameamuliwa na mahakama kukamata mali za *ATCL.* Kamati, inashauri Serikali itoe fedha za kutosha kulipa madeni haya ili kulinusuru shirika hili na kuondoa aibu kwa Taifa letu. Aidha, Serikali iwekeze kiasi cha kutosha cha fedha ili kuifufua *ATCL. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *ATCL,* ina ndege tatu ambazo zote kwa sasa hazifanyi kazi. Licha ya hali hiyo, Kampuni hii ina wafanyakazi 182 wanaoendelea kulipwa na kupata huduma zingine za kiutumishi. Hii ni gharama kubwa katika uendeshaji na kuitia hasara Serikali kwani pamoja kutokuzalisha au kutokutoa huduma yoyote wanalipwa mishahara na stahili zingine za utumishi. Kamati inashauri kuwa wafanyakazi hawa wapewe vitendea kazi vya kutosha sanjari na Serikali kuhakikisha kuwa ndege zilizopo zinafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya matatizo makubwa katika uendeshaji wa Mashirika ya Umma ni kuingiliwa katika utendaji na maamuzi yake. Kamati inashauri kwamba Makampuni yetu yapewe mamlaka ya kufanya kazi kibiashara bila kuingiliwa na Serikali. Kuna wakati menejimenti inashindwa kutoa maamuzi ya kujiendesha kibiashara kwa sababu ya kupokea maelekezo kutoka Serikalini au kushindwa kufanya maamuzi kutokana na kuchelewa maelekezo au vibali kutoka Serikalini. Aidha, urasimu usio wa lazima uondolewe katika kutoa maamuzi yanayohusu uendeshaji wa Kampuni hii na nyinginezo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ushindani wa kibiashara kuwa mkubwa Kamati inashauri kuwa *ATCL* ishirikiane na *airlines* zingine duniani badala ya kufanya kazi peke yake. Moja ya sababu kubwa za mafanikio ya Shirika la Ndege la Kenya ni kushirikiana na mashirika ya ndege makubwa tisa duniani na pia ni mwanachama wa *Skyteam* yenye mashirika ya ndege 14 duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umekuwepo mjadala kuhusu mfumo sahihi wa umiliki, uendeshaji na umiliki wa Shirika la Ndege. Wapo wanaoamini kwamba Shirika hili ni lazima limilikiwe na Serikali kwa asilimia 100 na wapo wanaoamini kwamba sio lazima iwe hivyo, na kwamba cha muhimu ni ufanisi katika uendeshaji wa Shirika. *(Makofi)*

Kamati inaamini kwamba moja ya sababu iliyofanya Shirika la Ndege la Kenya lifanikiwe ni kuondoa ukiritimba kwenye umiliki wake na kuiendesha kibiashara. Mpaka kufikia tarehe 31 Machi, 2006 wanahisa walikuwa kama ifuatavyo; Taasisi za Kenya 37.20%, Wananchi wa Kenya 30.94% lilipobinafsishwa mwaka 1996. Hata hivyo halikubinafsishwa kwa nchi moja au Shirika moja bali kwa watu na Taasisi tofauti ikiwemo, raia wengine wa Afrika Mashariki 0.03% Taasisi zingine za Afrika Mashariki 0.13%, raia wa kigeni 1.36% na Taasisi za kigeni 30.34%.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utabaini kuwa 68.14% ya hisa zote za Shirika la Ndege la Kenya ni mali ya Wakenya wenyewe, sio Serikali. Utaratibu wa umiliki huu ndiyo unaofaa katika michakato ya ubinafsishaji wa Mashirika na Taasisi zetu hapa nchini ikiwemo reli, bandari na zingine nyingi kwani unaondoa ukiritimba ambao umekuwa ukisababisha migogoro katika uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo hoja kwamba Shirika la Ndege Tanzania halina haja ya kuwepo, na kwamba cha msingi tu ni uhakika wa usafiri wa ndege. Kamati haikubaliani na hoja hii. Kamati inaamini kwamba ni muhimu kuwa na kampuni kubwa ya Ndege ya Tanzania ili pato kubwa linatokana na usafiri wa anga libaki hapa nchini. Kwa mfano, katika sekta ya utalii utafiti unaonyesha kuwa 60% ya mapato yanayotokana na utalii wa ndani ya nchi yanaenda kwenye makampuni ya ndege yanayosafirisha watalii. Hii ina maana kwamba juhudi kubwa zinazofanywa na nchi yetu kutangaza vivutio vya utalii nchini zitanufaisha zaidi mashirika ya ndege yanayowaleta watalii nchini kuliko sisi wenye vivutio hivyo, *ATCL* ingeimarishwa ingesaidia kuongeza mapato hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bandari na usafiri wa majini, asilimia zaidi ya 60 ya Watanzania wanaishi umbali sio zaidi ya kilomita 100 kutoka kwenye aidha fukwe za bahari au maziwa. Kwa maana hiyo, Watanzania wengi wanategemea usafiri wa maji na uchumi na maendeleo ya sehemu kubwa ya nchi yetu yanategemea pia usafiri wa majini. Usafiri huo ni rahisi kwa gharama, huchukua watu wengi zaidi, husafirisha mizigo mizito na mikubwa kwa uhakikia zaidi. Vilevile, ni usafiri salama ukipangwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri katika Maziwa ya Tanganyika, Nyasa na Viktoria kwa sehemu kubwa unahudumiwa na Kampuni ya Huduma za Meli *(MSCL).* Kampuni hii imeanzishwa mwaka 1999 ikiwa na meli 15, bandari, vyelezo, miundombinu, karakana na majengo ya ofisi. Hata hivyo mwaka 2006 ilianzishwa Mamlaka ya Bandari Tanzania ambayo ilichukua kila kitu pamoja na meli ya Mv. Umoja na Kampuni hiyo ikabakiwa na meli 14 tu. Hata hivyo, meli zinazofanya kazi ni tano tu, tena zikiwa chakavu na hivyo kuhatarisha usalama wa wasafiri. Vilevile Kampuni hii haina ofisi, haina bodi ya wakurugenzi na hivyo haiwezi kutoa mahesabu ya shirika. Vilevile upo utata wa umiliki wa meli ya Mv. Umoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali itoe mtaji wa kutosha ili Kampuni hii iweze kujiendesha kwa faida. Kwa mwaka 2011/2012 Serikali imeahidi kutoa shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya kulipa madeni na bima za meli za Kampuni hii. Hata hivyo, Bajeti halisi inayoweza kuikwamua Kampuni hii ni shilingi bilioni 5.4. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Huduma za Meli *(MSCL)* ilikuwa sehemu ya Mamlaka ya Reli na Bandari Tanzania. Mpango wa kubinafsisha reli na bandari haukuweka wazi hatima ya Kampuni ya Huduma za Meli *(MSCL)* jambo linalosababisha kutakuwa bayana iwapo kampuni hiyo nayo iko katika mpango wa kubinafsishwa au laa. Hali hii inaathiri utendaji wake kwani

haiwezi kutoa ajira za kudumu kwa kutojua hatma yake ikiwemo kushindwa kuwa na uwekezaji mkubwa. Hali hii imekatisha tamaa wafanyakazi wengi na hivyo kuzorotesha Kampuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bandari ya Dar es Salaam, zipo nchi duniani kwa mfano Singapore na Hong Kong ambazo uchumi wake unaendeshwa na bandari tu. Nchi yetu inayo bahati kubwa ya kuwa na ufukwe unaoweza kuhudumia nchi nane zisizo na bahari. Lakini pia tunao ufukwe mrefu zaidi ya kilomita 800, unaowezesha kuwa bandari kubwa zaidi ya sita – Tanga, Mwambani, Bagamoyo, Dar es Salaam, Lindi na Mtwara. Hii ni fursa kubwa ambayo nchi chache sana duniani zimejaaliwa. Hata hivyo, bado hatujafanikiwa kutumia fursa hii ya kijiografia. Kamati inaamini kwamba ni lazima hali hii ibadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Dar es Salaam ni muhimu sio tu kwa uchumi wa nchi yetu bali pia kwa ustawi wa nchi jirani. Hata hivyo, kwa kipindi kirefu sasa kumekuwa na malalamiko makubwa kutoka kwa Watanzania na majirani zetu kuhusu ufanisi na matatizo ya bandari hii na viongozi wa Wizara na wengineo Serikalini wanayajua matatizo haya. Kamati inatambua kwamba kumekuwa na jitihada mbalimbali, ikiwemo za viongozi wakuu katika Serikali za kuyapatia ufumbuzi, hata hivyo, matatizo hayo bado hayajapatiwa ufumbuzi. *(Makofi)*

Kamati inashauri kwamba sasa ufike wakati matatizo hayo ambayo mengi yanahusu maamuzi ya Serikali yamalizwe na vilevile Kamati inaamini kwamba Bandari ya Dar es Salaam ni lazima ipanuliwe kukidhi mahitaji yanayoongezeka. Kamati inashauri bandari ya Dar es Salaam iendelee kuimarishwa ili iweze kuhudumia mizigo mingi zaidi hasa kwa kujenga gati namba 13 na 14. *(Makofi)*

Kamati inashauri pia Mamlaka ya Bandari ipewe eneo la Vijibweni lenye ukubwa wa hekta 112 pamoja na eneo la Kurasini lenye ukubwa wa hekta 63 kwa ajili ya upanuzi wa bandari pamoja na shughuli nyingine za bandari. Aidha, ili kupunguza msongamano, ni vema Mamlaka ya Bandari iweke utaratibu wa kutumia mageti mawili, moja la kuingilia kwenda kuchukua mizigo na lingine la magari yanayotoka baada ya kuchukua mizigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka ya hivi karibuni kumekuwa na mabadiliko makubwa ya tabianchi ambayo yanasababisha kuongezeka kwa joto duniani, uharibifu wa ukanda wa Ozoni na mvua ya asidi na matukio makubwa yanayoendana na mabadiliko ya hali ya hewa. Matukio haya yameanza kuwa na athari kubwa kiuchumi, kijamii na katika mazingira yetu na athari hizi zinategemewa kuongezeka. Ili kukabiliana na matatizo haya, Mamlaka ya Hali ya Hewa hufanya kazi ya kuchunguza, kufuatilia, kutafiti na kutoa matokeo, tahadhari na ushauri kwa jamii na Taifa kwa ujumla juu ya namna ya kuepuka athari zinazotokana na mabadiliko ya hali ya hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri na tahadhari zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa ni muhimu sana kwa mustakabali wa maendeleo ya nchi yetu katika nyanja za kilimo, usafiri wa anga, huduma za usafiri na uvuvi wa baharini na shughuli za kila siku za maisha ya watu. Katika nchi zilizoendelea duniani, watu wake wakiamka asubuhi kitu cha kwanza kuangalia ni utabiri wa hali ya hewa ya siku hiyo. Shughuli na mipango mingi hupangwa kutegemea taarifa za utabiri wa hali ya hewa. Hata hivyo, Kamati inasikitishwa na hali iliyopo kwani pamoja na umuhimu wa Mamlaka hii, kwa mwaka wa 2011/2012, haijatengewa kiasi chochote cha fedha kwa ajili ya maendeleo yake, Kamati inashauri Mamlaka hii iimarishwe. Ni muhimu ipewe vifaa vya kisasa na kujengewa uwezo wa kutosha wa kitaalamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhitimisha, Kamati inashauri kwamba ili kuiwezesha sekta ya uchukuzi kuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi, kuna umuhimu mkubwa wa kuzihusianisha huduma zote zinazohusika na uchukuzi na usafirishaji na kuziendeleza kwa pamoja. Kwa mfano, bandari haiwezi kufanya vizuri kama reli haifanyi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kueleza maoni na ushauri kuhusu usafiri Dar es Salaam, napenda kukumbusha kuwa suala la usafiri Dar es salaam ni tatizo linalohitaji kufanyiwa kazi ipasavyo. Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu namna suala hili la kisera linavyoshughulikiwa na hatimaye kuishauri Serikali juu ya utatuzi wa kero hii sugu. Naomba kutoa taarifa kwamba kwa

kuzingatia nafasi ya Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA) katika uboreshaji wa usafiri jijini humo, Kamati ilikutana na Wizara ya Uchukuzi mara mbili pamoja na baadhi ya wadau wengine ikiwemo Menejimenti ya Shirika hilo ili kuona hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kuboresha huduma ya usafiri. *(Makofi)*

Kutokana na taarifa zilizowasilishwa kwenye vikao hivyo, Kamati ilibaini kuwa utendaji wa Shirika la UDA umeendelea kuzorota na kwamba kuna dalili za ubadhirifu wa mali na mapato ya Shirika hilo. Kwa mfano, mchakato wa kuendelea kuuza hisa za Serikali umeonekana kuwa na mashaka. Katika ubinafsishaji unaoendelea, malipo yanaoneka kufanyika kwa kupitia akaunti za watu binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia hali hiyo, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(a) Serikali iharakishe mchakato wa Wanahisa kujadili suala zima la uuzaji wa hisa za UDA;

(b) Serikali ifanye tena mapitio ya Mkataba wa mauzo ya Hisa zisizogawiwa *(unallocated shares)* ulioingiwa kati ya UDA na Kampuni ya *Simon Group;*

(c) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aagizwe kufanya ukaguzi maalum *(Special Audit);* na

(d) Aidha, TAKUKURU itekeleze wajibu wake ipasavyo kwa kufuatilia na kuchunguza mchakato huo. *(Makofi)*

Kwa upande wa Bunge, Kamati ya Bunge ya Miundombinu imeunda Kamati ndogo ili kufuatilia jambo hili na taarifa ya ufuatiliaji wa Kamati itatolewa katika Mkutano wa Tano wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara imetengewa jumla ya shilingi 69,585,671,800/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 167,978,130,000/= kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Kamati yangu ilipitia na kujadili kwa kina Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Miundombinu na kupitia kifungu kwa kifungu na kuipitisha, Kamati yangu inaliomba Bunge lako Tukufu kukubali kupitisha maombi hayo ya fedha kwa Wizara ya Uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Bandari ya Dar es salaam iendelee kuimarishwa ili iweze kuhudumia mizigo mingi zaidi hasa kwa kujenga gati namba 13 na 14. Kamati inashauri pia Mamlaka ya Bandari ipewe eneo la Vijibweni lenye ukubwa wa hekta 112 pamoja na eneo la Kurasini lenye ukubwa wa hekta 63 kwa ajili ya upanuzi wa bandari pamoja na shughuli nyingine za bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijahitimisha hotuba yangu, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati yangu. Nawashukuru pia Mhesimiwa Omari Rashid Nundu, Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Athumani Rashid Mfutakamba, Naibu Waziri wa Uchukuzi, *Engineer* Omar Abdallah Chambo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi pamoja na wataalamu wote wa Wizara hii na taasisi zilizo chini yake kwa ushirikiano, ushauri na utaalam wao ambao kwa kiwango kikubwa umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha taarifa hii leo katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo ada naomba pia niwashukuru wajumbe wenzangu wa Kamati hii kwa busara zao, hasa kwa kutekeleza kazi za Kamati kwa umahiri na umakini mkubwa wa kupitia na kuchambua Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii na hivyo kufanikisha taarifa hii, ambayo kwa niaba yao naiwasilisha leo katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa napenda kuwatambua Wajumbe wanaounda Kamati ya Miundombinu, ambao ni Mheshimiwa Peter Serukamba, Mwenyekiti, Mheshimiwa Anne Malecela, Makamu Mwenyekiti na wajumbe ambao ni Mheshimiwa Saidi Arfi,

Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Innocent Kalogeris, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Moses Machali, Mheshimiwa Salvatory Machemli, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa na Mheshimiwa *Engineer* Ramo Makani.

Wengine ni Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Regia Mtema, Mheshimiwa Mbarouk Rajab Mohamed, Mheshimiwa Faith Mitambo, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mheshimiwa Henry Shekifu Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Haroub Mohammed Shamis, Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa Jeremiah Sumari, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya na Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashillilah, kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa na Katibu wa Kamati hii Ndugu Angumbwike Ng'wavi kwa kuihudumia Kamati ya Miundombinu kwa ufanisi mkubwa na kuandaa taarifa hii. Nawashukuru pia watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao mzuri wa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamaliza naomba nitumie nafasi hii kushukuru familia yangu, nimshukuru mke wangu, watoto wangu wawili Ilakoz na Bizimana kwa moyo wanaonipa na najua wananikosa sana lakini nahudumia Taifa letu, naomba Mungu awasaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba sasa kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Peter Serukamba, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu baada ya uwasilishaji wake mzuri na kupokea hizo salamu ingawa hujatutajia mke wako anaitwa nani basi naomba sasa nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya. Wasemaji leo wote wanatoka Mkoa wa Kigoma. Huku Kigoma nadhani treni inatakiwa kwa nguvu sana huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mhonga kwa niaba ya Kambi ya Upinzani. *(Kicheko)*

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni ya 99(7) toleo la Mwaka 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, kwa kuniteua kuwa Waziri Kivuli wa Wizara ya Uchukuzi. Namshukuru kwa miongozo yake na uongozi thabiti akishirikiana na Naibu wake Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe pamoja na Mnadhimu Mkuu wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Tundu Antiphas Lissu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru wananchi wa Mkoa wa Kigoma hasa akinamama kwa imani yao kwangu na kunipitisha ili kuwa mgombea Ubunge kwa Viti Maalum na hatimaye kuwa Mbunge. Aidha, nishukuru kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kazi zangu. Natoa ahadi kwenu kuwa nitazidi kusimamia yale yote mliyonituma niyafanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa naomba pia kumshukuru Mama yangu mpenzi Kuruthum Mohamed pamoja na ndugu na jamaa zangu wote kwa kunipa moyo pale mikiki mikiki ya kisiasa inapokuwa katika hali ya juu. Pia napenda kutambua uwepo wa *Aunt* yangu *Mrs. Joyce Makele* na *group* zima la watendaji *Project Honour* wanaosaidia wanawake wanaopitia mazingira magumu Afrika, wapo hapo juu kwenye *gallery*. Nawashukuru kwa kusubiri hotuba yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Uupinzani Bungeni bila ya woga wala upendeleo imekuwa ikisema ukweli kuhusiana na jinsi Taifa letu linavyoongozwa na kufichua maovu yote kwa lengo la kuhakikisha kuwa mlipa kodi wa Tanzania anapata maendeleo kulingana na thamani ya kodi anayolipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya sekta ya uchukuzi ni miongoni mwa sekta za kimkakati katika uchumi wa Tanzania. Nafasi ya kijiografia ya Tanzania inatoa upendeleo wa kipekee kwa sekta hii kuwa sekta kichocheo kwa ukuaji wa uchumi wa Taifa letu. Sekta hii hutengeneza mazingira mazuri yanayosaidia kusukuma maendeleo katika shughuli nyingine za kiuchumi na inatengeneza ajira nyingi sana. Sekta hii inajumuisha usafiri wa reli, barabara, anga na usafiri wa majini. *(Makofi)*

Hapa Tanzania, sekta hii ni mojawapo ya sekta zinazokua kwa kasi na mchango wake katika Pato la Taifa ni takribani asilimia 5.1; hii ni takribani mara mbili ya mchango wa sekta ya madini katika *GDP* na zaidi ya mara nne ya mchango wa sekta ya uvuvi katika uchumi. Ukuaji huu wa asilimia 5.1 maana yake ni kuwa sekta hii imechangia shilingi trilioni 1.6 katika uchumi wa nchi kwa mwaka 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya kuimarisha sekta ya uchukuzi ni ndogo mno kulinganisha na majukumu ya Wizara. Kwa mwaka 2011/2012 fedha za maendeleo zilizotengwa ni shilingi bilioni 167.98, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 95 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 72.98 ni fedha za wadau wa maendeleo. Mahitaji halisi ya fedha za maendeleo ni shilingi bilioni 492.02. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya majukumu ya msingi yaliyomo katika sera ya uchukuzi ya mwaka 2003 ni kuhakikisha usafirishaji wa bidhaa zinazopitia kwenye bandari zetu kwenda nchi jirani ni salama. Kambi ya Upinzani inaona hili litawezeshwa vizuri kama bidhaa hizo zitasafirishwa kwa kutumia usafiri wa reli badala ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya uchukuzi imeweka wazi kile ambacho Kambi ya Upinzani katika hotuba yake mbadala ilisisitiza yaani kukuza uchumi katika maeneo ya vijijini hasa maeneo ambayo yanatoa mazao kwa wingi. (Sera ya uchukuzi ya mwaka 2003, kifungu cha 3:4:1). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafiri wa nchi kavu, wananchi wengi wanatumia aina hii ya usafiri katika kutimiza majukumu yao ya kila siku, iwe kwa mabasi, treni au magari madogo. Lakini kwa safari ndefu, yanayotumika zaidi ni mabasi. Inasemekana kwamba mabasi mengi yanayotumika hapa nchini yanatokana na malori yaliyobadilishwa bodi na kutengenezwa kuwa mabasi. Mabasi yanayopatikana kutokana na hali hii mara nyingi huwa hayana ubora na mengine yanakosa sifa ya kuweza kubeba abiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miji yenye mabasi mengi yanayotoa huduma kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine ni Dar es Salaam mabasi 7573, Mbeya mabasi 1433, Mwanza mabasi1152. Miji hii haina tatizo la usafiri kutokana na barabara kuwa nzuri. Lakini kuna mikoa ambayo ina matatizo ya usafiri wa reli pia barabara ni mbaya sana, hivyo hata idadi ya mabasi yanayotoa huduma katika mikoa hiyo si kubwa, Rukwa mabasi 52, Manyara 51, Bukoba 21, Tabora 18, Lindi 54 na Kigoma 152. Serikali iharakishe kutengeneza barabara ili wananchi wapate usafiri ambao utakuwa wa haraka, lakini pia reli ni muhimu hasa kwa baadhi ya mikoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajali nyingi za barabarani zimesababisha Watanzania wengi kupoteza maisha na kumekuwepo na vyombo vingi vya kuzuia ajali, ikiwemo *speed governor* ambayo imeshindwa. Lakini kwa sasa kuna mpango mpya ulioletwa na Kampuni ya *U-Track* ambao kwa mantiki hauna tofauti na unaotumiwa na Jeshi la Polisi (matrafiki) maarufu kama tochi tofauti ni kwamba *u-track* unategemea sana minara ya simu za mikononi na *Vodacom* ni wadau wakubwa katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka inayodhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini *(SUMATRA)* imehusika vipi katika hili, mkataba una unaonyesha kuwa *TABOA* ndio walioingia makubaliano na

*U-Track Africa Ltd.,* kampuni ambayo kwa taarifa zilizopo ni kuwa imeshindwa kutoa tija nchini Kenya na uwezo wake ni mdogo sana. Ajali zinazotokea si za mabasi ya abiria tu bali ni magari ya aina zote, hivyo *TABOA* kuchukua jukumu la *SUMATRA* ni kosa kubwa, *SUMATRA* ndio wasajili wa magari yote yanayobeba abiria sio *TABOA. (Makofi)*

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge kwa nini mambo yanayosababisha wananchi kuongezewa bei ya nauli bila kuhusisha asasi zilizoundwa kisheria kwa kazi yanatendeka bila Serikali kutoa taarifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji *(NIT)* ni taasisi muhimu katika kuandaa madereva, wataalamu wa sekta ya usafirishaji pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa mamlaka mbalimbali katika kuboresha usafiri. Hata hivyo, chuo hicho kimekuwa kikikabiliwa na tuhuma na migogoro mbalimbali pamoja na matatizo ya kiutendaji hali inayoathiri ufanisi wa chuo hicho. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza namna ambavyo imeshughulikia matatizo mbalimbali katika Chuo hicho pamoja na kuwa na mkakati wa kukiboresha kwa ajili ya manufaa kwa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA), Serikali ilikuwa inamiliki asilimia 100 ya hisa za UDA. Mwaka 1983 Msajili wa Hazina alitoa hisa 51% kwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa madhumuni ya kwamba Jiji liboreshe na kuendeleza usafiri wa kisasa Jijini. Hivyo Serikali ilibakiwa na hisa 49%. Kwa Tangazo la Serikali *(Government Notice)* Na. 543 la 1997, UDA iliwekwa chini ya Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(PSRC)* kwa lengo la kubinafsishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *PSRC* ilitangaza uuzaji wa hisa za Serikali katika UDA ambapo kati ya wawekezaji waliojitokeza hakupatikana mwekezaji mahiri wa kununua hisa hizo. Zoezi hili lilirudiwa tena bila mafanikio na hadi *PSRC* inamaliza muda wake mwezi Desemba, 2007 na shughuli zake kuchukuliwa na *CHC,* mwekezaji mwenye sifa alikuwa bado hajapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008 ilijitokeza Kampuni ya *Simon Group* ikiwa na nia ya kununua hisa za Serikali. *Simon Group* alitambulishwa na Bodi ya UDA kwenye Kamati ya Bunge ya Miundombinu. Wizara ya Fedha baada ya kupata taarifa za kupatikana kwa mnunuzi wa hisa za Shirika la UDA iliishauri Wizara ya Miundombinu iandae Waraka wa Baraza la Mawaziri ili kupata kibali cha Serikali cha kutekeleza azma hiyo. Mchakato huu haukukamilika kwa sababu wadau walishauri kuwa Kampuni ya *Simon Group* ishindanishwe na mwekezaji atakayepatikana afanyiwe tathmini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mchakato wa maandalizi ya Waraka ukiendelea, Bodi ya UDA bila kuihusisha Serikali (Msajili wa Hazina) zilipatikana taarifa kuwa hisa ambazo zilikuwa hazijagawiwa *(unalloted shares)* zimeuzwa kwa Kampuni ya *Simon Group,* hisa 7,880,000 kwa shilingi 1,142,643,935/= kwa mkataba uliosainiwa tarehe 11 Februari 2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *Simon Group* ilitakiwa ilipe shilingi milioni 400 kama *commitment fee* kwenye akaunti binafsi ya Mwenyekiti wa Bodi kwa sababu iliambiwa kuwa akaunti za UDA zilikuwa na *overdraft* kwa wakati huo. Waliambiwa kuwa mara akaunti za UDA zitakapokuwa na fedha na *overdraft* kumalizika, hiyo *commitment fee* ingehamishiwa kwenye akaunti ya UDA. Inadaiwa kuwa kiasi cha shilingi milioni 320 zililipwa kwa utaratibu huo. Lakini hadi Kampuni ya *Simon Group* ilipochukua uongozi wa UDA, fedha hizo zilikuwa bado hazijahamishiwa kwenye akaunti ya UDA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa vifungu vya mkataba huo, ilitakiwa Mkutano Mkuu Maalum wa Kampuni *(Extra Ordinary General Meeting)* ufanyike ndani ya wiki mbili tangu mkataba huo ulipotiwa saini ili Kampuni ya *Simon Group* itambulishwe kwa wanahisa wengine, Bodi ya UDA iliyopo ivunjwe na iundwe Bodi mpya na Menejimenti ya UDA ikabidhiwe kwa *Simon Group.* Hata hivyo, mkutano huu maalum haukufanyika kama ilivyotarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkutano maalum wa wanahisa uliohudhuriwa na *Simon Group* na Halmashauri ya Jiji ulifanyika tarehe 10 Juni 2011. Katika mkutano huu, Msajili wa Hazina

hakuhudhuria. Kwenye mkutano huu Meneja Mkuu wa UDA alisimamishwa kazi, wajumbe wa Bodi ya UDA (Iddi Simba, Bakari King'obi na Salum Mwanking'inda) walisimamishwa, mamlaka ya wanaosaini akaunti za UDA kutoa pesa yalitenguliwa na *Simon Group* alipewa mamlaka ya kuiendesha UDA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani imebaini kuwa Mkutano uliofanyika tarehe 10 Juni, 2011 kati Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na wajumbe kutoka Kampuni ya *Simon Group* haukuitishwa kihalali kwa sababu ulikiuka Katiba *(Articles of Association)* ya UDA (Kifungu cha 45) na kikao hicho kilikuwa hakina akidi *(quorum)* kwa kukosekana Msajili wa Hazina. Kwa hiyo, kikao hicho cha tarehe 10 Juni, 2011 kilikuwa hakina mamlaka ya kufanya maamuzi na maazimio yote yaliyofikiwa katika kikao hicho na hivyo yalikuwa batili. *(Makofi)*

Aidha, Kambi ya Upinzani imebaini kuwa Serikali kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitatu imekuwa haina uwakilishi kwenye Bodi ya UDA. Hali hii iliifanya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kuwa na maamuzi makubwa katika UDA na Serikali kushindwa kufahamu ni nini kilichokuwa kinaendelea ndani ya Kampuni ya UDA. Pia kwa kipindi chote hiki haujawahi kufanyika mkutano wa wanahisa wa kila mwaka *(Annual General Meeting)* au Mkutano Maalum *(Extra Ordinary General Meeting).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mwenendo huu ni dhahiri kuwa kumekuwa na ubadhirifu mkubwa ndani ya uendeshaji wa Shirika la UDA na hali hii inapaswa kufanyiwa kazi mapema kwani inavyoonyesha ni kuwa uuzaji huu wa hisa na ubadilishaji wa uendeshaji wa shirika , unaelekea katika kutaka kutumia mali za UDA kwa masilahi binafsi zaidi badala ya kuliimarisha shirika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inataka kupata majibu yafuatayo juu ya suala hili, kwanza nini msimamo/tamko la Serikali katika suala hili na haswa ikizingatiwa kuwa mkataba ulioingiwa haukushirikisha wanahisa muhimu, je, Wizara imechukua hatua gani mpaka sasa kuhusiana na waliohusika kwenye suala hili? Mali za UDA zilikuwa na thamani kiasi gani? Na ni lini tathimini ya mali hizo ilifanyika na ni nani walihusika katika kugharimia utathimini huo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la Reli Tanzania *(Tanzania Railways Corporation – TRC),* Reli ya Kati ni kichocheo kikubwa sana cha uchumi kwa wananchi wanaoishi katika mikoa ambayo imeunganishwa na reli hii na pia ni kiunganishi kikubwa kati ya bandari na nchi ambazo hazina bandari. Hivyo basi jambo la kwanza ni kuiboresha reli ya sasa ili ifanye kazi kwa uwezo mkubwa kusafirisha abiria na mizigo. Kwa miaka ya hivi karibuni, shirika letu hili limeyumba sana kutokana na uendeshwaji mbovu wa shirika hili na uchakavu wa miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti iliyoombwa mahitaji halisi kwa fedha za Matumizi ya Kawaida ni shilingi bilioni 63.68 na fedha iliyotengwa na Serikali ni shilingi milioni 900 kiasi ambacho ni pungufu sana ya fedha iliyoombwa. Je, kwa hali kama hii kuna jambo linaweza fanyika? Kambi ya Upinzani kwa kuona umuhimu wa reli yetu, ilitenga kiasi cha shilingi bilioni100 katika Bajeti mbadala kuliwezesha Shirika la Reli Tanzania kufanya kazi yake ya msingi ya kusafirisha mizigo na abiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa ufafanuzi ni jinsi gani mtandao wa mawasiliano wa *fiber optic* unaoanzia Dar es Salaam hadi Mwanza unaomilikiwa na Shirika unavyotumika kibiashara na kama hautumiki kibiashara, kuna mpango gani wa mtandao huo kutumika kibiashara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sababu zinaoongeza gharama za uendeshaji wa Shirika la Reli ni tozo ya mafuta yanayoendeshea injini za shirika, tozo hiyo ni kwa ajili ya mfuko wa barabara. Kambi ya Upinzani haioni sababu ya Shirika la Reli kuchangia mfuko wa barabara, kwani ni kuwaimarisha washindani wa shirika hilo ambao ni wasafirishaji wa mizigo kwa njia ya barabara. Kama makampuni ya madini yanasamehewa kulipa tozo hiyo wakati ni watumiaji wa barabara ni kwa nini Shirika la Reli nalo lisisamehewe kulipa tozo hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na sababu mbalimbali *TRL* ikiwa chini ya Menejimenti ya *RITES Ltd.* kwa takribani miaka mitatu imeshindwa kwa kiasi kikubwa kuhakikisha kuwa miundombinu ya reli, injini za treni, mabehewa ya mizigo na ya abiria pamoja na mali zote zilizokabidhiwa kwake vinafanyiwa matengenezo na kukarabatiwa kama ilivyoainishwa kwenye *Concession Agreement.* Kwa sababu hizi hali ya sasa ya miundombinu ya reli, injini za treni, mabehewa ya mizigo na ya abiria pamoja na mali zingine ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TRL* ilipoanza kazi tarehe 1 Oktoba, 2007 ilikabidhiwa jumla ya injini 79, mabehewa ya mizigo 1,357 na mabehewa ya abiria 97 yaliyokuwa yakitumiwa na *TRC.* Lakini badala yake *TRL* kwa makusudi iliamua kukodisha injini za treni 25 na mabehewa ya abiria 23 kutoka India. Hata hivyo, kutokana na kutofanyiwa matengenezo kati ya injini 79 zilizokabidhiwa *TRL* na Serikali tarehe 1 Oktoba 2007, ni injini 39 tu zinazofanya kazi hivi sasa tena zikiwa chini ya kiwango cha ubora, huku injini 40 zikiwa zimekufa kutokana na kutokarabatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mabehewa 1,357 ya mizigo ni 638 tu yanayofanya kazi na kati ya mabehewa 97 ya abiria ni 45 tu yanayofanya kazi na kwamba yote hayo yako chini ya kiwango cha ubora. Kwa upande wa mabehewa ya mizigo1,357 yaliokabidhiwa *TRL* hadi sasa mabehewa 719 hayafanyi kazi na kwa upande wa mabehewa ya abiria 97 mabehewa 52 hayafanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla hali hii ilisababisha hadi kufikia mwezi Aprili, 2010 toka kubinafsishwa *TRC* Shirika hilo limepata hasara ya shilingi bilioni 98.386 kutokana na kushuka kwa usafirishaji wa mizigo kutoka tani laki 5.7 zilizosafirishwa mwaka 2007 hadi kufikia tani laki 2.7 mwaka 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, treni za abiria kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma na Mwanza zilipungua kutoka treni nne kwa wiki hadi kufikia treni moja kwa wiki kwenda Kigoma pekee mwaka 2010. Hali hii ilipelekea idadi ya wasafiri wa treni kupungua, kwa mfano, abiria 290,046 walisafiri mwaka 2010, wakati mwaka 2009 walisafiri abiria 543,000, hii inaonyesha upungufu wa abiria 252,954 karibu na nusu ya abiria waliosafiri mwaka 2009 sawa na 46.6%. Hii ni aibu kwa Serikali inayotarajia kusherekea kutimiza miaka 50 ya Uhuru, badala ya kwenda mbele tunarudi nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, makubaliano ya Serikali katika ukodishaji wa *TRC* yalikuwa ni kuboresha sekta ya usafirishaji kwa njia ya reli kupitia utendaji wenye tija kutoka kwenye sekta binafsi. Serikali ilitarajia pia kuwa *TRL* ingewekeza kwenye miundombinu ya reli, injini za treni, mabehewa na vifaa mbalimbali vya kufanyia kazi ili kuongeza uwezo na ufanisi katika sekta ya usafiri wa reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasema kuwa kitendo cha *TRL* kutelekeza injini 79 zilizokuwa zikitumiwa na *TRC* na kuamua kukodisha injini chakavu toka India ni hujuma ambayo tunadhani inatakiwa iwe mojawapo ya ajenda katika kadhia nzima ya uvunjwaji wa mkataba na urejeshwaji wa hisa ambazo *RITES* wanamiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Biashara wa *RITES/TRL* uliowasilishwa Serikalini ulionyesha kutakuwepo na treni sita za abiria kwa wiki kuanzia Dar es Salaam kwenda Kigoma na Mwanza. *TRL* ilitarajiwa kuanza kupata faida kuanzia mwaka wa kwanza wa biashara, lakini mwaka huo huo wa 2007 *TRL* ilipata hasara ya Shilingi bilioni 4.87, mwaka 2008 hasara ilikuwa Shilingi bilioni 26.914, mwaka 2009 hasara ilikuwa Shilingi bilioni 56.532 na hasara iliyopatikana mwaka 2010 mpaka kufikia mwezi Aprili ilikuwa Shilingi bilioni 10.07.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imeamua kuchukua hisa zote za Kampuni ya Reli Tanzania, Serikali haina budi kuiwezesha *TRL* kuwekeza katika miradi muhimu ya maendeleo, mtaji wa kufanyia kazi pamoja na kulipa madeni yote ambayo yataachwa na Menejimenti ya *RITES* kama ilivyo kubaliwa katika makubaliano ya kuvunja mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano kati ya *RITES* na Serikali *Invoice* Na. 055 ya mwezi Julai 2011, inaonyesha kuwa Serikali hadi sasa bado inailipa *RITES Management Service Fee* ya

dola za Marekani US$10,982 kwa mwezi. Pia *Invoice* Na. 056 ya Julai ya Dola za Marekani 40,498.20, kama fedha za mishahara kwa watumishi wanne wa *RITES.* Pesa hizo Zilitakiwa ziingizwe akaunti Na. 0011407376, *AXIS BANK MUMBAI INDIA*.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa ufafanuzi, wakati mkataba na *RITES* ulishavunjwa, inakuwaje *RITES* waendelee kulipwa wakati mkataba umeshavunjwa? Aidha, Serikali inatakiwa kulipia matengenezo ya injini aina ya 88 *class* kiasi cha Dola za Kimarekani 1,538,000 tarehe 30 Septemba, 2011*(Extract from Deed of Settlement Between RITES & GOT* barua ya tarehe 20 Julai, 2011 iliandikwa na HL Chaudhary, Mkurugenzi Mtendaji wa *TRL*). Kambi ya Upinzani inaona huu ni mchezo wa kuigiza ambao Serikali inawafanyia Watanzania. Kama mkataba umevunjwa ni kwa vipi Ndugu Chaudhary bado ndiye Mkurugenzi Mtendaji na nyaraka zote zinazohusiana na shirika hilo anaendelea kuzimiliki yeye? Kambi ya Upinzani inaomba kupata maelezo, ni kwa vipi pale mbia anaposhindwa kutimiza masharti yaliyomo kwenye mkataba na alipwe pale mkataba utakapovunjwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbukumbu za Serikali zinaonyesha kuwa tumeingia gharama kiasi cha Shilingi bilioni 63.68 katika kufidia kuvunjwa kwa mkataba baina ya *TRC* na *RITES* ya India. Kambi ya Upinzani inasema, ili kuwa makini na masuala ya matumizi ya fedha za wananchi, ni lazima wahusika wakuu wa mkataba ulioingiwa, nao wawajibishwe kwa uzembe kama ambavyo Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba na Mheshimimwa Daniel Yona pamoja na Grey Mgonja walivyofunguliwa mashtaka ya kulitia Taifa hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili likiachwa bila ya wahusika kuchukuliwa hatua itaonekana kuwa sheria zinabagua *(double standards)* katika kushughulikia wale wote wanaoliingizia hasara Taifa letu au wahujumu uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna reli iendayo ukanda wa Kaskazini (Tanga, Kilimanjaro) ambayo kwa muda mrefu imeshindwa kufanya kazi na hivyo kusababisha usafirishaji wa mizigo kutumia njia ya barabara jambo linalosababisha uharibifu wa mara kwa mara wa barabara zetu, turejee barabara hasa katika eneo la Chalinze. Ni tarajio letu kuwa sasa ni muda muafaka wa Serikali kuunganisha usafiri wa reli kati ya Dar es Salaam, Tanga na Kilimajaro. Hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kuokoa fedha za matengenezo ya mara kwa mara ya barabara na kupunguza ajali za mara kwa mara zinazosababishwa na malori ya mizigo katika njia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inashauri yafuatayo kama mpango wa muda mfupi wa kuliimarisha Shirika la Reli:-

(i) Serikali iwekeze Mtaji kutoka katika vyanzo vya ndani ya nchi kama vile kuwashirikisha wadau ambao wako tayari;

(ii) Serikali kuunda upya Bodi ya wataalamu wa mambo ya reli, Menejimenti adilifu na mifumo mipya ya kiutawala ya kuendesha Reli;

(iii) Ukarabati wa njia ya reli, mitambo, injini na mabehewa ya abiria na mizigo ufanywe na wataalamu Wazalendo;

(iv) Kwa kuwa tatizo kubwa ni injini za kuvuta mabehewa, tunashauri Serikali inunue injini haraka iwezekanavyo kwani gharama ya iInjini moja ni kati ya *USD* 2,000,000 na *USD* 2,500,000;

(v) Kwa kuwa Ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam, Tanga Kigoma na Mwanza utatokana na Reli, hivyo basi, tunapendekeza Kampuni ya Reli na Bandari ziungane kama ilivyokuwa wakati wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki;

(vi) Kuboresha mazingira ya kufanyia kazi, maslahi ya wafanyakazi ikiwa ni pamoja na mishahara, madai mbalimbali na kadhalika; na

(vii) Kuwe na mafunzo kwa watumishi ya mara kwa mara *(skill upgrading).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mawasiliano ya barua kati ya Wizara ya Uchukuzi ya tarehe 19, Julai 2011 yenye Kumb. Na.WUC/GEN/2011/89 iliyokwenda kwa Kampuni ya *Glasgow International General Trading International LLC,* ya Dubai kuhusiana na kukaribishwa kwa Kampuni ya *IPEX* ambayo ni kampuni dada, kwenye kikao na Wizara cha tarehe 27 Julai 2011 kwa ajili ya kujadiliana na ikiwezekana kusaini *Memorundum of Understanding (MoU)* kati ya Serikali na mwekezaji huyu kwa ajili ya matengenezo na uendeshaji wa reli zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo taarifa kwamba Serikali imesaini *(MoU)* na Kampuni ya Dubai *(HLG)* kwa ajili ya kufanyia marekebisho Reli ya Kati na mnamo tarehe 05 Julai, 2011 Kampuni ya *Habtoor Leighton Group* ya Dubai, waliandika barua kwenda kwa *Cansulate General* wa Tanzania ndugu Cleophas Kasenza Ruhumbika wa Dubai kuhusu mkataba kati ya Serikali na kampuni hii *(MoU)* ambayo ilikuwa inaishia tarehe 4 Agosti, 2011 ili aweze kuongezewa muda wa miezi mitatu hadi Novemba 4, 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu walizotoa kwenye barua yao ni pamoja na kuhitaji muda zaidi kwa ajili ya kwenda kuwasiliana na taasisi mbalimbali za kifedha ili waweze kupata fedha za kutekeleza ujenzi huo. Kambi ya Upinzani inahoji, hivi Serikali inatumia vigezo gani katika kuingia mikataba na makampuni mbalimbali ya nje na hasa ikizingatiwa kuwa hii kampuni inaonyesha dhahiri kuwa haina fedha ni mpaka waweze kukopa na wameshindwa kupata mkopo hadi muda wa *MoU* unamalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunahangaika kuvunja mkataba na *RITES* wakati huohuo tunakwenda haraka mbele kutafuta mbia mwingine. Kambi ya Upinzani inataka kujua Serikali imezingatia mazingira yaliyosababisha Mkataba na *RITES* kuvunjwa? Je, Maslahi ya Taifa yanazingatiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 13 - 21 Juni, 2011 Benki ya Dunia ilituma wataalamu wake kuja Tanzania kwa ajili ya kufuatilia hali ya Shirika letu la Reli na kikubwa walikuwa wanakuja kukagua kama tunastahili kupata mkopo wa dola milioni 150 ambazo tuliomba, na hii inathibitishwa na barua ya tarehe 6 Juni, 2011 yenye Kumb. Na. CA230/505/01/93 iliyosainiwa na F. Mwanyika kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara kwenda kwa Mameneja wa *RAHCO* na *TRL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa mambo ambayo Mameneja hawa walitakiwa kutengeneza ni pamoja na mpango kazi *(constructive business plan)* na mpango wa kusimamia mradi husika *(project implementation plan).*

Kambi ya Upinzani tunataka kupata majibu, hivi ni kweli kuwa Shirika letu la Reli halina mpango kazi? Kama haupo, kwanini tunawalipa *RITES*? Walikuwa wanafanya nini kwa muda wote wa Mkataba? Je, Serikali ilifanikiwa kupata mkopo huu wa Benki ya Dunia? Kama ndio, fedha hizo zimeingizwa kwenye bajeti hii? Zitatumika kufanya jambo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanisi wa Shirika la Reli la Tanzania na Zambia *(TAZARA)* umepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na kupungua kwa kiasi kikubwa cha injini zake na kuchakaa kwa mabehewa kulikochangiwa kwa kiasi kikubwa kwa bajeti finyu na migomo ya wafanyakazi inayohusiana na ubaguzi ki-maslahi kati ya wafanyakazi wa Tanzania na Zambia. Mwaka 2010 wasafiri walikuwa 757,987 ikilinganishwa na 794,983 mwaka 2009 ukiwa ni upungufu wa asilimia 4.7%. Barabara zimeendelea kuharibika kutokana na kubeba mizigo mizito inayotoka na kupelekwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini pamoja na nchi jirani ya Zambia hasa shaba, mbao, vyuma na *cement*.

Kambi ya Upinzani, tunataka kupata majibu juu ya malalamiko kuhusiana na Mkataba ambao *TAZARA* kwa upande wa Zambia waliingia na Shirika la Reli la Zambia *RSZ* ambao uliridhiwa na Bodi mwezi Mei, 2011 kwa ajili ya shirika hilo kuendesha shughuli za *TAZARA* na mwaka wa fedha 2009/2010 *RSZ* waliweza kuchukua asilimia 44 ya mapato ya *TAZARA* ambayo yalikuwa US$ 38 milioni. Je? Katika Mkataba huu, Serikali ilishiriki kwa kiasi gani? Nini manufaa ya Mkataba huu kwa Taifa la Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Usafiri wa Anga - *(Tanzania Civil Aviation Authority – TCAA)* ni moja kati ya mamlaka muhimu sana katika kuchangia mapato ya Taifa. Kwa mantiki hiyo, hapana budi kwa Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi kuitilia maanani mamlaka hii na kuipatia kila msaada ili ibaki kuwa miongoni mwa mihimili mikuu ya uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka hii inakabiliwa na changamoto ya udhaifu wa miundombinu muhimu katika kutekeleza majukumu yake. Karibu viwanja vingi vikiwemo vile vinavyomilikiwa na *TANAPA* na Idara ya Wanyamapori ni changamoto na kikwazo kinachowafanya watalii wasifike kwa urahisi kwenye vivutio muhimu vilivyomo nchini mwetu. Kwa hiyo, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali pamoja na hali inayoelezwa kuwa uchumi wetu ni duni, lazima itoe kipaumbele katika kuboresha miundombinu hiyo. Ikumbukwe kuwa shilingi hutafutwa kwa shilingi. Bila kuwekeza, watalii wala fedha haiwezi kuja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama kubwa ya kununua na kukarabati mitambo ya kuongozea ndege, bado nayo ni changamoto inayoikabili mamlaka. Hii inatokana na mabadiliko makubwa na ya haraka ya teknolojia na utaalamu katika mitambo ya kuongoza ndege. Sambamba na hili, mamlaka lazima iwapatie wafanyakazi wake mafunzo ya mara kwa mara ili waendane na mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha takriban miaka 12, kampuni iliyopewa dhamana ya kuendeleza uwanja wa ndege wa Kilimajaro imewekeza kiasi cha dola za Kimarekani milioni nne tu sawa na Shilingi bilioni 6, wakati imekusanya jumla ya Shilingi bilioni 56.94 kutoka vyanzo mbalimbali katika uwanja huo. Kushindwa kuuweka uwanja huo katika mazingira bora na ya kisasa ni kasoro kubwa itakayosababisha uwanja huo kukosa kabisa ndege za nje kutua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya Serikali kuendeleza porojo za kujenga uwanja wa ndege wa kimataifa wa Misenye Mkoani Kagera na uwanja wa ndege wa kimataifa wa Bukoba Mjini, eneo ambalo lina umbali wa takribani kilometa 50 kama ambavyo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Jakaya Kikwete alivyoahidi wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu uliopita, Serikali iachane na porojo hizo na badala yake iwekeze katika ukarabati mkubwa katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii ya kuachana na porojo za ujenzi wa uwanja wa ndege wa Misenyi na Bukoba Mjini ni muhimu kwa kuwa jirani zetu wameanza kujenga uwanja wa ndege wa kisasa eneo la Taveta mpakani mwa Tanzania na Kenya kwa lengo la kukiua kabisa kiwanja cha ndege cha Kilimanjaro na hivyo biashara yote inayohusiana na usafiri wa anga kati ya Afrika ya Mashariki na Mataifa mengine kuwa vituo vyake Nairobi, Mombasa na Taveta, jambo ambalo litaathiri kwa kiwango kikubwa biashara ya utalii nchini. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kupanga kibiashara zaidi ili kukabilina na ushindani wowote wa kibiashara ambao unatishia sekta zetu muhimu za kiuchumi. Serikali haina budi kuboresha huduma *(ground handling facilities)* zinazosababisha wafanyabiashara wetu wa bidhaa zinayowahi kuharibika kwenda uwanja wa Ndege wa Nairobi kwa ajili ya kufuata huduma hiyo huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TCAA* waliweka ushindani katika viwanja vyote vya ndege isipokuwa *KIA* katika suala la *ground handling* ambapo ni Kampuni moja tu ya *Swissport* inaruhusiwa kutoa huduma. Kwa sababu ya ukiritimba, ni rahisi kwa kampuni hii kukataa kutoa huduma kwa makampuni mengine yenye wateja na hata kufanya huduma hizo kuwa ghali sana. Wizara iseme ni lini itaondoa ukiritimba huu ili kuongeza ufanisi katika huduma za usafiri wa anga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa hauwezi kuzungumzia usafiri wa anga hapa nchini bila ya kuzungumzia Shirika la ndege ya Taifa letu *(ATCL).* Shirika hili ndilo kioo cha Taifa nje ya nchi. Hivyo basi, Serikali haina budi kufanya kila iwezalo kuhakikisha Shirika letu linafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya ufanisi katika Shirika la Ndege Tanzania *(ATCL)* ilibaini mambo yafuatayo ambayo yamesababisha Kampuni hii kushindwa kabisa kujiendesha:-

(i) Shirika linakabiliwa na madeni yanayofikia Shilingi bilioni 23.3;

(ii) Kampuni ina mtaji hasi wa Shilingi bilioni 14, hivyo inahitaji kupatiwa mtaji;

(iii) Kuanzia mwaka 2007/2008 Serikali ilisitisha rasmi utoaji wa ruzuku ya Shilingi milioni 500 kwa mwezi kwa *ATCL,* hivyo kuiacha Kampuni bila msaada au ruzuku yoyote;

(iv) Ukiritimba uliokidhiri katika kufanya maamuzi yahusuyo Shirika; na

(v) Kwa zaidi ya miaka mitano sasa Serikali imetafuta mwekezaji wa kuwekeza kwenye *ATCL* bila mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada za makusudi zinatakiwa kufanywa ili kuiokoa *ATCL* ili hata kama mwekezaji atapatikana aikute Kampuni ikiwa inajiendesha, hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaungana kukazia mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma *(POAC)* kuwa:-

(i) Serikali kuchukua madeni yote ya *ATCL* na baada ya hapo kutoa mtaji (unaofikia dola za Kimarekani bilioni 31) wa kuanza kuliendesha Shirika hili ikiwa ni pamoja na kutoa dola laki saba ili kuirudisha ndege ya *ATCL* iliyopo kwenye matengenezo ili ianze kufanya kazi mara moja.

(ii) Serikali kuangalia uwezekano wa kuunda upya Bodi na Menejimenti ya *ATCL* ili iweze kukabiliana na changamoto zilizopo kwenye Shirika hilo kwa haraka na kwa ufasaha imetoa mapendekezo yake kuhusu ufufuaji wa *ATCL* kwenye sehemu ya maoni katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, katika hotuba yake ya bajeti mbadala ilipendekeza Shirika letu la Ndege lirudi tena kwenye biashara. Hivyo ilitenga Shilingi bilioni 200 kulifufua upya Shirika la Ndege la *ATC*. Hata hivyo, tunashauri kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kurekebisha umiliki wa Shirika la Ndege la Taifa kwa kuhusisha Taasisi za Umma ambazo zinafaidika zaidi katika biashara zao kutokana na uwepo wa Shirika la Ndege la Taifa. Pia tunaitaka Serikali itoe maelezo ndege iliyokuwa ikitoa huduma kati ya Dar –Kigoma kupitia Tabora iko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa ndege za *Precision* hazitui uwanja wa Tabora na Kigoma kutokana na viwanja, hivyo kutokuwa na viwango. Hivi sasa ni vigumu sana kusafirisha wagonjwa wanaohitaji huduma ya haraka katika Hospitali za Rufaa. Hii kauli ya miaka mingi ya Serikali kuwa itaukarabati uwanja wa ndege wa Tabora na Kigoma ni hadithi ambayo tunauliza itatekelezwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2006/2007 Serikali ilitueleza kwamba itashirikisha sekta binafsi katika uwekezaji na utoaji huduma katika viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tunamtaka Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho atueleze yafuatayo:-

(i) Kwa kiasi gani mpango huu umefanikiwa?

(ii) Ni makampuni gani binafsi yaliyoshirikishwa katika mpango huu na katika maeneo gani?

(iii) Faida gani na kiasi gani imepatikana kutokana na ushiriki wa sekta binafsi katika mpango huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna wasiwasi juu ya suala zima la usimamizi na ukaguzi wa vyombo vya usafiri wa majini, kama vile meli na maboti. Tunaitaka Serikali kupitia *SUMATRA* iweke utaratibu ulio wazi na makini juu ya usimamizi na ukaguzi wa vyombo vya usafiri wa majini. Taarifa ya hali ya uchumi inaonyesha kuwa ajali zilizotokea baharini na katika maziwa na zilisababisha kupotea watu 54 mwaka 2010 ukilinganisha na watu 40 mwaka 2009. Kambi ya Upinzani inaliona

hili kuwa ni kutokuwepo kwa mfumo wa ukaguzi wa mara kwa mara kwa vyombo vinavyofanya safari baharini na maziwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA),* ni miongoni mwa mihimili muhimu ya Taifa katika kukuza na kuinua uchumi wa nchi. Aidha, bandari hii inahudumia takribani nchi sita. Umuhimu wa Mamlaka hiyo unatokana na kuingizia Serikali mapato ya kutosha. *TPA* inasimamia bandari kuu tatu nchini zilizopakana na Bahari ya Hindi. Bandari hizo ni Tanga, Mtwara na Dar es Salaam ambayo ndiyo kubwa na kitovu cha biashara zote za kimataifa. Pia *TPA* inasimamia bandari nyinginezo ndogondogo kama vile Kilwa, huku kukiwepo mkakati wa kupanua Bandari ya Bagamoyo. Bandari nyingine ziko katika maziwa Nyasa, Tanganyika na Victoria, kukiwepo bandari kama vile *Mbamba Bay*, Itungi, Kigoma, Mwanza, Kemondo, Bukoba na Musoma. Awali bandari hizo zilikuwa chini ya lililokuwa Shirika la Reli Tanzania *(TRC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo maana ya kaulimbiu 'Bandari ni Lango la Biashara', hutumika sana kwa maana ya umuhimu wake katika kukuza biashara na uchumi kitaifa, na hii ndiyo bahati ambayo nchi yetu imepewa na Mwenyezi Mungu kwa kulinganisha na nchi jirani zetu. *TPA* kupitia vyanzo vyake imekuwa ikikusanya mapato kusaidia maendeleo ya nchi, licha ya kukabiliwa na changamoto nyingi na hasa malalamiko yahusuyo utendaji kazi wake usioridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa malalamiko ya muda mrefu, ni mizigo kukaa muda mrefu bandarini, mlundikano wa makontena na wizi wa vipuri vya magari unaodaiwa kufanyika katika Bandari ya Dar es Salaam, changamoto nyingine ni kuongezeka kwa meli katika bandari hiyo kutoka nje na ushindani uliopo na Bandari za Mombasa, Afrika Kusini na Msumbiji. Hivyo, Kambi ya Upinzani inaiasa Mamlaka kukaa kibiashara zaidi ili kukabiliana na changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Benki ya Dunia ya Julai, 2011 inaonyesha kuwa msongamano wa mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam ulikuwa ukiliingizia hasara Taifa letu ya dola za Kimarekani milioni mbili kwa siku kwa mwaka 2009. Hii ni hasara kubwa sana kwa nchi changa ambayo inapambana kuondokana na umasikini. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze wananchi ni mkakati upi umewekwa kumaliza hasara hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa iliyotolewa na jarida ya "*the Econimist*, 2009" inasema kuwa China imeamua kuwekeza katika kupanua miundombinu ya Bandari za Uganda na Kenya ili kupata urahisi wa kusafirisha malighafi yake toka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo badala ya kutegemea Bandari ya Dar es Saalam ambayo imejaa ukiritimba. Kambi ya Upinzani inaona nchi yetu haikukaa kiushindani katika kuimarisha na kuendeleza vile vitu ambavyo sisi tunavyo kwa kulinganisha na jirani zetu na mwisho wake ni kupoteza fursa zetu kiuchumi, kama inavyotokea kwenye Shirika la Ndege na sasa kwenye Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonyesha kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ilihudumia shehena zenye uzito wa tani 10,045,462 kwa mwaka 2010 ambazo ni ongezeko la asilimia 12.4 ukilinganisha na mwaka 2009. Ongezeko hili linatokana na uingizaji mkubwa wa shehena za magari, mafuta, mbolea na ngano kwa ajili ya nchi jirani. Ongezeko kubwa lilitokea katika Bbandari ya Dar es Salaam. Shehena katika Bandari za Kigoma na Mtwara zilipungua kutokana na kupungua kwa mazao yanayosafirishwa nje ya nchi, kukosekana kwa meli zinazofanya kazi katika mwambao wa Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa meli maalum ya kubeba mabehewa katika *Ziwa Victoria* na Tanganyika nalo ni tatizo kubwa sana linalosababisha utendaji wa bandari kuwa wa hali ya chini. Aidha, kukosekana kwa miundombinu imara ya kuunganisha bandari na vyanzo vya shehena nalo ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Serikali, ni kuwa tathmini ya upanuzi wa Bandari ya Kigoma umekamilika na Wizara hiyo kupitia msimamizi wa Bandari ya Kigoma na kuwasilisha maombi ya dola milioni 10 za Marekani katika Shirika la *JICA* baada ya kuonyesha nia ya kugharamia mradi huo. Aidha, *JICA* wanafanya tena tathmini halisi nyingine ya mradi huo huo. Kambi ya Upinzani inataka kuelewa ni nini maana ya tathmini kufanywa mara mbili mbili? Je, huu

siyo ucheleweshwaji wa muda usio na msingi wowote? Muda ni mali, pindi upoteapo siyo rahisi kuupata tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Benki ya Dunia inasema kuwa upanuzi wa bandari yetu ya Dar es Salaam kwa kushirikiana na sekta binafsi unashindikana kutokana na kuingiliwa na wanasiasa na hivyo kusababisha nchi yetu kuzidi kupoteza fursa za kibiashara na nchi jirani hasa Uganda, Rwanda, Burundi na *DRC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhuu ujenzi wa gati *(Berths)* 13 na 14 Bandari ya Dar es Salaam, kuna pendekezo la kujenga gati kwenye mlango namba 13 na 14 na ambazo zitajengwa kutokana na mkataba ambao umesainiwa kati ya Serikali ya Tanzania na ile ya China wa kupata mkopo kutoka *Exim Bank* ya China ambao unafikia kiasi cha dola za Kimarekani US$ milioni 525.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upembuzi yakinifu uliofanywa na *CPCS Transcom* ambao ulifanyika mwaka 2009 ulionyesha kuwa kujenga Gati hizo, gharama zake zilikuwa ni kiasi cha dola za Kimarekani milioni 280, ila kwa sasa gharama hizo zimepanda hadi kufikia dola milioni 525 na hizi gharama zinapigiwa chapuo na Kampuni ya Ujenzi ya kichina ambayo inaitwa China *Road &Bridge*. Hizi ni gharama kubwa mno ukilinganisha na gharama ambazo zinatumika katika ujenzi kama huo ambao unafanyika katika Bandari ya Mombasa kule Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia utaweza kuona kuwa mradi huu wa upanuzi wa bandari yetu unafanyika huku tukipata mkopo kutoka China na hapo hapo kampuni za kichina ndiyo zimefanya upembuzi wa ujenzi na kuja na gharama kubwa ukilinganisha na hali halisi na hata hivyo kampuni za kichina ndiyo zinataka kupewa kazi kwa ajili ya ujenzi wa Gati husika.

Kambi ya Upinzani inaona kuwa ili kuweza kujenga Gati hizi na kuweza kuimarisha Bandari yetu, hatua zifuatazo zichukuliwe:-

(i) Kandarasi kwa ajili ya ujenzi iwe ya wazi na itangazwe ili makampuni yaweze kushindanishwa na hivyo tuchague aliye na gharama nafuu zaidi na mwenye sifa ndiyo apewe kazi ya ujenzi huo.

(ii) Tutumie mfumo wa kujenga Gati hizi kwa mfumo wa ‘*Built-Operate-Transfer’ BOT*. Hili litavutia mitaji kutoka sekta binafsi na hivyo ujenzi uweze kufanyika.

(iii) Kuchukua Mkopo huu wa USD milioni 525 wenye masharti haya ni wizi mkubwa wa mchana kwani tutakuwa tunalipia madeni makubwa kuliko inavyotakikana na ambayo tungeweza kuyapunguza, hasa ikizingatiwa kuwa fedha hizi zote zitaelekezwa China, kwani masharti yake ni kuwa lazima mkandarasi atoke China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasikitishwa na hali ya usalama katika Bandari ya Dar es Salaam ambayo hutumiwa siyo tu na wananchi wetu, bali hata nchi jirani kama zile za Burundi, Zambia, Rwanda na Congo. Hii ni kutokana na wizi wa mali za wananchi na watu wengine ambao wanatumia bandari hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa tulizonazo ni kuwa, baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushauriana na wadau wa Bandari ya Dar es Salaam, alimwagiza Inspekta Jenerali wa Polisi *(IGP)* kupeleka kikosi maalum cha Askari Polisi kwa kuwa kitengo hicho kilikuwa chini ya *Auxiliary* Polisi na hivyo kutoweza kukidhi haja ya ulinzi katika eneo hilo

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa kuwa Inspekta Jenerali wa Polisi *(IGP)* aliweza kuunda kikosi hicho mnamo tarehe 17 Novemba, 2009 kwa barua yenye Kumb. Na. PHQ AD, 21/VOL.XVIII/227 na tayari walisharipoti kwenye kikosi cha *Marine Dar es Salaam* ila mpaka sasa kutokana na Mkurugenzi wa Bandari kukaidi kwa malengo anayoyajua yeye binafsi, askari hao wamekuwa wapo kituoni bila kupangiwa kazi za kufanya na wanaendelea kulipwa mishahara bila kazi yoyote wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata baada ya *IGP* kupeleka kikosi maalum cha askari 51katika eneo hilo, taarifa zinaeleza kuwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Bandari amekataa kuwapa ushirikiano kwa madai kuwa anajitosheleza kiulinzi hata baada ya Rais kuagiza kufanya hivyo. Hata hivyo, upo ushahidi wa wizi wa makontena na vitu vingine ulioripotiwa katika kikosi maalumu cha Polisi hao wa Bandari ya Dar es Salaam ambao hata hivyo haujafanyiwa kazi. Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kutoa majibu ya kina juu ya tuhuma hizi zinazoelekezwa kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Bandari kwa kuwakingia kifua watuhumiwa wa wizi unaofanywa na watumishi wa bandari na wengine walio karibu naye, na pia kukaidi agizo la Rais la kuunda kikosi maalumu cha Polisi kwa ajili ya kuboresha ulinzi wa eneo tajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tunataka kupewa taarifa juu Makontena yaliyoibiwa Bandarini na taarifa zake kufunguliwa *RB* kwenye Kituo cha *Police Marine* na kisha faili hizo kupelekwa Kituo cha Polisi *Kilwa Road.* Baadhi ya namba za RB hizo ni MUD/RB/51/11 hadi MUD/RB/56/11 na MUD/RB/106/11 hadi MUD/RB/113/11. Ni jukumu la chombo gani kulinda mali za raia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Huduma za Meli *(MSCL)* imeendelea kutoa huduma katika maeneo ya Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika. Kampuni hii imejiendesha kwa muda mrefu bila kupata fedha toka Serikalini jambo ambalo kwa kiasi kikubwa imechangia uchakavu wa meli zinazohudumiwa na Shirika hili. Kutokufanyiwa matengenezo ya mara kwa mara kwa meli hizo umesababisha shirika kuendeshwa kwa madeni. Hadi sasa shirika linahitaji jumla ya Shilingi bilioni 1.6 ili kulipia madeni yanayolikabili shirika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliwezesha shirika hili kimkakati ili liweze kutoa usafiri wa viwango kwenye maziwa ya Victoria, Nyasa na Tanganyika. Mizigo mingi inayotoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda nchi jirani, usafiri wa uhakika wa meli ndiyo suluhisho pekee la usalama na uhakika. Aidha, Kambi ya Upinzani inashauri kuwepo na umiliki wa pamoja kati ya Halmashauri za Wilaya husika kwa meli zinazotoa huduma kwenye maziwa tajwa na Kampuni ya Huduma za Meli *(MSCL).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Hali Tanzania - *(Tanzania Metorological Agency-TMA)* ni chombo muhimu sana katika kutoa huduma hapa nchini. Mikakati ya Serikali katika kuunda mamlaka nchini ni kuweza kufanya shughuli zake kibiashara. Ili kutimiza majukumu yake, *TMA* lazima ijipinde katika kupanga mikakati ambayo itawawezesha kukabiliana na changamoto ambazo zinawakwaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya majukumu ya mamlaka hii ni kufanya uchunguzi wa hali ya hewa ya anga za juu. Katika kulitekeleza hili, mamlaka ilikuwa inategemea vituo vyake vitatu ambavyo viwili kati ya hivyo, kile cha Kigoma na Mtwara havifanyi kazi kwa sasa. Vituo hivyo vinahitaji matengenezo ya gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iiwezeshe Mamlaka hii kifedha ili imudu kufanya matengenezo ya vituo hivyo kwa ajili ya kupata uwezo wa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, *TMA* haina budi kuwezeshwa ili ikidhi dhamira yake kuu ya kutoa huduma za hali ya hewa zilizo bora zitakazokidhi matarajio ya wadau na hivyo kulinda maisha yao, mali zao, mazingira na kusaidia katika kuondoa umaskini nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nia ya Mamlaka hii ni kuwa kitovu bora cha utoaji huduma za hali ya hewa zenye hadhi ya kimataifa ifikapo 2015, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itimize ahadi yake ya kuipatia *TMA* rada mpya ya kisasa ambayo itaendana na wakati huu wa ongezeko la tekinolojia na hivyo kuiwezesha kukidhi malengo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani ina imani kwamba, kama Serikali itakuwa makini kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazoikabili *TMA* kama vile kuboresha mitambo ya uchunguzi, mifumo ya mawasiliano, miundombinu ya uchoraji na uchambuzi wa taarifa, kupata kompyuta yenye uwezo mkubwa wa kuendesha mifumo ya utabiri wa *WRF* na *High Resolution*

*Model (HRM),* pamoja na yale niliyoyaeleza katika ibara ya hapo juu, Mamlaka hii itaweza kufanya shughuli zake kwa ufanisi, kibiashara na hivyo kuondokana na kutegemea ruzuku ya Serikali. Watanzania watapata tabiri ya uhakika ya hali ya hewa na hivyo kupanga shughuli zao, hasa za kilimo kitaalamu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:**Nakushukuru sana Mheshimiwa Mhonga, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kigoma kwa uwasilishaji wako.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupokea taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, sasa naomba niwaite wachangiaji wetu wa mwanzo. Tutaanza kumsikiliza Dkt. Charles Tizeba, atafuatiwa na Mheshimiwa Freeman Mbowe na Mheshimiwa Abdulkarim Shah atafuatia.

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu. Kwa masikitiko makubwa sana na kwa jambo ambalo sikutarajia kulifanya katika kipindi kifupi cha kuwepo katika Bunge hili, naomba nianze kwa kusema kwamba siungi mkono hoja iliyopo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaunga mkono kwa sababu kubwa kama sita hivi zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tulipitisha hapa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, kubwa ambayo naamini Wabunge wote na Watanzania waliifurahia sana. Leo Waziri ameomba fedha ambazo hata kwa masikio ya Watanzania zinaonyesha kabisa jinsi sekta hii ambavyo haijapata kipaumbele cha kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa la kwanza ambalo mimi naliona katika Sekta hii ya Uchukuzi ni la kimuundo, jinsi ambavyo mipango ya Wizara haihuishwi na mipango ya sekta nyingine ambazo zina uhusiano wa moja kwa moja katika ufanisi wa Wizara hii. Kwa mfano, mipango yote ya uchukuzi hapa ambayo tumeisikia haihusishwi na barabara, mipango yote tuliyoisikia hapa ya Bandari na Reli haihusishwi na sekta nyingine ambazo zina *compliment* utendaji wa Wizara hii. Ndege na Utalii hatusikii imehusishwaje, umeme na Reli sikusikia umehusishwaje. Kwa hiyo, hayo ni mambo ambayo ukiyatazama utaona kwamba hapa hatuanzi chochote, Watanzania watatupuuza sana leo tukikubali hapa bajeti hii ipite kwa bilioni hizi zilizotajwa hapa, bajeti ambayo kimsingi inapaswa kuwa ndio inashikilia uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini kwamba Wajerumani hawakuwa wajinga, walioingia Tanzania wakaanza kujenga reli kwanza kabla ya barabara. Dunia nzima inafahamu, hapa wamesema Wasemaji wa Kamati ya Kudumu ya Bunge na Kambi ya Upinzani kwamba inapaswa barabara zi- *supplement* reli na siyo kinyume chake kwamba reli ina-*supplement* barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka mitano iliyopita reli yetu ilikuwa inaweza kusafirisha tani milioni 1,500 kwa mwaka. Mwaka jana wamesafirisha tani 400,000 tu. Hili ni anguko kubwa kiuchumi. Gharama za usafirishaji zimepanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kibaya zaidi ninachokiona katika utaratibu huu ni pale ambapo tumewekeza fedha nyingi sana kwenye barabara bila kuona waziwazi kwamba barabara hizo hazitadumu kwa sababu zitakuwa zimetumiwa zaidi na magari isivyostahili. Mimi nasikitika kwamba hizi trilioni moja na nusu tumempa jana Mheshimiwa Dkt. Magufuli na Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, baada ya miaka mitatu tutaanza kuwatukana kwamba wanajenga barabara za kiwango cha chini kumbe siyo wao. Tatizo ni Wizara hii ya Uchukuzi ambayo haijajenga hoja vizuri ili iweze kupewa fedha za kutosha kuweza kuwekeza katika reli. Reli ibebe mizigo mikubwa, barabara zitumike kwa mizigo myepesi kusafirisha kupeleka kwenye vituo vya reli ili iweze kusambaa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia hapa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, amezungumzia mpango ulioko wa Angola kujenga reli na *Mozambique* na wapi, lakini naomba niseme kwamba hakuna sera yoyote ulimwenguni, anayependa kusafiri *Atlantic* kule, kwa hiyo, wale wameingia kwenye hizo *program* baada ya kuona sisi wenye fursa nzuri huku tumelaza damu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo randama mkononi hapa ya Wizara hii, nilikuwa najumlisha *program* yote ya maendeleo katika reli jumla ni Sh. 17,708,000,000/=. Hii nailinganisha na bilioni elfu moja na mia nne sijui na ngapi ambayo imekwenda Wizara ya Ujenzi. Ni *percent* ngapi hii? Halafu tuseme tuko *serious* tunataka reli ifanye kazi vizuri! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi nilikuwa nawatafuta Watendaji wa Reli, wote wanapiga piga chenga, nikawa najiuliza, hawa kwa nini hawataki kuwasiliana na Mbunge? Baadaye tu nikafikia tu kwenye *realization* kwamba wanaona labda wakiniambia mambo yao nitakuja tu kusema, lakini nitasema tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama ya kujenga kilometa moja ya reli kwa leo, nina hakika siyo zaidi ya kujenga kilometa moja ya barabara ya lami. Tuko tayari kuwekeza trilioni moja na nusu kwenye barabara, lakini hii reli yetu kwa mfano ya Mwanza - Dar es Salaam ya kilometa 1,300 tu, tunasuasua nayo wakati tunajua kabisa reli ile ikiwa imara, ndio barabara zetu zitadumu kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Wala hii siyo hadithi ya yai na kuku. Mtu anaweza kudhani labda hapa tuanze kuchagua kipi kitangulie, yai au kuku? Hapana, hapa inajulikana reli kwanza, barabara baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililopo hapa ni kwamba barabara inagusa kila Mbunge na hili naomba nitumie nafasi hii kulaumu sana Waheshimiwa Wabunge, mniwie radhi kwa sababu reli haiwezi ikakuongezea umaarufu binafsi kwenye Jimbo, ndio maana kwa miaka mingi tu Wabunge wamekuwa wanakazania zaidi barabara kuliko reli. Lakini tungelitazama kitaifa na tukaona umuhimu wa reli tusingepiga kelele na kila mtu kutaka barabara ya lami kwenye Jimbo lake tungepiga kelele ya reli kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigoma wakati reli inafanya kazi vizuri hawa akina Zitto walikuwa hawasemi, wako pembezoni hawa, walikuwa kimya kwa sababu reli ilikuwa inafanya kazi. Reli ilipoanza kusuasua tu, hata hisia za kuwa pembezoni zikaanza. Tunapoteza uchumi! Huu utandawazi jamani unaanzia miguuni hapa. Kwangu mimi utandawazi wa Tanzania ungekuwa kuimarisha miundombinu hasa reli, Dar es Salaam, Kigoma tukavuna hayo mabilioni ya fedha. Bandari zote za Bahari ya *Atlantic* hakuna anayezitaja. Lakini tunafanya mchezo na hili jambo sasa wanaanza wa Angola wale kujenga reli, Mozambique wanajenga reli, Kenya wanajenga reli, wamewekeza kiasi cha kutosha tu kwenye Bajeti yao, sisi tupo tunatazama, fedha yote tumepeleka kwenye barabara. Mimi naomba sana Waheshimiwa Wabunge hili tulirudishe, hela zaidi kwenye reli zikatafutwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono pia kwa sababu ya porojo nyingi iliyopo *around* Uwanja wa Ndege wa Mwanza. Mimi natoka Mwanza. *Issue* ya *BADEA* mmeisikia muda mrefu tu. Nakumbuka sana hotuba nzuri kabisa ya Rais mwaka 2006 wakati anazindua Bunge hapa, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete, aliongea kwa hisia na kwa msisitizo kwamba Mwanza itakuwa *hub* ya maendeleo ya maziwa Makuu. *Six years down the line,* hiyo *hub* iko wapi? Watu wamemwangusha, ziko hadithi tu, *BADEA* mwaka huu, *BADEA* mwaka kesho na hivi leo humu nimesikia tena kuna *BADEA* hapo hapo Mwanza. Hivi jamani tunapoteza fursa. Entebbe ungekuwa uwanja *redundant* ule kama Mwanza ingekuwa inafanya kazi vizuri. Leo kwa kushangaa shangaa kwetu hivi hivi Kenya wanajenga hapo Taveti Uwanja wa Ndege. *Now, take it from me* Mwenyekiti, Kilimanjaro itakufa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mheshimiwa Ndassa aliuza swali fupi sana la *second* mbili kwamba, Mheshimiwa Waziri ndege ngapi zinaruka? Nikamwona Mhandisi mwenzangu Mfutakamba anavyohangaika, maana amebeba, akaanza takwimu. Mwaka kesho, jamani, *we are sick and tired of these* takwimu. Watu wanataka ndege zilizoko angani. Mipango mitamu

mitamu tangu enzi zile tunaambiwa sasa wanakuja *South African Airways*, shirika litakuwa zuri sana na kadhalika. Hivyo hivyo Rais anakuja, reli itaboresha, itaongezwa sijui uwezo, yote haya hapana jamani. Mimi hata yangekuwa maneno machache, lakini kazi inaonekana, wala tusingehoji. Kwa sababu ukidanganya asubuhi, ukadanganya jioni kesho kutwa ukasema ukweli, mtu anafikiri ndiyo kazi yake huyu kusema uongo hata yale uliyosema ya ukweli wanajua si ndio utaratibu wake Yule! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *UDA,* ujanja ujanja mtupu pale! Watu wanachakachua kila kitu. Nasikia kuna kiwanja kile kiko mbele ya *TRA* pale kimeshauzwa, halafu jamaa anataka aweke uzio, sijui sasa kituo cha *station* mtakihamishia wapi? Lakini najiuliza sana, huyu Msajili wa Hazina aliyepigiwa upatu sana hapa siku moja kwamba achukue nafasi ya *CHC,* kazi yake iko wapi? Huyu si ndiye msimamizi wa hisa za Serikali? Ameingia mitini kwenye vikao, halafu baadaye anarudi kinyumenyume, nilikuwepo Mwenyekiti kwenye Kamati ya Miundombinu, siku anajieleza pale, nikamwuliza swali moja, Bwana Mkubwa Msela wewe, ulikuwa wapi mpaka shirika linafilisiwa?

Wewe si kwa niaba ya Serikali? Ssasa ulikuwa wapi wameuza nyumba ya kwanza, ya pili, ya tatu, wameuza *yard* sasa sijui kumekodishwa nini hii *UDA* itakuja kuuzwa na nini, bure! Maana kwa *trend* ile kama leo, nimesikia maneno ya kulinusuru, nadhani kulinusuru kwa kikweli kweli Shirika la *UDA* ni kwa kulikabidhisha sasa lisimamiwe vizuri. Wale waliokuwa wanalisimamia wangelimaliza ndani ya miezi ijayo. Zimeuzwa mali za Shilingi bilioni sijui ngapi, bure, kwa sababu bei zilizouzwa na tathmini iliyokuwa imefanywa havifanani. Kwa hiyo, tuombe sana ushauri wa Kamati ufuatwe mara moja. *CAG* nenda pale haraka, Tume ya Mheshimiwa Serukamba inaweza hata isiende, lakini Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali aende afanye kazi pale *UDA fast. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, meli huko ziwani kwetu tunakoishi Mamlaka walikabidhiwa meli 14 Umoja, sasa haijulikani ni ya nani. Ilikuwa inapeleka mabehewa Uganda na ndiyo leo sasa mnaanza kumwona Museveni anakazana kuungana na Kenya ili mabehewa ya mizigo yake yakatokee Mombasa kwa sababu Umoja iliyokuwa inachukua mabehewa Mwanza haifanyi kazi, hata ingekuwepo mabehewa hayaendi kwa sababu reli yetu ni mbaya. *(Makofi)*

Ndugu zangu, wako watu huko ziwani maisha yao yalikuwa yanategemea sana hizi *MV Clarious* zote *grounded*. Inasikitisha sana kuona kwamba mipango ya Wizara hata fedha zinazoombwa, naamini siyo kwamba Serikali haikutaka tu kuwapa fedha, kasungura haka ndugu zangu si kaelekezwe kwenye mambo ya msingi? Kama unakata mnofu, si unakatia huko kwenye mambo ya msingi? Mimi naomba sana, kweli tukairejee tena upya tuvione vipaumbele vyetu vya kitaifa na suala la uchukuzi ni la umuhimu wa juu sana. Kama Mheshimiwa Waziri wamemtolea macho akaona shida kumsukuma zaidi Mheshimiwa Mkullo, iombe Kamati ikusaidie, liombe Bunge hili likusaidie, lakini usife kimya kimya eti mimi zilizotolewa ndizo hizi hizi, kasungura, hapana. Kasungura haka ni ka Watanzania wote na tuwe na macho mazuri tuyaone yapi tunahitaji kwanza, na yapi ya kipaumbele cha juu ili uchumi wa nchi yetu uweze kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa nigongewe kengele ya pili, lakini kwa kweli siungi mkono hoja hii kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya pili kuchangia hoja muhimu sana inayohusu Wizara ya Uchukuzi. Kwanza niungane na Mheshimiwa Dkt. Tizeba kwamba sitaunga mkono hoja hii. Ninaomba Wabunge wote wenye mapenzi mema na nchi yetu wasiunge mkono hoja hii. Kama Wabunge tulivyoungana kwenye Hoja ya Wizara ya Nishati na Madini, na kwa kweli kama tunaitakia nchi yetu mema, tukaweka dhamira ya kuweka tofauti zetu za Vyama vya Siasa pembeni, tukipitisha hoja hii haina maslahi kwa Taifa. *(Makofi)*

Nalizungumza hili na ninashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu Peter Kayanza Pinda yuko hapa anisikie vizuri. Tunajaribu na tunajitahidi tuisaide Serikali katika hili ili Serikali ikatafakari upya kama kweli kwa mkakati wa kuiondoa nchi hii kwenye umaskini kwa mkakati wa kutumia miundombinu

ya Taifa hili na kama chanzo cha kukuza uchumi wa Taifa letu, vile vile kwa mkakati wa kuwasaidia Watanzania walio maeneo mbalimbali na kwa lengo la kuwa *competitive* au kuweza kuingia kwenye ushindani wa nchi za jirani, kweli tukipitisha bajeti hii tunaliangamiza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeeleza katika kabrasha hili, inahitaji nini angalau kuweza kujisukuma kidogo. Waliomba jumla ya shilingi bilioni 565 kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo, lakini wamepewa Shilingi bilioni 95 kutoka ndani na Shilingi bilioni 75 za kutegemea wafadhili wa nje jumla tumepata Shilingi bilioni 168, tuna *deficit* ya Shilingi bilioni 397. Ni hakika hatutaboresha *airport* zetu, ni hakika hatutaboresha Bandari zetu, ni hakika tutaendelea kuwa tegemezi kwa wafadhili. Nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, kwa mara nyingine tena naomba tuungane pamoja kwa nia njema sana tukatae hoja hii. Kwa upande wa pili, msifikiri nazungumza siasa, nampongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kisekta, ametofautiana kimsingi na Waziri wake, ametofautiana kimsingi na Serikali, amesimama na upande wa Watanzania. Nampongeza sana Mheshimiwa Peter Serukamba. *(Makofi)*

Ukiangalia alichokizungumza Mwenyekiti wa Kamati ya Kisekta, utafikiri tunazungumza Serikali mbili hapa Bungeni. Lakini tunamshukuru kwa sababu tumeondoa ushabiki wa Vyama vya Siasa, tumeweka maslahi ya Taifa letu mbele. Leo tunazungumza reli ya kati. Hii reli ni muhimu mno. Lakini hebu tuambie, hata kwenye Hotuba ya Wizara haijazungumzia reli ya Tanga, tumeacha reli ya Tanga imekufa, reli ya kwenda mpaka Arusha imekufa, reli ya kwenda Voi kutuunganisha na Kenya imekufa, hakuna mpango wowote wa kuifufua. Tunazungumza kujenga reli mpya; za zamani tumeshindwa kuzi-*maintain. TAZARA* iko hoi, Mashirika yote yaliyoko chini ya Wizara hii, *TRC* iko hoi, *TAZARA* hoi, *ATCL* ndiyo mfu kabisa. *UDA, KADCO, TICS, TTCL*, tunapitisha bajeti ya nini hapa? Mashirika yetu haya hayawezi kujiendesha, yote yanaingiza hasara kwa Taifa. Tunapitisha bajeti, tunamfurahisha nani kupitisha bajeti hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli leo mimi nasema kwamba nitashangaa sana kama Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wakiamua kupitisha bajeti hii!

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwenda kwenye mfano mwingine *specific,* nizungumze suala la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa *KIA* na nalizungumza hili kwa sababu *KIA/ KADCO* iko kwenye Jimbo langu na ni uwanja wa ndege ambao nautumia sana. Hapa niibane Serikali, niwaulize, hivi mnaona shida gani kueleza ukweli kuhusu *KADCO*? Ni kwa nini mnatumia fedha za Watanzania bila kuweka mambo haya wazi? Mheshimiwa Waziri? Mnatumia fedha kufanya mambo ya ajabu ajabu ambayo hayana uwazi na ukweli, matokeo yake tunalazimika sisi kufanya tathmini zetu na tafiti zetu kukusanya nyaraka mbalimbali zinazoonyesha matumizi mabaya yanayofanyika katika Uwanja wa Kimataifa wa *KIA*. Niliuliza hapa mara ya mwisho nikasema, Waziri alisema uongo, mkanikatalia na leo nitaendelea kuzungumza hivyo na nitatoa vielelezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Watanzania wenzangu wanisikie kuhusu Uwanja wa *KIA.* Uwanja wa *KIA* ni aibu kwa Taifa, yaani kama Serikali inaweza kuingia mkataba kwa misingi ya Uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro ya *KADCO;* ni kwamba, tunadharauliwa dunia nzima kwamba pengine sisi hatuna akili timamu. Kwa kumkodishia mtu Uwanja wa Ndege miaka 25 analipa kodi kwa mwaka dola 1,000, akapewa uwanja wenye eneo la kilomita za mraba 110, yaani 110 *square kilometres of land* tunampa mtu na Uwanja wa Ndege na kila kitu kwa kiwango cha dola 1,000 kwa mwaka! Huyu mtu akaahidi atajenga uwanja mkubwa, yaani atapanua uwanja, atajenga mahoteli makubwa, atajenga *resorts*, atajenga nini, *investment* kubwa kweli kweli. Tukampa uwanja kwa miaka 25! Jamaa alikusanya pesa, na mimi niliuliza swali hili makusudi hapa Bungeni na Waziri namshukuru sana alinipa majibu ambayo nilikuwa nayataka. Nikauliza huu uwanja umezalisha nini? Ambacho aliniambia Mheshimiwa Waziri ni kwamba katika kipindi tangu uwanja huu umebinafsishwa mwaka 1999, uwanja huu wamepata pesa kiwango cha shilingi bilioni 56.94.

Nikauliza Serikali ilipata nini katika vyanzo hivi vya mapato? Nikaambiwa vyanzo vya mapato ya Serikali katika kipindi hiki ilikuwa ni shilingi bilioni tatu. Kwa hiyo, Shilingi bilioni 56.9, Serikali Shilingi bilioni 3, nikauliza Halmashauri yangu ya Wilaya ya Hai ambayo ina-*host* uwanja

huu, imepata nini? Nikaambiwa imepata Shilingi milioni 84 ama sawasawa na Shilingi milioni saba kwa mwaka kwa miaka hiyo kumi na mbili.

Sasa ndugu zangu, hawa wenzetu wamekaa na uwanja, nikamwambia Waziri tumekopa pesa, Serikali imekopa pesa na leo niseme basi, ilikopa pesa kutoka *EIB (European Investment Bank)*, tulikopa dola milioni nne kwa riba ya *one percent* kwa kipindi chote, pesa ambayo tunatakiwa Watanzania tuilipe katika *installment* kumi na mpaka sasa tumeshalipa *installment* ya saba na risiti iliyolipiwa mwaka wa mwisho, imelipwa, na risiti ya Serikali hii hapa mwaka jana, Oktoba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi hawa wenzetu hawakuwekeza fedha, hawakupanua uwanja wa ndege, hawakuboresha masilahi ya wafanyakazi, lakini mwisho wa siku Serikali tukaiambia huu uwanja, huu mkataba una matatizo, Serikali ikaona kuna matatizo, haikutaka kuweka mambo wazi, ikaamua kisirisiri wakachukue ile kampuni ya *KADCO* wairudishe Serikalini bila kutangazia umma, bila kufanya mambo wazi, Serikali imekwenda kuchukua uwanja wa *KADCO* mwaka jana. Mmechukua uwanja wote kutoka kwa wawekezaji ambao hawakuingiza senti tano, lakini bado mkaendelea kuwalipa pesa za Watanzania masikini, mmelipa mapesa chungu nzima ambao leo nataka niyaweke wazi katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mwekezaji kaja, tumempa uwanja, amekusanya mapesa yake, hakuwekeza pesa, tumekopa sisi *EIB*, tunalipa sisi *EIB* na bado Serikali ina *installment* tatu za kulipa *EIB*, lakini hawa jamaa tumewalipa pesa, waliolipwa ni akina nani? Kuna watu wanaitwa *inter-consult,* hii ni kampuni ya Watanzania wenzetu na mnawafahamu, wamelipwa dola za Kimarekani 339,737.1. Hawa wanasemekana wana hisa asilimia nne *point something* ya Uwanja wa *KIA*.

Kuna watu wengine wanaitwa *Mott McDonald*. Hii kampuni tulii-*doubt* tangu siku ya kwanza na mimi nime-*search* kuanzia vyanzo mbalimbali mnasema ni Kampuni ya Uingereza, hii kampuni hatumjui mmliki wake ni nani. *Mott McDonald* wamelipwa dola milioni tatu. Kampuni ya tatu inaitwa ni *South African infrastructure Funds (SAIF)*, kampuni hii tume-*search* vilevile, haikuwekeza fedha yoyote katika Uwanja huu, imelipwa mwaka jana dola za Marekani 2,250,000, jumla tumelipa pesa mbalimbali zaidi ya dola milioni tano *point something* ambayo ni zaidi ya bilioni tisa ya Tanzania. Nataka kuwauliza Watanzania wenzetu, hivi ninyi jamani uchungu wa nchi hii mnao? Dola milioni tisa inalipwa, yaani kama vile ni fedha ya mtoto, haina mwenyewe, na hamtaki kuweka wazi basi mambo haya yakajulikana. Sasa leo naangalia *Revenue Book* ya Serikali kwamba tumechukua uwanja huu Oktoba, 2010, *Revenue Book* ya Serikali kama hadi mwaka jana wa fedha kwa ripoti, jibu alililoleta Waziri hapa Bungeni, *KADCO* ilitengeneza shilingi bilioni 8.4, naangalia kwenye *Revenue Book* ya Serikali, yako wapi mapato ya *KADCO*? Hayapo. *(Makofi)*

Tumebinafsisha uwanja *a hundred percent*, tumeacha wafanyakazi wote wako chini ya Mzungu pale *KIA*, kama Serikali imechukua hisa zote za *KADCO* ni kwa nini imeshindwa kuchukua wafanyakazi wake Watanzania wenzetu wawarudishe chini ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege vya Tanzania, *Tanzania Airport Authority*, tumewaacha chini ya *KADCO*, hawana usimamizi unaoeleweka, mambo hayaeleweki, wafanyakazi wanalalamika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu ambayo naitoa mahali hapa, haiwezekani makosa kama haya yakafanyika, Serikali ikakiri makosa, ikaenda ika- *uy back* zile *share* na bado hakuna mtu hata mmoja anawajibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda *TRL* matatizo hivyo hivyo. Tunaingia mikataba hatuwajibishi watu. Serikali gani inashindwa kuchukua hatua? Wawekezaji wa nchi za nje wanatuona sasa sisi ni majuha tu, yaani wanaona CHADEMA ni majuha, CCM ni majuha, *TLP* ni majuha, *NCCR* ni majuha, Watanzania sisi ni majuha kwa sababu ninyi watu wachache mnashindwa kufanya maamuzi ambayo ni magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ATCL* leo ni aibu. Inakufa, mnalipa tu mishahara ya bure, hakuna mtu anayewajibishwa hata mmoja wala kufukuzwa kazi, mko *busy* mnavuana magamba. Ukienda

*THA, TTCL,* Makampuni mbalimbali nchini fedheha tupu! Haki ya Mungu nasema Waheshimiwa Wabunge wenzangu tukipitisha bajeti hii, hatuwatendei haki Watanzania. *(Makofi)*

Nyie Mawaziri masikini ya Mungu, wageni tu mmekuja, kwa hiyo, inabidi uwajibikaji wa pamoja, lakini Serikali hii ndiyo hiyo hiyo na lazima tupinge kwa nguvu zetu zote kabisa katika dunia hii kupitisha Wizara hii. Kipekee Mheshimiwa Waziri nataka majibu ya uhakika, ya *fate* ya wafanyakazi wa *KIA* na ni kwa nini wasirudi Mamlaka ya Hali ya Hewa *TAA* na *TCAA*? Halafu nasoma Wizara hapa eti bado mnatafuta mbia mwingine, yaani nchi hii ya ajabu kweli kweli. *(Makofi)*

*A hundred and twenty,* anasema Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, imenunua hisa zote za Kampuni inayoendesha kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro *KADCO*, taratibu za kumtafuta mshauri mwelekezi, *transaction advisor* atakayeshauri Serikali kuhusu namna ya kumpata mwekezaji katika kiwanja hicho zimekamilika. Yaani unataka kuutoa tena uwanja huu, na taratibu zimekamilika? Tunawaambia, jamani, tunataka *fate* ya wafanyakazi wetu katika ule uwanja wa ndege, wafanyakazi wetu warudishwe katika Mamlaka za Viwanja vya Ndege.

Wabunge wamezungumza hapa kuhusu *strategic plan* za wenzetu wa nchi za jirani, yaani tunacheza wakati tunaingia katika soko la pamoja, tunacheza wakati tunaingia katika ushindani na nchi za jirani, tunacheza wakati tunashindana na makampuni makubwa ya Kimataifa, *multi nationals!* Nimewaambia siku nyingi, tufike mahali tuamini kwamba sisi wasiasa kuna masuala mengine ya kiuchumi hatuna uwezo nayo, tu-*source brain* za Taifa hili zisaidie katika mipango mbalimbali ya kurekebisha uchumi wa nchi yetu, kwa sababu ukiangalia mashirika yote yako hoi, lakini bado tunazungumza habari ya nia njema ya kutumia *economic* sijui, *I don't know*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hoja yangu ya msingi nilitaka nimalizie hapo, ninahoji huu usiri mkubwa wa Serikali unakuwa wa nini? Hivi kweli Wizara hii ilijiandaa? Hivi kweli Baraza la Mawaziri mlikaa kabisa mkaridhika, yaani mkaridhika kabisa, Waziri Mkuu akaridhika, Mawaziri mkaridhika, Rais akaridhika sasa tupeleke Bungeni, Wabunge wale watapitisha tu kwa sababu si wanaangalia tu? Kweli mkatuletea Wizara kama hii ambayo haitoi matumaini yoyote kwa Mtanzania? *(Makofi)*

Mnaua reli, sasa mnaweza ku-*manage* nini? Mmeshindwa ku-*manage* ndege, mmeshindwa ku-*manage* Bandari, mmeshindwa ku-*manage* Viwanja vya Ndege, mpaka mabasi *UDA* mmeshindwa ku-*manage*, KAMATA mlishindwa ku-*manage*, halafu mnajisema ninyi ni watu makini, umakini uko wapi? *(Makofi)*

Tukiandamana mnapiga kelele, kwa nini tusiandamane? Sisi tutasema nini jamani? *Honestly to good God* tuache mambo ya ushabiki wa Vyama vya Siasa, kuna mambo mengine Serikali mnafanya ni aibu. Hata mimi najisikia vibaya sana hapa kuweza kusema maneno makali mbele yenu na nyie mmekaa mnaniangalia, ni marafiki zangu, ni Viongozi wangu, nawaheshimu sana. Lakini nifanye nini kingine zaidi ya hicho? Kwa mipango kama hii, tufanye nini Watanzania wengine? Wako Watanzania wengi nje huko wanalalamika, watu wananung'unika, ukihesabu mashirika haya ambayo yako chini ya Wizara ambayo yote yako hoi, Waziri asimame kama kweli yeye ni mcha Mungu wa dini yoyote, aseme. Tena nasikitika nasema na mama yupo hapa, mama utanisamehe sana, lakini ni mambo ya kazi tu. Nasema Waziri asimame aseme ni shirika gani moja linalofanya kazi kwa ufanisi chini ya Wizara hii na tunategemea watafanya lini kazi kwa ufanisi chini ya Wizara hii kwa utaratibu wa bajeti hii?

Mimi ninachosema, sitaki kusema uwezo wenu wa kuongoza Wizara hii umeshindikana, lakini ningependa kusema tu kwamba tuna sababu za msingi za kuwakatalia bajeti hii siyo kwa faida ya CHADEMA, wala siyo kwa faida ya CCM, ni kwa faida ya nchi yetu, ni kwa faida yenu na sisi. Tunaona aibu kuwasuta sana, mrudishe hii Wizara mkakae tena mfikirie kama ile ya Madini na Nishati ili mkishakaa vizuri, mkajipanga, mtuletee mpango ambao unawapa Watanzania matumaini. Kateni pesa maeneo ambayo siyo ya msingi, pelekeni pesa kwenye maeneo ya msingi yatakayoweza kuboresha miundombinu ya Taifa hili na lazima mje hapa na mpango wa kutuambia Reli ya Kilimanjaro, Reli ya Arusha, Reli ya kwenda mpaka Voi, Reli ya kwenda mpaka

Kigoma, Mpanda zina mpango gani na hela ziko wapi? Siyo kutuambia mipango, mipango mizuri inaendelea, mipango inaendelea. mpaka lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo kwa sasa. Naomba nisiunge mkono hoja na naomba Wabunge wote msikubali kuunga mkono hoja hii. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii. Ni wajibu wangu kuishukuru Serikali kwa ujenzi wa Gati, ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Mafia na upanuzi na utengenezaji wa barabara ya kutoka Kilindoni *Airport* mpaka Utende. Nasema tunashukuru sana na tunawatakieni kila la heri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini haya yanayosemwa, wanayoyazungumza Waheshimiwa Wabunge, sisi ni washauri, na bahati nzuri nasema Serikali yetu ni sikivu na viongozi wetu ni sikivu kwa maana ya Mawaziri, lakini kwa kuwa natokea Chama cha Mapinduzi, hata wale Wajumbe wa Chama waliokuwa ndani ya Bunge na nje ya Bunge wanasikia kilio cha Waheshimiwa Wabunge wanavyolalamika hapa ndani. Tunaomba ushauri huu unaotolewa waupokee na waufanyie kazi. Lakini kama mnaona raha, maana yake inawezekana na wengine wana *hobby* kwamba mpaka nisemwe, nidhalilishwe ndiyo nifanye. Ni aibu, ni aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani kila siku iwe kazi yetu ni kusema na kila Bunge linalokuja hapa kikao kinachokaliwa watu wanasema, lakini hakuna kinachofanyika kwa maana ya utendaji ule unaozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge humu ndani. Naomba sana Waheshimiwa Mawaziri, msikubali kuwa makafara. Ninyi sio mbuzi wa kafara, ninyi ni binaadamu ambao mna familia zenu na mmewekwa hapa kwa kuaminiwa, na mkaaminiwa na Serikali pamoja na Mheshimiwa Rais, sasa mnapokaa kimya kule watu wanafanya madudu, ninyi mmekaa, labda ndiyo mnaona raha, basi sasa yote yanayowasibu mtakuwa ninyi wenyewe ndio mnawajibika. Tafadhalini, kuweni wakali, wasimamieni Watendaji. Ni aibu kwa haya yanayotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa Mafia nimemaliza kwa sababu kila mtu anafahamu, Bunge hili na Watanzania wanajua na dunia inajua kwamba Gati linajengwa na linakaribia kukamilka pamoja na uwanja wa ndege, isipokuwa ninachouliza; kuna fidia jana wakati tunachangia Wizara ya Ujenzi, nilisahau tu nikaghafilika, nitaomba Mheshimiwa Waziri kwa kuwa mradi huu wa barabara unaendana na mradi wa uwanja wa ndege, basi pata maelezo kutoka Wizara ya Ujenzi. Siyo vibaya ukituambia kwamba fidia za watu wale watakaoathirika na ubomoaji wa nyumba inayopita barabara ile kilomita 14, lini utaanza kulipwa na watu watapewa muda gani wa kuanza kujitaharisha kuhama kwa maana ya kujenga majumba yao na kuweza kuhamia na kupisha ujenzi wetu mzuri wa barabara ya lami katika Wilaya ya Mafia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nataka kabla sijaendelea na mengine, nikushukuruni sana Waheshimiwa Mawaziri wawili, jana Mheshimiwa Waziri Omar Nundu na Mheshimiwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Mponda, nawashukuruni sana kwa imani yenu mliyoionyesha jana na kutumia wadhifa wenu na huo ndiyo uongozi. Baada ya Mashirika ya Ndege yanayokuja Mafia kukataa kubeba mgonjwa, mkatoa amri na nimefuatilia mpaka kwa *Captain* Aziz alipata taarifa kutoka kwa Mkurugenzi wake wa kampuni na mgonjwa yule amesafirishwa, hivi sasa yuko Muhimbili japo kuwa mpaka sasa tunaongea bado hajapata fahamu. Namwombea kila la heri na *Inshaalah* Mwenyezi Mungu atampa afya njema na aweze kuendelea na masomo katika Shule ya Aekondari Kilindoni kwa kuwa yuko Kidato cha Tatu. Naomba Waheshimiwa wenzangu mumwombe dua apate kupata afueni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aibu! Aibu ninayotaka kuizungumza, mimi kwetu Mafia, wazazi wangu baba na mama wametokea huko, lakini nimeishi Dar es Salaam, nimekulia Dar es Salaam Gerezani, nimeishi pale, nimesoma Shule ya Muhimbili, nimesoma Kinondoni kwa maana nimetumia mabasi ya *DMT* mpaka yakaja kuwa *UDA.* Tunaomba, ni aibu kusikia shirika hili limeuzwa, halafu linauzwa kihuni kama lilivyozungumzwa. Yapo magazeti hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi tunasema tusitumie ushahidi wa magazeti, lakini mengine wanayoyazungumza ni ukweli. Leo mtu mmoja anakwenda kuingiziwa kwenye akaunti yake binafsi eti kwa sababu *UDA* inadaiwa. Sasa ukiingiza kwenye Shirika la *UDA*, benki itatoa. Ina maana ninyi mnapanga kuziibia hizo Benki? Uongozi mnakaa kuiibia Benki? Kwa nini? *(Makofi)*

Kwa nini mlikaa mpaka mmeshindwa kulipa wakati shirika lilikuwa lina uwezo? Tulianza kutumia kupanda kwa senti 15, mpaka mimi nimeacha kupanda mabasi ya *UDA* baada ya kuhamia Mafia kwa shilingi karibu 100 hadi 150. Lakini hakika ni tendo la aibu tukisikia Serikali hii inakubali Shirika hili la *UDA* ambalo ndiyo shirika litakaloweza kutusaidia hata kwa wanafunzi wetu ambao wanatumia mabasi haya bila kubugudhiwa na wenye madaladala. Naomba sasa Mheshimiwa Waziri wasikutose. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa kwanza ni kwamba, kamata wote waliohusika, usiwaonee huruma. Kamata wote waliohusika kuanzia Meya, Mkurugenzi wa Jiji, Bodi ya *UDA*, Wakurugenzi wote kamata weka ndani na Mkurugenzi wa TAKUKURU afanye kazi apekele vijana na akaunti zao zote wazi-*cease* kwanza mpaka ijulikane hizi pesa zinaingizwa kwa nini na haya yote yanatokea. Bila ya hivyo pale Dar es Salaam na madaladala tunasema yatakuwa hayatembei. Wewe unakwenda kuuza *terminal* ya Kurasini kwa Shilingi bilioni 1,400 hata Wabunge watano hapa tungejikusanya tukachanga, wako akina Abood hawa, *Abood Bus* wana uzoefu, wana uwezo, wapeni waendeshe, wapo akina Shabiby hatujawahi kusikia ukorofi hata siku moja kwenye Makampuni yao, madereva kugoma au kufanya hivi, leo unakwenda kuuza ardhi ile! Imezungumzwa hapa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hapa *station*, tumezoea kuita *station*, *city drive*, aibu! Nasema *Wallah Bilah* na Ramadhani hii mkikubali, basi bora mwondoke wote hapa, yaani ni aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nasema TAKUKURU, Edward Hosseah fanya kazi yako haraka iwezekanavyo, tena nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kamata, toa amri hawa watu wote waliohusika, hakuna kujali huyu nani wala nani. Wote kamata weka ndani kwanza, halafu wapishe uchunguzi ufanyike na hata ukifanywa na naishukuru san *CHC* kwa kutoa maelekezo kwa Wizara ya Ardhi kwamba hati zote za viwanja zisibadilishwe, ni aibu. Kama wamechukua, basi wameuziana huko huko kwao walikotoka, tunasema hatukubali Shirika la *UDA* liendelee kuwa la Serikali tena kwa asilimia 100, hatutaki hizo hamsini na ngapi wala ngapi, hatukubali na kama uchambuzi, basi ufanyike, washirikisheni na Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam, wanafanya uhuni, vikao vinafanyika Dar es Salaam kwa sababu Wabunge wanaona wako huku, ushauri wao labda watakuja kuharibu dili lao. Tunasema vikao vifanyike vya uwazi na hili liweze kufanyika. *(Makofi)*

Wabunge wa Dar es Salaam wanalalamika na sisi wote tunakaa Majimboni kwetu, lakini na Dar es Salaam tunakaa. Kama mimi sipandi *UDA*, basi mwanangu na mtoto wangu, jamaa, yangu, shangazi yangu na mjomba wangu watapanda. Tunasema sisi shirika lile ni la wote, siyo la kikundi cha watu wawili.

Mheshmiwa Mwenyekiti, la mwisho, nilichotaka kusema ni kwamba kuna matatizo baharini. Kuna ujangili mkubwa sana na bahati nzuri na Serikali imeshuhudia jinsi ujangili ulivyokuwepo na hata Mafia upo kwa sababu tumeshakamata baadhi ya watu na mimi mwenyewe nilihusika katika kuwakamata hawa watu na wakathibitika tukakabidhi kwenye vyombo vya sheria na wakaweza kuchukuliwa hatua. Sasa tunaiomba Serikali, Wizara ya Uchukuzi, Jeshi la Polisi ikiwa JWTZ ikiwa Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), tunaomba pale Mafia kituo cha doria kiwepo, kituo kikuu cha baharini kiwepo, kwa sababu ujangili unaofanyika siyo wa meli. Mwezi mmoja uliopita Mafia walikuja watu na boti na wakaivamia boti iliyokuwa safarini kutoka Mafia kwenda Kilwa na wakawakatakata mapanga, watatu wakawatosa na wengine wakajifanya wamekufa wakaogelea mpaka Kisiwa cha Bwejuu, ndiyo wakatoa taarifa.

Sasa tulipotaka kwenda kuwafuatilia tukashindwa, hatuna vyombo vya kasi vya doria. Kwa hiyo, tunaomba kwamba utakapoweka kituo cha doria Mafia utaweza kusaidia kutoka Dar es Salaam kwa maana maeneo ya Buyuni, Pemba Mnazi, unakuja mpaka maeneo ya Mkuranga Kwale, Koma, Sukuti, Kuruti, tunakwenda mpaka maeneo ya Rufiji, yote kuanzia Mchungu, mpaka Mbwera na maeneo ya Kilwa unarudia Kisiwayuni na Songo Songo. Pale likitokea tatizo, boti ikiwa

pale ya *rescue* tutaweza kuwasaidia wale watakaoathirika. Kwa hiyo, kwa kupitia Wizara, hii naleta ombi la kusema kwamba Mafia tupatiwe Kituo cha kuweza kuokoa watu kwa maana ya ujangili na hata hatari za baharini zinapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wetu ni msomi mzuri sana na bahati nzuri alikuwa katika Kamisheni ya *Air Navigation Canada.* Kwa hiyo, naamini hayo unayoambiwa kwanza usikubali kubughudhiwa, na kama ulikwenda kuomba pesa; hivi, hii Wizara ya Fedha kila siku ina maana hapa tunakaa, lakini baadaye Wizara zitakwenda zitapewa hela zitarudi, mpaka mwone wanadhalilishwa wenzenu, kwa nini? Kwa maana tunaona kikwazo ni Wizara ya Fedha. Maelezo yanayosemwa na Wabunge labda maelezo yanayotolewa na Waheshimiwa Mawaziri na Kamati zao huko wanakokaa na wataalam wao labda Wizara ya Fedha hayawaingii. Labda wanaona raha kukaa na zile hela pale wakiona huku mabilioni yamemzunguka Mama Mamunyange anaona hapa nikitoa mimi itakuwa tatizo. Tunaomba Mama Mamunyange fungua hela wananchi wanaathirika, Serikali yako iliyokuweka madarakani inaadhibiwa, inasemwa chanzo ni nyinyi Wizara ya Fedha. Tunaomba sana waachieni hela ili na wenzenu waweze kuendeleza na wananchi wapate kunufaika na matunda na uhuru wa nchi yao.

Mheshimiwa Mweyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Nianze rasmi kabisa kwa mara yangu ya kwanza kabisa kuona ndani ya Bunge hili ambapo, ni mwaka wangu wa sita kuirejesha bajeti hii ya leo kwa nia njema kabisa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, inatosha. Mpeni nafasi ana mambo mengi ya kusema.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Kwa nia njema kabisa, tunapofanya hivi, hatuna nia mbaya, ili wakae tena upya na kuona jamani Wizara hii imekosea wapi au ishike wapi kuona ni jinsi gani waweze kutukombolea reli yetu, waweze kutukombolea njia zetu za anga na mengine yote waliyotuletea kwa siku ya leo.

Mheshimia Mwenyekiti, Shilingi bilioni 237 kwa Wizara hii hazitoshi. Tunazungumza, ndiyo maana mimi na nadhani na wengine wote mmezoea katika masikio kusikia maneno mikakati, harakati, michakato, tuko mbioni; yanachosha watu kuja kutuambia hapa kwa sababu hatuko *serious.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukidhani kwamba maneno kama haya yatatuweka sawa, lakini ni bure. Narudia, tuna nia njema kabisa. Sisi ambao tunatoka kwenye maeneo ambayo yanatumia usafiri huu wa reli na anga ni adha kubwa sana. Wote hawa wanaotoka Kigoma, Tabora kama kweli watasema hali halisi ya namna hii ni sahihi, hapana. Watakuwa kwa kweli wanajivalisha gamba ambalo siyo lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekit, reli hii ya njia ya kati imeleta mateso makali sana kwa Watanzania walio wengi wanaotumia njia hii. Zamani wakati ikiwa hai kabisa, njia hii treni ilikuwa ikifika Mwanza Treini utadhani labda Wazaramo wote leo wamehamia Mwanza, Wagogo wote wamehamia Mwanza, ukiwaacha watu wa Tabora na katikati hapa jinsi watu walivyokuwa wanapenda njia hii, wanaitumia njia hii kwa amani na utulivu. Lakini leo tunavyoleta kabisa ulelemama lemama wa kuijadili kwa undani suala hili mnadhania labda watu wote wana uwezo wa kutumia magari binafsi kwa kutumia lami ambayo imejengwa kwa usanifu mkubwa katika nchi hii. Kwanza ni jambo la kushukuru sana kwamba Wizara ya Ujenzi imefanya kazi ambayo inaeleweka nchini na kimataifa huko nje. Vinginevyo ingekuwa ni hali ya hatari mno kama hata barabara zetu zingelikuwa bado mbovu, na treni na naamini na njia za reli ndiyo hizi, na njia ya anga ndiyo kabisa sifuri. Hivi tungekuwaje nchini humu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kushukuru sana kwamba tumepata angalau barabara hizi kwa asilimia karibu 90 zinafanya kazi. Njia ya reli ilikuwa ni mkombozi sana kwa mtu mnyonge. Mtu mwenye nauli ndogo, mtu mwenye mizigo yake mingi midogo midogo, anapanda anafika anakokwenda. Msidhani kwamba hii reli, watu wanaotumia barabara ndiyo wanafaidika.

Lakini walio wengi kwenda kufika katikati kwa mfano ya kutoka Dodoma mpaka Tabora pale, hawana usafiri. Kutoka Tabora katikati ya kwenda hata hapo Shinyanga hawana usafiri. Wanahitaji njia hii, tuwahurumie watu hawa, tuwahurumie kabisa. Watu hawa wa katikati hawa wamekosa uzalishaji mdogo mdogo, hizi biashara ndogo ndogo tunazozisema hizi, walikuwa wanauza vinyago vyao, walikuwa wanauza mikeka yao, wanauza vitu vidogo vidogo ndiyo kujikwamua kwao kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wanauza wapi? Ni vitu vidogo vidogo vyenye faida ndogo ndogo, lakini walikuwa wanapata kitu kwenda kusomesha watoto wao, kwenda kutafuta chakula, riziki ya siku. Sasa wamedumaa tu Wagogo katikati hapa. Potelea mbali hata na Wanyamwezi wangu hawa. Hawana, wanasuka mikeka yao mpaka anasubiri tajiri mmoja anapita kwenye barabara ndiyo anauza. Wamerudi nyuma, tumewarudisha nyuma. Lakini Bajeti ndiyo inakuja ya Shilingi bilioni 237 hapana, zikatafutwe pesa. Zikatafutwe pesa jamani! Tumeteseka kwa muda mrefu mno sisi tunaotegemea usafiri huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikiwa humu, ile bajeti ya kwanza nyuma ya miaka ile mitano, tukaona kasi kubwa kweli, uwanja wa Ndege Mwanza unatengezwa. Tukasema naam, na sisi tunaingia kwenye ulingo. Sasa hivi kimya. Sera zililetwa baadaye tena ikawa kimya, tukasikia kwamba kuna fedha zimetolewa kwa ajili ya kuendeleza uwanja wa Mwanza. Ghafla kimya. Zilihamishwa? Zilikwenda wapi pesa hizo? Leo nitakumbuka nitaziweka kwenye maandishi, nitatafuta hizo pesa ambazo najitahidi kuzikumbuka, lakini ikawa kimya. Uwanja wa Mwanza umesimama, umebakia wa kuzungumzwa tu. Sijui sasa hivi kuna shirika gani ambalo mwekezaji gani amejitolea kuja kutengeneza na kwenyewe mpaka sasa kuko kimya. Fedha zilizotolewa humu kweli zinatosha kuja kurekebisha kwa hali halisi ilivyokuwa imepangwa hapo mwanzo? Hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba huu uwanja uchangamkiwe kuanzia sasa, laini kwa kwenda kutafuta pesa wapi zinapatikana. Ukweli ndiyo huo, narudia kusema kwamba tunapowarudisha siyo kwamba hatuwapendi. Tunataka mkabanane huko huko na wafanyakazi na hao wataalam. Mtajua tu kwa kushika. Mimi kipindi hiki nimeuliza juu ya shirika hili la ndege. Nilizungumza hapa, niliuliza swali, nikapata jibu. Niliwauliza watu, kwa nini hata hawa wanaoua mashirika haya hatujasikia lolote kwa mtu kuchukuliwa hatua? Hatujasikia. Nilisema humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasikia tu hizo hizo ndiyo labda haya maneno niliyoanza nayo. Mko katika harakati ya kuwakamata, mko kwenye michakato ya kuwakamata, mko mbioni kuwakamata, mmejipanga kuwakamata, vitu vinakwisha hivi hivi. Jamani, wakati wa usichana wetu, yaani Tanzania hii ilikuwa nzuri mno. *It was beautiful!* Sasa vipi kitu kikianza kuporomoka ndiyo kinakwenda mwisho kabisa? Hatuna mahali pa kuidakia! Hakuna mahali pa kudakia tatizo mpaka linakwisha, linateketea!

Mheshimiwa Mwenyekiti sijatumia kauli za namna hii, ni leo. Lakini kwa machungu makubwa kwamba kweli tunahitaji reli ifufuke. Tunahitaji njia za anga jamani, ndege ya *ATC* imechorwa twiga. Nembo ya utalii wa nchi yetu ni nembo ya nchi yetu, sijui imepakiwa wapi. Hata Dar es Salaam imekwenda kutengenezwa? Jamani mtakapokwenda kujipanga, pamoja na kuifufua hii ndege, hebu leteni, sasa nikiruhusu tena hiyo mikakati na harakati na michakato kutafuta ndege nyingine mpya na sisi tujipange kununua vitu vipya, hata moja tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimalizie tu kabisa hasa katika hili suala la uwanja wa ndege wa Mwanza. Nilikuwa nazungumza hapa hata na viwanja vingine. Viko viwanja vidogo vidogo hivi vya Mtwara, Shinyanga pale Ibagapuru, sijui nini na vyenyewe vimeduwaa tu, vimefubaa, tu wenyewe mmo humu mtazungumza, na ndege zenyewe hatuzioni. Tunabaki kutajirika mashirika ya watu binafsi, wametajirika sana hawa watu na wanafanya kazi kwa maringo hasa. Utaambiwa ndege inakuja saa sita, inakuja saa tisa. Utaambiwa itakuja saa saba, ikiingia saa saa tano haisubiri msafiri uliye-*book* kwa uhakika kwamba nimeambiwa *reporting time* ni saa fulani, wanaondoka. Mtawafanya nini? Kitu chake mtu binafsi utakifanya nini? Tuna uwezo wa kuijadili *Precision* humu? Nawaomba kabisa kwa nia njema, uzalendo tuuweke jamani kwa

kufufua mali zetu. Tutabakia wa kukodi. Hata kama mnakodi na kwenyewe ni aibu tu. Ni afadhali kudunduliza mkawa na chenu cha uzalendo katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, nashukuru kwa kupata nafasi hii na kwamba na Wanamwanza ndio walionifikisha hapa, hasa akina mama, naomba mwapelekee treni, nawaomba mwafufulie kabisa njia yoyote ili kusudi waweze kuwa na maisha bora kuanzia sasa kama tutaungana katika hili ili wote turejee ile raha yetu ya zamani. Sisi hata kupiga ile honi ya treni ilikuwa, hata kama ulikuwa unasonga ugali unasema, aaah, hebu nikaone labda leo nitapata mgeni. Sasa hivi starehe zote hizo tumezikalia. Hapana! Nasema, hapana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tufute ile misemo yangu ya kwanza yote, tuifute tuingie kazini. Tuingie kazini, CCM haishindwi, ninaamini kweli kama mtaingia kazini. CCM ni Chama bora chenye sera nzuri, chenye mikakati, tuacheni uongozi wa Chama tutaiweka tu mikakati mizuri, mtafanya kazi vizuri. Naishia hapo, lakini naamini nimeeleweka. Asanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. ANGELLAH J. M. KARIUKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami pia nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. La kwanza kabisa kabla sijapoteza mwelekeo, naomba nisiunge hoja mkono Bajeti ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wafanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania pamoja na *TAZARA* ambao ninawawakilisha katika Bunge hili Tukufu nitakuwa sijawatendea haki endapo nitaunga mkono Bajeti ya Wizara hii, wakati wanakabiliwa na matatizo mengi na matatizo haya yamekuwa hayapatiwi ufumbuzi licha ya wao kutangatanga katika Wizara hii na mara kwa mara hata Waziri amekuwa akiwaahidi atakwenda kuonana nao, lakini wamekuwa wakiyumbishwa na wamekuwa hawamwoni akitokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ya uchukuzi ni sekta muhimu sana katika maendeleo ya uchumi wa nchi yetu pamoja na uchochezi wa shughuli mbalimbali za kiuchumi. Inasikitisha sana kuona ufinyu wa bajeti uliotengwa kwa Wizara hii. Yamesemwa mengi na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliotangulia kusema, lakini kwangu mimi, napata hofu endapo mipango yote mizuri ambayo tumeipitisha katika Bunge hili, hususan Mpango wa Maendeleo wa Taifa letu ambao tumeupitisha siku za karibuni. Kwa kweli itakuwa ni ndoto na hatutaweza kupata matunda tunayoyatarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nisiwe mchoyo wa fadhila. Niishukuru Serikali kwa kusitisha Mkataba wa Uendeshaji wa Kampuni ya Reli Tanzania. Sote tunafahamu kwamba tangu mwaka 2007 Shirika hili limekumbwa na misukosuko tangu Kampuni ya *Rites* ya India ilipoingia nchini kuendesha shirika hili. Serikali iliwaahidi wafanyakazi kwamba endapo Shirika litabinafsishwa, hali yao ya kimaisha itaboreka na maslahi yao yatakuwa mazuri zaidi, lakini hili halikutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majadiliano yalikuwa ya muda mrefu kuanzia mwaka 2009 mpaka Julai, 2011 na naamini sote tumesikia wiki iliyopita Kampuni ya *Rites* ya India inaanza kufunga virago na nimeona barua yako, lakini aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji kufikia mpaka hivi sasa haijakabidhi nyaraka muhimu kwa Menejimenti ya muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo kweli tunataka Sekta yetu ya Uchukuzi iendelee, ni dhahiri kwamba ni muhimu kuhakikisha tunajitahidi kufufua Reli ya Kati na niipongeze Serikali kwa hilo. Lakini tunaamini tatizo siyo *viability,* tatizo letu katika nchi hii tuna mipango mizuri, lakini hatuwezi kuitekeleza kama hatutafuta *financing* kwa ajili ya mipango yote ambayo tunaipanga.

Napenda Waziri atakapokuja kutoa majumuisho yake kesho atueleze ni wawekezaji wangapi wamejitokeza kuwekeza katika Reli hii ya Kati? Vilevile, napenda kufahamu Serikali imejipanga vipi kushiriki kama mbia katika uendeshaji wa Reli hii ya Kati, kwani tunafahamu kupata Dola za Kimarekani Bilioni 3.5 kutoka kwa Sekta Binafsi pekee si rahisi. Kwa hiyo, atueleze Serikali wamejipanga vipi kutenga fedha kwa ajili na wao kushiriki kama Mbia katika uendelezaji wa Reli hii ya Kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninalopenda kuongelea ni Reli za Tanga na Moshi. Sote tunafahamu Nchi yetu ilivyojipanga kijiografia. Tunayo fursa nzuri sana ambayo tukiitumia inaweza kukuza uchumi wetu, kwani ipo mizigo mbalimbali ya nchi za jirani kama vile Uganda na Kenya, ambayo inapitia katika Bandari zetu kama vile ya Tanga. Hivyo basi, napenda kufahamu Serikali imejipanga vipi kuchangamkia fursa hii ya kijiografia ambayo ipo na nchi yetu imejaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, napenda niongelee Reli ya *TAZARA.* Kuna malalamiko mengi sana kuhusiana na Reli ya *TAZARA.* Tatizo kubwa la Shirika la Reli kwa ujumla na la *TAZARA* ni Menejimenti. Shirika hili la *TAZARA* haliendeshwi kibiashara na sote tunafahamu, endapo tunayo dhamira ya dhati kwa Shirika hili kuweza kuendelea, hatuna budi kuhakikisha tunarekebisha Sheria inayounda Shirika hili la *TAZARA. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria inayounda *TAZARA* inatulazimisha kuwa na Mkurugenzi Mkuu Mtendaji ambaye ni Mzambia! Hivi kweli, Mtanzania hawezi kuwa Mkurugenzi Mkuu katika Shirika la *TAZARA?* Ni kwa nini? *TAZARA* Mtanzania anashikilia Unaibu Mkurugenzi Mtendaji peke yake? Shirika hili limeundwa tangu miaka ya 1980, tumebadilisha Sheria Mwaka 1995, lakini yote haya tumekuwa hatuyaoni? Wakati umefika sasa Serikali ya Tanzania mkae na wenzenu wa Zambia mjadiliane, hatuwezi kuwa tayari Sheria hii ikaendelea kutumika kama ilivyo hivi sasa huku Watanzania wakiwa wananyonywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niingie kwenye hoja mahsusi za wafanyakazi kwenye *TRL* pamoja na *TAZARA.* Tumeona Mipango mingi sana kuhusiana na uboreshaji wa Miundombinu ya Reli pamoja na Menejimenti za reli. Nawahakikishia Serikali, msipoboresha maslahi ya wafanyakazi, yote haya itakuwa ni bure! Ni muhimu maslahi ya wafanyakazi yakapewa kipaumbele kikubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye Shirika la *TRL,* mwaka 2002, Shirika hili lilikuwa *Specified* na likawekwa chini ya uangalizi wa *PSRC.* Kwa miaka 10 tangu Shirika hili lilivyokuwa *specified,* wafanyakazi hawajapata nyongeza ya mishahara, wamekuwa na mishahara duni! Ukichukulia mwaka 2004, aliyekuwa akipata mshahara wa chini kabisa alikuwa akipata shilingi 69,000/=! Kweli shilingi 69,000/= ume-*specify* Shirika hili kwa miaka 10 bila nyongeza ya mishahara, mtu huyu anaishi vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hii tu, wanapo-*calculate* fedha ya *gratuity,* Mashirika yetu ya Hifadhi ya Jamii, yalikuwa yakitumia wastani wa Sh.69,000/= hizi, jambo ambalo lilimsababishia mfanyakazi wa Shirika la Reli usumbufu mkubwa na alikuwa akipata *gratuity* ndogo sana pindi anapostaafu. Sasa napenda kufahamu kutoka Serikalini; kwa kuwa ni makosa yao kwa kuliweka Shirika hili kwa miaka 10 kama *specified corporation,* itawasaidiaje wafanyakazi waliostaafu kipindi hicho cha nyuma ili angalau waweze kuhuisha mishahara yao ya wakati huo na waweze kupata fidia ambayo kweli inaeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Kampuni ya *RITES* ilileta matatizo makubwa pale *TRL!* Wafanyakazi walifanya kazi katika mazingira magumu sana! Walifanya kazi bila ya kuwa na vitendea kazi, walifanya kazi bila ya kuwa na karakana nzuri, walifanya kazi bila ya kuwa na ofisi! Si hilo tu, walikuwa hawajaliwi. Kulikuwa na ubaguzi wa hali ya juu. Sambamba na hilo inanisikitisha, nilete masikitiko yangu kwa niaba ya Wafanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania, mwekezaji huyu *RITES,* alipoingia kuendesha Shirika la Reli Tanzania alisitisha fursa ya wafanyakazi kukopa katika Taasisi za Fedha, kweli ni halali? Sote tunafahamu jinsi mishahara yao ilivyo hafifu na duni! Nimewaeleza waliokuwa wakipata mishahara ya shilingi 69,000/= halafu leo hii kweli humpi hata fursa ya kuweza kukopa! Kwa kweli, kwa hili naomba sana, namwomba Mheshimiwa Waziri, ikiwezekana kuanzia mchana huu... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, unavunja Kanuni, Mheshimiwa Angellah, endelea.

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, leo hii hapa atoe agizo kwa Menejimenti hii ya muda chini ya Injinia Kinsafu, wafanyakazi wa Shirika la Reli kuanzia sasa wapewe dhamana ili kuweza kukopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati *TRL* inabinafsishwa wafanyakazi wa *TRL* hawakuweza kulipwa kifuta jasho. Wameomba kifuta jasho hiki kwa muda mrefu sana! Inashangaza nchini Tanzania *TRL,* sio Shirika la Kwanza ambalo lilikuwa likimilikiwa na Serikali. Yamekuwepo Mashirika mengi ya Umma kama vile *NBC, NMB, Mbeya Cement* na mengine mengi, yote haya wakati yanabinafsishwa watumishi ambao waliendelea na ajira zao walilipwa kifuta jasho. Ni kwa nini, Serikali inavuta miguu kuwalipa wafanyakazi wa *TRL* kifuta jasho, haki ambayo ni ya msingi kwao? Kwa kweli kwenye hili sitaunga mkono hoja hii Mheshimiwa Waziri mpaka wafanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania waweze kupata maelezo yatakayowaridhisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wa *TRL* wamefanya kazi kwa uzalendo mkubwa sana na kwa ufanisi wa hali ya juu, pamoja na kwamba, wamekuwa wakipata maslahi duni. Mmeona wote kupitia vyombo mbalimbali vya habari, wafanyakazi hawa wamekuwa wakijitahidi kupitia uzalendo wao kufufua reli, kufufua mabehewa na wamekuwa wakilipunguzia shirika hasara nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niongelee madeni ambayo yalihamishiwa katika Shirika Hodhi la *RAHCO,* madeni ambayo wafanyakazi wa *TRL* walikuwa wakidai. Hivi sasa ratiba imetolewa ya malipo lakini cha kusikitisha, ratiba hiyo inafahamika mjini Dar-es-Salaam peke yake! Kwa hiyo, niiombe *RAHCO* kupitia Serikali, taarifa hizi na ratiba za malipo haya ziweze kusambazwa nchi nzima ambako kuna stesheni za *TRL* ili wafanyakazi wajue ni lini watalipwa madeni wanayodai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze pia masikitiko yangu kuhusiana na Shirika la *TAZARA.* Shirika la *TAZARA* kupitia Mkurugenzi wake Mkuu, amepewa mamlaka makubwa sana! Amepewa mamlaka kisheria ya kuweza kupanga bei ya kusafirisha mizigo na mizigo mikubwa, hususan usafirishaji wa shaba kutoka Zambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei halisi ya kusafirisha tani moja ya shaba ni dola 127 lakini Mkurugenzi Mkuu huyu, kupitia mamlaka ambayo anayo na kupitia Utaifa wake, yeye na wafanyabiashara wa Zambia, ambao ndio wafanyabiashara wakubwa wa bidhaa hii ya shaba amekuwa akiihujumu Serikali na amekuwa akipanga bei ambayo ni dola 81 mpaka 85 pungufu ya dola 42 kwa tani. Sote tunafahamu gharama ya mafuta ilivyo juu na kama kweli tunataka kuipatia nchi yetu kodi na kama kweli tunataka maslahi ya wafanyakazi yaweze kutunzwa, kwa kweli kwa hakika na kwa hali hii ambayo anaifanya Mkurugenzi Mkuu huyu, hatuwezi kufika popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia tarehe 01 Julai 2011, Bodi ya *TAZARA* ilipitisha bei mpya ya usafirishaji wa Shaba ya dola 127 kwa tani, lakini cha kushangaza wafanyabiashara hawa wa Zambia walisitisha kutuma mizigo yao kwa muda! Hii imekuwa ni tabia, Mkurugenzi Mkuu huyu amekuwa akishirikiana na Wazambia wenzake kuhakikisha mizigo hailetwi ili baadaye aje ajenge kesi yake kwamba, mnaona hakuna mizigo, bei iweze kushushwa tena! Kwa kweli, kwa hili hatukubali na kwa niaba ya wafanyakazi wenzangu wa Reli hatuwezi kukubali hata kidogo. Waziri, tunaomba tupate jibu kuhusiana na hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kuzungumzia ni uuzaji kiholela wa nyumba za *TAZARA.* Inasikitisha, mali ziko kwa upande wa Tanzania na mali za *TAZARA* ziko pia kwa upande wa Zambia lakini mali zilizouzwa ni zile za upande wa Tanzania peke yake! Kwa hiyo, napenda Waziri leo hii anieleze kwa niaba ya wafanyakazi na Bunge lako Tukufu, mchakato uliotumika na walitumia vigezo vipi kuamua mali za Tanzania pekee ziuzwe na si za Zambia au vinginevyo? Napenda pia kufahamu endapo kuna Tume maalum ambayo imeundwa kuweza kuchunguza Mchakato huo kwani ulikuwa hauna haki hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni masuala ya matibabu. Katika Shirika la *TAZARA* kumekuwa na ubaguzi mkubwa baina ya matibabu yanayotolewa kwa wafanyakazi wa Kizambia na wafanyakazi wa Kitanzania. Wafanyakazi wa Kizambia, wamekuwa wakipata huduma ya afya ya daraja la juu, wamekuwa wakitibiwa katika Hospitali ya Agakhan na Ebrahim Hajj. Wafanyakazi wa Kitanzania, walikuwa wakitibiwa katika Hospitali ya *Ocean Road* lakini hata huduma hiyo ya *Ocean Road* na yenyewe imesitishwa kwani Shirika linadaiwa shilingi milioni 30, jambo

linalosababisha wafanyakazi wa Kitanzania kutibiwa katika zahanati mbalimbali zilizoko katika Stesheni za *TAZARA* ambazo hazikidhi mahitaji. Napenda Waziri leo hii atueleze ni lini deni la *Ocean Road* litalipwa na ni lini ubaguzi huu wa dhahiri utaondolewa baina ya wafanyakazi hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kulizungumzia kuhusiana na *TAZARA,* ni tatizo la kutokuwasilishwa kwa michango ya pensheni kwa Mashirika yetu ya Hifadhi ya Jamii. Kwa kipindi cha miaka 10 hadi kufikia mwaka 2004 kumekuwa na tabia ambayo imejijenga, michango ya pensheni ilikuwa haipelekwi katika Mashirika ya Hifadhi ya Jamii! Jambo hili limewasababishia wastaafu usumbufu mkubwa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja hii, mpaka nitakapopata maelezo ya kuridhisha. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, utaratibu unasema Kiongozi aliyeko Mezani akishasimama, Mbunge yeyote atakaa kwanza chini.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niseme kwamba, nimepokea hapa malalamiko kwamba kuna wachangiaji wamechangia mara tatu na mambo mengimengi hapa! Naomba niendelee kuwaambia, orodha iliyopangwa, imepangwa kiutaratibu. Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, anayo heshima ya pekee hapa ndani na ndio maana anaposimama wakati wa maswali ya nyongeza, lazima apewe nafasi hiyo. Sasa Mheshimiwa Kafulila umenipiga hapa swali na ukasema unajiandaa kunipiga Mwongozo, basi naomba tu nitoe hiyo taarifa mapema. *(Makofi)*

Vilevile, orodha hii kadri ilivyopangwa, inategemea pia maamuzi ya Kiti. Kwa mujibu wa Kanuni, Waheshimiwa Wabunge naendelea kuwakumbusha, Kanuni ya 60(7), inampa Mheshimiwa Spika mamlaka ya kuwapanga wachangiaji kwa mujibu wa yeye atakavyoona inafaa, kwa jinsia, kwa uelewa wa mambo haya na mambo mengine. Kwa hiyo, naomba sana Waheshimiwa Wabunge, muelewe Mwongozaji wa Kiti, anakuwa na mamlaka gani.

Niseme sasa watakaochangia mchana tutakaporudi, wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Salvatory Machemli, atafuatiwa na Raya Khamisi, atafuatiwa na Deo Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Zambi. Orodha itaendelea kufuatwa, ni utaratibu wa kawaida ndani ya Mabunge yote kwa hiyo, naomba muuheshimu.

Tangazo nililonalo hapa, linawaomba Waheshimiwa Wabunge, wajiandae kwa mechi nzito sana tarehe 6/8/2011 Jumamosi. Mechi ya mpira wa miguu na wa mikono kati ya *Bunge Sports Club* na Timu ya *British Council.* Lengo la mchezo huu ni kukuza michezo baina ya watu wa jinsia zote na umri wote wakiwemo walemavu. Kwa hiyo, mechi hiyo itakuwa ni kali sana, Mheshimiwa Idd Azzan, ameniomba niitangaze na ameiomba Timu ya Bunge kwa kushirikiana na Wabunge wote, wajiandae katika kuhakikisha mechi hiyo inakuwa na ushindi mkubwa.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni. Naomba mnisamehe, tumebadilisha Kanuni, mpaka saa 10.00 jioni.

*(Saa 7.15 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 10.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Sylvester M. Mabumba) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyotangaziwa, majadiliano yanaendelea, tutaanza na Mheshimiwa Salvatory Machemli, Mheshimiwa Raya Khamis, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Deo Sanga ajiandae, sasa tutaanza na Mheshimiwa Salvatory Machemli.

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi hii adimu kwa mara nyingine tena nimesimama sijui mara ya tatu, sijui ya tano, sijui ya kumi, lengo hasa ni kufikisha ujumbe kwa Watanzania na ujumbe kwa wapigakura wa Jimbo la Ukerewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja iliyoko mbele yetu ni Wizara ya Uchukuzi, Wizara mfu, Wizara ambayo imepoteza uhai wake, tunakwenda kusherekea miaka 50 ya Uhuru bila reli, tunakwenda kusherekea miaka 50 bila ndege, tunarudi kwenye enzi za ujima, enzi za punda, Tanzania ya leo hiyo yenye Chama kinachoongoza, kinachojiita Chama sikivu, chama makini, usikivu uko wapi wakati Mashirika ya Umma yanafilisika? Waliyoyafilisi wapo viongozi hawachukui hatua, wamenyamaza kimya kazi yao kuvuana magamba, ni nani kawaambia kwamba nyoka anavuliwa gamba? Nyoka havuliwi gamba anajivua mwenyewe akizeeka. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hatuhitaji mvuane magamba, tunataka muwavue magamba hao wanaokwenda kinyume, wanaofilisi mashirika yetu. Wako wapi akina Mataka walilolifilisi Shirika la Ndege la Tanzania, wako uraiani wanatembea nyie mnakaa mnavuana magamba. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukuambia wazi pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba binafsi siungi mkono hoja, kwa sababu nchi inakwenda kupotea, sisi tunapiga vigelele, tunashangilia tunasema kidumu Chama cha Mapinduzi, kidumu cha lita ngapi hicho? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko kwenye hali ya hatari zaidi, tunataka ndege zetu sasa hivi, ndege zenyewe tuliletewa bure, mtu anakupa kitu bure unashindwa ku-*maintain,* hatuna ndege hata moja. Waliofilisi ndege hizo wapo, tunawajua akina Mataka na wenzake, ni nani atachukua hatua? Si Waziri Mkuu, si Rais wa nchi, tunajenga hoja moja tu ya kuvuana magamba ili kuficha maovu yaendelee, watu waendelee kutanua na nchi hii, waendelee kujenga masinagogi Ulaya wakati Watanzania wanarudi kwenye enzi za ujima, enzi za kusafiri na punda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipokuwa makini hata vile tulivyobaki navyo, navyo vitakwenda. Hapa ni kutaka kusisitiza u-*serious*, kwamba tuwe *serious,* viongozi wetu wawe makini. Wanapokuwa wanaongea kitu wakimaanishe kwa maslahi ya umma. Kama Shirika la Ndege limeshindwa basi wabinafsishieni hata TANAPA, wanao uwezo wa kununua ndege na kuziendesha, haya mabilioni waliyonayo TANAPA wanayapeleka wapi, wanayafanyia nini kama siyo watu kubadilisha ma-*VX* na ma-*V8*? Ushauri wangu tuwape TANAPA sasa kama ni hivyo wanunue ndege, waendeshe Shirika la Ndege Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nalia na reli, wakati mimi nafika mara ya kwanza kabisa Dar es Salaam nimekuja na reli, nimepanda treni, maarufu kama kajamba nani, tumebanana humo ndani sikuwa na uwezo wa kupanda basi wala ndege. Nayo haipo leo, kazi yetu sisi tukiona mtu mweupe tu tunajua anaweza, basi wapeni hata Zeruzeru wa Tanzania wenye uwezo si nao ni weupe? Kuliko kuja kutokea tukio lililokuja kutokea la kuwapa wale wa Shirika la *TRL,* wamekuja na *briefcase*, wamekuta reli zetu ziko kamili, wamekuta mabehewa yapo, karakana zipo leo karakana mpaka zile za Morogoro zimekufa, mabehewa yakiharibika wanakwenda kutengenezea Ulaya, hawa wafanyakazi walioko kwenye karakana ile wanafanya kazi gani na wanalipwa mshahara? Leo Mheshimiwa Nundu na Wizara yake wanatuomba sisi tuidhinishe fungu la kulipa watu ambao hawana kazi.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu kumpa taarifa rafiki yangu na pengine kwa uungwana wake anaweza akaondoa hiyo kauli kwamba hawa wenzetu Wenye Ulemavu wa Ngozi hawaitwi Zeruzeru. Kwa hiyo, nakuomba tu Mheshimiwa Mbunge kama inawezekana kwa uungwana wako uondoe hilo neno Zeruzeru uwaite Wenye Ulemavu wa Ngozi.

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeondoa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, tuendelee.

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo lilikuwa ni kufikisha ujumbe kwamba tusiangalie watu weupe kutoka nje hata kama hawana uwezo tukawapa kumiliki rasilimali zetu, kumiliki mali zetu, kumiliki Mashirika yetu ya Umma. Nilikuwa naamanisha hii kampuni ya *TRL*, iliyokuja ikabinafsishiwa Shirika letu la Reli, matokeo yake kumbe ni weupe lakini hawana kitu yaani siyo weupe wa ngozi ni weupe hata kichwani, hawana uwezo wa kuliendesha, leo limekufa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa Serikali kwa juhudi itenge fungu itakapoona na kuna sehemu hapa mimi nitawaelekeza wapi mtachukua pesa, kwa sababu kila siku mnalalamika hamna hela, mimi nilishaziona ziko hapa, ili tuweze kutengeneza reli yetu, mtuwezeshe hata sisi watu tunaotoka Kanda ya Ziwa kule, wanaotoka Kigoma, waweze kusafiri wale ambao hawana uwezo wa kupanda basi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo inasababisha hata barabara zetu zinakufa. Jana Mheshimiwa Magufuli ameomba matrilioni ya hela hapa ya kutengeneza barabara, hata tutengeneze barabara ya chuma acha ya lami, itakufa kwa sababu ile mizigo iliyokuwa inabebwa na reli imehamia kwenye barabara. Sasa tuta-*maintain* vipi barabara ambayo ina mzigo mzito inaouzidi uwezo, bila kurekebisha reli? Hatuwezi hata kutengeneza barabara za kutokea Burundi kwenda wapi sijui anazozitaja Mheshimiwa Magufuli hazitadumu, tunazitengeneza baada ya mwaka mmoja zitaharibika. Tunachotakiwa sasa hivi hapa ni kutengeneza reli, imaarike ili mizigo ile mikubwa iliyokuwa inasafirishwa na reli irudi kwenye reli na hii mepesimepesi isafiri kwenye barabara zetu*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kutounga mkono hoja kulingana na tatizo kubwa zaidi lililoko kwenye Jimbo langu, usafiri wa majini. Nimewahi kuuliza swali la msingi hapa nikajibiwa kwamba wanafanya sijui ukadiriaji, sijui tathmini inafanyika kwa Shirika la Canada kuleta meli mpya. Leo wananchi wa Jimbo la Ukerewe wameweka maisha rehani, wameweka maisha mkononi, kwa sababu ya kukosa usafiri. Tuna meli ya zamani ya enzi za mkoloni, meli MV-Craliasi inakwenda ikifika katikati ya Ziwa inazimika. Ile zahama, iliyotukuta kwa MV-Bukoba, inakwenda kutukuta kwenye MV-Craliasi. Nimemuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba niambie kuhusu hatma ya Craliasi, ananiambia oooh, wameshaifanyia ukarabati, ukarabati gani ule inavuja mpaka ndani, watu wanatoa maji utadhani wanatoa maji kwenye mtumbwi, zitafutwe juhudi za makusudi. Kwa hiyo, naomba Waziri wakati wa majumuisho utuambie hatma ya usafiri wa meli katika Jimbo la Ukerewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la UDA, hapa sasa ndiyo kuna ngoma nzito. Mimi ni mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, tumeletewa *agenda* ya kuuzwa kwa Shirika la Usafirishaji Dar es Salaam (UDA), limeuzwa kwa Kampuni ya Simon *Group*, tena kwa utapeli. Utapeli ulitokeza pale mtu binafsi Mwenyekiti sijui na Katibu wa Bodi ya UDA, wanamwandikia Simon *Group* barua ya kutumbukiza pesa kama *advance* ya kununulia Shirika lile kwenye akaunti ya mtu binafsi. Simon naye sijui kwa kutoelewa, sijui alikuwa anaelewa mchezo unaoendelea anaambiwa atumbukize milioni 400 kwenye akaunti ya kina Idd Simba, akatumbukiza milioni 320 jamaa wakazimeza. Sasa ana-*lobby* Kamati, anakuja anatuambia sisi tuokoe jahazi, tukafikiria, tukamwona hivi kweli huu wizi alikuwa hujui? Akaunti ya mtu binafsi! Ooh, niliambiwa akaunti ya UDA ina madeni, kwa hiyo, nikiweka kule hela zitapotea, kwa hiyo, hizi zake ndiyo zimeokoka? Hatujui hatma yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukaunda Kamati ndogo ya Kuchunguza Sakata la Uuzaji wa UDA, UDA ilikuwa na wanahisa wawili, Hazina na Manispaa ya Mji wa Dar es Salaam. Katika hili, mmoja anatambua uuzaji mwingine hatambui uuzaji. *CHC* wanakuja na Wakala wa Usimamizi wa Mali ya Serikali wanasema hatukujua walivyouziana, hivi kweli wako makini? Wanauza Shirika la Umma hamjui, *CHC* mnafanya kazi, jivueni gamba na ninyi, huu ni uhuni, huku ni kuchezea mali ya Watanzania, hatuwezi kufika kwa stahili hii. Tukienda kwa stahili hii hatufiki, nchi inafilisika watu wanaangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukaunda Kamati Ndogo ya Kuchunguza Sakata la UDA na cha kusikitisha zaidi naomba nikiseme wazi mbele ya Bunge lako Tukufu, tukaweka wajumbe wa

kwenda kuchukunguza sakata la UDA, kumbe kesi ya nyani tunampelekea ngedere. Tukamweka Mheshimiwa Kapuya mle ndani ya Kamati, Mheshimiwa Kapuya, ameshindwa ku-*declare interest* kwamba yeye ni mwanahisa wa *Simon Group* na Mheshimiwa Juma Othman Kapuya anamiliki hisa 10,000 kwenye kampuni hiyo, halafu huyohuyo ndiye tuliyemtuma kwenda kuchunguza wizi wa Kampuni ya *Simon Group* kununua UDA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Bunge hili tunaomba vunja Kamati hiyo, siyo halali, ni wizi mtupu na Mheshimiwa Kapuya, alitakiwa a-*declare interest* kwamba alikuwa anatudanganya na ni wizi ndani ya wizi mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaja mwanzoni kwamba reli inakufa wakati watu wanaiangalia na Serikali haisemi kitu chochote kazi yao kuomba Miongozo tu hapa, pesa zipo nyingi. Wakati mimi nawasilisha hotuba yangu kwa Wizara ya Ujenzi, nilihoji kiasi cha pesa shilingi bilioni 348 ambazo hazikuonyeshwa zinafanya kazi gani kwenye Wizara ile. Mheshimiwa Magufuli jana wakati anafanya majumuisho hakutaja, amemeza tu japokuwa aliona ni chungu lakini akameza kama *chloroquine*, nataka sasa hizi shilingi bilioni 348 ambazo zimeonyeshwa kwenye *vote* 4168 ambazo matumizi yake hazikuonyeshwa basi wapelekewe reli ili tuimarishe reli, tuweze kuokoa barabara zetu kuliko kuziacha tu, jamaa wanatia mfukoni, wanachukua wanaweka waa, kama ilivyo kawaida yenu Chama cha Mapinduzi, mnakwenda kujenga masinagogi Ulaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba pesa hizi sasa zitolewe kwenye Wizara ya Ujenzi…

**T A A R I F A**

**MWENYEKITI:** Taarifa!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Mheshimiwa Mbunge asiendelee kupotosha na kujenga mahekalu hewani, nilitaka kumueleza kwamba hizo pesa zilizopitishwa hapa jana ni za Mfuko Maalum ambao unaisaidia Serikali pale ambapo mfadhili wa nje kwa mfano, anaamua kufadhili ujenzi wa barabara fulani na anasema Serikali ichangie *ten* bilioni, utaitoa wapi kama wewe huna Mfuko Maalum? Serikali ikaona *logic* ya kuweka Mfuko Maalum ili isitulazimu tena kuitisha Bunge kupitisha pesa hizo, sasa zianze kuleta maneno, kutufanya wote ni wahuni kama yeye na hii siyo vizuri kusema kwamba tutapeleka hizo pesa wapi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa taarifa yako. Mheshimiwa Salvatory taarifa umepewa, naomba uzingatie kutokana na ukweli ambao Mheshimiwa Naibu Waziri ametuelezea, naomba uendelee.

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naendelea, lakini kwanza afute kauli ya kuniita mhuni, mimi ni Mheshimiwa kama yeye hawezi kuniita mhuni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nadhani tunatakiwa tutumie lugha ambayo haiudhi watu, umeanza Mheshimiwa Machemli, neno la uhuni umelitumia mwanzo, halafu ukasema kwamba CCM wana kawaida ya kuchukua na kuweka waaa! Hayo maneno hayatakiwi, naomba pia wewe usahihishe kauli zako, uchangie hoja zako, hoja zako ni nzuri sana lakini usiweke maneno ya vionjo vya ushabiki sana.

*(Hapa kuna Mheshimiwa Mbunge alikuwa anaongea bila ruhusa)*

**MWENYEKITI:** Tafadhali na wewe unayeongea bila ruhusa yangu naweza nikakutoa nje, naomba mfuate utaratibu, haya endelea Mheshimiwa Salvatory. *(Makofi)*

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashukuru, kama Kiti kinakuruhusu kunitoa, unaweza kunitoa lakini sijavunja Kanuni. Nilichosema ni kwamba mwenzangu ameniita muhuni, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa usinijibu mie, sijakuambia wewe nitakutoa nje, nimemwambia anayeongea bila idhini ya Kiti, wewe endelea changia vizuri ahsante.

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijamwita Mheshimiwa Mbunge mhuni ila kauli yake ni ya kihuni, huwezi ukatamka kwamba pesa fulani zinachukuliwa na wengine wakati zimepitishwa na Bunge hili Tukufu hapahapa, ndiyo hicho tu, sikumsema yeye mhuni ila kauli yake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ukae. Naomba Waheshimiwa Wabunge msijibishane, tuna hoja muhimu sana mbele yetu, nimewaomba wote mjizuie kwa maneno ambayo hayaruhusiwi kutokana na Kanuni zetu. Tutumie maneno ambayo ni ya kiugwana, tuna hoja muhimu mbele yetu, sasa naomba hizo pointi zetu tuziweke vizuri, tuchangie kwa manufaa ya Watanzania kusaidia Wizara hii, Mheshimiwa Machemli naomba uendelee.

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kutuweka sawa. Lengo zaidi nililokuwa nimesimamia hapa kulizungumzia ni kwamba Bunge halikuelezwa matumizi halisi ya zile pesa? Wala sikujibiwa hoja yangu kuhusiana na pesa hizi shilingi bilioni 348, nahoji tena je, zisipotumika zitakwenda wapi kama hazitaishia mikononi mwa watu? Ndiyo ilikuwa hoja yangu ya msingi kwamba tunapoteza pesa kwa mazingira fulani ambayo watu wakihoji tunanyosheana vidole, mimi nazihoji kwa mara nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uuzaji wa Shirika la UDA, kuna nyumba nyingi na viwanja vya mali ya UDA ambavyo vimeuzwa kinyemela. Nashangaa, ndiyo maana nasema kwamba Serikali haitilii maanani vitu hivi, huyo Mkurugenzi mpaka leo yuko huru anaendelea kutanua tu wakati mali za UDA zimeteketea na nyumba ameuza. Kachukua hati ya kiwanja kampa Mhindi kwenda kuchukulia pesa benki, mali ya Serikali! Tusiposema hapa Bungeni tukasemee wapi? Tukisemea nje yatakuwa ni majungu lakini hii ndiyo sehemu ya kusemea, tuokoeni UDA na UDA ndiyo *solution* kwa usafiri wa Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wa Jiji la Dar es Salaam ukiwemo Mzee wa TMK msiunge mkono hoja hii na Waheshimiwa Wabunge wenzangu naendelea kuwashashiwi tusiunge mkono hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri ya kuomba aidhinishiwe mapesa mengi ambayo anakwenda kulipa mishahara hewa. Unakwenda kulipa watu wa Shirika la Ndege, hivi wana ndege gani? Wao kazi yao ni kuingia ofisini na kusoma magazeti halafu tuwalipe mishahara? Haiwezekani! Kama wameshindwa basi wachukue jembe wakalime mashamba yapo mengi tu Morogoro pale kuliko kuwa tunalipa mtu mshahara ambao hatujui tunamlipa nani na kwa manufaa ya nani?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, muda umekwisha.

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naomba sasa kumwita Mheshimiwa Kabwe Zitto kwa niaba ya Mheshimiwa Raya wamebadilisha, karibu!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimekubaliana na Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis kwa sababu hajisikii vizuri na ana udhuru kwamba nafasi yangu ya kesho atazungumza yeye na mimi nichukue nafasi ya kuzungumza leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru kwa kukubaliana na mabadiliko haya na kunipa fursa ya kuchangia hotuba ya Wizara hii yaani bajeti ya Wizara ya Uchukuzi. Ni Wizara nyeti sana kama jinsi ambavyo Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu amezungumza na Msemaji Mkuu wa Upinzani na Wabunge wengine wote ambao wamezungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi kabla sijaja hapa Bungeni, nilipata fursa ya kukutana na Viongozi Wakuu wawili wastaafu yaani Mheshimiwa Dkt. Salim Ahmed Salim na Mheshimiwa Mzee Joseph Sinde Warioba. Waliniomba nikutane nao kwa sababu ya jinsi wanavyoona tunavyokwenda na mwenendo wa Bunge lakini hili ni kwa pande zote kwa maana ya Wabunge wa Kambi ya Chama Tawala na Kambi ya Upinzani pamoja na Meza Kuu ambao wanaongoza vikao vya Bunge. Ujumbe walionipa ni kwamba tuna kazi ya kuendesha nchi, kwa hiyo, tujikite katika kuhakikisha kwamba tunawasemea wananchi, tuna nchi ya kuongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa pamoja na ndiyo maana nimeona nitumie fursa hii kuweza kutoa ujumbe huu wa Wazee hawa kwamba tuwe makini sana kwa kufahamu kwamba tuna nchi ya kuongoza. Inawezekana kabisa tukawa tunafurahi kutumia jukwaa hili la Bunge kwa ajili ya kujaribu ku-*score some political points* lakini *a day* inayopita kurushiana vijembe ni *a day* inayopita kuendesha nchi yetu. Kwa hiyo, ni vizuri sana wote kwa pamoja, haiwezekani kuacha kufanya siasa ndani ya Bunge ni lazima tufanye, lakini *overriding goal* iwe ni kuendesha nchi yetu kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ndiyo ujumbe ambao wazee wamenipa, inawezekana ikawa siupendi mimi mwenyewe lakini wameniomba niuseme na nimeufikisha na ninadhani huko Mzee Joseph S. Warioba na Dkt. Salim Ahmed Salim watakuwa wanafurahi kwamba kijana wao ameweza kuufikisha ujumbe waliompa kwa niaba ya Wabunge na wamesisitiza Wabunge vijana. Kwa hiyo, nadhani vijana Wabunge wote wamesikia na nimewaomba wafanye utaratibu wa kukutana na Wabunge wote vijana waweze kuwapa huo uzoefu na kadhalika ili wapate fursa pia ya kuweza kujua nchi hii inakwenda namna gani. Nadhani wamekubali na wataweza kukutana na Wabunge wa Kambi zote mbili siyo Wabunge wa CHADEMA peke yake au CCM peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna bajeti ya Wizara ya Uchukuzi ambayo ni pungufu sana na napenda nichukue fursa hii kuwapongeza Wabunge wenzangu wawili wa Kigoma, yaani Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba na Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalumu kutoka Kigoma. Kwa niaba ya Kambi na kwa niaba ya Kamati, waliweza kutoa maoni ambayo yamedhihirisha kabisa kwamba iwapo Bunge hili litaidhinisha makadirio haya ya Wizara ya Uchukuzi, hatutakuwa tumefanya jambo lolote la maana kwa sababu hakuna jambo lolote jipya ambalo limo ndani ya bajeti ya Wizara hii. Inawezekana tukamshughulikia sana Waziri lakini hapa nina barua ya Waziri ya tarehe 27 Aprili, 2011, amemwandikia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ajili ya kuonyesha *concern* zake za udogo wa bajeti ya Wizara yake. Pia akawa ameomba kwamba kutokana na udogo wa *ceiling,* naiomba Ofisi yake iingilie kati suala hili kwa kutafuta njia ya kutenga fedha kwa ajili ya Sekta ya Reli ambayo miradi yake mingi haitakuwepo kwenye bajeti zilizopita kutokana na *TRL* kuwa chini ya *Management* ya *RITES*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini maombi haya ambayo Waziri aliyapeleka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu hayajafanyiwa kazi yoyote ile na leo tumeletewa bajeti ambayo haiwezi kabisa kutatua tatizo la reli, haiwezi kabisa kutatua tatizo la usafiri wa anga na hasa *ATCL* na wala haiwezi kusaidia katika kuendeleza nchi yetu. Nafikiri na nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Tizeba aliyeanza, baadaye Mheshimiwa Mbowe na Wabunge wengine wote kwamba ni vema tufanye *retreat*, tuombe Serikali ikakae, iangalie upya namna gani ya kuweza kusaidia Wizara hii iweze kupata bajeti ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 43 wa hotuba ya Waziri amezungumzia suala la reli na kama nilivyosema na kama wazungumzaji wote walivyosema kwamba kimsingi hakuna jipya ambalo linafanywa. Kwa mfano, Waziri anasema kwamba Serikali imezungumza na Benki ya Dunia na nafahamu hili limekuja baada ya mara ya kwanza Kamati ya Miundombinu kuikataa bajeti baadaye wakasema kwamba Benki ya Dunia wanakuja watatupatia pesa lakini wanasema taratibu za kumpata Mtaalamu Mwelekezi wa kufanya utafiti kuhusu mahitaji ya Reli ya Kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii bado tunafanya utafiti kuhusu mahitaji ya Reli ya Kati? Kweli tunahitaji Benki ya Dunia ije kutupa fedha tumtafute Mtaalamu Mwelekezi, tumlipe atuambie mahitaji ya Reli ya Kati? Hii ni aibu kabisa na ni jambo ambalo wala haliingii akilini. Haiwezekani

kwa sababu mahitaji ya Reli ya Kati yanafahamika toka alipojenga Mjerumani mwaka 1905, leo hatuwezi kukaa kutafuta fedha eti kumtafuta Mtaalamu Mwelekezi wa Benki ya Dunia lakini tunajua miradi ya Benki ya Dunia. Hata kama kungekuwa na nia njema kabisa na kwamba Benki ya Dunia inakuja itatuwekezea kwenye Reli, Benki ya Dunia tunajua na ninyi Wabunge ni mashahidi wa miradi ya haraka ya maji kwenye Wilaya zetu jinsi ambayo inachukua miaka na miaka kupata *no objection* kutoka Benki ya Dunia. Hakuna mradi wowote mkubwa wa *infrastructure* toka Benki ya Dunia ambao umefanikiwa kwa kiasi kikubwa na inachukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Kigoma, ile *Airport* ya Kigoma tumeanza kuitafutia fedha kutoka Benki ya Dunia toka mwaka 2006 mpaka sasa hazijaingia na kila mwaka kwenye bajeti tunaziweka, leo tunaambiwa kwamba Reli ya Kati nayo Benki ya Dunia. Hii ilikuwa ni *statement* ya kuwapashapasha kidogo na kuwalainisha watu wa Kamati ya Miundombinu ili waweze *at Committee level* kuweza kuipitisha bajeti na leo Mwenyekiti amekuja hotuba yake mwanzo mpaka mwisho ni matatizo tu lakini mwisho anasema kwamba tumekubali fedha hii ipitishwe, kwa ajili ya kufanyia nini?

Waheshimiwa Wabunge, nawaomba na naomba nitoe rai kwamba katika jambo hili tuachane kabisa na *political ideologies,* kabisa! Tusimamie nchi yetu, haiwezekani tukaruhusu bajeti ndogo kiasi hiki. Ni lazima tuwape fursa Serikali waende wakakae, wafikirie upya, waangalie vyanzo vingine, wajue wapi kwa kukopa, wapi pa kukata, wapi pa kuongeza lakini tupate fedha kwa ajili ya bajeti ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani amezungumzia vizuri sana suala la *ATCL* na kila Mtanzania anaelewa tatizo tulilonalo na *ATCL*. Leo hii Tabora hakuna ndege, ukitaka kwenda Kigoma inabidi upite Mwanza ndiyo uende Kigoma kisha upande ndege ndogo za *ORIC Air* na *return ticket* kwenda Kigoma sasa hivi ni shilingi milioni moja, *one million*. Mkisema mpitishe bajeti hii kama jinsi ilivyo maana yake ni kwamba mnatuonea sisi watu wa Kigoma na Tabora, hamtuonei huruma Watanzania wenzenu lakini mkikataa kupitisha bajeti hii ili Serikali iende ikakae ifikirie upya, ipate fedha za *ATCL*, kwa kufanya hivyo mnawaunga mkono na mnawafuta machozi Watanzania wenzenu wa Kigoma na Tabora. Nawaomba mtufute machozi kwa kuikataa bajeti hii ili Serikali iende ikakae, iweze kuangalia ni namna gani tutakavyoweza kupata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ATCL* wanahitaji fedha, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu ametoa mfano wa *Kenya Airways* hapa namna ambavyo *share capital* ya *Kenya Airways* ilivyo yaani *Institutional Investors* na kadhalika. Katika mapaendekezo yetu ya Bajeti Kivuli tulielekeza kwamba kuna watu ambao wanafaidika moja kwa moja na utalii yaani TANAPA na Ngorongoro wapeni *up to 60%* ya *shares* waingize *capital* ili tupate fedha za kuanzia lakini baada ya miaka mitatu wakifanya vizuri tutangaze *IPO.* Ethiopia, Wazungu wamemnyima Meles Zenawi pesa za kutengeneza *Hydro Power Station,* anatengeneza *Hydro Power Station* kubwa sana lakini Wazungu wamemkatalia kwa mambo ya mazingira na kadhalika lakini yeye ameamua kuitisha *a National Bond, an Infrastructure bond* ambayo kila Mu-ethiopia ananunua, wamepata fedha mara mbili ya walizokuwa wanazitafuta kwa ajili ya kufungua *Hydro Station*. Washirikisheni Watanzania wawe sehemu ya *ownership* ya hiki kitu, 60% ya fedha zinazotokana na utalii zinabakia kwenye nchi kama nchi hiyo ina *National Carrier*, ndiyo maana Kenya wanafaidika na utalii. Sisi kwa maana hiyo ni kwamba tunabakia na *only a third* ya fedha ambazo zinatokana na utalii. Kwa hiyo, naomba na Waheshimiwa Wabunge na ninawa-*convince* suala hili tuweze kwenda nalo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bandari. Kuna *improvement* ambazo zimetokea kwenye bandari. Kiwango cha meli kukaa majini kimepungua sana na tunawashukuru sana kwa hilo na nawapongeza sana watu wa Mamlaka ya Bandari. Tuna *develop base 13 & 14,* tumeamua kwenda China kuomba mkopo, sina tatizo hata kidogo na mikopo kutoka China lakini naomba nitoe ushauri tu *as an Economist*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo mingi ya China gharama yake ni kubwa sana. Sasa hivi kwa sababu ya matatizo ya madeni ya Marekani, Wachina wanakimbilia nchi za Afrika, lakini

wanatupa mikopo kwa gharama kubwa sana. Kwa mfano, gharama halisi za kutengeneza *base 13&14* katika Bandari ya Dar es Salaam hazizidi dola milioni 340, mkopo ambao Wachina wanataka kutupa ni wa dola milioni 525, lakini kuna *the easiest way* ya kwenda kutangaza *International Tender through PPP,* watu wa-*bid* waje watengeneze, wa-*own* na baadaye wa-*transfers* kwa Mamlaka ya Bandari, *that is the easiest way* wala nchi haiingii kwenye mikopo. Kwa hiyo, naomba muangalie hizo *options*, mikopo ya China, msiende tu kukopa ni ghali sana kwa sababu inaendana na *conditionality* kwamba tunakupa mkopo lakini *Contractor* atoke China maana yake ni kwamba hela yote inarudi China. *So you have to be very careful* katika maamuzi haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la UDA. Waheshimiwa Wabunge wamelizungumza sana na ukiangalia unakuta watu wamezungumza na taarifa zipo tofautitofauti. Nataka niseme jambo moja kwamba mwaka 1997 UDA ilikuwa *listed specified* kama Shirika linakwenda kubinafsishwa. Ilitolewa *Government Notice* mpaka leo tunavyozungumza *Government Notice* hiyo haijawahi kufutwa. UDA bado ni *specified corporation* na kuna watu wanadhani kwamba hisa za UDA zilizokuwa *specified* ni zile 49% ya Serikali peke yake, *no,* Shirika zima la UDA lilikuwa *specified*. Maamuzi yoyote ya ku-*privatise* UDA yalipaswa kuwa *approved* na *Consolidated Holdings*, kama kuna mtu yeyote ambaye amenunua hisa za UDA hakuna *approval* ya *Consolidated Holdings* ameingia choo cha kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmetugawia mamlaka, ndani ya Bunge, kuna Kamati za Bunge. Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma kwa mujibu wa Kanuni za Bunge ndiyo mmeipa majukumu ya kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Ubinafsishaji na mimi ndiye Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Alianza kunipa fursa hiyo Mzee Samuel J. Sitta na baadaye Mama Anne S. Makinda akaendeleza na nadhani nitamaliza miaka mitano hii kama Mwenyekiti wa Kamati ya Mashirika ya Umma na kwa niaba ya Wajumbe wangu wote *as far as we are concerned, UDA* haijawa *privatised* kwa sababu taratibu za kisheria hazijafuatwa. Sheria ya *Public Corporations Act, 1992* na ya *Consolidated Holdings* hazijafuatwa na hapa ndiyo matatizo ambayo Mheshimiwa Mbunge mmoja amezungumza ya Ofisi ya *TR*. Tunawaambia kila siku na tunalalamika, jamani hisa za Serikali ambazo tuna chini ya 51% zinaendeshwa vibaya kwa sababu Ofisi ya *TR* haina nguvu ya kuweza kuzifuatilia, ndiyo mambo ambayo yametokea kwenye *TR*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Eng. Salvatory Naluyaga Machemli amezungumzia kwamba ni mambo ya *CHC*, siyo mambo ya *CHC*, hili ni suala la ofisi ya *TR* na kwa muda mrefu imekaa bila kuteua Wajumbe wa Bodi ya UDA. Wajumbe wa Bodi ya UDA waliokuwa wanafanya kazi ni wale walioteuliwa na Halmashauri ya Jiji peke yake. Wamekwenda wanauza wanasema eti wanauza *unallotted shares.* Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali atanisaidia, *unallotted shares* ni sehemu ya *ownership* ya *shareholders* na siyo mali ya Board *Members. So it is wrong* kuuza *unallotted shares.* Maana yake ni nini? Jiji inamiliki 51%, Serikali…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, naomba kumwita sasa Mheshimiwa Deo Sanga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa namna ambavyo inafanya kazi nzuri za aina mbalimbali. Niishukuru kazi ya jana ya miundombinu, kwa kweli fedha tulizopitisha jana tumeanza vizuri kwa miundombinu ya barabara, kwa namna ambavyo tumeanza sasa tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niingie kuchangia upande wa ndege, Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia na mimi naomba nichangie pia. Ndege zetu kwanza zina nembo nzuri kama walivyosema wenzangu, nembo ya Twiga inapendeza sana lakini Shirika hili linafanya biashara na biashara hii haikui, kwa hiyo ina maana miaka hadi miaka imekuwa ikienda kwa

hasara. Inashangaza sana kwamba biashara yoyote inapoanzishwa ni lazima ikue. Sasa tuombe Wizara muongeze fedha kwa ajili ya kujipanga vizuri ili kuweza kutengeneza ndege hizi ili ziweze kuruka angani kama wenzangu walivyosema. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia juu ya reli. Wenzangu pia wamesema lakini na mimi niseme juu ya reli nayo ilianza vizuri, kuna mdudu gani anayedhoofisha hii biashara, haikuwi, imekuwa ikifilisika tu, tatizo liko wapi? Nadhani pana kadudu mtu pale! Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ijipange vizuri kwani bajeti hii ni ndogo, iongeze hela kwa ajili ya kuimarisha reli. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie juu ya Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA), ingawa wenzangu wengi wamelizungumzia. Nadhani UDA walianza wakiwa na magari kadhaa, hivi tunapofanya biashara ya magari si maana yake tunatarajia yaongezeke mwaka hadi mwaka? Maana ni biashara inafanyika na ni nzuri tu. Sasa leo UDA imefilisika, kuna kadudu mtu pale napo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo? Mimi ni mfanyabiashara, mimi Sanga, *Jah People,* Mtu wa Watu, nilianza na biashara ndogo, nikaja na *semi-trailer* moja, mbili, leo nina *semi-trailer* kila barabara. *Jah People*! Ndiyo biashara! Sasa UDA yenyewe haikui? Hebu tuangalie, tujipange vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu bajeti ya viwanja vya ndege. Pale Njombe tuna uwanja wetu mzuri tu wa ndege, sijaona bajeti juu ya ukarabati. Kuna uwanja wa ndege pale Nduli, sijaona bajeti. Tunaiomba Serikali, kesho mtakapofanya majumuisho, mniambie ni kiasi gani ambacho mtaongeza kwa ajili ya kukarabati viwanja vya Njombe na Iringa ili ndege hizo ambazo mtazitengeneza ziweze kuruka kwenda Njombe na Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna wenzetu wa Ziwa Nyasa sijaona bajeti yoyote ambayo inaonesha aidha kununua boti au kukarabati meli. Tutawapoteza wananchi wa Nyasa wale na Waheshimiwa Wabunge wa kandokando ya Ziwa Nyasa. Leo Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, alikuwa anatuambia hapa kwamba wenzetu kule usiku wa kuamkia leo boti imezama lakini bahati nzuri wote wamesalimika. Tunaomba Serikali itilie mkazo juu ya vyombo vya usafiri katika Ziwa Nyasa ili kuwaokoa wananchi wetu wa Ziwa Nyasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Serikali yetu ni sikivu. Nitakuwa tayari kuunga mkono bajeti hii kama haya yote yaliyozungumza mtaongeza fedha. Nitakuwa tayari kama mtaongeza fedha. Nawaomba na Wabunge wenzangu wote wakiwemo na wa CCM, kama wataongeza fedha basi tuunge mkono bajeti hii. Ndugu zangu, kupanga ni kuchagua, wamesema Kasungura ni kadogo, inawezekana katika kupanga bajeti hii mmeanza vizuri, lakini tuongezewe fedha ili tuweze kupitisha Bajeti hii kama nilivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu ambayo inasimamia Wizara hii imeeleza vizuri sana na mimi nakubaliana nayo kabisa. Kuna jambo ambalo nilitaka niliseme, lakini naomba liishie moyoni mwangu. *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI**: Lipi hilo tena?

**MBUNGE FULANI:** Huo ni unafiki!

**MBUNGE FULANI:** Hamkawii kujinyonga nyie!

**MHE. DEO K. SANGA:** Aah, hatuna tabia ya kujinyonga! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kusema kwamba, haya yote nimekuwa nikisema yatawezekana tu kama sisi sote tutajenga umoja, upendo na mshikamano. Mambo yatakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua dakika zangu bado zimebaki, lakini sipendi kugongewa kengele, naomba tu niishie hapo lakini niiombe sana Wizara hii kwamba, kama nilivyosema ongezeni fedha ili kesho tuweze kupitisha bajeti hii. Tukishakubaliana katika haya tuliyosema, mimi na Waheshimiwa Wabunge wenzangu nadhani tutaunga mkono hoja mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba ya bajeti ya Wizara ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niseme tangu mwanzo ili nisije nikasahau pale mwishoni kwamba siungi mkono bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko sababu nyingi sana za kutounga mkono bajeti hii. Jambo la kwanza ambalo ni bichi kabisa naomba nianze na hili la Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA). Dar es Salaam ni yetu wote. Wabunge wote tunakaa Dar es Salaam wakati tuko kwenye Kamati, kwa hiyo, wote ni wana Dar es Salaam na UDA inatunufaisha wote. Naomba niseme kwamba, Serikali iliishatoa maagizo kwamba UDA isiuzwe na iko barua ya Ofisi ya Waziri Mkuu ya tarehe 28 Februari, ambayo ilikuwa inakwenda Jiji ikiagiza kwamba Shirika hili lisiuzwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeweza kusema kwamba ni ukaidi wa viongozi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, kupuuza maelezo ya Serikali. Ni ukaidi wa hali ya juu sana. Nadhani nchi hii kuna Serikali mbili, hamna Serikali moja. Kama Serikali ni moja tunamtaka Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe kauli hapa na mimi kauli ambayo napendekeza kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu na mniunge mkono, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ivunjwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam iliwahi kuvunjwa, hivyo hakutakuwa na kitu cha ajabu sasa Waziri Mkuu kuamua ivunjwe. Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa anajenga heshima kubwa sana ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi kama tukiamua Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ivunjwe. Mimi nasikitika sana kwamba Mstahiki Meya wa jiji la Dar es Salaam, Dkt. Didas Masaburi, yeye *personally* amehusika moja kwa moja katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini watu wazima na mashuhuri sana katika nchi hii, Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya, anahusika moja kwa moja, akijuwa ana hisa mle naye anakubali kuwa kwenye Kamati ya Uchunguzi. Tumeambiwa fedha hizi zimengia kwenye akaunti ya Mheshimiwa Iddi Simba, lakini fedha nyingine zimeingia kwenye akaunti ya Pride Tanzania ambayo Iddi Simba ni Mwenyekiti wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni wizi wa mchana kabisa na tunaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, ili kurudisha imani kwa Watanzania kwanza UDA isiuzwe, lakini pia Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, ivunjwe mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia viko viwanja vingi vya UDA ambavyo vimeuzwa kinyemela. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aagize pia viwanja vyote virejeshwe hata kama itamaanisha Serikali kugharamia urejeshwaji wake. Leo tunapata shida sehemu za kupaki magari Dar es Salaam, vile viwanja vilivyokuwa vinamilikiwa na UDA vingeweza kutumika kwa ajili ya kujenga majengo ambayo yangetumika kama *parking*. Leo barabara zote za Dar es Salaam zimegeuzwa kuwa *parkings* za magari, haiwezekani! Isiwe tu watu wanasema Serikali ya CCM ni sikivu, tunasema sikivu kama wanavyosema wenzetu lakini kumbe hatusikii. Itakuwa ni *contradiction* kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono bajeti hii kwa sababu nyingine inayofuata. Kamati hii ya Miundombinu iliikataa bajeti hii tangu mwanzo lakini kwa mazingira ya ahadi za Serikali, Waziri akasema Serikali imeahidi kwamba wanaweza wakatupa shilingi bilioni 95.6. Hiyo ni ahadi ambayo hatuna hakika nayo, imeandikwa kwenye taarifa ya Kamati. Tunaomba *commitiment* ya Serikali, hizi shilingi bilioni 95.6 ziko wapi? Maana tusiandike tu kwenye vitabu au barua! Leteni

*supplementary* bajeti hapa tujue ni hakika hizi fedha zipo lakini siyo kuandikiana barua kwamba hizi pesa zipo, maana hakuna *commitiment* kwa maana ya kuandika barua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko deni lingine ambalo Kampuni ya *Celtic Capital Corporation* na kampuni ya ndege ya Afrika Kusini inaidai Serikali na hizi ni shilingi bilioni 75.99. Hizi pesa zenyewe ziko wapi? Tuzione ili tujue kabisa kwamba Serikali ina *commitiment* na hapo tunaweza tukazungumza kwamba bajeti hii inakuwa na mwelekeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba ipo Kampuni ya Meli ya Serikali. Kampuni hii iliomba shilingi bilioni 5.4 lakini kwa kushangaza sana Serikali ikatoa shilingi bilioni 1.6 na pesa ambazo zimetolewa na Serikali hizo shilingi bilioni 1.6 ni kwa ajili ya kulipa madeni na bima za meli. Kwa maana nyingine kampuni hii haina fedha yoyote kwa ajili ya kujiendesha katika shughuli nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kampuni hii ndiyo inayoendesha meli za Serikali ambazo Watanzania wengi maskini wanapanda. Kama hatuipi fedha, Watanzania hawa wanaotupigia kura na kutuleta humu ndani hasa walio katika Ukanda wa Maziwa tunataka wafanye nini, watembee wapi na wasafirie nini? Hakuna *seriousness* kwa upande wa Serikali, tunataka Serikali iwe *committed*, ioneshe *seriousness* katika masuala haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la *TAZARA*. Namshukuru sana Mheshimiwa Angellah Kairuki amezungumzia masuala ya reli akagusia na *TAZARA*. Naomba nizungumze kwamba matatizo ya *TAZARA* kimsingi yanatokana na matatizo ya kiuongozi, siyo kitu kingine chochote. Chimbuko la matatizo ya *TAZARA* ni suala la uongozi wa *TAZARA*. Mimi nina *Act* ya *TAZARA*, hii hapa ambayo ni *Act* Na. 4 ya mwaka 1995. *Act* hii ni ya ajabu kidogo, inasema kwamba Mkurugenzi Mkuu (*Managing Director*) wakati wote lazima atoke Zambia. Wakati wote na kwamba Makamu wake (*Deputy Managing Director- DMD*) lazima awe Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niieleze Serikali na hili jambo nimewahi kulizungumza mara kadhaa katika Bunge la Tisa (9) lakini Serikali haijataka kufanyia kazi yale ambayo Wabunge tunapendekeza. Kiongozi wa *TAZARA* kwa mujibu wa *Act* hii anatakiwa ateuliwe na Bodi. Kazi itangazwe na Bodi, afanyiwe usaili na Bodi, lakini hilo halifanyiki. Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya *TAZARA* aliyepo leo, Ndg. Akashambatwa ameletwa na Serikali ya Zambia kinyume na Sheria yenyewe na Bodi ilichofanya ni kwenda kuthibitisha jina lake. Serikali yetu ya Tanzania inakubali. Mkurugenzi huyo wa *TAZARA* ni Mwanasiasa na ametoka kwenye Chama cha Siasa moja kwa moja wakamtupa wewe nenda *TAZARA*. Kinachofanyika leo ndani ya *TAZARA* ameeleza Mheshimiwa Angellah Kairuki, ni mambo ya ajabu, Shirika linaibiwa tunaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkurugenzi Mkuu wa *TAZARA* aliyepita ni Mzambia mwingine anaitwa Mwiya. Amekula dola za Kimarekani milioni kumi (US$ 10mil) na leo yuko mitaani na hakuna hatua iliyochukuliwa. Dola milioni kumi (10), bado tunataka *TAZARA* iendelee kustawi, haiwezekani! Jamani Serikali ichukue madaraka, ifanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hivyo haitoshi Mkurugenzi huyu anaposafiri, yuko na *DMD* wake ambaye ni Mtanzania hata kazi hizo hakabidhi kwa *DMD* wake, kinyume na Sheria ambayo imeanzisha *TAZARA* maana inasema kama *MD* hayupo basi *DMD* wake atafanya kazi hizo. Yeye hafanyi hivyo, anaweza akaamua kumuachia Mkurugenzi au Meneja yeyote ili mradi awe Mzambia na siyo Mtanzania. Tunaambiwa hata anaposafiri akirudi, akikuta maamuzi yamefanywa na *DMD* ambayo hayapendi anayafuta*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mashaka na utendaji wa *TAZARA*, ndiyo sababu nasema matatizo yaliyopo *TAZARA* ni ya kimenejementi na si vinginevyo. Wazambia na Watumishi wa Zambia wamekuwa wanatuibia sana. Ngoja niwaeleze Waheshimiwa Wabunge, wafanyakazi wa Zambia, Tanzania wako wengi sana nadhani wanaweza wakafika hata mia moja (100) lakini kwa upande wa Zambia wafanyakazi Watanzania ambao wako kule hawazidi watano (5). Kuna kitu kinaitwa *inter-territorial allowance* ambayo hulipwa kwa wafanyakazi ambao hufanya kazi katika nchi ambayo siyo ya kwao. *Inter – territorial allowance* inayolipwa ni asilimia hamsini na tano (55%) ya mshahara. Mfanyakazi analipwa mshahara wake kamili na *fifty five percent on top* ya

mshahara wake. Kwa maana nyingine ni kwamba, mshahara ambao ungeweza kulipwa wafanyakazi mia tatu (300) wa Tanzania, unalipwa Wazambia mia mbili (200). Hamna *fairness* katika uendeshaji wa *TAZARA* na ndiyo maana *TAZARA* haiwezi kustawi, itaendelea kubaki ilipo miaka nenda rudi. Naomba Serikali ichukue maamuzi tena ya haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine Mheshimiwa Angellah Kairuki ameyazungumza hapa kwamba wafanyakazi wa *TAZARA* wanalalamika wakati wote lakini jambo lingine ni kwamba wapo wafanyakazi wa *TAZARA* ambao wamestaafu kuanzia mwaka 2005 mpaka leo hawajaweza kulipwa, jamani huruma iko wapi? Serikali ilikubali kubeba mzigo huu kwamba *CAG* wa Tanzania na Zambia wafanye ukaguzi na tathmini ya madeni, waliishafanya lakini sioni kwenye bajeti fedha za kuwalipa wafanyakazi hawa wastaafu waliotumikia *TAZARA* kwa uaminifu, fedha ziko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ichukue hatua na haya ndiyo yanayofanya Wabunge tuikatae bajeti ya Wizara hii kwa sababu haioneshi kama Serikali inawajali Watanzania. Watanzania hawa ndiyo wametuweka madarakani. Leo tunapowanyima haki yao ikiwa ni miaka sita, saba toka wamestaafu tunategemea waishi namna gani? Leo tuko hapa watasema Wabunge hawajali kwa sababu wanalipana *allowances*. Ni kweli tunalipana *allowances,* lakini hawa waliotuingiza humu ndani tunawajali namna gani? Haya hayawezekani, ni lazima Serikali ichukue hatua za dhati kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la mikataba mibovu sana kwa upande wa *TAZARA*. *TAZARA* imeingia mkataba na *Railway Systems of Zambia* (*RSZ*). Mikataba iliyoingiwa kimsingi haina faida kwa *TAZARA* na badala yake inainyonya zaidi *TAZARA*. Mabehewa yanayotumika ni ya *RSZ* na mizigo inayosafiri inasafiri zaidi katika mabehewa ya *RSZ*. Kwa hiyo, Wazambia wanachofanya ni kuhakikisha kwamba wanaikandamiza *TAZARA* kwa upande wa Tanzania kwa kadri inavyowezekana na mizigo yote ya Tanzania haiwekewi punguzo la bei, lakini ile ya Zambia yote inasafirishwa kwa bei ya chini sana. Taarifa nilizonazo ni kwamba huyu *Managing Director* wa Zambia nadhani ana-*plan* kugombea Urais mwaka huu kama Zambia itakwenda kwenye uchaguzi. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile atakuwa anatafuta fedha za uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TAZARA* haiko salama, naomba Serikali ichukue hatua na mimi katika hatua hii Waheshimiwa Wabunge wenzangu, naomba niseme kwamba nataka kuleta Hoja Binafsi humu Bungeni katika Bunge la mwezi wa Kumi na nitaaomba Bunge hili liniunge mkono. Utaratibu unaotumika leo kuendesha *TAZARA* umepitwa na wakati na hauko kwa manufaa ya Tanzania na Zambia hata kidogo. Wakati mwingine unaweza kusema kwa nini Tanzania tusiendeshe kipande chetu cha *TAZARA* na wale waendeshe kipande cha kule? Eeh, maana leo *TAZARA* iko kwa faida ya Wazambia zaidi kuliko faida ya Watanzania, tuzungumze! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipowasemea Watanzania na nchi hii, hakuna atakayesema. Kwenye Biblia imeandikwa kwamba msipomwimbia Mungu hata mawe yatamwimbia. Sasa Serikali msipofanya, basi sisi tuseme, maana Watanzania wametuweka humu ndani ili tuseme. Mimi naomba niseme Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ina dhamana kwa Watanzania. Tunaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na mimi nafurahi uko ndani ya jengo, uchukue hatua Watanzania waone kwamba Serikali inafanya kazi ili tuweze kwenda kufanya kazi na tuwe na amani zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Tanzania Air Corporation Limited* (*ATCL*) naweza nikasema kwamba ni aibu tu, ni aibu sana. Wengi wamesema na wakati ule tumekuwa tunasema waende viongozi wazoefu wa kuendesha Mashirika haya, lakini badala yake Tanzania tumewapeleka viongozi waliostaafu kwingine ndiyo tunawapeleka wana-*manage* Mashirika, tunategemea nini? Maana yake hawa watu wamekula sana huko Serikalini, sasa tunasema nendeni mkapumzike, hivi Tanzania hakuna vijana hata watu wenye umri ambao wanaweza wakafanya kazi kwa ufanisi zaidi. Maana hapa tunakuja tunalia tu, lakini mengine ni makosa ya Serikali ni ya waziwazi kabisa. Unampeleka mtu alikuwa ana-*manage* sijui *NPF, NSSF* hapa unamwambia nenda ka-*manage* Shirika la Ndege wapi na wapi. Haiwezekani! (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unamwondoa mtu huyo huyo katika Shirika la Ndege, nenda sasa ukawe *Consultant* kwenye Shirika lingine katika nchi. Huku amefeli unampeleka kwingine na kwenyewe akafeli vile vile. Haiwezekani. Serikali haioni *seriousness* na mimi najisikia faraja

kuzungumza kama Mbunge wa CCM, maana wapo Watanzania ambao wanafikiri Wabunge wa CCM hawawezi wakazungumza, tuzungumze na tuikosoe Serikali yetu waone. Katika pointi hii naomba niseme naishukuru, naipongeza Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi kwenye vikao vyake imeiagiza Serikali itafakari suala la kupandisha bei ya mafuta ya taa. Nilizungumza hapa ndani Mheshimiwa Waziri Mkuu nikasema bei ya mafuta ya taa ni mzigo kwa Watanzania ambao hawana uwezo wa kujitwisha, sikuweza kusikilizwa lakini Kamati Kuu imeona hilo na naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu mafuta ndio nishati ambayo Watanzania wanaitegemea vijijini naomba kama ilivyoagiza sasa Serikali mlitafakari upya jambo hilo tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuwe na huruma kwa Watanzania hao. Lakini kingine hivi wafanyakazi wale 182 waliopo *ATCL* leo tunapata wapi fedha za kuwalipa kama leo, tuna deni kubwa la sh. 75,000,000,000 ambalo *ATCL* inadaiwa kwa maana hiyo Serikali inadaiwa bado tuna mzigo wa wafanyakazi 182 tunafanya nao nini? Serikali imenyamaza, nini majibu ya Serikali katika hili, watu hawawezi kuelewa. Kwa hiyo, ndiyo nasema ziko sababu nyingi za kuikataa bajeti ya Serikali. Leo Waziri anatwambia kwamba wanaangalia wawekezaji wengine, huko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri nilikuweko katika Bunge la Tisa, nilikuwa kwenye Kamati ya Bunge ya Miundombinu. Tulielezwa hadithi kwamba tunataka kuingia ubia na Shirika moja la China linaitwa *Sonango*l, leo *Sonangol* limeishia wapi leo? Serikali inakuja na hadithi mpya leo. Ndiyo yale ya mama yangu, Mama Hewa, alikuwa anasema leo tuna mchakato, tuna mikakati, tunajipanga vizuri ndio yale yale. Tulijipanga kwa *Sonangol***,** tumetoka sasa tunajipanga kwa watu wengine, tutamaliza lini kujipanga huku. Yote haya yanaonyesha kwamba tulimweleza Waziri wakati huo Mheshimiwa Kawambwa kwamba, hizi hatutaweza na Waziri alituhakikishia kwamba inawezekana kabisa na tumefika mahali leo *Sonangol* tumeachana, tunazungumza mambo mengine leo. Hii haiwezekani kwa Serikali ambayo iko *serious*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nizungumzie *TMA* ambayo hatuonyeshi *seriousness* nyingine, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa, Mama Kijazi amekuwa anakaimu ile nafasi karibu miaka miwili na ni mama, kwa nini msimpe na huyu tatizo ni nini? Huyu mama hawezi kufanya maamuzi sawa sawa akiwa anakaimu miaka yote hiyo. Walishafanya usaili, leo mnasubiri nini Serikali? Yote hii ni kuonyesha *laxity,* hakuna *seriousness.* Kama hamjaridhika naye si mwondoeni. Lakini naamini yule mama ni mchapakazi na naomba niseme, nilifanya *TMA,* nimefanya kazi naye, anafanya kazi vizuri.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele ya kwanza au ya pili?

**MWENYEKITI:** Ya pili. Nakushukuru

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Sasa naomba kumwita Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Augustino Maselle ajiandae, Mheshimiwa Deo Filikunjombe ajiandae.

**MHE. HALIMA J. MDEE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue fursa hii kukushukuru, lakini vile vile naomba nichukue fursa hii kusema kwamba hili suala ni letu sote. Hili suala halichagui chama, halichagui kabila na wala halichagui rangi. Kimsingi nichukue fursa hii kuwapongeza kwa dhati Wabunge wote waliochangia kwa kutokuunga hoja hii mkono kwa sababu na mimi siungi mkono hoja. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge kutoka Mkoa wa Dar es Salaam. Tunapozungumzia Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam nikiwa kama Mbunge wa Jimbo pamoja na Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Dar es Salaam ni Wajumbe. Kwa hiyo, aibu ya *UDA* ni aibu ya Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam wote. Kwa hiyo, ninapozungumza hapa Halima ndivyo ujue anavyozungumza Mheshimiwa Iddi Azzan, ndivyo ujue anavyozungumza Mheshimiwa Zungu na ndivyo ujue anavyozungumza Mheshimiwa Mnyika na wengine wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maamuzi haya ya kubariki ufedhuli huu yalifanywa kwa kuvizia wakati sisi hatupo. Sisi ni Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam kikaitishwa Kikao cha Kamati ya Uongozi kwa tarehe 29 Juni, 2011 na kikaitishwa kingine cha Baraza tarehe 20 Julai, 2011, sisi tuko huku na mbaya zaidi vikao vyote havina akidi. Ndio maana tunasema kwa hili Meya wa Jiji hawezi kukimbia uwajibikaji hapa, watazunguka wee! Meya hawezi kukimbia uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshukuru kwamba hatimaye leo tunazungumza lugha moja. Tarehe 15 Julai, 2011 kama sikosei. Mheshimiwa Mnyika aliuliza swali hapa akai-*task* Serikali kwa Waziri Mkuu, jamani *UDA* kuna uchafu huu na huu umefanyika. Serikali inachukua hatua gani, alijibiwa kisiasa. Alijibiwa kwa sababu tu aliangaliwa Mheshimiwa Mnyika anazungumza hakuangaliwa hoja yake. Sasa matokeo yake leo tunafika *final* maana watu wa *Simons* wapo wanasema waliitwa na Wizara kuja kutoa *inputs* zao kuhusiana na Wizara masuala ya uchukuzi na *UDA*, kwa maana yake wanatambulika na Serikali. Tumefika *final* kama suala la umeme tunajibizana wee, tukiona huku wananchi wame-*react* na sisi tunakwenda na upepo wa kisiasa, hatutaendesha nchi hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo mambo ndio yamefika shingoni, tunategemea Waziri kiujanja ujanja atasema hili sio lake ni la Waziri Mkuu ili hotuba yake ipitishwe, lakini Serikali ni hii moja. Kwa hiyo, tusitarajie mtupe majibu ya kupindapinda, hamtoi majibu ya uhakika kwa *UDA* hakipiti kitu hapa. Hamtoi majibu ya uhakika kwa reli, aibu. Shilingi bilioni sijui 15, sijui 17 *rehabilitation.* Lakini wakati huo huo Mheshimiwa Mwakyembe, Mwalimu wangu hapa wakati anamjibu Mheshimiwa Machemli kuhusiana na sh. 348,000,000,000/= ambazo mmesema kwenye kile kitabu hamjazichambua kuonyesha zinatumika kwa matumizi gani? Majibu ya Mheshimiwa Mwakyembe anasema fedha hizi ni *Special Road Construction Projects* kwa ajili ya kama akitokea mtu anataka kujenga ama *offer* kutoka nje inayotaka Serikali ichangie, hizi ndio fedha zimetengwa mahsusi kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama nilikosea kukupata unaweza ukanirekebisha kwa lugha sahihi. Lakini kama ni fedha ambazo zinasubiri ambazo hata kwenye maandiko yetu ya barabara mbalimbali hazipo lazima tufikirie cha kufanya hapa. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mwongozo wa Spika. Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba utuache kwanza tuendelee baadae nitakukaribisha mwishoni. Mheshimiwa Halima endelea.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Hansard* ipo.

**MWENYEKITI:** Nikukumbushe tu Mheshimiwa Mwakyembe ni Naibu Waziri wa Ujenzi, kwa hiyo, mtaje kwa cheo chake.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba kama Kambi na tunaamini Wabunge wenzetu wanatuunga. Kama hizi sh. 348,000,000,000/=, tafsiri yake ni maelezo aliyoyatoa wakati akitoa taarifa kwa Mheshimiwa Machemli, tuna kila sababu ya kutoa mafungu kwenye hizi fedha kuboresha bajeti ya Wizara hii. Tuna kila sababu. Lazima tuongezee kwenye nishati, tutoe hapa. Kwa sababu hatuwezi kukaa ku-*forecast* vitu ambavyo hatuvijui kama vitakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la *UDA* watu wamewataja watuhumiwa mbalimbali. Kinachonisikitisha na naweza kuwataja kwa majina naogopa kwa sababu nawaheshimu kweli. Kinachonisikitisha ni kwamba kama nchi tumekuwa hatujifunzi kuwapa mamlaka watu ambao sio waaminifu, kwa nini nasema hivyo. Wanaotajwa hapa kipindi kilichopita kwa kashfa hizi hizi ilibidi wajiuzulu. Wanaotajwa hapa ni watu ambao walianzisha Kampuni inayoitwa *NICO,* Watanzania wakakusanyishwa fedha zao, lakini kinachonisikitisha zaidi tunakoelekea tumesikia Kampuni inaitwa *AGRISOL* ambayo inatoka Mkoa wa Rukwa kwa Waziri Mkuu ambayo itapora ardhi ya Watanzania isiyopungua hekta laki mbili, hawa jamaa wamo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujifunzi ule mkataba ambao Halmashauri inapewa shilingi mia tano, mia tano na mia mbili, mia mbili wameingia hapo Serengeti sijui *Consultants* sijui nini, *Advisors,* fedheha! Kwa hiyo, anaonekana *they know how to manipulates,* inaonekana wana *connection within* kwa maana wako *protected.* Kuna *documents* zinaonesha kabisa fedha hii imeingia sehemu fulani. Jamani leo Shirika la *UDA* limekuwa *PRIDE*. Leo Shirika la *UDA* limekuwa mtu fulani kwa jina, lakini wanatembea mtaani. Wakati vibaka huko wakikamata kitu hizo hizo fedha shilingi 200/= yuko selo. Sasa naomba Serikali ituambie hawa watu ambao kuna ushahidi wa dhahiri kwamba wameiba fedha zetu za umma wamechukuliwa hatua gani? (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika mantiki hiyo hiyo, mimi nilikuwa Mjumbe wa Mashirika ya Umma kipindi kilichopita. Kuna mtazamo kwamba labda maneno yakiwa yanasemwa na mtu fulani hayakai vizuri. Mheshimiwa Zitto alikuwa Mwenyekiti wangu nakumbuka tulizungumza miaka ile miwili na nusu kama 2010, tukasema jamani Serikali yetu ina hisa kwenye Makampuni mbalimbali ambayo ni chini ya asilimia 50 lakini hatuna mamlaka ya kukagua kwa sababu sheria zimeelekezwa tuna mamlaka ya kukagua Makampuni ambayo Serikali ina hisa kiasi gani, chini ya asilimia 50 hatuwezi kuzikagua. Kuna Kampuni kubwa kama BP hebu *just imagine* utajiri gani uliopo *BP*, lakini *we know nothing. ZAIN we know nothing*, Kiwanda cha Urafiki *we know nothing*. Hii *UDA* ni cha mtoto, sasa tunasema lini tutajifunza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli tunatoka kwenye madini tumeliwa wee, tunaamka wakati madini yamepotea. Tunakuja kwenye ardhi sasa, ardhi wameshaibariki, Ofisi ya Waziri Mkuu wanafanya mikataba, *worst* kinyume cha Sheria ya Ardhi inavyotaka mwekezaji mgeni kumiliki ardhi. Hatukomi sasa tumekuja kwenye *UDA,* watu wamegeuza *UDA* mali yao binafsi. Sasa niiombe Serikali ilichukulie hili suala kwa mapana yake. Niiombe Serikali yale maagizo na mapendekezo yanayotolewa na Kamati mbalimbali, tulizungumza hapa jamani Wabunge msiingie kwenye Bodi mnakuwa wapole, tukija kusimamia Serikali tunapigwa maneno. Lakini unakuta Wabunge hao hao ambao wako kwenye hizi Bodi hawazisaidii. Kama ni Wajumbe wa Kamati wanakuja ku-*lobby* kwenu, mnaambiwa jamani eeh Bodi yangu inakuja kaukeni. Hatuendi hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi tunaomba tunapoangalia maslahi ya nchi jamani, tuweke maslahi yetu pembeni. Nasikitika kwa sababu kuna *lack of seriousness* kubwa sana. Mwenyekiti wa Kamati ya Mashirika ya Umma amezungumza vizuri sana, lakini hapa kuna hii taarifa nadhani ya Serikali ya *CHC If, I am not mistaken.* Ukurasa wa (4) anasema kabisa "Bodi ya *UDA* ilikiuka kanuni za Utawala Bora kwa kutowashirikisha wanahisa katika mchakato wa kuuza hisa za *UDA* na ambazo hazijagawiwa na *Simon Group*. Hata hivyo, kwa kuwa taratibu zilizokiukwa ni za ndani ya Kampuni *internal matters* kosa hili halitaathiri kisheria mauzo ya hisa yaliyofanywa kwa *Simon Group"*. Hii ni taarifa ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine linasema "Mkataba wa kugawa hisa *UDA* ingawaje mkataba huu ni halali, ulikuwa haujaanza kutumika kwa sababu masharti yaliyoko katika kifungu fulani ilikuwa bado haijatekelezwa". Wanakiri kwamba mbali na mapungufu mkataba ulikuwa umevunjwa haijakiuka, lakini wanahalalisha kuvunjwa ama kukiukwa kwa mkataba ili *Simon Group* waendelee kuwa Kampuni. Kitu kibaya kuna barua mbalimbali zinazoonyeshwa kulikuwa kuna mawasiliano kutoka *UDA* kwa Mwenyekiti kwenda kwa Miundombinu kwenda kwa Wizara ya Fedha na vile vile ikatoka nyingine kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu kwenda kwa Meneja Mkuu wa Shirika la Usafiri wa UDA. Kila barua inazungumza lugha yake. Kutoka *UDA* kwenda Wizara ya Fedha inasema tumepata mwekezaji. Kutoka Wizara ya Fedha kwenda Miundombinu wanaambiwa andaeni utaratibu wa kumpa huyu mwekezaji pamoja na hizo *annulated shares.* Ukitoka huko kwa Waziri Mkuu naye anakuja na lugha yake *at least* ikawa inatia matumaini, lakini tumechelewa. Lakini Wazungu wanasema *it's never too late,* nyie ndio watawala. Unapokuwa mtawala maana yake umeshikilia mpini sio, sasa tuonyesheni kwa namna gani mmeshikilia huo mpini mtusaidie kuokoa Shirika letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, wananchi wa Dar es Salaam wajue Wabunge wao wote tuko *against* na huu ufisadi na ufedhuli unaofanywa wa kuliuza Shirika la UDA.

Wakiona bajeti hii imepitishwa, wakiona Shirika la *UDA* limeuzwa wajue ni Serikali imeshindwa kuwasikiliza Wabunge pasipo kujali chama. Ahsanteni sana. (*Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naomba sasa kumwita Augustino Maselle na Mheshimiwa Filikunjombe ajiandae. Pia Mheshimiwa Josephine Genzabuke ajiandae.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupewa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hii hotuba ya Waziri wa Uchukuzi. Kwanza kabisa kabla sijaendelea na mchango wangu ningependa ninukuu aya 1.3 ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu ambaye amesema kwamba:-

"Naomba nilikumbushe Bunge lako Tukufu kuwa Wizara hii imeundwa mwezi Novemba 2010 kwa sababu hiyo haikuwa na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011. Hata hivyo, Kamati ilipata fursa ya kujadili utekelezaji wa shughuli za Wizara hii tangu ilipoanzishwa hapo Mei, 2011 pamoja na kuchambua bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2011/2012 kama yalivyowasilishwa mbele ya Kamati. Napenda kutoa taarifa baada ya kuipitia bajeti ya Wizara hii Kamati yangu haikuridhishwa na bajeti finyu ambayo haikidhi mahitaji ya utekelezaji wa shughuli za msingi za Wizara hii kutokana na hali hiyo Kamati iliitaka Serikali kutafuta fedha za kutosha kwa ajili ya kuimarisha usafiri wa reli, usafiri wa majini na kuzikomboa ndege za Shirika la Ndege la Tanzania zilizoko kwenye matengenezo nje ya nchi. Kutokana na hali hiyo Kamati iliitaka Serikali kutafuta fedha za kutosha kwa ajili ya kuimarisha usafiri wa reli, usafiri wa majini na kukomboa ndege za Shirika la Ndege la Tanzania zilizoko kwenye matengenezo nje ya nchi". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ifanye juu chini kuhakikisha kwamba fedha zinapatikana za kuweza kulifufua Shirika la Reli maana Shirika la Reli ni la muhimu sana katika uchumi wa Taifa. Nchi zote ambazo zimeendelea nyingi zimenufaika kwa kujaliwa kuwa na bandari, kuwa na nchi kavu na vilevile kuwa na anga. Majaliwa haya Tanzania na sisi tunayo. Kwa mantiki hiyo basi Serikali katika hili naiomba kabisa ihakikishe kwamba inatenga fedha za kutosha kuhakikisha kwamba mashirika haya yanafufuliwa na kuanza kufanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nijaribu kushangaa kitu kimoja. Kwamba mashirika mengi yanayoanzishwa katika nchi hii mara nyingi yanakuwa hayana ufanisi yanapokuwa chini ya usimamizi wa umma. Lakini yanapobinafsishwa ufanisi unaonekana. Kuna nini hapa? Mifano *TBL* wakati ikiitwa Tanzania *Breweries* ikimilikiwa na Tanzania asilimia mia moja vinywaji vya bia nchini vilikuwa adimu mno. Lakini watumishi ni hao hao Watanzania, Shirika hili lilipobinafsishwa ikapewa menejimenti ya wazungu lakini watumishi ni hawahawa, bia sasa hivi ni za kumwaga, mtu anakwenda kujimwagilia yeye mwenyewe anavyotaka na anaziacha huko. Waliofanya kazi ni watanzania hawahawa. Sasa shida ni nini? Twende kwenye Kampuni ya Sigara. Likiwa linamilikiwa na Watanzania wenyewe sigara zikawa adimu na watu wakawa wanagongeana. Likabinafsishwa na menejimenti ikabadilika lakini watumishi walio wengi ni Watanzania hao hao. Sasa hivi wanazalisha sigara za kila aina na Watanzania wavutaji wanavuta mpaka wengine wanaamua kustaafu. Sigara bado zinaendelea kuzalishwa na kampuni inafanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna nini nyuma ya mashirika ya umma. Sasa leo Shirika la Reli, Shirika la Ndege, Shirika la Bima haya yote yako chini ya usimamizi wa Serikali. Lakini yote yako taabani vibaya sana. Hii ni aibu. Ukiangalia kwa mfano na kuna mingine ipo hapahapa. Angalia Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) inaendeshwa na Watanzania hawa hawa lakini ilifanyiwa marekebisho ya kimenejimenti ikapewa mamlaka, sasa hivi inakusanya mapato na ni mamlaka ambayo sasa ina ufanisi wa hali ya juu na linakuwa ni shirika la kupigiwa mfano. Sasa kama Serikali iliweza kuliona hili ikaamua kuanzisha *TRA* kwa nini sasa inashindikana kwa Shirika la Reli na kwa nini inashindikana kwa Shirika la Ndege? Leo hii nchi hii ina ndege tatu, watumishi 182, ndege hizo zenyewe hazifanyi kazi zingine, sijui ziko wapi? Lakini sasa leo watu hawa 182 unaendelea kuwalipa mshahara, *logic* iko wapi? Inabidi kwa vyovyote vile tutafakari upya na kuchukua hatua. Tujisahihishe tuweze kuona ni wapi ambapo tunakosea, vinginevyo sasa nchi hii itakuwa katika matatizo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokuwa na bandari, unapokuwa na reli na meli maana yake unazungumzia habari ya usalama wa nchi kiuchumi na kisiasa. Sasa sisi Watanzania tumejaliwa kuwa na bahari ambayo ina vina tu vizuri na kwa maana hiyo tunaweza tukaanzisha bandari nzuri za kuweza kusababisha mapato mazuri na kuimarisha uchumi wetu. Tuna bandari ya Tanga, bandari ya Dar es Salaam na ya Mtwara, naomba kabisa kabisa Serikali ifanye juu chini kuhakikisha kwamba bandari hizi inaziboresha kwa upande wa baharini. Lakini tukienda kwenye maziwa vilevile tuna bandari ya Mwanza, tuna bandari ya Bukoba na bandari ya Musoma. Tukienda Ziwa Tanganyika tunazo bandari ya Kigoma. Bandari hizi hata mkoloni wa kwanza Mjerumani aliona umuhimu wake ndiyo maana akajenga reli ya kati na ile inayokwenda kule kaskazini. Alikuwa na maana nzuri kwa maana ya kuimarisha uchumi wake. Sasa sisi tuliokuja kurithi, tunaamua kupuuza jambo hili matokeo yake madhara kwenye uchumi wetu yanaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niiombe Serikali kwa dhati kabisa kama ilivyochukua jukumu la kujenga barabara za lami nchi hii, basi na Wizara ya Uchukuzi katika bajeti zake zijazo na kwa sababu bajeti hii ni ya mwanzoni, tunayo bajeti nyingine mpaka kufika mwaka 2015, tutakuwa na bajeti za kutosha. Serikali ifikirie namna ya kutoa pesa za kutosha kwa ajili ya Wizara hii. Nazungumza haya kwa sababu kama Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu ilivyoshauri wakasema kwamba hii Wizara ni mpya na kwa maana hiyo mambo mengi hayajakaa sawa. Lakini katika siku za baadaye Serikali ichukue jukumu zuri. Labda kwa upande na kabla sijamaliza niishukuru tu Serikali kwanza kwa kuwa na mashirikiano mazuri na Serikali za nchi jirani za Burundi na Rwanda. Kwa upande wa Jimbo langu ushirikiano huu umekuwa na manufaa mazuri sana kwa sababu sisi watu wa Jimbo la Mbogwe na Wilaya ya Bukombe na Kahama tumenufaika sana na ushirikiano huu kwa sababu tumepata barabara ya lami inayotoka Isaka–Rusahunga mpaka inayokwenda nchi jirani za Rwanda na Uganda na hivi sasa hapa Serikali na naomba napo ninukuu kushirikiana na Serikali za Rwanda na Burundi kuanza ujenzi wa reli mpya kutoka Dar es Salaam kwenda Kigali Rwanda na Msongati Burundi. Anasema:

"Serikali za Tanzania, Rwanda na Burundi zimekubaliana kwa pamoja kutengeneza mradi huu mkubwa awamu ya kwanza ya mradi huu ambayo ni upembuzi yakinifu imekamilika Disemba 2009, usanifu wa kina wa uendeshaji wa reli kutoka Dar es Salaam mpaka Isaka–Keza–Kigali kilomita 1464 na Keza–Msongati kilomita 197 unatarajiwa kuanza kufanyika katika mwaka wa fedha 2011/2012."

Naomba katika hili Serikali ilifanyie kazi na sisi watu wa Mbogwe, Bukombe, Kahama tutanufaika na Shirika hili la Reli litakalokuwa limeanzishwa na Serikali zetu hizi tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nihakikishiwe tu kwamba, itapatikana hela kwa ajili ya utengenezaji wa reli ya kati, Kiwanja cha Ndege cha Mwanza na ndege za *ATCL* zianze kufanya kazi. Kama hela haipatikani kufikia kesho kwa kweli nitakuwa siko tayari kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasahau, kwanza nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuliomo humu ndani, nitoe kabisa azimio langu. Kwamba siungi mkono kabisa bajeti hii. Bajeti hii naipinga kwa moyo wangu wote na kwa nguvu zangu zote. Nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge tufike mahali humu ndani tujue kwamba sisi ni mhimili mwingine kabisa na sisi sio Serikali, sisi ni Bunge. Naomba sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu tusifanye kazi za Mawaziri humu ndani. Tufanye kazi zetu za Kibunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa nafasi za pekee naomba niwasihi sana Wabunge wenzangu wa Chama cha Mapinduzi tuungane na Kambi ya Upinzani kwa pamoja leo tuipinge bajeti hii. Hili nilitaka niseme mwishoni lakini nimeona niliseme sasa kwani ningeweza kulisahau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza nataka niwapatie pole wananchi wa Ludewa ambao walikuwa wakisafiri kutoka Kyela kwa boti leo usiku wakapata ajali katikati ya Lumbila na Kilondo. Walikuwa 13, nashukuru Mungu wote wameokolewa salama lakini boti na mizigo vyote vimezama. Nawapa pole sana. Tuko pamoja. Tumetuma boti nyingine kwenda kuwasaidia. Ndiyo

usafiri wetu duni huo na ndiyo maana humu ndani napinga bajeti hii kwa sababu yao. Lakini pia na mimi mwenyewe mnipe pole kwa sababu na mimi yalinikuta hayo hayo wiki mbili zilizopita. Miaka 50 ya uhuru leo bado wananchi wa Ludewa wanasafiri kwa mitumbwi. Bado wananchi wa Ziwa Nyasa mnaambiwa Serikali yenu ni sikivu; Bajeti inakuja hapa, hamjatengewa chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii naipinga kwa sababu nyingi sana na nianze na sababu ya kwanza. Sababu ya kwanza ukisoma bajeti yote ya Wizara mle ndani Shirika la Huduma za Meli ambalo linapaswa kuhudumia Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria na Ziwa Nyasa halijapewa fedha. Shirika la Meli (*MSL*) waliomba pesa kidogo tu *5.4 billion* wamepewa *1.4 billion* kwa ajili ya bima na madeni tu. Kwa fedha hii maana yake hata kesho Shirika hili tukiliruhusu haliwezi kununua hata lita moja ya mafuta, haliwezi kukarabati meli. Sisi Wabunge tumejisahau tuna magari na Waheshimiwa Mawaziri wana magari. Wapiga kura na wananchi walionituma wanapata tabu, wanazama kwenye maji kila siku. Wananchi wa Ludewa mnataka leo wazame kisha mtume rambirambi. Wananchi wa Ludewa hawataki rambirambi. Leo ningezama mngetuma rambirambi, rambirambi hatutaki, boresheni usafiri Ziwa Nyasa. Serikali hii iwe na huruma. Serikali sikivu iyafanye hata kwa vitendo. Serikali sikivu ioneshe kwenye bajeti kwamba inawajali wananchi na kuwathamini. Nawaomba sana Wabunge mnaotoka Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na mnaotoka Ziwa Nyasa wote mniunge mkono bajeti hii isipite mpaka hapo Shirika la Huduma za Meli litakapopewa fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Lupingu wamenituma, wananchi wa Makonde, Lufuma, Kilondo Lumbila na Manda haya ninayosema si yangu wameniambia leo nikatae na nipinge hii Bajeti. Wananchi wa maeneo hayo niliyoyataja hawajakuwa na meli kubwa toka mwaka 1974. Mwaka huu mwezi Januari tena kwa kusumbuana na kwa kulibembeleza sana Shirika la Huduma za Meli wameanza angalau kutuhudumia kwa meli hizo mbovu na chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Shirika la Huduma za Meli kwanza halijakuwa *specified*, kwanza wengine ni wepesi sana kusema kwamba shirika hili ni kama *TANESCO,* mnasema *TANESCO* wao tulikuwa tunashindwa kuwahudumia kwa sababu walikuwa *specified*. Shirika la Huduma za Meli nani ameli-*specify,* Hatulihudumii, tumeliacha na tumelitelekeza. Tunawasahau wapiga kura, tumesahau wananchi wanaotoka Ziwa Nyasa na wanaotoka Ziwa Tanganyika na wanaotoka Ziwa Victoria. Hii haiwezekani, msipoleta fedha kwa ajili ya wananchi wa Ludewa nitawaomba sana, sisi ni wepesi sana kusema CHADEMA wanaandamana, lakini nitakwenda kuwahamasisha, mimi ni Mbunge wa Chama cha Mapinduzi, lakini nitakwenda kuwahamasisha wananchi wa Ludewa tuandamane. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni miaka 50 sasa ya uhuru. Serikali hii ni ya ajabu sana, jana wanasema sungura ni mdogo, hivi aliyewaambia mfuge sungura ni nani? Kwa nini msifuge tembo? Kwa nini msifuge ng'ombe? Sungura mdogo miaka 50 ya Uhuru sungura mdogo? Huu ni uonevu na ni upendeleo. Hivi leo wananchi wa Ludewa tena kwa mbinde na kwa kusuguana anapewa kilomita moja na nusu ya lami. *This is a shame to our Nation.* Hii ni aibu kwa Serikali yetu, haitutendei haki. Hatuwatendei haki wapiga kura na wananchi wetu maskini tumewasahau. Wananchi wale 13 wa Ludewa wangezama leo hii zingetumwa salamu za rambirambi. Nasema salamu za rambirambi Ludewa hatutazipokea. Kama ni kufa basi wananchi Ludewa wamekufa sana. Wizara hii itusaidie na Serikali yetu itukumbuke. Iwe na huruma kwa watanzania. Kuna masuala fulani ni masuala ya Kitaifa na ni masuala ya msingi. Tuache itikadi zetu. Tusisubiri CHADEMA au *CUF* waseme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya mambo hawa ndugu zetu wa CHADEMA sisi ndiyo tunawapa sifa. Tunafanya makosa huku, tunafanya uzembe, Serikali yetu inatuangusha. Wenzetu wanayachukua wanaandamana. Sisi tunabaki kulalamika tu. Nasema na sisi Ludewa tutaandamana kupinga bajeti hii *whether* ni CCM au la bila kujali itakadi zetu. Miaka 50 ya Uhuru! Hamtutendei haki ndugu zanguni. Bajeti hii siiungi mkono na nataka kutoa pendekezo. Huu ni uzembe, tazama Wizara hii, nilishawahi kuwaambia siku moja Mawaziri wetu hawapendani, Wizara hii ya Uchukuzi na mimi niite Wizara ya Uchokozi tu, kwanza Katibu Mkuu na Waziri wake hawaongei, hawapendani na hawazungumzi. Sasa tutapata Bajeti nzuri? Itawezekana? Haiwezekani. Katibu na Waziri wanakaa hawaongei! Inawezekanaje? Tutakwenda! Tutafika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kwa majozi makubwa sana. Wananchi wa Ludewa tumevumilia sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri naomba ukae chini. Mheshimiwa Mbunge endelea.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kwamba tufike mahali sasa tuweke *standard* kwa Mawaziri wetu kwa mfano, Waziri anayeshindwa kufanya kazi na anayeleta matatizo kama haya tumshughulikie na tuweke sheria. Wenzangu wamesema mengi tena kwa uchungu sana na mimi nasema haya kwa uchungu sana kwa sababu wananchi wa Ludewa wanapata tabu, wanakufa kila siku, Mkandarasi toka China aliyejenga ule uwanja wa Taifa ameuawa haijapita miezi mitatu, nataka kusema ili kusudi Mawaziri wetu wafanye kazi na wajitume, tuwape hadidu za rejea, wasipofanya kazi, Waziri huyu anyongwe. Ndiyo watafanya kazi! Ni afadhali afe Waziri mmoja kuliko kufa watu kumi na tatu au watu kumi na tano! Haiwezekani! Haya ni mauaji tunayafanya sisi kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napinga hoja mpaka Shirika la Meli lipewe fedha za kutosha na tutaandamana sisi wenyewe Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie Reli ya kutoka Mtwara, Songea, Peramiho, Mbamba Bay kwenda Liganga na Mchuchuma, kwenye kitabu Waziri anasema mwekezaji ndiyo anatafutwa sasa, haiwezekani! Haya ni maneno ya kutaka sisi tupitishe Bajeti tu. Haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Liganga na Mchuchuma ni kwa ajili ya wananchi wote siyo kwa ajili ya wana Ludewa peke yake. Acheni ubinafsi huo. Leo utasema Mwekezaji amepatikana kuwekeza Liganga na Mchuchuma. Halafu miundombinu hakuna nani atawekeza, nani atakuja Ludewa kwenye mazingira duni kama haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti naipinga na nawasihi Waheshimiwa Wabunge wenzangu tupinge kwa nguvu zetu zote, bila kujali itikadi ya vyama vyetu humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara imeshindikana tumesema sungura mdogo, reli ndiyo hiyo, hata *air strip* hakuna! Mheshimiwa Mbowe anaomba uwanja wa Ndege, sisi tunaomba hata *air strip* ndogo tu, hako nako inashindikana? Serikali gani sikivu, haitaki kusikiliza wananchi wa Ludewa? Tumewakosea nini wananchi wa Ludewa kwa Mwenyezi Mungu? Haiwezekani bajeti yenu tutaipinga. Tuungane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mtemvu na Wabunge wote wa Dar es Salaam pia wamenituma kuhusu Shirika la UDA na *Air Tanzania*. *Air Tanzania* ni shirika ambalo ukilitazama sana unashindwa kuelewa kama kweli tuko makini, wenzetu Uganda wana shirika lao la Ndege na wao ni maskini kama sisi lakini wanafanikiwa, Kenya pia wanafanikiwa wana ndege hamsini sasa. Sisi hata ndege moja hatuna, tuna wafanyakazi 182. sijui wafanyakazi hawa 182 watawabeba abiria mgongoni, hata sielewi. Lakini kwenye Wizara zingine tumetenga fedha na *surplus* na *standby* zimekaa, kwamba ikitokea hivi *standby* fungu hili hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwe na huruma. Haiwezekani Mashirika yetu yanakufa na sisi tunayatazama, naomba Wabunge wenzangu, ninyi ni Wabunge tufanye kazi za Kibunge tusifanye kazi za Serikali. Najua kabisa maneno haya kuna baadhi ya watu yanawakwaza hapo mbele mtusamehe sana, najua kuna watu wanakasirika mtuwie radhi lakini ndiyo wajibu wetu. Wengine wanasema nimemchoma mkuki Waziri hapo mbele, lakini nasema siyo kwamba wachomwe mkuki tu mkishindwa kutimiza napendekeza Mawaziri ambao hawafanyi kazi wanyongwe! Ni afadhali akafa Waziri mmoja kuliko kuua wana Ludewa 20 au 30 kila mwaka na kila siku. Hii ni dhambi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la UDA, naomba niweke bayana kwamba kimsingi sipingi kupata Mwekezaji wa ndani, lakini taratibu na kanuni ni lazima zizingatiwe, Mwekezaji huyu anakuja hapa ndani leo anasema kabisa Shirika hili ni la kwangu lakini unamwuliza malipo umeweka wapi, malipo anasema fedha ya kwanza nimemuwekea Idd Simba, sh. 250,000,000/=, sasa UDA ni ya nani? UDA ni ya Idd Simba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zimewekwa kwenye akaunti ya Idd Simba, benki M, Tarehe 2 Septemba mwaka 2009, yeye anadai ni kwa ajili ya kununulia UDA. Tulisema hapa. Tatizo letu sisi Wabunge wa Chama cha Mapinduzi tunatumia wingi wetu vibaya, kwa sababu yale maoni yalikuwa ni ya Kamati lakini kwa sababu aliyatoa Mheshimiwa Zitto Kabwe sisi tulimpinga, tulitoa mapendekezo *CHC* waongewe muda wa kufanyakazi *perpetually* lakini pia waongezewe jukumu la kuhakikisha kwamba wanatazama mashirika yote ambayo hisa zake ziko chini ya hamsini ambako sisi Wabunge hatuwezi kwenda. Tulipinga kwa sababu alisema mtu wa Upinzani lakini tulisahau kwamba kuna maslahi ya Taifa pale ndani na mashirika yanayopigwa hivi yapo mengi ndugu zanguni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa leo wanalalamika tunayajua kwa sababu wamedhulumiana, hii pesa aliyopewa Idd Simba ilikuwa ni *ten percent* hii, wala haikuwa ya kununulia UDA alishachukua mgawo wake.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wangu wote napinga kabisa bajeti hii isipite. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kweli tuna uchungu na nchi yetu lakini naomba maneno kama Waziri anyongwe kwenye *Hansard* yasiandikwe, *Hansard* isichukue maneno hayo, tuna uchungu na nchi yetu, tuongee kwa maneno ya kusaidia Serikali yetu. Baada ya maelezo hayo, naomba kumwita Mheshimiwa Josephine Genzabure na Mheshimiwa Alhaji Rage ajiandae.

**MHE. *ENG.* STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti Mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Naomba tuendelee mwongozo baadaye.

**MHE. JOSEPHINE J. NGENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii adimu, nimekuwa nikiitafuta nafasi tangu Wizara ya Ujenzi, lakini leo kwa miujiza mikubwa nimeweza kupata nafasi kwenye bajeti hii ya Wizara ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuchangia naomba nirekebishe jina langu, naitwa Josephine Ngenzabuke siyo Ngenzabure.

**MWENYEKITI:** Nakuomba radhi sana kwa usumbufu.

**MHE. JOSEPHINE J. NGENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza leo, sitaweza kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Viongozi wote wa Wizara ya Uchukuzi, isipokuwa nitampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Peter Serukamba na nitampongeza Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, mdogo wangu Mhonga, nawapongeza sana kwa hotuba zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua watu wengi watashangaa leo kutokuunga mkono hoja hii ya uchukuzi. Nikiunga hoja hii ya uchukuzi, watu wa Wilaya ya Kibondo watanishangaa, watu wa Wilaya ya Kakonko watanishangaa, watu wa Buhigwi watanishangaa, watu wa Kasulu watanishangaa, Kigoma Vijijini watanishangaa, Kigoma-Ujiji watanishangaa, sitaunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze kwa dhati kabisa viongozi waliotutangulia, kwa sababu ni utamaduni wetu sisi Watanzania kuyaenzi mambo mazuri yaliyofanywa na viongozi waliotutangulia, naomba niwashukuru Wabunge wote wa Mkoa wa Kigoma mwaka 2005/2010 kwa umoja wetu tuliokuwa nao tulipokuwa hapa Bungeni. Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Mhonga, Mheshimiwa Nswazungwanko, Mheshimiwa Kijiko, Mheshimiwa Chiza, Mheshimiwa Serukamba, Mheshimiwa Sijapata mnajua alivyokuwa anapambana kuhusu reli,

Mheshimiwa Msambya na mimi Josephine tulikuwa kitu kimoja hatukujali itikadi, wote ilikuwa ni Kigoma kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyojidhihirisha leo kwenye hotuba ya viongozi wetu, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu Mheshimiwa Peter Serukamba, Kigoma-Ujiji, Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Viti Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie kusema tena kwamba kwa Waheshimiwa Wabunge wa Kigoma walioingia sasa hivi, mambo ya Vyama kwanza pembeni. Maana ni juzi tu tumekwenda nyumbani tukasimama majukwaani tukasema Wabunge wa CCM hawawatakii wananchi mema, naomba niseme kwa masikitiko makubwa hakuna mtu anayewapenda watu wa Kigoma kama mimi Josephine na Wabunge wa Kigoma. Tunawapenda wote na kwa ushirikiano tutahakikisha tunasemea Kigoma kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niseme, kikwazo cha usafiri wa reli imekuwa ni mtihani mkubwa kwa wananchi wa Kigoma, tumesema tangu mwaka 2005 reli inatuathiri sisi watu wa Kigoma, ndiyo maana nasema kwamba akiwepo mtu wa kusema kwamba Wabunge wa CCM hawana uchungu na watu wa Kigoma hatutendei haki kwa sababu hata sisi ni waathirika kati ya waathirika. Mimi ninayeongea napanda treni kuja huku ndiyo uliokuwa usafiri, lakini leo hii nahangaika sana, kwa sababu ndege hakuna, inabidi nisafiri kwa kuunga unga nafika Dar es Salaam nimeshachoka, lakini wakati ule treni ilipokuwepo siku mbili tu nimeingia Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukimwona mwananchi wa Kigoma anavyoteseka utashangaa sana, sisi viongozi tukiwa huku hatujui adha wanayokutana nayo wananchi wa Kigoma, wananchi wa Kigoma wanateseka sana. Usafiri hauaminiki, leo inaweza kuwa ni ratiba ya treni unajua kwamba jioni leo Jumapili treni itaondoka, ukifika pale wanasema treni hakuna, wananchi wanalala pale, wanalala njaa, watoto wadogo wanapata shida, wanapigwa na baridi, mbu wanawauma kwa sababu ratiba za treni haziaminiki kwa sababu reli haiaminiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimesema nikiunga mkono bajeti hii nikirudi nyumbani sina pa kujificha, watafanya maandamano ya kunizomea na leo nasema sitaki kuzomewa. Nataka pesa ziongezwe ili mustakabali wa utengezaji wa reli ujulikane. Watu wa Mkoa wa Tabora, Mkoa wa Mwanza, Mkoa wa Katavi, Waziri Mkuu hawezi kusema ngoja tumsemee, kati wa waathirika wa reli hii na Mkoa wa Katavi wamo. Watu wa Rukwa wote hao ni waathirika wa reli hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeteseka sana, watu wa Kigoma tumepata mateso makubwa sana tuhurumieni, ongezeni pesa ili reli iweze kutengenezwa, treni ziweze kupita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano tuliletewa mabehewa ambayo ukiingia kwenye mabehewa yale yalikuwa tofauti na mabehewa tuliyokuwa nayo kabla reli haijabinafsishwa kupelekwa kwa *TRL*. Kwa sababu mabehewa tuliyoletewa yamewekewa nondo, kwa hiyo, ukiwa ndani ya chumba huwezi kutoa kichwa kuchungulia nje nondo zitakuminya utarudisha mwenyewe kichwa ndani bila kupenda, ndiyo mabehewa tuliyoletewa sisi. Sisemi vibaya kwamba Wafungwa siyo ndugu zetu kwa sababu siwezi kujua kama mimi nitamaliza maisha yangu nikiwa sijaingia mle ndani. Lakini mabehewa tuliyoletewa sisi ni sawa na jela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa hivi Kigoma hatuna behewa la daraja la pili, daraja la kwanza behewa ni moja, na lenyewe ni chumba cha watu wawili na chumba kinachofuata ni cha wafanyakazi wa reli, mambo ya *buffet* hamna, mambo ya *second* class hakuna, katika hili naomba Serikali ijipange upya iongeze pesa ili tuweze kutatua tatizo la reli, Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri wa reli ilikuwa ni mkombozi wa wananchi wa Kigoma, leo Taifa limepoteza pato kubwa sana kwa sababu mzigo inayopelekwa Kigoma kwa njia ya reli hakuna, kwa hiyo, Serikali imepoteza mapato haiingizi pato la Taifa, lakini wananchi wameathirika sana, wameshindwa kufanya biashara, hawawezi kufanya kwa njia ya kupeleka mizigo kwa njia

ya reli, wanalazimika kukodi malori kutoka Dar es Salaam kwenda mpaka Singida, Kahama, ndiyo wanajua kwenda Kigoma, mizigo inakaa njiani siku mbili hadi tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na wananchi kukosa usafiri wa treni lakini bado mizigo haisafirishwi, Taifa linapoteza mapato, wananchi hawazalishi, kwa sababu hiyo, wananchi wa Kigoma tunaathirika sana kutokana na treni kutokuweza kufanya vizuri na mabehewa ya mizigo kutokuweza kwenda Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara wa Kigoma walishasahau kusafirisha mizigo kwa njia ya reli, wanasafirisha kwa njia ya mabasi, wanaungana wawili wawili wanakodisha roli wanapeleka mizigo yao Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu jaribuni kuwa wacha Mungu, muwahurumie watu wa Kigoma na wenyewe hawakujitakia kuishi mpakani. Usafiri wa treni ndiyo usafiri ambao una bei ya chini kwa mtu mwenye kipato cha chini. Wananchi maskini, wananchi wenye kipato cha chini, usafiri wao rahisi ni treni. Ukitoka Kigoma Kuja Dar es Salaam nauli shilingi elfu ishirini lakini kwa basi ni shilingi elfu hamsini. Watanzania wengi hawana elfu hamsini, uwezo wao ni elfu ishirini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi wanakufa pale wanapokuwa pengine wamekwenda hospitali wametibiwa na wamepewa rufaa kwenda hospitali ya Bugando au Muhimbili, wanakufa kwa sababu ya uwezo mdogo wa kutoweza kusafiri kwa mabasi, maana yake mgonjwa anaposafiri anahitaji mtu wa kumsindikiza, sasa akiwaza nauli ya watu wawili shilingi elfu hamsini hana, matokeo yake anasema namuachia Mwenyezi Mungu. Tunaomba Serikali irudishe usafiri wa reli ambao ni mkombozi wa maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumepakana na nchi ya DRC na nchi ya Burundi, tumekuwa tukifanya biashara na wananchi wa DRC na wananchi wa Burundi kwa kupitia bandari na kwa kupitia reli yetu. Sasa hivi tunapoteza pato kutoka kwa watu hawa, kwa sababu usafiri haueleweki na wao sasa wanaanza ku-*plan* jinsi ya kuondoka Burundi wanakwenda Dar es Salaam wananunua mizigo yao wanasafirisha kwa kutumia malori. Baadaye tutabaki tunawatafuta waje wasafirishe mizigo kwa kutumia treni yetu, hatutawapata tena, naombeni tujipange, soko tulilonalo tusinyang'anywe, mbona tunafanya uzembe ndugu zangu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mliangalie suala hili, tusipoteze watu wa DRC, watu wa Burundi, wakipotea kutokupitisha mizigo katika bandari yetu, katika reli yetu, tutakuwa tumepoteza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafiri wa ndege, kiwanja cha Ndege cha Kigoma hakitamaniki ni vumbi tupu. Leo ninavyozungumza tangu mwezi Disemba ndege haziruki kwenda Kigoma, wenye ndege walishaghairi kupeleka ndege zao, ilikuwa inakwenda *Precision Air,* leo haiendi Kigoma, ilikuwa inaenda *Air Tanzania* nayo ndiyo kama hivyo tunavyosikia, hatujui iko wapi. Tukitaka kusafiri siku hizi kama alivyosema Mheshimiwa Zitto Kabwe uwe na milioni moja ndiyo utaweza kuja Dar es Salaam na kurudi Kigoma, wananchi hawana uwezo huo ndugu zangu. Tunaomba wanaohusika mwongeze pesa kiwanja cha ndege kiweze kutengenezwa haraka iwezekanavyo ili muweze kutusaidia wananchi wa Kigoma, tuweze kusafiri kwa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mtu anapata msiba, au anaanguka hata kwa ajali ya gari au anapata ajali yoyote analazimika kwenda kutibiwa Muhimbili ili kuokoa maisha yake, leo ndege hakuna utaokoa maisha hayo? Inawezekana pengine anatakiwa kusafirishwa kukaa kwenye gari hawezi, kitu ambacho kingeweza kumsafirisha kwa urahisi zaidi ni ndege lakini ndege hakuna, wahurumieni watu wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama kile kiwanja cha ndege Kigoma kingekuwa kizuri, kingewekewa lami, leo tungeweza kuingiza pato la Taifa kwa kuweza hata kuuza mbogamboga na matunda nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wangeweza kuja Kigoma wakanunua matunda, wakanunua mboga mboga, sisi pale Bugaga tunalima Kabeji, tunalima karoti, kwa hiyo kama

kukiwa na usafiri wa uhakika, ndege zikiwa zinaruka watu watakuja kununua bidhaa zao kupeleka *DRC*, kupeleka Burundi na kupeleka nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipenda sana Serikali ya CCM lakini katika hili wananchi wa Kigoma hawatanielewa naomba niseme siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Alhaji Ismail Rage na Mheshimiwa Amina Amour ajiandae.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote naungana na Wabunge wenzangu wote na mimi na siungi mkono hoja hii. (*Makofi*)

Kwenye mpira hii bajeti naweza nikafananisha na mtu anayepiga kona, anataka aje afunge mwenyewe inawezekana? Haiwezekani. Kwa hiyo, hii bajeti haina *impact* yoyote ya kuangalia tutaiokoaje nchi hii kutokana na matatizo ya reli, tutaiokoaje nchi hii kutokana na matatizo ya ndege, tutaiokoaje nchi hii kutokana na matatizo ya bandari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ndugu zangu wa Tabora ambao wananisikiliza, nitaongea maneno mengine wasikasirike wala wasilie. Tabora ni Mkoa ambao umeonewa, umenyanyaswa, umepuuzwa kwa muda mrefu bila sababu yoyote. Historia ya nchi hii iko wazi kupata uhuru Mkutano wa Kura Tatu ulifanyika Tabora Parish *Hall* 1958, matokeo yake Tabora tunasifiwa tu. Baba wa Taifa alisoma Tabora, Mzee Kawawa alisoma Tabora, Jaji Mkuu alisoma Tabora, Waziri Mkuu aliyemaliza kipindi chake Mheshimiwa Edward Lowassa alisoma Tabora. Sasa hiyo sisi inatusaidia nini watu wa Tabora?

Historia iko wazi, ndege ya kwanza kutoka Ulaya ilitua Tabora Tanganyika kabla ya Mji wowote katika nchi hii. Leo ukienda kuona Uwanja wa Ndege wa Tabora hauna tofauti na handaki la kwenye vita. Uwanja wa Ndege wa Tabora tume-*sacrifice* wakati wa Vita vya Idd Amin Waheshimiwa Wabunge, mlikuwa hamuelewi, kulikuwa na fedha imetengwa kwa ajili ya kujenga Uwanja wa Tabora, kulikuwa na mkandarasi yuko pale Tabora, kulikuwa na vifaa vya kujengea Uwanja ule wa Tabora. Lakini kwa ajili ya kupambana na Nduli Idd Amin vifaa vyote na yule mkandarasi na fedha zote zikapelekwa Mwanza. Leo Tabora uwanja ule hauna thamani hata kidogo, maana yake nini halafu mnataka mimi niunge mkono hoja hii, sikubali hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye bajeti kuna milioni 16 zimetengwa kwa ajili ya kukarabati uwanja. Lakini hizo zinaongelewa kwenye kitabu sina hakika mpaka pale, bahati nzuri Waziri ni kaka yangu ni rafiki yangu, namheshimu sana pamoja na Dokta Mfutakamba Mbunge mwenzangu wa Tabora. Naelewa kabisa ndugu yangu Waziri wewe ulikuwa Rais kule Toronto, Canada umeacha mamilioni kule kuja kutusaidia hapa. Lakini nataka nikwambie, wamekuzunguka watu ambao hawataki ufanikiwe katika Wizara yako. Haya ndio matatizo ambayo yamekuwepo kwa muda mrefu katika nchi yetu. Tunaoneana, haya watendaji sisi tuliofanya kazi Serikalini wakati wa awamu ya kwanza, ukijenga nyumba kinyume na uwezo wa mshahara wako unaulizwa umetoa wapi. Leo wafanyakazi wa Serikali wana nyumba nzuri kuliko wafanyabiashara, wewe uliona wapi nchi gani hiyo? Hatuchukui hatua yoyote. Unakuta huyu anafanya kazi katika Halmashauri ana gesti 20 au 30, haulizwi hela hiyo ya kujengea hizo gesti umepata wapi wewe? Lakini watu tunaangalia, jamani mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Nchi hii tunaitafuna, mwisho tutashindwa kutafuna tutatafunana wenyewe kwa wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuongelea suala la reli, bahati mbaya huko nyuma nako alikuweko mwenzangu mmoja hapa akawa anaunga mkono Bodi ya wale watu walioua reli yetu. Mimi siungi mkono hata siku moja. Mwanzo wa kuua reli yetu ya kati ngoja leo niwaeleze Waheshimiwa Wabunge, muelewe. Wakati wa *East African Railways Corporation* karakana kuu Tanganyika nzima wakati ule Tanzania ilikuwa iko Tabora. Lakini kwa bahati mbaya kwa ubinafsi wetu karakana ile ikahamishwa na kupelekwa Morogoro. Huhitaji kujifunza (*economics*) masuala ya uchumi katika *issue* ndogo kama hii. Tabora ndio katikati ya reli za kwenda Mwanza, Tabora

ndio katikati ya reli ya kwenda Kigoma njia panda, Tabora ndio kuna reli ya kwenda Mpanda, Tabora ndio kuna reli ya kwenda Dodoma, Morogoro na Dar es Salaam. Unakwenda kuweka karakana kubwa Morogoro maana yake nini kama siyo dharau? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haikutosha hivyo, Tabora tulivyoonewa tunalima tumbaku sisi asilimia 68 kuliko mtu yeyote katika nchi hii. Hakuna zao linaloingiza fedha za kigeni kama tumbaku. Bei ya tumbaku inachezewa ovyo ovyo. Leo zao la pamba wamesema kidogo tu watu hapa, imeundwa Kamati, tumbaku hata haijaundwa Kamati. Nasema kabisa natoa taarifa, natengeneza hoja kwa Serikali nipate maelezo kwa nini bei ya tumbaku imeshushwa ovyo na haijatengenezwa taarifa yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, karakana ya Tabora zamani ilikuwa na wafanyakazi takriban 380, sasa hivi nenda kaangalie wako 13. Hiyo karakana ikipiga mvua hawafanyi kazi, yaani huko kunavuja ni balaa tupu. Tabora tulikuwa na karakana pale Rufita karibu ya Kiloleni, tunatengeneza mabehewa yote ya abiria yanapoharibika, yakifika pale Tabora yalikuwa yanatengenezwa vizuri sana. Tulikuwa na vyuo vikubwa viwili vya reli kimoja kilikuwa *Nairobi Training College* na kingine *Tabora Training College* leo kile chuo kimekaa, unashangaa kabisa watu wa Tabora ni maskini jamani hatuna kiwanda hata kimoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru jana angalau Waziri wa Ujenzi amenikumbuka kunitengenezea barabara. Lakini wananchi wa kawaida wengi hawana uwezo wa kupanda mabasi, uwezo wao uko kwenye treni. Kwa hiyo, napenda kutoa ushauri kwamba kwa kuwa bahati nzuri Waziri Mkuu yuko hapa na Mawaziri, wenyewe wengi wako hapa, hebu leo jioni mkutane jamani muokoe hili jahazi. Uwezo upo, nyumbani kama kuna shida, watoto wanalia baba na mama wapo hamuwezi kusema mnajadiliana kesho kutwa au mtondogoo, mnaitana baba na mama mnaamua, mnamaliza matatizo. Kwa hiyo, ninachosema nina imani kabisa Wabunge wengi hawana ugomvi na Serikali yao wala hawana ubishi, wana imani kubwa na viongozi wao. Lakini wanachoomba Wizara hii iongezewe fedha basi, hakuna kitu chochote wanachogombea hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala limeongelewa la UDA. Suala la UDA linatugusa watu wote. Nchi yetu sisi waoga sana wakati mwingine, watu wanatuchezea mnawatazama. Kule Gaddaf wameona kwamba hawakubaliana naye wametaifisha mali zake zote. Hivi Serikali kama mtu anatukorofisha kwa nini hatutaifishi mali zake? Iraq walipokuwa wanamwondoa Sadam Hussein wametaifisha mali zake zote. Hapa Tanzania kwa nini kama watu wanatudhulumu hatutaifishi mali zao na wanajulikana tunangoja nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na kwa kuwa namwamini Waziri wa Uchukuzi na Naibu wake na Katibu wake Mkuu, wanaweza wakakutana na kuhakikisha kwamba ili bajeti hii iweze kuangaliwa vizuri kesho, basi waangalie reli itengewe siyo chini ya sh. 60,000,000,000/= kwa kweli naweza nikaunga mkono. Nasema kabisa ili tuhakikishe kwamba matatizo hayo yanakwisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuongelea alichoongelea Mbunge mwenzangu asubuhi, niliongea na wafanyakazi wa reli wa Tabora kabla sijaja hapa, wanadai mabadiliko ya nyongeza ya mshahara zaidi ya miaka kumi mpaka leo hayajafanyika. Jamani hawa ni binadamu, tena nina hakika watumishi wengine wa Serikali wanaopitisha hizi bajeti na wenyewe wanafunga, hivi hamuogopi dhambi ninyi mwezi wa Ramadhani kufanya mambo mabaya kama haya? Hata Mwenyezi Mungu hamwogopi? Basi mtuonee sisi hata Mwenyezi Mungu mnataka kumdanganya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kabisa kwamba Serikali yangu ya CCM, nina imani nayo ni Serikali sikivu na wala sina kusudio lolote la kuwaambia wananchi wangu wa Tabora waandamane, sitaki, kwa sababu najua haya ninayoyaongea kuna uwezekano mkubwa kesho, ninavyomjua Waziri Mkuu alivyokuwa mkali akaja na msimamo murua, wananchi wote tukafurahi. Lakini nataka kuhakikisha kabisa kwamba, siungi mkono hoja hii hata kidogo na sitaki kupoteza muda wenu nitoe nafasi na kwa wengine wachangie. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuongelea hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujikita kwenye bandari, lakini kabla ya hapo nitagusia usafiri wa ndege, reli na wa baharini. Nilitarajia leo Waziri atatwambia kwa kuwa tayari amekwishanunua ndege mbili na hivi sasa ziko njiani na wakati wowote zitafika hapa nchini. Lakini la kusikitisha anatwambia kwa kuwa ndege moja iko matengenezo na tayari tarehe 8 itakuja hapa kuanza kazi. Sisi hatutaki mitumba Mheshimiwa Waziri tunataka aje na kauli hapa atuambie ni lini ndege mpya angalau moja itanunuliwa, hilo ndio tunalolitaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikigusia kidogo kwenye usafiri wa reli, usafiri wa reli watu wengi wanautumia hasa wenye kipato cha chini wanasafirishia mizigo yao na wao wenyewe. Lakini la kusikitisha sana na huu usafiri haupo. Nilitaka kuelezea teknolojia ambayo wanatumia nchi za wenzetu kwa usafiri wa reli, lakini nimeshindwa hapa kwa sababu huu tuliokuwa nao unatushinda tutaweza wanavyofanya wenzetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye usafiri wa meli, kuhusu meli hiyo imesahaulika kabisa utafikiri Tanzania hatuna bahari. Huduma za meli hazipo kabisa wala hatukumbuki kama tuna bahari na tunaweza kuwa na usafiri wa meli. (*Makofi*)

Sasa najikita kwenye suala la bandari. Huduma za bandari zina usumbufu. Mtu yeyote akiwa wakala wa forodha, wafanyabiashara au mtu binafsi anapomaliza huduma za *TRA* na kulipia malipo anahitaji siku ya pili ndio akachukue mzigo wake. Lakini badala yake unakwenda Bandari Kuu, unaambiwa mzigo hauko Bandari Kuu uko Keko, kuna bandari kavu siku hizi, sijui Mwenyekiti unazifahamu ama huzifahamu. Ukitoka huko Keko unakwenda kutazama mzigo wako unaambiwa hauko uko Buruguni na huko kuna bandari kavu. Ukifika huko Bandari Kavu ukaukuta huo mzigo wako unaanza tena kulipia mambo yote *wolfage* umeshalipia lakini ule mzigo kutoka bandari kuu kufikishwa pale inabidi ulipe *handling* na malipo chungu nzima unatozwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu umekuwa usumbufu sana kwa wananchi na wizi pia upo. Lakini hayo yote tisa, kumi hivi bandari zinamilikiwa na wageni, iweje Tanzania nchi yetu, ardhi yetu wenyewe kwa nini tusijenge hizi bandari kavu tuwaruhusu wageni ndio waje wajenge hizi bandari kavu? Sisi hapa kila wakati tunakaa tukisema tunakusanya mapato kidogo na vyanzo vya kupata mapato vipo lakini tunazembea. Tayari kuna makampuni kama manne nitayataja baadaye ambayo wanaalikwa wageni na nina wasiwasi na makampuni haya, yalikuwa yanaalika wageni au wageni ni kivuli? Kwa hiyo, namwomba Waziri, hapa atoe ufafanuzi wa mikataba wa haya makampuni ambayo yanamilikiwa na wageni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa hapa, makampuni haya naomba niyataje majina yake, naomba nipewe maelezo ya kampuni hizi, kampuni ya wasomali ambayo inaitwa *Mass*, kuna kampuni ya *FARION* ya Waarabu, kuna kampuni ya wazungu ambayo inaitwa *Toll* je, *TPA* wameshindwa kazi hiyo, kama mmeshindwa kuhifadhi mizigo yetu ni bora mkapeleka bandari nyingine ndio maana sasa hivi tunakaa tunanung'unika kwa nini watu wote wanatumia Bandari ya Mombasa, wanashusha mizigo yao katika Bandari ya Mombasa, ni kwa sababu ya usumbufu na ukifika hawa Wazungu na hawa Wasomali, ukimkuta Msomali ukimuongelesha Kingereza hajui, Kiswahili hajui, ukienda kwa Mzungu vile vile Kiswahili hajui wanapita wakihangaisha wananchi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamenituma wamechoka wanataka mambo haya yamilikiwe na wenyeji wenyewe. Kweli Watanzania hawapo wanaoweza kumiliki hivi, wakajenga kwani wanajenga nini, mabati yapo, saruji zipo, unajenga *yard* halafu mnaweka mizigo, lakini kwa nini Serikali hii kila siku inapoteza mapato kwa njia ambazo hazina maana. Vyanzo vya mapato vipo lakini kwa nini ni wazembe halafu tunasema tunakusanya mapato kidogo. Kwa hali hii tutaendelea kukusanya mapato kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimeanza kuzungumzia Shirika la Ndege, nikazungumzia reli, nikazungumzia bandari, nikaja hili kwa sababu hili ni dogo mno. Hata hili nalo linawashinda Serikali kulifanya? Naomba hapa Waziri atakapokuja ku-*windup* asisahau kunijibu haya makampuni na anionyeshe mkataba wa hizi kampuni nilizozitaja. Nina mashaka kuna kivuli cha

mtu hapa. Kampuni hii inakusanya mapato chungu nzima kwa sababu ukienda useme gari yako imekaa siku sita wanachukua kama milioni moja kwa siku ikikaa. Kuna chaji zingine, chaji kibao na kwa nini tupoteza mapato? Kwa nini hatuwezi kujenga wenyewe, waje wageni wachukue ardhi yetu, wajenge na sisi tuko hapa hapa wanatutazama, halafu wanafanya ufedhuli juu ya nchi yetu. Hili namwambia Waziri alione na mara moja wapewe masaa 24 au 48 waondoke wote tubaki wenyewe tufanye kazi hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja hii. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Amina Abdallah Amour. Kwa vile muda umekwisha sana naomba nimwite Naibu Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa Dokta Harrison Mwakyembe aliomba mwongozo kwangu sasa nimruhusu azungumze ili baadaye niweze kutoa mwongozo. Pia Mheshimiwa Stella Manyanya alitaka kuongea naye nitamruhusu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishasahau kabisa. Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane, sisimami kwa Mwongozo kupinga au kuunga mkono hoja ila kuturejesha tu kwenye mstari maana tunaongozwa na kanuni hapa. Kanuni ya 64 (1)( c) inazuia kufungua mjadala katika hoja iliyoamuliwa katika Mkutano uliopo. Hivyo basi, nataka niseme si sahihi kuanza kujadili vipengele vya bajeti iliyokwishapitishwa na Bunge jana. Kama ni suala la kuhamisha mafungu, hili si jukumu la Bunge tena iachiwe Serikali imesikia. Naomba Mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri nakushukuru sana Mwongozo wangu ni kwamba kama ulivyosema kwa vile jambo hili Bajeti ya Wizara ya Ujenzi ilipitishwa jana, basi na itoshe kusema kwamba Bunge hili kwa umoja wake Bajeti yake jana liliridhia na hivyo kuitakia baraka Wizara ya Ujenzi kutekeleza majukumu yake. Kwa hiyo, hilo suala limekwisha jana. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. *ENG.* STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda umepita kidogo, naomba niseme ni taarifa. Taarifa yangu nilikuwa nimpe Mheshimiwa Deo Filikunjombe kwamba, wakati anachangia nadhani kwa ajili ya uchungu kuhusiana na mambo ambayo ameyaona alizungumzia kwamba yeye atahamasisha wananchi wake kama mambo haya hayatakuwa kama anavyotarajia waweze kufanya hata maandamano. Taarifa yangu ni kwamba sisi kwenye Chama chetu cha Mapinduzi Sera ya Maandamano hatuipendi, tunapenda kufanya mikutano au vikao vyenye tija kama ambavyo tunajadili hapa badala ya kuandamana bila kupata majibu. Nilikuwa naomba mimi nikiwa kiongozi wake kwenye NEC alielewe hilo. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nashukuru taarifa itakuwa imemfikia Mheshimiwa Deo Filikunjombe. Baada ya taarifa napenda kuwashukuru sana kwa ushirikiano ambao mmeonesha. Lakini napenda pia niseme kwamba, kweli tuna uchungu na nchi yetu ila tujizuie maneno makali kama Waziri anyongwe na nini, haya tusiyatumie sana tuelekeze Serikali kwa upendo baada ya kusema hivyo, naahirishwa shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.27 jioni Bunge liliahirisha mpaka siku ya Alhamisi, Tarehe 4 Agosti, 2011 saa tatu asubuhi)*